Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA SITA

**Kikao cha Kumi na Nane - Tarehe 2 Julai, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kabla hatujaanza, ningependa kueleza kwamba, leo kuna nyuso ngeni za Wapiga Picha za Televisheni. Nataka kuwatambulisha kwamba, hawa ni Wapiga Picha za Televisheni ya Oman na wamekuja wameomba ruhusa ya kuwa hapa leo kupitia kwa Mbunge wa Mafia, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, ili waonyeshe huko kwao jinsi demokrasia inavyofanya kazi Tanzania. *(Makofi)*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kwa Mwaka 2004/2005.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU (k.n.y. MHE. PROF. HENRY R. MGOMBELO - MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU):**

Taarifa ya Kamati ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2004/2005.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 168

**Ukarabati wa Vituo vya Afya Buchosa**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA (k.n.y. MHE. SAMWEL M. CHITALILO)** aliuliza:-

Kwa kuwa Wananchi wa Buchosa wanayo haki ya kupatiwa huduma bora za afya hasa kupitia katika zahanati na vituo mbalimbali vya afya. Je, ni lini Serikali itaboresha kwa kuvikarabati vifaa vya hospitali vilivyochakaa pamoja na majengo au kujenga majengo mengine katika Vituo vya Afya vya Nyamiswi, Mwangika, Nyehunge na sehemu nyingine zilizoko Buchosa, hasa ikitiliwa maanani kuwa hivi sasa watu ni wengi kuliko hapo zamani?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Samwel Chitalilo, Mbunge wa Buchosa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua hali ya uchakavu na pia haja ya kupanua majengo au kujenga majengo mapya katika Vituo vya Afya vya Nyamiswi, Mwangika, pamoja na Nyehunge na sehemu nyingine zilizoko Buchosa. Katika kutatua tatizo hili, Serikali imechukua hatua mbalimbali. Kati ya mwaka 2002 na sasa majengo ya wagonjwa wa nje katika Kituo cha Afya cha Nyamiswi na Zahanati za Lugata na Kafunzo yamekarabatiwa na yanatumika. Aidha, jengo la wagonjwa wa nje katika Kituo cha Afya cha Mwangika limekarabatiwa na linatumika. Katika mwaka 2003, jengo la huduma za mama na mtoto *(MCH)* katika Kituo cha Afya cha Mwangika limekarabatiwa na kukamilika. Kazi ya ukarabati wa jengo la wagonjwa wa nje katika Kituo cha Afya cha Kome inaendelea. Jumla ya Sh.21,804,576.90 zimetumika kutekeleza kazi hizi kutoka Mfuko wa Pamoja wa Afya pamoja na ruzuku kutoka Serikali Kuu.

Vile vile kituo cha Afya cha Nyamiswi kimewekewa umeme unaozalishwa kwa nguvu za mionzi ya jua. Vituo vingine vya tiba vilivyofanyiwa ukarabati ni pamoja na Zahanati za Nyanzenda, Kasisa, Lushamba na Bupambwa. Zahanati za Bukokwa, Kalebezo na Nyakasungwa zimejengwa upya. Vifaa vilivyosambazwa ni pamoja na vitanda, mashuka, mablanketi na vifaa vingine vya kufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, ili kuendelea kuboresha kiwango cha utoaji huduma katika Jimbo la Buchosa, katika mwaka wa fedha wa 2004/2005, kazi zitakazofanyika ni pamoja na ukarabati wa jengo la wodi ya wazazi, jengo la huduma za mama na mtoto na nyumba ya mtumishi katika Kituo cha Afya cha Kome na jumla ya Sh.8,533,000 zitatumika, ukarabati wa nyumba tatu za watumishi katika Kituo cha Afya cha Nyakaliro, jumla Sh.5,733,000 zitatumika, ukarabati wa jengo la wodi ya wazazi katika Kituo cha Afya cha Mwangika lenye jumla ya Sh.3.533,000 na ukarabati wa jengo la wagonjwa wa nje katika Zahanati ya Iligamba yenye jumla ya Sh.5,147,000/=.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza uwezo wa kuboresha huduma za afya, Halmashauri imeanzisha Mfuko wa Afya wa Jamii. Bodi ya Afya pamoja na Kamati

mbalimbali katika ngazi za Zahanati, Vituo vya Afya na Kata, zimeundwa na uhamasishaji katika jamii umefanyika. Uchangiaji utaanza rasmi mwezi Julai, 2004.

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Nakushukuru Mheshimiwa Spika, kwa kunipa niulize swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa ni kweli vituo hivi vya Nyamwisi, Mwangika, Nyehunge pamoja na vile vya Nyamhwale na Karumwa jimbo la Nyamhwale vina hali mbaya; na kwa kuwa bado vituo hivi havina magari ya kubebea wagonjwa; na kwa kuwa mwaka huu bajeti ya Wizara hiyo ya Afya itakuwa nzuri; je Serikali sasa itatenga pesa kwa ajili ya kununulia magari ya kuchukua wagonjwa katika vituo hivyo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimhakikishie tu kwamba, ziko juhudi za dhati kabisa upande wa Serikali za kukarabati Vituo vya Afya na Zahanati pamoja na Hospitali kupitia Mfuko wa pamoja wa Afya na maelezo niliyoyatoa ni ushahidi dhahiri kabisa.

Kuhusu magari, nafikiri nilieleza hapa Bungeni sikumbuki labda juzi au hivi karibuni kwamba, tatizo hili tunalitambua, lipo, ni kubwa na tumejitahidi sana kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha, kuja na Programu Maalum kwa ajili ya kununua magari kwa nchi nzima. Lakini kwa miaka miwili mfululizo bado hatujafaulu na tunaendelea kufanya mazungumzo. Kwa hiyo, kwa sasa tunachoomba tu ni kwamba, Halmashauri zinao uwezo kabisa wa kuweza kufanya mazungumzo na wahisani mbalimbali kuweza kutenga fedha kutokana na bajeti zake na nilitoa mfano wa Kilwa ambao wameweza kununua magari manne kutokana na fedha za Halmashauri. Kwa hiyo, tunaishauri Halmashauri itumie *initiative* kujaribu kutafuta mbinu wakati Serikali inaendelea kutafuta ufumbuzi wa kudumu.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, nina swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa Serikali imeamua sasa hivi kupeleka fedha nyingi sana katika Halmashauri kwa mpango wa *Other Charges,* kiasi kimepanda kwa asilimia karibuni 140 kuliko miaka mitano iliyopita. Sasa je, Waziri anaweza kutoa tamko kwamba fedha hizo siyo za kuagizia chakula *OC*, fedha hizo zielekezwe kwenye ukarabati wa Hospitali zilizoko kwenye Wilaya zao, vikiwemo hivi Vituo vya Afya vya huko kwa Mheshimiwa Mbunge na maeneo ya kule Jimbo la Morogoro Kusini Mashariki na Tanzania kwa ujumla? *(Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, masuala ya Bajeti yana utaratibu wake. *OC* inapotengwa inakuwa imeshapewa vile vile majukumu ya kufanya katika kila eneo. Kwa hiyo, kwa kweli tunachosisitiza tu hapa ni kwamba, kila Halmashauri itumie fedha hizo kulingana na maelekezo yaliyokuwa yametolewa na Serikali. Vinginevyo tukifanya kama Mheshimiwa Semindu Pawa anavyosema, basi inawezekana hata fedha zako za barabara pale tukaamua ziende kuchimba visima. Jambo ambalo nina hakika hutapenda.

Na. 169

**Utumiaji wa Takwimu za Mamlaka ya Hali ya Hewa**

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA (k.n.y. MHE. HAMAD RASHID MOHAMED)** aliuliza:-

Kwa kuwa mipango mizuri ya nchi inategemea sana ukusanyaji na utumiaji mzuri wa takwimu:-

(a) Je, Serikali inazitumiaje takwim,u zinazokusanywa na Idara ya Hali ya Hewa?

(b) Je, kwa nini wakati mwingine hutumia vigezo vya Kimataifa na wakati mwingine hubuni vigezo vya kwake?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mbunge wa Kuteuliwa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuafuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inatumia taarifa na takwimu za hali ya hewa katika shughuli mbalimbali. Ninapenda kutoa ufafanuzi wa matumizi ya taarifa husika kisekta kama ifuatavyo:-

Wizara ya Kilimo na Chakula inatumia huduma za hali ya hewa kwa kupanga vipindi vya kulima, kupanda mbegu na kuweka mbolea na kadhalika, kutathmini hali ya mazao kabla ya mavuno, kupata utabiri wa mwelekeo wa mvua na kuwashauri wananchi kupanda mazao ya muda mfupi au yanayohimili ukame pale panapoonekana kutakuwa na upungufu wa mvua.

Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, Kitengo cha Maafa, hutumia taarifa za hali ya hewa katika kutoa tahadhari kwa wananchi endapo kutatokea madhara yatokanayo na hali ya hewa kama vile mafuriko, ukame, upepo mkali, vimbunga na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, katika Sekta ya Ujenzi taarifa hizo hutumiwa na makandarasi kabla ya kuanza ujenzi wa barabara, madaraja, majengo mbalimbali ili yawe na uimara unaostahili. Kwa upande wa Sekta ya Usafiri, taarifa ya hali ya hewa hutumika katika safari za anga na baharini kwa ajili ya usalama. Katika Wizara ya Maliasili na Utalii, hutumia taarifa za hali ya hewa katika kuandaa na kupanga majira ya watalii nchini na Wizara ya Maji na Mifugo, hutumia utabiri wa hali ya hewa kwa mvua za msimu kusaidia wafugaji kujua hali ya malisho ya wanyama na pia kusaidia kufanya utafiti wa vyanzo vya maji.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Nishati na Madini, hutumia taarifa au takwimu za hali ya hewa katika kufanya tathmini na tafiti za kutafuta vianzio vya nishati nchini na katika utafiti mwingine. Kwa upande wa Sekta ya Bima, takwimu za hali ya hewa husaidia makampuni ya bima na vyombo vya sheria katika kuhakiki madai na hivyo kulipa bima mbalimbali ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya hutumia taarifa/takwimu za hali ya hewa katika kukabiliana na milipuko ya magonjwa, kwa mfano, kukiwa na mvua nyingi mbu huongezeka na kusababisha ugonjwa wa malaria. Hii husaidia Serikali huchukua hatua madhubuti za kupambana na magonjwa kama hayo. Hali kadhalika, Ofisi ya Makamu wa Rais, Kitengo cha Mazingira, hutumia takwimu/taarifa za hali ya hewa katika kufanya uchunguzi juu ya uchafuzi wa hewa *(Air Pollution)* na uchunguzi wa mabadiliko ya hali ya hewa *(Climate Change).*

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kawaida Mamlaka ya Hali ya Hewa hutumia vigezo vilivyowekwa na Shirika la Hali ya Hewa Duniani *(World Meteorological Organization)* katika kutekeleza majukumu yake. Hivyo, takwimu zote zinazotumiwa na kutolewa na Mamlaka ya Hali ya Hewa zina viwango vya Kimataifa.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Kwa vile msemo tuliouzowea kwamba mvua za kwanza ni za kupandia na kwa kuwa misimu yetu imebadilika na hali ya mvua imebadilika na mvua sasa hivi zimeachwa kuwa za kupandia. Je, Serikali inasema nini kuhusu kauli hiyo kwa wakulima wetu ambao mara nyingi wameathirika na usafiri ambao hautabiriki na ambao si wa hakika na watu wamepanda na mazao yameharibika?

La pili, kwa vile huko nyuma tulikuwa na vituo vingi vya kupimia na kupata takwimu za hali ya hewa kama vile *Barometer* na vituo vya kupimia hali ya mvua. Vituo hivyo vingi vimekufa na vimeachwa na sasa hivi sehemu nyingi hatuna tena vituo. Je, Serikali inatoa kauli gani kwamba labda hata hali na taarifa tulizonazo zinakosa uhakika kutokana na vituo hivyo kutokuhudumia vizuri?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, swali la kwanza napenda nimfahamishe Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa kwamba, ingawa mabadiliko ya hali ya hewa tunayaona hivi sasa takwimu na taarifa za hali ya hewa zinatolewa kila mara ili wananchi waendane na wakati katika kukabiliana na mambo yao mbalimbali, kwa mfano, wakati wa kulima na mambo mengine. Kwa hivyo, tunaendana na wakati kutokana na hali halisi ilivyo ya mabadiliko ya hali ya hewa.

Pili, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kuwa, kufungwa kwa baadhi ya vituo vya hali ya hewa hakufanyi kwamba shughuli za hali ya hewa zisiwe na ubora au zisitoke. Hivi sasa tunavyo vituo 25 na vyote vinafanya kazi hiyo na tunamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, shughuli hizo zitaendelea ipasavyo.

**MHE. BENEDICTO M. MUTUNGIREHI:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Kwa kuwa Mamlaka ya Hali ya Hewa mara nyingi hutoa utabiri wake kuhusu hali ya hewa itakavyokuwa kama ilivyofanya wakati wa *El-Nino*. Kufuatana na njaa iliyotupata mwaka uliopita wa 2003 na Serikali ilijua kwamba kutakuwa na njaa haikuchukua hatua. Je, kwa tatizo hilo la Serikali kutokuchukua hatua inaweza ikakubali lawama kwamba ilifanya uzembe kwa kutokuwahudumia wananchi na kuwahakikishia kuwaambia kwamba walime mapema?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, ni kweli taarifa tunatoa mapema kama tulivyotoa wakati wa *El-Nino* na tuliwapa taarifa wananchi mapema kwamba, mvua zitakuwa nyingi, walioko mabondeni wahame ili wasifikwe na majanga. Lakini kama ilivyo kawaida, bado wananchi walibaki na wengine tuliwaokota katika mito. Ni kawaida yetu sisi binadamu. Tulitoa taarifa kwamba, mvua safari hii hazitakuwa za kutosha na tukatoa taarifa kwamba, wananchi wapande kilimo ambacho kinastahimili ukame. *(Makofi)*

Kwa hiyo, sidhani kama Serikali itaweza kumpa kila mtu mkononi muhogo ambao unastahimili ukame. Lakini tulikuwa na wajibu wa kuona kama mvua safari hii zitapungua, mimi na familia yangu najiandaa vipi ili nisiishi katika njaa. Napenda nisisitize kwamba, taarifa hizi tunazozitoa, Serikali inazipeleka mpaka kwa Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa yote Tanzania Bara na Visiwani. Naamini taarifa hizi zitatumika ipasavyo. *(Makoni)*

Na. 170

**Hospitali ya Rufaa - Mnazi Mmoja**

**MHE. PARMUKH SINGH HOOGAN** aliuliza:-

Kwa kuwa Hospitali ya Mnazi Mmoja kule Zanzibar ni ya rufaa na kwa kuwa hivi sasa yapo matukio mengi ya ajali za barabarani na yanazidi kuongezeka kwa kiasi kikubwa na kwamba jambo hilo limekuwa kero kubwa kwa wananchi wa Zanzibar:-

(a) Je, Serikali iko tayari kushirikiana na Wizara ya Afya Zanzibar na ina mpango gani wa kuweka mashine ya *CT Scanner?*

(b) Je, kuna mpango wowote ule wa kuweka wataalam wa maabara ya kisasa kule Zanzibar?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ya Afya ni moja ya Wizara ambazo haziingii katika kundi la Wizara za Muungano. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Muungano wa Tanzania zina Wizara za Afya zinazojitegemea. Wizara ya Afya Zanzibar inaratibu shughuli zote za Sekta ya Afya Tanzania Visiwani na Wizara ya Afya ya Jamhuri ya Muungano inaratibu shughuli hizi kwa Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kuwa Tanzania ni nchi moja, kumekuwa na ushirikiano mkubwa wa kupeana mbinu za mikakati ya kupambana na adui maradhi kati ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii Zanzibar na Wizara ya Afya Tanzania Bara.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Muungano iko tayari kushirikiana na Wizara ya Afya Zanzibar na kwa kweli Wizara hizi mbili zimeunda Kamati ya Ushirikiano. Pia ipo mikutano ya mara kwa mara ya mashirikiano ambayo Wenyekiti wake ni Makatibu Wakuu wa Wizara hizi mbili.

Mheshimiwa Spika, Serikali ya Muungano itaendelea kushauriana na Serikali ya Mapinduzi na kuona uwezekano wa Serikali ya Mapinduzi kuweka mashine ya *CT Scanner* kwenye Hospitali ya Mnazi Mmoja Zanzibar.

Aidha, mazungumzo bado yanaendelea kati ya Wizara ya Afya Tanzania Bara na Tanzania Visiwani, juu ya namna tutakavyoweza kuazimana wataalam wa fani mbalimbali za Sekta ya Afya wakiwemo wataalamu wa maabara.

**MHE. DR. MWITA HAJI MWITA:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa shughuli hizi za *CT Scanner* ambazo zimetajwa katika swali (a) zinahusiana sana na masuala ya *X-Ray* na hivi karibuni Tanzania Bara wamepata msaada wa *X-Ray* katika hospitali mbalimbali za Wilaya.

Je, katika kudumisha huu uhusiano ambao Mheshimiwa Naibu Waziri ameutaja hapa, kuna utaratibu gani au mpango gani wa mashirikiano yao kuipatia *X-Ray* Zanzibar kama walivyofanya Tanzania Bara? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kulikuwa na Mradi wa *ORET* ambao umezipatia karibu Wilaya zote, Mikoa yote na Hospitali zote za Rufaa mashine za *X-Ray*. Mradi huu ulipangwa kwa madhumuni ya kuzipatia hospitali hizo tu kwa idadi na mradi huu ulichangiwa na Serikali kwa asilimia 40 na asilimia 60 ilitolewa na Waholanzi.

Mheshimiwa Spika, ninachoweza kusema ni kwamba, tutakuwa tayari kuzungumza na wafadhili hawa ili waangalie uwezekano wa kuisaidia Zanzibar. *(Makofi)*

**MHE. MOHAMED ABDULLY ALLY:** Ahsante Mheshimiwa Spika. Ni kweli kwamba Wizara ya Afya siyo ya Muungano, lakini ni kweli kabisa Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania, kupitia Wizara ya Afya, ilikuwa na desturi ya

kupeleka Zanzibar wataalam kwa wiki tatu kukaa kule Zanzibar kwa ajili ya kusaidia watu kujua matatizo yao badala ya kuwaleta Tanzania Bara.

Je, Mheshimiwa Waziri hivi sasa atakubali kurejesha mpango ule wa wataalam *(Specialists)* waliopo Bara waende Zanzibar kusaidia Serikali ya Mapinduzi Zanzibar? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, nimesema katika jibu langu la msingi kwamba, hivi sasa tuna Kamati ya Ushirikiano baina ya Wizara hizi mbili na Wenyeviti ni Makatibu Wakuu. Bila shaka suala hili likipelekwa katika Kamati hiyo, hakuna wasiwasi kwamba wanaweza wakapatikana madaktari ili kuweza kusaidia kule Zanzibar.

Na. 171

**Madhara ya Dawa ya *SP***

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA** aliluliza:-

Kwa kuwa Serikali ina jukumu kubwa la kuangalia raia wake katika masuala ya afya zao na imeunga mkono matumizi ya dawa ya *SP*:-

(a) Je, Serikali ipo tayari kuwalipa fidia wale wote walioathirika kutokana na matumizi ya dawa hiyo?

(b) Je, tangu dawa hiyo mpya ianze kutumika Serikali imeorodhesha wagonjwa wangapi walioathirika kwa matumizi ya dawa hiyo?

(c) Kati ya hao, je, ni wangapi walioathirika vibaya?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Afya, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Ninakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, Serikali ina jukumu kubwa la kuangalia raia wake katika masuala ya Afya zao na kwamba Serikali imeamua kutumia dawa za kundi la *SP* kama tiba sahihi ya malaria. Hata hivyo, Serikali haina mpango kwa sasa kulipa fidia kwa watu waliothibitika kuathirika kutokana na matumizi ya dawa ya *SP*.

Mheshimiwa Spika, *SP* kama dawa nyingine zote duniani zinaweza kuleta madhara *(Side Effects)* kwa baadhi ya watumiaji. Hii *(Side Effects)* ni tabia ya dawa takriban zote zitumiwazo na binadamu.

(b) Mheshimiwa Spika, kuna utaratibu wa kupata taarifa za madhara ya dawa mbalimbali ikiwemo *SP* kwa kutumia mtindo ujulikanao *(Yellow Card)* kutoka hospitali na vituo vyote vya kutolea huduma za tiba. Mpaka sasa tumepata taarifa ya watu 48 walioathiriwa na *SP*. Inawezekana idadi ikawa kubwa zaidi ya hii kwani huenda wagonjwa wengine wameathirika bila Wizara kupata taarifa. Taarifa hii ni kwa kipindi cha toka tarehe 1 Agosti, 2001.

(c) Mheshimiwa Spika, taarifa tulizoletewa hazikuchanganua viwango vya kuathirika.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Ahsante sana Mheshimiwa Spika, kwa kuniona. Nina swali moja tu fupi la nyongeza. Nilitaka kumwuliza Mheshimiwa Naibu Waziri, Serikali inakuwa na utaratibu gani au ina mkataba gani na makampuni yanayotengeneza dawa au makampuni yanayoingiza dawa ambazo baada ya kutumika zinakuwa na *side effects* na hasa kuhusiana na suala la fidia?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kila kampuni inayotengeneza dawa inaweka karatasi ndani ya *box* lile la dawa kuonyesha *side effects* ambazo dawa ile inaweza kusababisha. *Side effects* hizo zinawekwa kwa sababu kama nilivyosema awali, karibu dawa zote zina *side effect.* Kwa hiyo, unaelezwa bayana kwamba, endapo utatumia dawa hii ya *SP* na endapo wewe ni mtu ambaye ni *sensitive* kwa *sulphur* basi utapata matatizo ambayo yanajulikana kwa lugha ya kitaalam kama *Steven Johnson Syndrom*. Ndiyo maana tukaweka safu ya pili kwa wale ambao dawa hii inawadhuru basi watumie *Amodierquine* si rahisi kuweka mkataba wa fidia kwa sababu makampuni ya dawa yatakuwa yanafidia kila siku kwa kuwa dawa zote zina *side effect.*

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, kwa kuwa mwananchi anapokwenda hospitali hajui kwamba yuko *alleged to sulphur,* yaani akipigwa *sulphur* ataumia. Sasa Serikali itawatambuaje wale ambao ni *alleged* kwa *sulphur* ili wasiumie na ni kwa nini Serikali isiitoe dawa hii ambayo huwezi ukapiga hata sindano kwa wananchi? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, suala hili tumelijibu mara nyingi kidogo. Lakini naomba nitumie muda wa nyongeza kidogo nilitolee ufafanuzi wa kina. Serikali imebadilisha matumizi ya *Chloroquine* kwenda kwenye *SP* kwa sababu maalum. Kuna vigezo vitatu ambavyo vinatumika katika kubadilisha kutoka dawa moja kwenda dawa nyingine. Vigezo hivyo ni kwanza, uwezo wa dawa kutibu. Pili, ni kiwango cha *side effects* ambazo dawa inaweza kuwa nayo na tatu ni gharama ya dawa husika. Sasa kutoka *Chloroquine* kwenda kwenye *SP* tumeamua kwa sababu uwezo wa *Chloroquine* kutibu umeshathibitika kwamba ni mdogo sana. Katika *SP* ni kweli kwamba inayo *side effect* kwa baadhi ya watu. Lakini ukiangalia kigezo cha tatu cha gharama kutoka *Chloroquine* ambayo ni Sh.100 kwa dozi. *SP* ni Sh.700 mpaka 1,000 kwa dozi. Ukitoka kwenye *SP* sasa kwenda dawa nyingine ambazo zipo, kwa mfano, zile dawa ambazo zina *container* ni Sh.6,000 kutoka 700 mpaka Sh.6,000.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Henry Shekiffu, anaposema tuitoe mimi nataka nijiulize suala moja kwamba tukiitoa tutaweka dawa gani. Kwa sababu unapoweka dawa nyingine yoyote unaondoa uwezo wa Serikali na watu binafsi kuweza kununua dawa hiyo, ndiyo maana bado *SP* ipo lakini tunakuwa waangalifu katika matumizi yake. Sasa nikija katika kutambua wagonjwa gani ni *sensitive* kwa *SP,* ndiyo sasa hivi Wizara imetumia fedha nyingi sana kutoa mafunzo kwa watu ambao wanaandika dawa hizi kwa wagonjwa. Tunatakiwa tuwaulize kwamba, je, wamewahi kutumia dawa yoyote yenye *sulphur* na si *SP* peke yake. Ugonjwa huu unaweza ukatokea kwa *SP,* unaweza ukatokea kwa *Sulphur Dimidine,* unaweza kutokea kwa *Thelazia* ambazo ni dawa za *TB.*

Kwa hiyo, ni muhimu watu waelewe kwamba *sulphur* ndiyo yenye kuleta tatizo hili na haiko kwenye *SP* peke yake. Sasa nataka niwahakikishie kwamba, ndiyo maana sasa hivi mgonjwa ukienda kwa Daktari unaulizwa, unataka kutumia dawa gani? Jambo hili si kawaida kwa Madktari kukuuliza wewe mgonjwa unataka kutumia dawa gani, kwa sababu ya tatizo hili. Kama una wasiwasi tafadhali tumia *Amodierquine.* *(Makofi)*

Na. 172

**Nyumba za Askari Polisi - Singida**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa nyumba za Askari Polisi Mkoani Singida ni chache na ndogo sana na kwa kuwa udogo wa nyumba hizo, yaani chumba na sebule haitoshi kwa askari mwenye familia yenye watoto wa jinsi zote na kwa kuwa askari hao wanatakiwa kuwalea/kuwafundisha watoto wao maadili mema:-

(a) Je, Serikali inafahamu kwamba kwa askari kukaa uraiani kunafanya ulinzi wao kuwa mdogo kulingana na kiwango cha kazi zao?

(b) Je, Serikali itawajengea lini nyumba zenye kukidhi haja na zenye kutoa nafasi nzuri ya kujenga maadili mazuri kwa watoto na familia zao?

**NABU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Diana Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali kwa sasa haina uthibitisho kwamba kwa Askari Polisi kuishi uraiani kunahatarisha maisha yao. Lakini imebainika kuwa raia wema hujisikia salama zaidi wanapoishi na Askari kwa kuelewa kuwa wapo jirani na walinzi wa mali na maisha yao. Serikali inaposisitiza suala la kuweka Askari makambini, sio kwa ajili ya usalama wao binafsi bali ni kwa ajili ya kujenga nidhamu ya Kiaskari na maadili ya Kijeshi.

(b) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, nyumba wanazoishi Askari Polisi kwa sasa ni chache, ndogo sana na hazina hadhi kwa ajili ya kuishi familia yenye watoto wa jinsia tofauti. Tatizo hili linawakabili Askari katika Mikoa yote nchini pamoja na Mkoa wa Singida. Kwa kutambua kero hii, Serikali imekwishaanza kuchukua hatua mbalimbali ikiwa ni pamoja na zifuatazo:-

(i) Serikali imenunua na inaendelea kununua nyumba za mashirika ya umma yaliyobinafsishwa kama ilivyofanya kwa nyumba za *NBC* huko Mtoni Kijichi Dar es Salaam, Moshi, Mwanza na kwingineko;

(ii) Serikali inaendelea na ujenzi wa nyumba mpya za Askari kama ambavyo tayari imeshafanya kule Ukonga *(FFU),* Kiteto, Chakechake (Pemba), Mwanga, Hai na kwingineko na kazi ya ujenzi wa nyumba za Askari inaendelea;

(iii) Inawashirikisha wananchi kujenga nyumba za Askari kwa njia ya kujitolea; na

(iv) Tunashirikisha mashirika na makampuni yenye fedha za kujenga nyumba kama *PPF, NSSF,* katika suala zima la ujenzi wa nyumba za Askari.

Serikali inatambua kuwa mahitaji ya nyumba za Askari ni makubwa mno na uwezo wa Serikali kuzijenga zote kwa pamoja ni mdogo. Hata hivyo, Serikali itaendelea kujenga nyumba za Askari kila mwaka kwa kadri ya uwezo wa Bajeti ili hatimaye Askari wetu wote wawe na nyumba zenye hadhi.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kumwuliza maswali madogo mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(a) Kwa kuwa nina taarifa za kuaminika kabisa kwamba Askari anapokaa uraiani anashindwa kumkamata mhalifu kwa kuhofia usalama wake kwani anaishi nao, Mheshimiwa Naibu Waziri anasemaje?

(b) Kwa kuwa nyumba za Maaskari zinaitwa makambi, je, ni lini basi nyumba hizi zitakuwa za kudumu na ziitwe makazi badala ya makambi maana makambi ni nyumba za kupita?

**NABU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika swali la msingi kwamba, tatizo la Askari kukaa uraiani tunaposema tunataka tuwaondoe huko kusema kweli sio kwa kuhofia usalama wao kwa sababu katika maeneo mbalimbali wanaishi vizuri tu. Tatizo linakuja kwamba, wako kule tunapowataka usiku huwezi kuwapata, unapotaka wakae katika hali ya nidhamu ya Kijeshi kwa kuwasimamia wakiwepo uraiani huwezi kuwasimamia, hii ndio dhana kubwa kwa kweli ni kuingiza nidhamu na maadili ya Kijeshi kuliko usalama wao wengi wanaishi vizuri tu huko uraiani lakini nidhamu ya Kijeshi ndio inayotafutwa hapa.

Mheshimiwa Spika, pili, kuhusu jina la makambi kuwa makazi. Sasa lugha ya Kijeshi mahali ambapo kuna nyumba hata kama ni za kudumu za ghorofa lugha ya Kijeshi ni *barracks* kwa Kiingereza, sasa tasfiri yake ya Kiswahili ni makambi. Sasa kama ipo tasfiri nzuri zaidi tuko tayari kuipa ili tutoke kwenye kambi lakini kwa sasa hivi makambi ni sehemu rasmi ambapo ziko nyumba za Wanajeshi wanaishi kwa pamoja.

Na. 173

**Askari Kulipwa Gharama ya Usafiri**

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD (k.n.y. MHE. ISSA MOHAMED SALIM)** aliuliza:-

Kwa kuwa Askari Polisi wanaoishi nje ya sehemu zao za kazi wanalipwa gharama za usafiri kupitia mishahara yao tofauti na Askari wa Pemba ambao hawalipwi kabisa:-

(a) Je, ni sababu gani zinazofanya Askari Polisi wa Pemba wasilipwe gharama za usafiri kupitia mishahara yao?

(b) Je, kama hakuna sababu za msingi, kwa nini wasianze kulipwa gharama hizo za usafiri katika mishahara yao ya mwezi huu?

**NABU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Issa Mohamed Salim, Mbunge wa Mkoani, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Utumishi katika Jeshi la Polisi za mwaka 1995, Kifungu Na.17(f), Askari Polisi anastahili kulipwa posho ya usafiri ili kumrahisishia gharama za usafiri wa kwenda na kurudi toka kazini. Posho hizo zilikuwa zinalipwa na Serikali ya Muungano kwa Askari wote wa Tanzania Bara na Tanzania Visiwani hadi mwaka 1996. Baada ya hapo, mnamo mwaka 1996/1997 miundo ya mishahara ya watumishi wote wa Serikali ilifanyiwa marekebisho. Kutokana na marekebisho hayo, posho ya usafiri kwa Askari, ilijumuishwa kwenye vianzia vya mishahara yao.

Kwa hiyo, kwa kuwa vianzia vya mishahara ya Askari Polisi wote vinalingana kufuatana na ngazi na vyeo vyao, ni dhahiri kwamba, Askari wa Pemba nao wanalipwa mishahara iliyojumuishwa na posho ya usafiri sawasawa na wenzao wa Unguja na Tanzania Bara.

**MHE. KHAMIS AWESU ABOUD:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize swali moja la nyongeza. Kutokana na maelezo yake kuwa pesa za usafiri zilikuwa zikilipwa kwa Tanzania nzima lakini amesema kuwa kutokana na mshahara sasa posho zile zimeingizwa kwenye

mishahara lakini kwa ninavyojua mimi mishahara yao ni midogo sasa hatuoni kuwa kuna sababu ya kuwarudishia zile pesa zao za usafiri ili mshahara wao uendelee kuongezeka zaidi?

**NABU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, mishahara ya Polisi kama ilivyo tu mishahara ya watumishi wengine wengi wa Serikali ni midogo ikilinganishwa na hali ya maisha, lakini sera ya kuondoa posho ile ya usafiri kwenye mshahara ili walipwe kama posho mbali na mshahara ni suala ambalo linashughulikiwa Kitaifa na Wizara ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Hili linatazamwa kwa ujumla wake kwa watumishi wote wa Serikali na hapo itakapoamuliwa hivyo basi na Polisi nao watanufaika lakini kwa sasa tunafuata mfumo mmoja wa Serikali nzima kwamba posho hizi za usafiri zimeingizwa ndani ya mishahara ya Askari.

Na. 174

**Barabara ya Tanga - Horohoro**

**MHE. MBARUK KASSIM MWANDORO** aliuliza:-

Kwa kuwa barabara kuu hasa zinazounganisha Tanzania na nchi jirani ni miundombinu muhimu sana kwa maendeleo ya uchumi na ustawi wa nchi yetu; na kwa kuwa Serikali imekamilisha ujenzi wa madaraja saba katika barabara kuu ya Tanga - Horohoro; na kwa kuwa barabara hiyo ilipewa kipaumbele *A1* katika barabara ambazo zimo katika mpango wa ujenzi kwa ushirikiano kati ya Serikali ya Tanzania na Jumuiya ya Afrika Mashariki:-

(a) Je, Serikali itapokea pongezi za wananchi wa Jimbo la Mkinga ambako sehemu kubwa ya barabara hiyo inapita kwa hatua hiyo kubwa ya maendeleo?

(b) Je, Serikali inaweza kulifahamisha Bunge kwamba ni lini ujenzi wa madaraja yaliyosalia na uwekaji lami kwenye barabara hiyo muhimu utafanyika?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali inakubali kupokea pongezi za Wananchi wa Jimbo la Mkinga kwa hatua kubwa ya kukamilisha ujenzi wa madaraja saba kwenye barabara hii ambapo imekuwa chachu ya maendeleo ya Jimbo lote la Mkinga na Taifa kwa ujumla.

(b) Mheshimiwa Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, ujenzi wa madaraja yaliyosalia pamoja na ujenzi kwa kiwango cha lami barabara yote

yenye urefu wa kilometa 64 utafanywa kwa mkopo kutoka Benki ya Dunia kuanzia mwaka wa fedha wa 2004/2005, kwa kuanza na kazi ya usanifu na uandaaji wa nyaraka za zabuni za ujenzi. Zabuni za kazi hii ilitangazwa rasmi mwezi Juni, 2004.

Na. 175

**Barabara ya Nyamwage - Somanga**

**MHE. BAKARI M. MBONDE** aliuliza:-

Kwa kuwa sehemu ya barabara ya kati ya Nyamwage Wilayani Rufiji na Somanga - Wilayani Kilwa ndiyo sehemu pekee katika barabara Kuu ya Dar es Salaam - Lindi - Mtwara ambayo haijaanza kujengwa:-

(a) Je, ni hatua zipi zilizofikiwa na Serikali hadi sasa katika kuhakikisha kuwa sehemu hiyo ya barabara inajengwa katika kiwango cha lami?

(b) Je, ni sababu zipi za msingi zilizosababisha sehemu hiyo ya barabara kutojengwa mapema?

Mheshimiwa Spika, naomba sasa swali langu Na.175 lijibiwe ili hata watoto wetu Wamakonde na Wamakua waweze kusikia.

**SPIKA:** Ili nini, hebu rudia hatukusikia. *(Kicheko)*

**MHE. BAKARI M. MBONDE:** Ili hata watoto wetu Wamakonde na Wamakua waweze kusikia.

**SPIKA:** Ahaa! *(Kicheko)*

Haya jibu Mheshimiwa Naibu Waziri ili wasikie.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Bakari M. Mbonde, Mbunge wa Rufiji, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, hatua ambazo Serikali imefikia kuhakikisha kuwa sehemu hii ya barabara inajengwa kwa kiwango cha lami ni pamoja na kupata mkopo mwaka 2000 wenye thamani ya Dola za Kimarekani 20.5 milioni kutoka Mfuko wa Kuwait na dola 7.0 kutoka *OPEC* kwa makubaliano kuwa Serikali ya Tanzania itachangia dola 4.0 milioni kwa mradi wa barabara ya kutoka Dar es Salaam hadi Somanga. Kati ya fedha hizo nilizozitaja, Mradi wa Nyamwage - Somanga umetengewa jumla ya dola 12.5 milioni. Hatua ya utekelezaji wa mradi iliyofikiwa hadi mwezi Juni, 2004 ni kupokea na kuchambua zabuni za kuipata kampuni itakayofanya usanifu wa kina na usimamiaji ujenzi. Zabuni husika zimechambuliwa na kupitishwa na Bodi ya Zabuni

ya Taifa mwezi Mei, 2004 na ripoti yake kutumwa Mfuko wa Kuwait mwezi huo wa Mei, 2004.

Tunategemea kupata kibali kutoka Kuwait mapema mwezi huu wa Julai, 2004 na kusaini Mkataba mwezi huu huu wa Julai, 2004. Kazi ya usanifu na uandaaji nyaraka za zabuni inatarajiwa kuchukua miezi minane kuanzia Septemba, 2004 hadi Aprili, 2005 na baada ya hapo kuitisha zabuni za ujenzi. Ni matarajio yetu kuwa kazi za ujenzi zitaanza mapema mwaka wa fedha wa 2005/2006.

(b) Mheshimiwa Spika, sababu za msingi zilizosababisha sehemu hiyo ya barabara kutojengwa mapema ni kutokana na Mfuko wa Kuwait kukiuka taratibu za mkopo mara baada ya mkopo kusainiwa mwezi Juni, 2000 na Serikali ya Tanzania kutuma nyaraka za kuyapata Makampuni ya Usanifu, Usimamizi na Ujenzi mwezi Agosti, 2000.

Pamoja na barua nyingi za kukumbusha Mfuko wa Kuwait, ilichukua zaidi ya mwaka mmoja bila ya Mfuko kujibu barua hizo hadi Serikali ilipoamua kutuma Ujumbe Maalum ulioongozwa na Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Naibu Waziri wa Ujenzi, mwezi Septemba, 2001. *(Makofi)*

Hata baada ya makubaliano yaliyofikiwa kati ya Ujumbe wa Serikali na Mfuko wa Kuwait, ilichukua muda mrefu tena hadi kukubaliana orodha ya makampuni yatakayoshiriki kwenye usanifu na usimamizi wa mradi huu kutokana na Serikali kuwa na msimamo kuwa haitakubali makampuni yenye sifa isiyoridhisha ya utendaji kazi hapa Tanzania kuruhusiwa kushirikishwa kwenye Mradi huu. Hatimaye mwezi Desemba, 2003, Mfuko wa Kuwait ulikubaliana na msimamo wa Serikali na hatua nyingine kufuata hadi kufikia maendeleo ya Mradi kama ilivyoelezwa kwenye sehemu (a).

**MHE. BAKARI M. MBONDE:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri na kwa kazi nzuri ambayo yeye binafsi ameifanya kwa niaba ya Serikali, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

(a) Mwaka huu wa fedha wa 2004/2005 barabara hii imetengewa Shilingi bilioni 2.5, je, hii ni kwa usanifu tu kama ni usanifu tu kwa nini usanifu na ujenzi usiende pamoja ili kuharakisha ujenzi wa barabara hii?

(b) Barabara ya Nyamwage - Utete ni kiungo muhimu kati ya Makao Makuu ya Wilaya pale Utete na hii barabara ya Kibiti - Lindi mwaka 2002 nilimwandikia Waziri na bahati nzuri wakatupa fedha kwa ajili ya barabara hiyo, je, mwaka huu ombi letu limefikia wapi?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, pesa zilizopangwa mwaka huu ni kwa ajili ya usanifu tu. Usanifu na ujenzi vinaweza kufuatana kama mkataba na mtoaji mkopo anakubaliana na hilo. Tunafanya tu sisi kwa pesa zetu wenyewe lakini kwenye masuala ya mkopo kuna masharti yake. Kwa hiyo, hii ni pesa ya usanifu.

Mheshimiwa Spika, je, Utete - Nyamwage mwaka huu imefikia wapi? Namwomba Mheshimiwa Bakari Mbonde, akitoka hapa tuonane nimwonyeshe kwenye Kitabu cha Bajeti. *(Kicheko)*

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwanza, nimshukuru mjukuu wetu kwa kuuliza swali hili. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza ifuatavyo:-

Kwa kuwa eneo hili toka Nyamwage - Somanga lina kilomita 60 na mara nyingi huwa ni baya na linapita katika sehemu ya msitu na magari kadhaa yameshawahi kuvamiwa na wahalifu katika maeneo haya. Je, Serikali itatuhakikishia wakati tunasubiri Mkandarasi eneo hili linapigwa *grader* mara kwa mara ili usafiri uwe rahisi badala ya mashimo, mashimo yaliyopo?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maria Watondoha, lililoulizwa na mjukuu wake kama ifuatavyo:- *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, barabara hii ya Nyamwage - Somanga ni kweli inapita katika msitu na ni sehemu mbaya kama alivyozungumza Mheshimiwa Mbunge, lakini kwa kawaida kila mwaka Tunajitahidi kuifanyia matengenezo na huu ni utaratibu tu wa Wizazra ya Ujenzi kujaribu kuhakikisha kwamba, barabara zote zinapitika na hata kama sio za changarawe, hata ikiwa ya udongo tunahakikisha kwamba, inapitika. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi tutapiga *grader* na itapitika.

Na. 176

**Ruzuku katika Usafirishaji wa Mbolea**

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI** aliuliza:-

Kwa kuwa katika bajeti ya mwaka 2003/2004, Serikali ilikubali kuweka ruzuku ya usafirishaji wa mbolea kwa baadhi ya Mikoa nchini kwa ajili ya kuhakikisha kuwa bei ya mbolea haiongezeki na hivyo kuondokana na tatizo la uhaba wa chakula nchini:-

(a) Je, tathmini inaonyesha kufanikiwa kwa kiasi gani katika zoezi hilo?

(b) Je, Serikali inaonaje kama utaratibu huo ungetumika kwa nchi nzima likiwemo Jimbo la Siha ili kuleta ufanisi zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aggrey Deasile Joshua Mwanri, Mbunge wa Siha, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Katika msimu wa kilimo wa 2003/2004, Serikali ilitenga jumla ya shilingi bilioni mbili kwa ajili ya kufidia sehemu ya gharama za usafirishaji wa mbolea kwenda Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Hadi mwezi Mei, 2004, jumla ya shilingi bilioni 1.27 zilikuwa zimetumika kufidia sehemu ya gharama za usafirishaji wa tani 38,935 za mbolea zilizopelekwa kwenye Mikoa hiyo. Tathmini iliyofanywa inaonyesha mafanikio yafuatayo:-

(i) Jumla ya tani 38,935 za mbolea zilipelekwa Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini chini ya utaratibu wa fidia. Mkoa wa Mbeya ulipata tani 14,016, Mkoa wa Iringa tani 14,955, Mkoa wa Ruvuma tani 8,771 na Mkoa wa Rukwa tani 1,193;

(ii) Katika vituo vikuu vya kupokelewa mbolea, bei ya mfuko mmoja wa mbolea wenye uzito wa kilo 50 ilishuka na kuwa kati ya shilingi 10,000 hadi 14,000 ikilinganishwa na wastani wa shilingi 16,000 hadi 25,000 kabla ya utaratibu wa fidia;

(iii) Katika msimu wa 2003/2004, matumizi ya mbolea katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini yaliongezeka kwa tani 7,500 ikilinganishwa na matumizi katika msimu wa 2002/2003; na

(iv) Tija katika uzalishaji wa mahindi katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini imeongezeka kutoka wastani wa tani moja kwa hekta kabla ya utaratibu wa fidia, hadi wastani wa tani 2.5 kwa hekta katika msimu wa 2003/2004.

Kwa kuwa msimu wa 2003/2004 ulikuwa wa kwanza wa utekelezaji wa utaratibu wa fidia, yalikuwepo matatizo mbalimbali yaliyojitokeza. Kwa mfano, utaratibu huo uliongeza mahitaji ya mbolea wakati hapakuwepo na utaratibu wa kuagiza mbolea kukidhi ongezeko hilo la mahitaji. Tatizo lingine lilitokana na udhaifu wa baadhi ya Kamati za Wilaya wa kutotekeleza majukumu ya uratibu na usimamizi kama zilivyoagizwa.

(b) Kutokana na mafanikio yaliyopatikana katika Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, Serikali imepanga kupanua utaratibu wa fidia ya sehemu ya gharama za usafirishaji wa mbolea nchini kote. Ili kutekeleza mpango huo, katika mwaka wa 2004/2005, Serikali imetenga shilingi bilioni 7.24 kwa ajili hiyo.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Namshukuru Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo ameyatoa.

(a) Kwa kuwa ameonyesha kwamba utaratibu huu umekuwa na matatizo ya aina mbalimbali ikiwemo pia kupanda kwa bei, je, anakubaliana nami kwamba kuna haja Serikali kupeleka mbolea hii mpaka mikoani na ndipo tuanze ku-*determine* bei yake kule?

(b) Je, kama Serikali ilifanya kama ilivyofanya, ni nini tena kilichokuja kusababisha bei ya mbolea ikapanda zaidi kuliko hata ilivyokuwa mwanzo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, utaratibu ulikuwa na matatizo kwa sababu kwanza ilikuwa ni mara ya kwanza tumefanya shughuli hii baada ya muda mrefu, kwa hiyo, uzoefu haukuwepo kama tungefanya toka siku nyingi hadi leo. Hilo ni tatizo mojawapo na hasa zile Kamati za Wilaya, upande wa Mkoa haukuwa na tatizo sana kwa sababu mbolea ilifika katika maeneo kamaa matarajio ya Serikali yalivyokuwepo. Lakini kuitoa pale Mikoani kupelekwa mpaka vijijini, Kamati za Wilaya hazikuwa na uzoefu tulioutegemea, ndio maana yalitokea matatizo haya.

Mheshimiwa Spika, bei ilikuwa kama tulivyotarajia kati ya Sh.10,000 na Sh.14,000 mpaka maeneo yale ya Mikoani. Sasa kupanda kwa bei kulitokea kwa sababu nyingi moja ni ule uzoefu haukuwepo, pili, vile vile kwa sababu mbolea ziliteremka kidogo bei kwa hiyo mahitaji yakapanuka, kupanuka huko kukafanya kuwa kile kidogo kilichokuwepo kisitoshe. Baada ya kutokea matatizo katika Soko la Dunia, mbolea haikuweza kuletwa kufuta tatizo hili kwa wakati.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kuniruhusu niulize swali moja la nyongeza pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa bei ya mbolea za *Urea, CAN* na *Sulphate of Ammonia* zilikuwa Sh.5,000 - 6,000 kwa mfuko wa kilogramu 50,000 *FOB* kule Dubai na kwa kuwa mbolea hiyo inauzwa kwa usawa wa Sh.10,000 - 12,000 katika nchi jirani za Malawi na Zambia, je, Serikali inajua ni kwa sababu gani mbolea hiyo inauzwa kwa Sh.25,000 katika Bandari ya Dar es Salaam? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, bei ilikuwa Sh. 25,000 Bandarini lakini kwa mradi huu, ningependa tena nirudie kumthibitishia Mheshimiwa Profesa Maghembe kuwa, bei yetu ilikuwa kati ya Sh.10,000 - 14,000 kwenye maeneo hayo. Sasa ilipofika kule kwenda vijijini ndiko kulikuwa na matatizo mojawapo kama nilivyosema uzoefu, lingine ubaya wa mawasiliano maana ilikuwa wakati wa masika na sehemu nyingi katika sehemu zile zina mvua nyingi sana kwa hiyo yakatokea matatizo ya kukwama na kufika kwa wakati.

Halafu mradi ulikuwa katika Mikoa minne Mikoa mingine haikuhusishwa sasa hatuelewi kama mbolea yote ilielekezwa huko kama tulivyotarajiwa kama mwingine hakutoka sehemu nyingine akaenda kuzichukua zile kulikuwa na sababu nyingi. Lakini tunapenda kutoa uhakika kuwa mwaka huu Serikali imetenga shilingi bilioni 7 kwa shughuli hiyo.

Pili, kuna miradi mitatu mingine itakayoshughulikia mbolea, uko ule *PADEP* utakaohusu Mikoa ya Kaskazini halafu uko Mradi wa *DADPs,* utakaohusu Mikoa ya Kanda ya Magharibi na *FINIDA.* Hivyo, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, mwaka huu kutakuwa na mafuriko ya mbolea. Tunaomba msaada wenu katika kusimamia kwenye Kamati ili kusudi yasije kurudia matatizo yaliyotokea kama kila kitu kitakwenda kilivyotarajiwa. *(Kicheko/Makofi)*

Na. 177

**Ruzuku katika Mbolea**

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI** aliuliza:-

Kwa kuwa katika bajeti ya mwaka 2003/2004, Serikali ilitangaza uamuzi wake wa kutoa ruzuku kwenye mbolea kwa Mikoa minne ya Nyanda za Juu Kusini, yaani Rukwa, Mbeya, Iringa na Ruvuma, uamuzi uliopokelewa kwa furaha, lakini baada ya karibu msimu kumalizika Mikoa hiyo haikupata mbolea na ile kidogo iliyopatikana iliuzwa kwa muda mfupi na wafanyabiashara ya mbolea wakawaeleza wananchi kuwa mbolea ya ruzuku imekwisha ndipo bei ya mbolea isiyo ya ruzuku ikapanda mara mbili ya ile ya mbolea yenye ruzuku:-

(a) Je, Serikali inaweza kutoa tamko kuhusu utaratibu uliotumika kugawa ruzuku hiyo?

(b) Je, ruzuku hiyo ilikuwa kiasi gani na kila Mkoa umepewa kiasi gani?

(c) Je, Serikali itaendelea kutoa ruzuku mwaka huu na ni utaratibu gani umebuniwa wa kuisambaza mbolea hiyo kwenye maeneo husika?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Prof. Simon M. Mbilinyi, Mbunge wa Peramiho, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mgawanyo wa fedha za fidia ya sehemu ya gharama ya usafirishaji wa mbolea kwa ajili ya Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini, ulitegemea viwango vya wastani wa matumizi ya mbolea kwa ajili ya uzalishaji wa mazao ya chakula katika kipindi cha miaka 10 iliyopita. Tathmini hiyo ilionesha kwamba, Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini hutumia wastani wa tani 59.43, Mkoa wa Iringa hutumia tani 20,713 za mbolea, Ruvuma tani 17,481, Mbeya tani 18,225 na Rukwa tani 3,007. Aidha, wafanyabiashara wa mbolea waliingia mikataba na Serikali kusafirisha viwango hivyo vya mbolea hadi vituo vikuu vya kupokelewa mbolea na kuiuza kwa bei isiyozidi Sh.14,000 kwa mfuko wa kilo 50.

(b) Serikali ilitenga jumla ya shilingi bilioni mbili ili kufidia sehemu za gharama za usafirishaji wa mbolea kwa ajili ya Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini. Kiasi cha fedha kilichotumika kwa kila Mkoa kilitegemea mbolea iliyosafirishwa na kuuzwa katika vituo vikuu vya usambazaji chini ya utaratibu wa fidia. Gharama hizo kwa kila Mkoa zilikuwa kama ifuatavyo: Mkoa wa Iringa ulipokea na kuuza tani 11707.3 kwa fidia ya Sh. 301.1 milioni, Mkoa wa Mbeya ulipokea na kuuza tani 12,850.2 kwa fidia ya sh. 401.4 milioni, Mkoa wa Ruvuma ulipokea na kuuza tani 7,932 kwa fidia ya Sh. 265.9 milioni na Mkoa wa Rukwa ulipokea na kuuza tani 1,003.2 kwa fidia ya Sh. 61.5 milioni.

(c) Mheshimiwa Spika, kama nilivyoeleza wakati nikijibu swali Na. 176, katika mwaka 2004/2005, Serikali itapanua utaratibu wa kutoa fidia ya sehemu ya gharama ya usafirishaji wa mbolea nchini kote. Utaratibu utakaotumika katika kusambaza mbolea hiyo umeshaandaliwa. Utaratibu huo unajumuisha matumizi ya Kamati ya Taifa, Kamati za Mikoa na Kamati za Wilaya zitakazosimamia na kuratibu usambazaji wa mbolea iliyofidiwa sehemu za gharama za usafirishaji katika ngazi husika.

Aidha, utaratibu huo unazitaka kampuni zitakazosafirisha mbolea chini ya utaratibu wa fidia kuingia Mkataba na Serikali juu ya viwango na gharama za fidia itakayotolewa baada ya kusafirisha na kuuza mbolea katika vituo vikuu vya kupokelea mbolea.

**MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na ya kuridhisha, lakini nina maswali madogo mawili ya nyongeza. Tatizo moja kubwa ni kuwa hatuna uhakika *rate* za *transport* kati ya Dar es Salaam na Mikoa hiyo iliyotajwa, aliyeweka hajulikani ni nani na kuwa inadhibitiwa vipi?

Mheshimiwa Spika, la pili, kuna chombo kinaitwa *TFC* bado kipo katika Mikoa ile na ni chombo cha Serikali pamoja na Serikali kujitoa kwenye mambo ya biashara lakini kwa kuwa watatumia fedha ya Serikali kwa nini hawakutumia vyombo hivyo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli tatizo la uhakika wa *rates* kwa sehemu za Vijijini kidogo linaleta utata, lakini tunachotegemea ni kuwa, Kamati za Wilaya ambazo zinahudumia usambazaji kutoka Kituo cha Mkoa kupeleka katika Wilaya tunaiomba iwe makini sana kuangalia masuala hayo na kutoa ushauri unaotakiwa kwa Kamati ya Kitaifa kusudi suala hili lipate ufumbuzi unaotakiwa na kwa bahati nzuri na sisi wote Wabunge humu hasa wa Majimbo ni Wanakamati.

Kwa hiyo, tunaomba mlichukue tatizo hili na kuliona kama ni tatizo na ni kero kusudi litoweke. Naomba tusiwaachie tu Wakuu wa Wilaya na wataalam wengine, hata sisi wenyewe Wabunge ni wadau wakuu kwa msimu huu unaokuja. Tafadhali mtusaidie kusudi tusipate tena tatizo kama ilivyojitokeza kwa mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, ni kweli *TFC* ni chombo cha Kitaifa kingefaa kifanye kazi hiyo lakini hapo katikati kilipata matatizo kidogo na taratibu zinafanywa ili chombo hiki kihame kutoka Wizara ya Viwanda kije Kilimo. Kwa kuwa kilikuwa na matatizo ya *liquidity* na *restructuring* ikaonekana kuwapa tatizo kama hili tena ni kujikwamisha.

Tukaona tutoe soko huru ili kupunguza tatizo, lakini azma ya Serikali ni hiyo ya kuwaongezea uwezo kusudi waweze kumudu zaidi huduma zao na kwa kweli tunawategemea sana na hasa sisi wenyewe Waheshimiwa Wabunge tafadhali mtusaidie kwa hilo.

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali yote yamejibiwa na muda wake umekwisha, sina matangazo kwa leo. Naona kesho hakuna semina. Kwa hiyo, tunaendelea tu na Shughuli za Bunge kama zilivyopangwa kwenye *Order Paper.*

## HOJA ZA SERIKALI

### Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2004/2005
### Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, baada ya kupokea taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, naomba kutoa hoja kwamba, sasa Bunge lako Tukufu likubali kupitisha makadirio ya matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, napenda niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kuwapongeza Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella, Mbunge wa Ukerewe, kuwa Rais wa Bunge la Afrika, Mheshimiwa Dr. William Shija, Mbunge wa Sengerema, Mheshimiwa Dr. Amani W. A. Kabourou, Mbunge wa Kigoma Mjini, Mheshimiwa Dr. Remidius Edington Kissassi, Mbunge wa Dimani na Mheshimiwa Athumani Janguo, Mbunge wa Kisarawe, kwa kuchanguliwa kuwa Wabunge wa Bunge la Umoja wa Afrika.

Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Sophia Simba, Mbunge wa Viti Maalum na pia Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kudumu ya Maendeleo ya Jamii, kwa kuteuliwa kuiwakilisha Tanzania katika Baraza la Wabunge wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika *(SADC)*. Nampongeza Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, Mbunge wa Muhambwe, kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Baraza la Kimataifa la Mazingira. Pia nawapongeza, Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere, kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais kuwa Mbunge na Mheshimiwa Danhi Makanga, Mbunge wa Jimbo la Bariadi Mashariki, kwa ushindi mkubwa alioupata katika uchaguzi mdogo uliofanyika tarehe 30 Mei, 2004. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa pole kwako wewe binafsi, Mheshimiwa Spika na Bunge lako Tukufu, kwa kifo cha aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini na Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Yete Mwalego. Mchango wake kwenye Kamati ya Miundombinu ulisaidia sana katika utendaji wa Sekta zetu za Mawasiliano na Uchukuzi, Mungu ailaze roho ya marehemu mahali pema peponi. Familia ya marehemu inawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa msaada mkubwa mlioutoa.

Aidha, nawapa pole Mheshimiwa Dr. Abdallah Omari Kigoda, Mbunge wa Handeni na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, pamoja na Mheshimiwa Dr. Aisha Omari Kigoda, Mbunge wa Viti Maalumu, kwa msiba wa kufiwa

na baba yao mzazi. Nawapa pole Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wa Mkoa wa Tanga, kwa kufiwa na Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi wa Mkoa. Mwenyezi Mungu azilaze peponi roho za marehemu. *Amina.*

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bunge ya Miundombinu chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Profesa Henry Robert Mgombelo, Mbunge wa Tabora Mjini, imeyapitisha makadirio ya matumizi ya Wizara kwa mwaka 2004/2005. Naishukuru. Tutazingatia maoni, maelekezo na ushauri wa Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuwasilisha hoja ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, napenda pia kuwapongeza na kuwashukuru Waheshimiwa Mawaziri wenzangu, walionitangulia kutoa hoja za Wizara zao, kwa hotuba ambazo zimefafanua utekelezaji wa sera mbalimbali, hali ya uchumi, ukuaji wa huduma za kijamii na matarajio yetu kwa kipindi cha 2004/2005. Aidha, napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wenzangu waliochangia hotuba za Mawaziri waliotangulia. Maoni yao yamesaidia kwa kiasi kikubwa kuboresha hotuba ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Spika, hotuba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Ubinafsishaji, Mheshimiwa Abdallah Kigoda na ile ya Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Basil Mramba, zimetoa ufafanuzi wa kina kuhusu hali na mwelekeo wa kiuchumi na fedha hapa nchini kwa kipindi cha mwaka 2003/2004. Hotuba zao zimeonyesha kuwa, pamoja na ukosefu wa mvua sehemu nyingi nchini katika kipindi hicho, kulikuwa na mafanikio makubwa. Jukumu letu ni kuendeleza mafanikio yaliyopatikana kwa kusimamia utekelezaji wa sera na programu zetu ili kuhakikisha kuwa kiwango kinachotakiwa cha ubora wa maisha ya jamii kinafikiwa. Ni matarajio yetu kuwa sekta za mawasiliano na uchukuzi zitaendelea kutoa mchango wake kwa Taifa kwa kuboresha miundo mbinu na kutekeleza mikakati na sera zake kwa kushirikiana na wadau wa sekta hizi. Wizara yangu itahakikisha kuwa vyombo vyake vya udhibiti wa shughuli za kisekta vinasimamia utoaji wa huduma bora zinazozingatia viwango vinavyokubalika kwa gharama nafuu.

Mheshimiwa Spika, maelezo yaliyotolewa katika Hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, yamefafanua vizuri kuhusu utekelezaji wa programu na mikakati ya Serikali yenye lengo la kuimarisha na kuboresha huduma za jamii na hivyo kuwapunguzia wananchi kero za umasikini na maradhi katika mazingira magumu yanayowakabili. Napenda kuwaomba Waheshimiwa WaBunge waendelee kuishauri Serikali ikiwa ni pamoja na Wizara yangu jinsi ya kufikia malengo ya maendeleo yanayokusudiwa. Mheshimiwa Waziri Mkuu, katika hotuba yake ametoa mwelekeo wa kijumla wa sekta za mawasiliano na Uchukuzi. Katika wigo alioutoa, kazi yangu leo ni kutoa ufafanuzi wa ziada na wa kina huhusu utekelezaji.

Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kueleza hali ya utendaji ilivyokuwa katika kipindi kilichopita, napenda kuchukua nafasi hii kutoa shukrani zangu za dhati kwa Kamati ya Bunge ya Miundombinu chini ya Mwenyekiti wake, Mheshimiwa Profesa Henry Robert Mgombelo, Mbunge wa Tabora Mjini, kwa maelekezo mbalimbali na ushauri mzuri ambao umeiwezesha Wizara hii kurekebisha kasoro mbalimbali katika

mipango na utendaji wa kazi za sekta zetu. Katika kipindi cha 2003/2004, Kamati ya Miundombinu ilipata fursa ya kutembelea maeneo mbalimbali muhimu kujionea utekelezaji wa programu za kisekta. Kamati ilitembea maeneo yafuatayo: Mamlaka ya Reli Tanzania na Zambia *(TAZARA)*, Shirika la Reli Tanzania *(TRC),* Mamlaka ya Bandari Tanzania *(THA)* (Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara), Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Kilimanjaro, Kampuni ya Huduma za Meli *(MSCL)*, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)*, Shirika la Posta *(TPC),* Kampuni ya simu Tanzania *(TTCL),* Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Anga *(TCAA)*, Shirika la Usafiri Dar es Salaam *(UDA)*, Shirika la Udhibiti wa Shehena za Meli *(TCFB)*, Wakala wa Ndege za Serikali *(TGFA)*, Chuo cha Usafirishaji *(NIT),* Chuo cha Ubaharia *(DMI)*, Makampuni ya *SCANDINAVIA, CELTEL, MOBITEL, VODACOM, DAHACO* na *DHL*. Kamati ilitoa maoni na ushauri wenye lengo la kuboresha na kuimarisha huduma za mawasiliano na uchukuzi nchini.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, sekta za Mawasiliano, Uchukuzi na Hali ya Hewa zimeendelea kuimarika zaidi kutokana na uboreshaji wa miundombinu pamoja na huduma zake. Utendaji katika sekta hizi umeendelea kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Sera ya kuondoa Umaskini, Sera ya Usimamizi wa Mazingira, pamoja na sera za sekta za Mawasiliano na Uchukuzi, na zile za sekta nyingine. Katika kutekeleza sera hizo, Wizara imeendelea kushirikiana na wadau katika jukumu la kurekebisha mifumo ya uendeshaji ya sekta ili kuongeza ufanisi na kuondoa kero zinazowakabili wananchi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, Wizara ilizindua rasmi Sera ya Uchukuzi. Sambamba na uzinduzi huo Wizara iliandaa Wiki ya Uchukuzi ambayo ilisherehekewa kwa mara ya kwanza hapa nchini. Kila Mkoa uliandaa maonyesho na kazi mbalimbali zinazohusiana na uchukuzi. Kitaifa wiki ya Uchukuzi ilisherehekewa Dar es Salaam. Kilele chake kilikuwa tarehe 7 Oktoba 2003.

Madhumuni makubwa ya wiki ya Uchukuzi ni kuwajulisha wadau wa sekta na wananchi kwa ujumla kuhusu sera, mikakati, programu, dira na dhamira zinazosimamia utendaji wa sekta hizo na huduma zitolewazo kwa wananchi. Mengine ni kuelezea wadau na wananchi kuhusu utendaji wetu, mafanikio, mapungufu na changamoto zilizopo katika utoaji wa huduma za sekta zetu. Midahalo, maonyesho na mijadala mbalimbali hutoa fursa kwa wananchi kuelezea kero wanazopata katika sekta na kutoa maoni na ushauri mbalimbali. Wizara inawashirikisha kikamilifu wananchi na taasisi mbalimbali katika maadhimisho hayo ili kwa pamoja tuweze kuinua kiwango cha huduma zetu. Aidha, wakati wa maadhimisho ya wiki hiyo mwaka jana, lilizinduliwa Jarida la Uchukuzi *(Transport Bulletin)*. Jarida hili ni sehemu ya juhudi za Wizara katika kuwafahamisha wadau na wananchi kwa ujumla masuala yanayohusu sekta ya uchukuzi nchini ikiwa ni pamoja na kuitangaza sekta hii. Jarida hili linatolewa kila baada ya miezi mitatu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Wizara itashirikiana na wizara nyingine husika kama vile Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto katika kuendeleza wanawake kwa kuanzisha miradi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

*(ICT)* vijijini, mfano vituo vya mawasiliano *(Tele-Centres)* kama sera za Uchukuzi na ile ya *ICT* zinavyoeleza.

Mheshimiwa Spika, kazi ya kutayarisha mkakati wa utekelezaji wa sera ya Taifa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano inaendelea. Zoezi hili linawahusisha wadau mbalimbali zikiwemo Wizara, sekta binafsi na mashirika yasiyo ya kiserikali. Wizara na Mashirika zinazohusika ni Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, Wizara ya Fedha, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Elimu na Utamaduni, Ofisi ya Rais, (Mipango na Ubinafsishaji), Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP).* Kazi hii itakamilika katika nusu ya kwanza ya mwaka wa 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua kwamba Tanzania ni sehemu ya Jumuiya ya Kimataifa ambayo hivi sasa imeelekeza juhudi zake katika mapinduzi ya kuelekea kwenye Jamii Habari na hatimaye kuwa na jamii yenye uelewa. Kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano *(ICT),* kasi ya kujiletea maendeleo itaongezeka na hivyo kuiwezesha jamii yetu kufikia malengo yaliyomo katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Kuhusu suala hili, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inaeleza kwamba, fursa zinazotolewa na teknolojia ya habari na mawasiliano zinaweza kutumiwa kwa ajili ya kufikia malengo ya Dira. Vile vile *ICT* itatuwezesha kufikia malengo yaliyowekwa na Umoja wa Mataifa ya Milenia hii yajulikanayo kama *'UN Millenium Development Goals (UNMDGs)'*. Baadhi ya malengo yaliyomo kwenye *UNMDGs* ni pamoja na kubuni mikakati ya kuharakisha maendeleo ya jamii ili kuondoa umasikini hasa kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, kwa kuelewa umuhimu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika maendeleo ya jamii na uchumi wetu, katika kipindi cha muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu, juhudi zetu zitaelekezwa katika kuendelea kuelimisha na kuhamasisha wananchi kuhusu umuhimu wa matumizi ya *ICT* na katika mchakato wa ujenzi wa Jamii Habari. Vile vile tutaimarisha mafunzo na utafiti kuhusu matumizi ya *ICT.* Tutaendelea kujenga mazingira mazuri ya kuvutia uwekezaji. Tutaendelea pia kushiriki katika jitihada za kimataifa za kujenga Jamii Habari na hatimaye jamii yenye uelewa.

Mheshimiwa Spika, juhudi zimeanza za kujenga uwezo wa watu wetu kwa kutoa mafunzo kwa kutumia *ICT.* Mafunzo ya aina hii tayari yameanza kutolewa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Kitengo cha *University Computing Centre* na Chuo cha Ufundi cha Arusha. Vyuo na asasi nyingine zilizo katika mtandao huu wa *Cisco* ni Chuo Kikuu cha Nyegezi Tawi la *SAUT* Iringa, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam *(DIT)* na Taasisi ya Teknolojia ya Mbeya *(MIT).* Mafunzo haya yanatolewa kwa kiwango cha Kimataifa na Kampuni ya Kimarekani iitwayo *Cisco* yenye Makao Makuu California, Marekani. Wizara yangu kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Utamaduni tunafanya juhudi kuhakikisha kuwa aina hii ya mafunzo inasambazwa katika vyuo vyote ikiwa ni pamoja na taasisi za elimu ya juu kwa kuanza, kwa kushirikiana na *Cisco* na wengine, kufundisha taaluma hii kwa wakufunzi katika Vyuo vya Ualimu nchini ili hatimaye waweze kufundisha vijana wetu.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 nililieleza Bunge lako Tukufu kwamba, maandalizi ya Sera ya Taifa ya huduma za Posta yanakamilishwa. Napenda kutoa taarifa kuwa Sera hii hivi sasa imekamilika na imeidhinishwa rasmi na Serikali. Sera ya Posta inalenga kuboresha huduma za posta nchini, uenezaji wa huduma hizo hasa vijijini na ushirikishwaji wa sekta binafsi katika utoaji wa huduma hizo mijini na vijijini. Sera pia inafafanua kuhusu utoaji huduma za posta katika maeneo yasiyo ya kibiashara *(Public Service Obligation - PSO),* ambapo ni jukumu la Serikali kuhakikisha kuwa huduma zinapatikana kwenye maeneo hayo. Hatua inayofuata ni kukamilisha mikakati ya utekelezaji wake. Hatua hii itasaidia sana kubadilisha muundo wa utendaji wa Shirika kwa lengo la kuliwezesha kujiendesha kibiashara.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza mpango kabambe wa uendelezaji wa miundombinu ya uchukuzi nchini, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Wizara iliendelea na maandalizi ya Programu ya muda mrefu (miaka 20) ya uendelezaji wa Sekta ya uchukuzi nchini ijulikanayo kama *Transport Sector Development Program.* Wizara bado inaendelea kuwasiliana na Benki ya Dunia na wafadhili wengine kuhusu mradi huu muhimu. Hadi sasa mwelekeo wa Benki ya Dunia kuhusu mradi huu ni mzuri baada ya wao kuonyesha nia ya kufadhili matayarisho ya programu hiyo yenye lengo la kuboresha miundombinu ya huduma za usafiri kwa ujumla wake na kwa uwiano.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Wizara imeendelea kuratibu zoezi la ubinafsishaji wa Mashirika na asasi zilizoko kwenye Sekta. Kwa upande wa ukodishaji wa Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* zoezi hili ilibidi lianze upya baada ya kushindwa kumpata mkodishaji katika hatua za awali. Kwa hivi sasa Makampuni saba yamepitishwa ili yashindane kuwania ukodishaji wa Shirika hilo. Makampuni hayo ni *The New Limpopo Bridge Projects Investments (NLP)* na *Spoornet Consortium, Great Lakes Railways Company Consortium (COMAZAR), Sheltan & Mvela Consortium, The East Africa Rail Consortium* na *Dynamic Rail.* Makampuni haya matano ni kutoka Afrika ya Kusini. Makampuni mengine ni *Rites Ltd. Consortium* ya India na *CANAC* ya Canada. Matarajio yetu ni kwamba, taratibu za kumpata mkodishaji zitakamilika ifikapo mwishoni mwa mwaka huu wa 2004.

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya mawasiliano kwa lengo la kuwa na uamuzi wa pamoja, Serikali za Zambia na Tanzania zimekubaliana kuirekebisha Reli ya Tanzania na Zambia *(TAZARA)* kwa mfumo wa ukodishaji. Taratibu za pamoja za kutekeleza azma hiyo zimeanza. Kamati ya pamoja *(Task Force)* imeundwa ambapo Kampuni ya *M/s. PriceWaterHouseCoopers* imeteuliwa kuwa Mtaalam Mwelekezi *(Consultant)* atakayeshauri namna ya kufanikisha utekelezaji wa uamuzi wa Serikali zetu mbili. Mtaalam Mwelekezi huyo anatarajiwa kukamilisha na kutoa taarifa yake kwa Serikali za Tanzania na Zambia ifikapo mwezi Desemba, 2004. Tunaishukuru Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China kwa mchango mkubwa katika ujenzi na kuiendeleza *TAZARA.* Tunawashukuru pia kwa kukubali kuendelea kuisaidia *TAZARA.*

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha usafiri kwa njia ya reli, mwezi Octoba, 2003, Serikali za Tanzania na Rwanda zilitiliana saini makubaliano ya uendeshaji wa

Ukanda wa Kati *(Memorundum of Understanding on the Central Development Corridor).* Makubaliano haya yanahusu uendelezaji wa kanda hiyo na utekelezaji wa miradi ya pamoja iliyomo kwenye ukanda huo. Baadhi ya miradi hiyo ni pamoja na ujenzi wa reli ya Isaka hadi Kigali. Serikali hizi kwa pamoja, zimeomba msaada kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* kufanya upembuzi yakinifu wa mradi huo wa reli ya Isaka hadi Kigali. Hadidu za Rejea za mradi tayari zimekamilika na zimewasilishwa *ADB.* Benki imeonyesha nia ya kugharamia utafiti huo na imeahidi kutoa Dola za Kimarekani milioni 2.5.

Mheshimiwa Spika, katika kukuza ushirikiano kwa upande wa usafirishaji kati ya Burundi na Tanzania, mwezi Mei, 2004 nilikutana na Waziri mwenzagu wa Burundi huko Kigoma na kufikia makubaliano yafuatayo:-

(a) Ukarabati wa bandari za Kigoma na Bujumbura, kwa kushirikiana na wafadhili, ili tuweze kuimarisha usafiri wa mizigo kati ya Kigoma na Bujumbura. Aidha, kwa kushirikiana na sekta binafsi katika kusafirisha mizigo kati ya bandari hizi ipatikane meli ya kubeba mabehewa *(Wagon Ferry).*

(b) Upatikanaji wa sehemu katika miji ya Dar es Salaam na Kigoma ili Serikali ya Burundi iweze kujenga maghala *(Depots)* ya mizigo yao.

(c) Kuanzisha usafiri wa ndege kati ya Tanzania na Burundi.

(d) Kuimarisha bandari ya Kasanga katika Ziwa Tanganyika ili iweze pia kuhudumia mizigo iendayo Burundi.

(e) Kuboresha barabara za Kigoma - Manyovu - Migina - Bujumbura na Tunduma - Sumbawanga - Kasanga ili kuimarisha na kuwezesha biashara kati ya Burundi na Tanzania.

Mheshimiwa Spika, wizara imeendelea kufanya mapitio ya Makubaliano ya Usafiri wa Anga kati ya Tanzania na nchi mbalimbali duniani *(Bilateral Air Service Agreements)*. Lengo ni kuwezesha mashirika ya ndege ya Tanzania kuingia katika masoko ya nje na pia kutoa nafasi kwa mashirika ya nchi nyingine kutoa huduma kati ya nchi husika na Tanzania. Katika kipindi cha 2003/2004, makubaliano yaliyopitiwa ni yale ya Tanzania na nchi za Botswana, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo *(DRC),* Kenya, Msumbiji, Malawi, Nigeria, Uganda, Falme za Kiarabu *(UAE)* na Zimbabwe. Wizara pia imeanzisha mazungumzo na Serikali ya Angola yenye lengo la kuwa na makubaliano ya usafiri wa anga kati ya Tanzania na nchi hiyo. Tarehe 28 Mei 2004, Tanzania na Uswisi zilitiliana saini mkataba mpya wa usafiri wa anga kati ya nchi hizo mbili. Mkataba wa awali ulikuwa wa mwaka 1979. Imebidi mikataba hiyo ipitiwe upya kutokana na mabadiliko ya sera za kiuchumi kuelekea soko huria na suala zima la usalama wa usafiri wa anga. Wizara itaendelea kufanya mapitio ya mikataba mingine na kuanzisha makubaliano mapya na nchi nyingine kwa lengo la kuyapatia makampuni yetu ya ndege fursa ya kutoa huduma katika masoko ya nje na pia kutoa nafasi ya ushindani.

Mheshimiwa Spika, kufuatia tukio la ugaidi nchini Marekani Septemba 11, 2001 na lile lililotokea Mombasa, Kenya mwezi Novemba, 2002, Wizara imeendelea kuhakikisha kwamba wakati wa kufanya mapitio na kuanzisha makubaliano mapya ya usafiri wa anga, suala la usalama linazingatiwa. Aidha, Wizara kupitia Mamlaka ya Viwanja vya Ndege kwa kushirikiana na taasisi nyingine za kitaifa tunaendelea kutekeleza mpango wa kuimarisha ulinzi na usalama katika viwanja vya ndege vya kimataifa Dar es salaam na Kilimanjaro. Juhudi zinaendelea kuimarisha ulinzi katika viwanja vingine.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, huduma za Usafiri wa Anga ziliendelea kuimarika. Huduma hizi zilitolewa na Kampuni ya ndege Tanzania *(ATCL)* na mashirika binafsi ya *Precision Air* na *Air Express. Precision Air* imeongeza huduma zake na sasa inatoa huduma katika Miji ya Arusha, Bukoba, Dar es Salaam, Kilimanjaro, Kigoma, Mtwara, Tabora, Shinyanga na Zanzibar. Kampuni pia inatoa huduma kwenye miji ya Nairobi, Mombasa na Johannesburg. *ATCL* imeongeza safari zake na inatoa huduma katika sehemu zifuatazo: Dar es Salaam, Kilimanjaro, Zanzibar, Mwanza na Mtwara. *ATCL* pia inakwenda katika Miji ya Johanesburg, Nairobi, Entebbe na Hahaya (Moroni). Serikali katika kukamilisha ubinafsishaji wa Shirika la Ndege Tanzania *(ATC)* mwezi Desemba, 2002, iliunda Shirika linaloitwa *Air Tanzania Holding Company (ATHCO),* ambalo linashughulikia madeni, mali na raslimali ambazo hazikuchukuliwa na Mbia wa *ATCL.* Katika kipindi cha takriban mwaka mmoja na nusu tangu kuundwa kwake, Kampuni imeweza kuuza baadhi ya mali na hivyo kulipa jumla ya shilingi milioni 36 kama mafao yaliyobaki ya waliokuwa wafanyakazi wa *ATC.* Aidha, Kampuni imeweza kulipa madeni ya nje yenye jumla ya shilingi bilioni 1.125 na madeni ya ndani ya shilingi milioni 296.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 nilitoa taarifa kwamba, Serikali na mwekezaji katika Kampuni ya Simu Tanzania *(TTCL)* yaani *MSI/Detecon,* walikuwa wanaendelea kutafuta njia muafaka ya kumaliza mgogoro wa malipo ya asilimia 50 yaliyohusisha usahihi (faida au hasara) wa mahesabu ya *TTCL* ya mwaka 2000. Napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba mgogoro huo sasa umekwisha baada ya Mtaalamu Huru wa Kimataifa kutoka katika taasisi iitwayo *The Institute of Chartered Accountants - ICA London* aliyekubalika kwa pande zote mbili, kutoa taarifa yake. Katika taarifa yake, mtaalam huyo alitoa mapendekezo kwamba Mwekezaji *(MSI/Detecon)* anatakiwa kuilipa Serikali Dola za Kimarekani milioni 5.5 kulingana na uchunguzi wa mahesabu ya mwaka 2000. Tunapenda kutoa shukrani za dhati kwa Kamati yetu iliyokuwa chini ya uenyekiti wa Bwana Marten Lumbanga, Katibu Mkuu Kiongozi, kwa kusimamia, kwa niaba ya Serikali, mazungumzo na hatimaye kufanikisha upatikanaji wa makubaliano kati ya Serikali na mwekezaji. Ni matumaini yangu kuwa baada ya kumalizika mgogoro huu, *TTCL* itatekeleza kikamilifu Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Simu na Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano. Teknolojia ya kisasa inawawezesha kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Simu 2000 Limited,* imeendelea na utekelezaji wa majukumu yake ya msingi ya kusimamia na kuuza mali zisizo za msingi*(non-core assets)* zilizokuwa zinamilikiwa na *TTCL* kabla ya kubinafsishwa. Kampuni vilevile ina

jukumu la kulipa deni la pensheni kwa wastaafu wa lililokuwa Shirika la Posta na Simu la iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Katika kipindi cha 2003/2004, Kampuni imeweza kuuza nyumba 35 na viwanja 11 na hivyo kulipa kiasi cha Shilingi bilioni 3.7 kwenye Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii *(NSSF)*, fedha ambazo ni pensheni na kamisheni. Kampuni imeweza kukidhi majukumu yake, hasa lile la kulipa deni la pensheni kwa kila kipindi kilichopangwa tangu ilipoanzishwa. Hata hivyo, kampuni inakabiliwa na tatizo la ulipaji wa kodi *(Capital Gains Tax).* Juhudi zinaendelea kufanywa kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha ili kuona uwezekano wa kumaliza tatizo hili.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mamlaka ya Bandari Tanzania, mpango wa ubinafsishaji wa vitengo vilivyobakia baada ya kitengo cha Kontena kubinafsishwa uliendelea kulingana na ratiba. Mkakati uliokubalika ni kwa Mamlaka ya Bandari kumiliki na kuendesha bandari kwa mfumo wa *Landlord Port Model.* Baadhi ya vitengo vitakodishwa kwa waendeshaji binafsi na vingine vitabakia chini ya Mamlaka mpya itakayoundwa. Muswada wa Bandari za Tanzania wa mwaka 2004 *(Tanzania Ports Bill, 2004)* tayari umesomwa mara ya kwanza Bungeni. Muswada huo unapendekeza kuifuta Mamlaka ya Bandari Tanzania *(THA)* na kuunda Mamlaka mpya, iitwayo *Tanzania Ports Authority (TPA)* itakayopewa uwezo zaidi wa kufanya kazi kama *Landlord.* Muswada huo pia unaipa *TPA* mamlaka ya kumiliki, kuendeleza na kukodisha bandari za mwambao na za maziwa makuu.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Usafiri Dar es salaam (UDA) linamilikiwa na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam na Serikali. Juhudi zinaendelea kufanywa ili kuweza kulibinafsisha Shirika mapema iwezekanavyo. Moja ya mikakati iliyowekwa ni pamoja na kuhakikisha kuwa uwiano wa wafanyakazi na idadi ya mabasi yaliyopo unarekebishwa, ili kupunguza gharama za uendeshaji; kuongeza vitendea kazi ili kuimarisha shughuli za Shirika na hivyo kuweza kuhimili ushindani uliopo. Shirika katika mwaka 2004/2005 limepanga kukarabati mabasi kumi na mbili yaliyokuwa yamesimama kutokana na ajali barabarani au kuhitaji matengenezo ya kawaida na makubwa.

Ili kuboresha huduma za usafiri katika Jiji la Dar es Salaam, mji unaokua haraka sana, kuna haja ya kuanza kufikiria njia za ziada za usafiri Dar es Salaam, ikiwa ni pamoja na usafiri wa reli *(sub-urban railway)* na usafiri wa majini kutoka katikati ya Jiji na maeneo ya karibu na Jiji.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Wizara iliendelea na jukumu la kusimamia na kuratibu shughuli za utoaji huduma za mamlaka mbalimbali chini yake ambazo ni pamoja na Mamlaka ya Usalama wa Usafiri wa Anga *(TCAA)*, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege *(TAA),* Mamlaka ya Hali ya Hewa *(TMA)* na Wakala wa Ndege za Serikali *(TGFA)*. Kwa ujumla, huduma za taasisi hizi zimetolewa kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Spika, Bunge lako Tukufu lilipitisha Sheria Namba 12 ya Mwaka 2003 kuhusu kuundwa kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(Tanzania Communications Regulatory Authority - TCRA),* baada ya kuunganishwa kwa Tume ya

Mawasiliano Tanzania *(TCC)* na Tume ya Utangazaji Tanzania *(TBC)*. Sheria hii imeweka bayana kuwa itatumika kwa Tanzania Bara na Visiwani kwa masuala yahusuyo mawasiliano tu. Kuunganishwa kwa *TCC* na *TBC* kumetokana na kukua na kuunganika kwa teknolojia za mawasiliano na habari. Chombo hiki kitasimamia biashara ya mawasiliano kwa njia ya simu, matangazo ya redio na televisheni, utoaji wa huduma za posta, ugawaji na usimamizi wa masafa ya matangazo ya redio pamoja na teknolojia ya Habari na Mawasiliano. *TCRA* imeundwa ili kuongeza ufanisi na kuweka mazingira mazuri ya kuendeleza sekta ya mawasiliano nchini.

Mheshimiwa Spika, *TCRA* imepewa majukumu mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuongeza ufanisi unaotokana na ushindani katika sekta ya mawasiliano, kulinda haki za wadau wa huduma za mawasiliano na kuelimisha wadau kuhusu majukumu ya Mamlaka. Aidha, majukumu ya kila siku ya Mamlaka yatakuwa ni pamoja na kutoa na pale inapolazimu kufuta leseni kwa makampuni ya mawasiliano nchini, kudhibiti tozo mbalimbali za huduma za mawasiliano, kuweka viwango *(standards)* vya huduma mbalimbali na kuvisimamia, kusuluhisha migogoro na migongano kati ya watoa huduma katika sekta. Baraza la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano limeundwa kwa mujibu wa sheria. Baraza hilo linaongozwa na Bwana Rajabu M. Yusufu aliyekuwa Postamasta Mkuu wa lililokuwa Shirika la Posta na Simu la Afrika ya Mashariki, Katibu Mkuu wa Umoja wa Mashirika ya Simu, Afrika na Mwenyekiti wa lililokuwa Shirika la Posta na Simu, Tanzania. Aidha, Baraza lina wajumbe tisa. Jukumu lake ni:-

(a) Kuwakilisha maslahi ya watumiaji kwa kushauriana na Mamlaka na Waziri anayesimamia sekta ya mawasiliano.

(b) Kupokea na kusambaza taarifa na maoni juu ya masuala yenye maslahi kwa watumiaji wa bidhaa na huduma zinazodhibitiwa.

(c) Kuanzisha Kamati za watumiaji za ndani na za kanda na kushauriana nazo.

(d) Kushauriana na makundi ya watumiaji wa sekta ya mawasiliano, Serikali na makundi mengine ya watumiaji.

Mheshimiwa Spika, Bodi ya *TCRA* nayo tayari imeundwa na inaongozwa na Balozi Richard E. Mariki, aliyekuwa Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, Wizara y Mipango na Ubinafsishaji. Bodi hii ina wajumbe sita.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, Bunge lako Tukufu lilipitisha sheria ya kuanzishwa upya kwa Mamlaka ya Usalama wa Usafiri wa Anga kupitia sheria mpya ya *Tanzania Civil Aviation Authority Act, 2003,* Sheria Na. 10 ya 2003. Sheria hii inaipa Mamlaka uwezo zaidi wa kisheria ili kusimamia na kudhibiti utoaji wa huduma za usafiri wa anga nchini kulingana na viwango vya kimataifa kama ilivyoainishwa na Shirika la Kimataifa la Usalama wa Anga *(ICAO)* na wakati huo huo ikijiendesha kibiashara. Tofauti na Mamlaka iliyokuwapo hapo awali, Mamlaka mpya itakuwa huru zaidi na itakuwa na Bodi ya Wakurugenzi. Kwa mujibu wa sheria limeundwa Baraza la

Watumiaji *(Consumer Consultative Council),* ambalo linawawakilisha watumiaji wa huduma za usafiri wa anga. Baraza hilo lenye wajumbe saba linaongozwa na Dr. C. V. Mpinga Mgana, aliyekuwa Mkurugenzi wa iliyokuwa Kurugenzi ya Usafiri wa Usalama wa Anga *(DCA).* Majukumu ya Baraza ni kama yale ya *TCRA* isipokuwa lenyewe linashughulikia masuala ya usafiri wa anga.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usafiri wa anga, moja ya miradi inayoendelea kutekelezwa katika kipindi cha 2003/2004 ni mradi wa Kituo cha Udhibiti na Kuongoza Ndege katika Anga ya Juu katika Eneo la Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC Upper Air Space Control Centre).* Mkandarasi wa mradi huu amepatikana na tayari amepewa Hadidu za Rejea. Utafiti zaidi kuhusiana na mradi huu unaendelea. Mkandarasi huyu atawasilisha taarifa ya utafiti wake kabla ya mwezi Desemba, 2004. Aidha, miradi mingine iliyotekelezwa katika kipindi hiki ni pamoja na ununuzi wa meza za kuongozea ndege *(ATC Consoles)* na vifaa vya redio na mawasiliano ya ndege katika viwanja vya Arusha, Mwanza, na Zanzibar. Pia mitambo ya mionzi ya jua ilifungwa katika viwanja vya Songea na Mtwara ili kukabiliana na kukatika kwa umeme mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kukamilisha taratibu za kukiwezesha chombo kitakachosimamia udhibiti wa Usafiri wa Nchi Kavu na Majini *(Surface and Maritime Transport Regulatory Authority-SUMATRA)* kuanza kazi zake. Kamati ya Uteuzi *(Nominations Committee)* ya *SUMATRA* imeteuliwa na Baraza la Watumiaji *(Consumer Consultative Council)* limeanzishwa. Mwenyekiti wa Baraza ni Ndugu Said El Maamry. Wizara imetangaza nafasi za wajumbe wa Bodi ya Mamlaka na nafasi ya Mtendaji Mkuu. *SUMATRA* itaanza kufanya kazi mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kama inavyofahamika Tanzania ni mwanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* na ile ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC)*. Katika kipindi hiki, ambacho nchi yetu ni mwenyekiti wa *SADC*, Wizara imeweza kushiriki kwenye mikutano ya *SADC* ikiwa ni pamoja na ule wa Wakuu wa nchi za *SADC*, Baraza la Mawaziri wa *SADC* na ule wa Wakuu wa nchi za *SADC* kuhusu Kilimo na Usalama wa Chakula ambayo yote ilifanyika hapa nchini. Katika mikutano hiyo, masuala mbalimbali ya ushirikiano na majukumu yanayohusu sekta zetu za Mawasiliano na Uchukuzi yaliainishwa. Majukumu hayo yanahusu uboreshaji wa miundombinu, huduma za posta, simu, usafiri wa anga, usafiri kwa njia ya maji hasa katika Ziwa Victoria, na sekta ya hali ya hewa.

Aidha, miradi mbalimbali inaendelea kutekelezwa chini ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki *(EAC)*. Miradi hiyo ni pamoja na huduma za usafiri wa reli, barabara, usafiri majini, usalama wa usafiri wa anga na huduma za mawasiliano na hali ya hewa.

Mheshimiwa Spika, mpango mpya wa Ushirikiano na Maendeleo ya Umoja wa Afrika *(NEPAD)* una lengo la kutaka nchi za Afrika kushirikiana katika kupiga vita umaskini. Kwa kupitia chombo hiki, nchi za Afrika zimebaini maeneo 11 muhimu ya kutekelezwa na kila nchi. Wizara ikiwa mratibu wa sekta ya miundombinu chini ya mpango wa *NEPAD*, imekamilisha mapendekezo ya miradi mbalimbali. Utekelezaji wa

miradi hiyo utaboresha miundombinu ya usafiri wa majini, barabara, anga na mawasiliano. Baadhi ya miradi iliyopendekezwa kitaifa ni pamoja na uboreshaji wa lango kuu la Bandari ya Dar es Salaam, ujenzi wa daraja la umoja kati ya Tanzania na Msumbiji, ukarabati na ujenzi wa miundombinu kwa ujumla. Utekelezaji wa miradi hii utasaidia kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi nchini.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Hali ya Hewa iliendelea kutoa huduma kwa kiasi cha kuridhisha. Wizara inaendelea na maandalizi ya Sera ya Hali ya Hewa ambayo ndio itakuwa mwongozo katika utekelezaji na utoaji wa huduma za hali ya hewa nchini. Sera hii inatarajiwa kukamilika katika kipindi cha mwaka huu wa 2004/2005. Aidha, katika kipindi cha 2003/2004, Mamlaka ya Hali ya Hewa ilipata vifaa vya kisasa vya utabiri wa hali ya hewa na vya kufundishia pamoja na fedha za kugharamia mafunzo kutoka Benki ya Kiarabu inayoshughulikia Maendeleo ya Afrika *(BADEA)*.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza kwa ujumla hali ya utendaji wa sekta za mawasiliano na uchukuzi katika kipindi cha mwaka 2003/2004, napenda kuchukua nafasi hii kueleza kwa undani zaidi mwelekeo, malengo, mikakati na utendaji wa maeneo mbalimbali ya Wizara kwa kipindi hicho na kutoa mwelekeo wa jumla na mpango wa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, sekta ya usafiri na uchukuzi kwa njia ya barabara imeendelea kuimarika katika kufanikisha shughuli za kiuchumi na kimaendeleo katika nchi yetu. Miradi ya barabara iliyoweza kutekelezwa katika kipindi hiki imefafanuliwa na Waziri wa Ujenzi katika hotuba yake.

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa Wizara imeendelea kushirikiana na Wizara ya Ujenzi katika masuala yanayohusu sera na mikakati ya uboreshaji wa miundombinu hasa katika nyanja ya uchukuzi wa barabara nchini. Aidha, Wizara pia inaendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa katika kuboresha miundombinu ya uchukuzi kwenye ngazi za Wilaya na Vijijini kwa kuzingatia maelekezo ya Sera ya Taifa ya Uchukuzi. Uboreshaji huu umeongeza huduma za uchukuzi na kuleta ushindani mkubwa miongoni mwa watoa huduma. Katika kipindi hiki wasafiri wanaoishi sehemu mbalimbali za Miji mikubwa wameendelea kuwa na uhuru wa kuchagua usafiri wanaoutaka kwa kuzingatia nauli, muda wa safari na ubora wa huduma.

Mheshimiwa Spika, usafiri wa Vijijini umeendelea kuwa kikwazo katika harakati za kuondoa umaskini nchini kutokana na kutokuwepo kwa miundombinu thabiti na hivyo kusababisha gharama za usafiri kuwa kubwa. Hata hivyo, maandalizi ya mikakati na programu madhubuti za kuondoa tatizo hilo zinaendelea kutayarishwa. Aidha, Wizara inaendelea kushirikiana na wadau wengine ikiwa ni pamoja na muungano wa wasafirishaji wa abiria na mizigo kupitia vyombo vyao ili kuboresha huduma za uchukuzi. Vyombo hivyo ni pamoja na Muungano wa wenye Mabasi nchini *(Tanzania Bus Owners Association - TABOA),* Muungano wa wenye kumiliki magari ya kusafirisha mafuta *(Tanzania Road Tankers Association - TAROTA)* na wale wenye kumiliki Malori *(Tanzania Truck Owners Association - TATOA)*. Wizara kwa kutambua mchango wa

sekta binafsi katika kutoa huduma za uchukuzi itaendelea kushirikiana na vyombo hivi pale inapowezekana kwa lengo la kuboresha hali ya usafiri mikoani na vijijini.

Mheshimiwa Spika, kumekuwapo na ushindani mkubwa wa huduma ya usafiri katika Miji yetu hapa nchini. Kwa kiasi kikubwa huduma hii imeendelea kutolewa na sekta binafsi. Ni matarajio ya wananchi wa Mijini kuwa wataendelea kupata huduma hii kwa urahisi zaidi na kwa gharama nafuu kutokana na kuwepo kwa ushindani. Hata hivyo, katika miezi ya hivi karibuni utoaji wa huduma hizi ulikabiliwa na tatizo la kupanda mara kwa mara kwa bei ya mafuta na vipuri kunakotokana na kupanda kwa bei ya mafuta ghafi duniani na kushuka kwa thamani ya Shilingi ya Tanzania ikilinganishwa na Dola ya Kimarekani, jambo ambalo limekuwa ni changamoto kubwa kwa watoa huduma.

Mheshimiwa Spika, tunapenda kushukuru na kupongeza Uongozi wa Mkoa wa Dar es Salaam kwa juhudi zao za hivi majuzi za kuleta muafaka baada ya wenye mabasi ya daladala mkoa wa Dar es Salaam kupandisha nauli bila kufuata taratibu zilizowekwa. Hatua ya Uongozi wa Mkoa, ambao ndio mamlaka ya udhibiti wa usafiri Dar es Salaam, inaonyesha jinsi Serikali ilivyo makini katika kutetea wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, matatizo mengine ni kutokuwepo kwa mabasi makubwa ya kutosha na yenye nafasi za kukaa abiria badala ya kusimama au kukaa kwenye viti vilivyosongamana na kubanana na hivyo kuwafanya wananchi washindwe kusafiri kwa raha na amani. Hali hii pia huhatarisha usalama wa abiria na hata mali zao na wakati mwingine hii husababisha ajali. Hata hivyo, Serikali itaendelea kutumia Mamlaka za Leseni za Usafirishaji za mikoa katika kusimamia utoaji huduma za usafiri hadi hapo chombo kipya cha udhibiti, *SUMATRA* kitakapoanza kazi rasmi. Aidha, kazi ya usalama wa magari na abiria utaendelea kufanyika kwa ushirikiano mkubwa na Jeshi la Polisi (kikosi cha Usalama Barabarani).

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, utendaji na huduma zitolewazo na Shirika la Usafiri Dar es Salaam (UDA) zimeimarika zaidi ikilinganishwa na mwaka uliopita. Utendaji wa UDA unakabiliwa na ushindani mkubwa wa kibiashara. Katika kipindi hiki, Shirika lilikuwa na mabasi 37 ikilinganishwa na mabasi 40 mwaka uliopita.

Aidha, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Shirika la UDA lilipata mapato ya shilingi milioni 792.6 kutokana na shughuli za usafirishaji ikilinganishwa na shilingi milioni 684.9 zilizopatikana mwaka 2002/2003. Hili ni ongezeka la asilimia 23. Hata hivyo, mchango wa Shirika hili bado ni mdogo sana ikilinganishwa na mabasi zaidi ya elfu tatu yanayotoa huduma katika jiji la Dar es Salaam. Vile vile katika juhudi za kuimarisha huduma za usafiri Jijini Dar es Salaam, mradi wa mabasi yaendayo kwa haraka *(Bus Rapid Transit - BRT)* unaendelea kutayarishwa na Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kama mpango maalumu wa kuboresha hali ya usafiri Jijini.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia ushauri wa kitaalamu ambao unahitajika kwa mradi kama huu, Halmashauri ya Jiji la Dar es salaam, iko katika hatua za kumpata Mshauri Mwelekezi kwa ajili ya kutekeleza mradi huu. Inategemewa kuwa mradi huu

utakamilika na kuanza kazi rasmi mwishoni mwa mwaka 2005. Kama nilivyolieleza Bunge lako Tukufu katika hotuba yangu ya mwaka jana, utekelezaji wa mradi huu utakuwa kwa awamu. Awamu ya kwanza itahusisha barabara kuu tatu ambazo ni barabara za Morogoro, Mandela na Nyerere. Maeneo mengine ya mradi huu yataainishwa kulingana na utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi. Mradi wa mabasi makubwa yaendayo haraka utashirikisha asasi zifuatazo: Benki ya Dunia, *USAID,* Kampuni ya *ANYWAY Solutions* ya Canada, *LEA International* (Asasi isiyo ya Kiserikali ya Canada) na Kampuni ya mabasi ya *ATAM* ya Italia. Kampuni mbili za mwisho zitatoa msaada wa wataalam.

Mheshimiwa Spika, udhibiti wa uchukuzi kwa njia ya barabara uliendelea kusimamiwa na Wizara na taasisi mbalimbali kama vile Mamlaka Kuu ya Leseni za Usafirishaji *(CTLA)* na Mamlaka za Leseni za Mikoa *(RTLAs),* chini ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, Wizara ya Ujenzi inayoshughulikia udhibiti wa uzito wa magari yanayotumia barabara, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi inayosimamia utekelezaji wa sheria na usalama barabarani, Wizara ya Fedha inayoshughulikia usajili wa magari, na Wizara ya Viwanda na Biashara inayoshughulikia Viwango na Ubora wa magari yanayotengenezwa au yanayoingizwa nchini. Majukumu haya mengi ya udhibiti na usimamizi wa sekta ya Uchukuzi kwa njia ya barabara yanahamishiwa *SUMATRA.*

Mheshimiwa Spika, Mamlaka Kuu ya Leseni za Usafirishaji ilitoa jumla ya leseni 7,474 kwa magari ya abiria na mizigo katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai, 2003 hadi Machi, 2004, ikilinganishwa na leseni 11,103 zilitolewa kwa magari ya abiria na mizigo katika kipindi cha mwezi Julai, 2002 hadi Machi, 2003 . Idadi ya leseni za magari ya abiria ni 1,493 na magari ya mizigo ni 5,981. Kiasi cha fedha zilizokusanywa kama maduhuli kutokana na ada za leseni hizo ni shilingi bilioni 1.13 ukilinganisha na shilingi billioni1.06 zilizokusanywa kipindi cha mwaka 2002/2003.

Mheshimiwa Spika, mafanikio yaliyopatikana katika taasisi hii yametokana na utaratibu uliowekwa na Mamlaka wa kufanya ziara za kikazi Mikoani mara kwa mara. Pia shughuli za Mamlaka zimekuwa zikiendelea kutangazwa kwenye televisheni na vyombo vingine vya habari, ili kuwaelimisha wamiliki wa magari kuzifahamu taratibu na hivyo kuona umuhimu wa kukata leseni. Mamlaka imeongeza ufanisi katika ukaguzi ambao unalenga kubaini watoa huduma za uchukuzi bila leseni. Ofisi za Mamlaka za Kanda zimeendelea kuimarishwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, jitihada zitafanywa ili kuvishirikisha vyama vya hiari kama vile *Tanzania Bus Owners Association (TABOA), Arusha and Kilimajaro Bus Owners Association (AKIBOA), Dar es Salaam Bus Owners Assiciation (DARBOA), Tanzania Tanker Owners Association (TAROTA), Tanzania Truck Owners Association (TATOA)* na *Tanzania Drivers Association (TDA),* viweze kuwashawishi wanachama wao waone umuhimu wa kukata leseni za usafirishaji kwa magari yao na kuzingatia kwa dhati masharti ya leseni hizo.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto nyingi zinazoikabili sekta hii ya uchukuzi kwa njia ya reli, Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* na Mamlaka ya Reli ya

Tanzania na Zambia *(TAZARA),* wameendelea kutoa huduma kwa kiwango cha kuridhisha. Mashirika haya mawili yanatoa huduma ya usafirishaji wa shehena nzito na zinazokwenda masafa marefu. Katika hatua za kuimarisha na kuboresha miundombinu na huduma za sekta hii, Serikali imefikia makubaliano na Benki ya Dunia ya kugharamia mradi wa uboreshaji wa huduma za miundombinu nchini. Mradi huu ujulikanao kama *Central Transport Corridor Project* unahusu uimarishaji wa barabara kuu pamoja na reli katika ukanda wa kati. Maeneo ya reli ambayo yatafaidika na mradi huu ni ukarabati wa baadhi ya sehemu za reli ya kati zilizoharibika, uboreshaji wa karakana, kurekebisha mazingira, kuhamasisha wananchi kutojenga katika hifadhi ya njia ya reli, kujenga uwezo wa kusimamia na kuendesha Kampuni ya *Railway Holding Company (RAHCO).* Maeneo mengine ni; kuboresha mazingira ya uwekezaji kwa kununua baadhi ya vipuri muhimu vinavyohitajika katika utoaji wa huduma, kuweka mazingira mazuri yatakayovutia wawekezaji wazuri wakati wa ukodishaji wa huduma, pamoja na kusaidia mchakato wa kuikodisha Reli ya *TAZARA*. Mradi huu umepangwa kutekelezwa kwa muda wa miaka minne kuanzia mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, utendaji wa Shirika la Reli Tanzania katika kipindi cha mwaka wa 2003/2004, ulikuwa wa kuridhisha ukizingatia hali ya vifaa na mtandao wa njia za reli zilizopo. Katika kipindi hiki Shirika lilisafirisha jumla ya tani milioni 1.442 ikilinganishwa na tani milioni 1.445 zilizosafirishwa mwaka 2002. Lengo la Shirika lilikuwa ni kusafirisha tani 1.400. Shehena iliyosafirishwa mwaka 2003 ni pungufu kwa asilimia 0.21 ikilinganishwa na ya mwaka 2002. Hata hivyo, kiasi hiki ni asilimia 3.1 zaidi ikilinganishwa na lengo. Aidha, mwaka 2003, Shirika lilisafirisha jumla ya abiria 683,481 ikilinganishwa na abiria 684,796 waliosafirishwa katika kipindi cha mwaka 2002. Lengo la Shirika lilikuwa kusafirisha abiria 568,820. Utendaji huu ni asilimia 0.19 chini ya ule wa mwaka uliopita na ni asilimia 20.16 juu ya lengo. Shirika liliweza kukusanya jumla ya shilingi bilioni 61.5 katika mwaka 2003 ikilinganishwa na shilingi bilioni 59.9 zilizokusanywa katika kipindi cha mwaka 2002. Lengo lilikuwa ni kukusanya shilingi bilioni 60.0. Hivyo mapato yalizidi lengo kwa asilimia 2.5, ikiwa ni sawa na ziada ya shilingi bilioni 1.5. Katika kipindi cha mwaka 2004, Shirika la Reli Tanzania limejiwekea lengo la kusafirisha abiria 720,000 na shehena zenye uzito wa tani milioni 1.45.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, Shirika lilikabiliwa na changamoto ya upatikanaji wa vipuri na uchakavu wa injini, mabehewa, na sehemu za njia ya reli. Changamoto nyingine ilihusu wizi wa nguzo za simu na vifaa vya mawasiliano. Ili kukabiliana na changamoto hizi, *TRC* katika kipindi cha 2004/2005, inakusudia kutekeleza miradi 37 itakayogharimu shilingi bilioni 21.31. Miradi hii inajumuisha miradi 11 ya kuimarisha njia ya reli kwa gharama ya shilingi milioni 367, miradi 14 ya madaraja na makalavati kwa gharama ya shilingi millioni 491, miradi 2 ya simu na mawasiliano ukiwemo mradi wa kuendelea kuweka nyaya za kisasa za mawasiliano *(Optic Fibre)* kati ya Dodoma na Tabora, kwa gharama ya shilingi bilioni 19.5.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine itakayotekelezwa ni pamoja na miradi saba ya uwekaji umeme katika majengo ya stesheni, kwa gharama ya shilingi milioni 208 na mradi wa kutengeneza mabehewa 10 ya abiria yaliyopata ajali kati ya stesheni za Igandu

na Msagali mwezi Juni 2002 kwa gharama ya shilingi milioni 630. Miradi mingine ni pamoja na ununuzi wa vitendea kazi kwa gharama ya shilingi milioni 80, uimarishaji wa reli ya Manyoni - Singida, na upembuzi yakinifu kwa ajili ya ujenzi wa reli ya Isaka - Kigali (Rwanda) utakaogharimu dola za Marekani milioni 2.5 zitakazotolewa na Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB).*

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia iliweka lengo la kusafirisha tani 650,000 za mizigo na abiria 1,000,000 katika mwaka 2003/2004. Katika kipindi cha nusu mwaka cha 2003/2004, Mamlaka ilisafirisha tani 310,758 za mizigo ikilinganishwa na tani 344,394 zilizopangwa. Upungufu huo ni asilimia 9.8. Katika kipindi cha nusu mwaka cha 2003/2004, Mamlaka ilikadiria kusafirisha abiria 500,000 na iliweza kusafirisha abiria 572,603 na hivyo kuvuka lengo kwa asilimia 14.5. Mamlaka ina lengo la kusafirisha mizigo ya tani 650,000 na abiria milioni 1.2 katika kipindi cha mwaka 2004/2005. Kwa pamoja shughuli hizo zinatarajia kuiingizia Mamlaka mapato ya shilingi bilioni 28.7. Matumizi yatakuwa shilingi bilioni 27.3. Ongezeko hilo la mapato litatokana na Mamlaka kujiwekea mikakati madhubuti na ya makusudi yenye kulenga kusafirisha shehena zinazokwenda masafa marefu kwa kutumia uwezo wake.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ilikabiliana na changamoto mbali mbali ikiwa ni pamoja na uchakavu wa vifaa kama vile injini za treni, mabehewa ya mizigo na ya abiria. Aidha, hali ya miundombinu hususan upande wa Tanzania bado hairidhishi, hivyo kusababisha kuwepo vidhibiti mwendo *(Speed-Restrictions)* katika sehemu kadhaa. Mmomonyoko wa ardhi upande wa Tanzania, maeneo kati ya Mlimba na Makambako, umeendelea kuathiri kwa kiasi kikubwa ubora wa njia ya reli. Pamoja na hayo yote Mamlaka iliendelea kufanya jitihada za kutafuta fedha za uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, *TAZARA* inajizatiti kukabiliana na changamoto zilizopo. *TAZARA* inatayarisha mipango ya muda mrefu ya kukarabati reli, kukarabati vichwa vya treni *(engines),* kununua injini mbili, *reconditioned,* pamoja na vipuri vya kufufua vichwa vya treni ambavyo ni vibovu, kununua mabehewa mapya na vipuri vyake kutoka China na uboreshaji wa mawasiliano kwa njia ya mitambo ya *Micro-wave* na *HF Radio.*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, ajali katika njia za reli za *TRC* na *TAZARA*, ziliendelea kuathiri utendaji. Katika kipindi cha 2003/2004, ajali 199 zilitokea katika Shirika la Reli Tanzania, ikilinganishwa na ajali 215 zilizotokea mwaka 2002/2003. Idadi hii imekuwa ni pungufu kwa asilimia 7.4. Kupungua kwa ajali kunatokana na juhudi za kuimarisha usalama sehemu mbalimbali kwenye njia za reli, na ukarabati wa injini na mabehewa. Katika kipindi cha nusu mwaka wa 2003/2004, ajali za treni katika *TAZARA* zilikuwa 129 ikilinganishwa na ajali 149 zilizotokea katika kipindi kama hicho mwaka 2002/2003; sawa na upungufu wa asilimia 13.4. Pamoja na mafanikio haya kidogo, bado rekodi ya ajali sio nzuri. Juhudi zitaendelea kufanywa kuendelea kupunguza ajali.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, miundombinu na huduma za usafiri na uchukuzi kwa njia ya maji ziliendelea kukua na kuboreshwa zaidi ikilinganishwa na kipindi kama hiki kwa mwaka uliopita. Huduma hii imekuwa

ikitolewa na Mamlaka ya Bandari Tanzania *(THA),* Kampuni ya Huduma za Meli *(MSCL),* Kampuni ya Meli ya China na Tanzania *(SINOTASHIP),* pamoja na makampuni binafsi hasa yale yanayomiliki meli.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Bandari Tanzania ina wajibu wa kuanzisha, kuendeleza, kutunza, kusimamia na kuendesha kibiashara bandari zote Tanzania Bara. Mamlaka pia inawajibika kuhifadhi mazingira katika bandari zake na fukwe za bahari. Bandari za Mamlaka ni lango kuu la biashara ya nje kwa Tanzania na nchi jirani za Zambia, Malawi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Uganda, Rwanda na Burundi.

Mheshimiwa Spika, hali ya utendaji katika bandari kuu za Mamlaka kwa miezi minane ya mwanzo ya kipindi cha 2003/2004, ilikuwa ya mafanikio. Hadi kufikia Februari, 2003, shehena iliyohudumiwa na Mamlaka ilikuwa tani milioni 3.19 sawa na asilimia 70.9 ya lengo la mwaka mzima. Kitengo cha Kontena kinachoendeshwa na Kampuni binafsi ya *Tanzania International Container Terminal Services - TICTS* kilitarajia kuhudumia Makontena *(TEUs)* 198,676 kwa mwaka. Katika kipindi cha miezi minane ya mwaka 2003/2004, *TICTS* ilihudumia makontena 128,254 sawa na asilimia 64.5 ya lengo la mwaka mzima. Aidha, utekelezaji wa viwango vya ufanisi ukilinganishwa na malengo katika kipindi hicho ulikuwa wa kuridhisha.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa 2003/2004, *THA* ililenga kuingiza pato la shilingi bilioni 78.9 na matumizi ya shilingi bilioni 64.70 na hivyo kupata ziada ya shilingi bilioni 14.1. Katika kipindi cha miezi nane ya mwanzo (Julai, 2003 - Februari, 2004) mapato yamefikia shilingi bilioni 57.1 na matumizi ya shilingi bilioni 42.43 na hivyo kupata ziada ya shilingi bilioni 14.71. Kutokana na utendaji huu, kuna matumaini makubwa kwamba Mamlaka itafikia malengo yake kifedha.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2003/2004, Mamlaka iliendelea kuimarisha miundombinu katika bandari zake ili kuinua kiwango cha huduma na tija kwa kutekeleza miradi ya maendeleo na ununuzi wa vifaa mbalimbali vya kufanyia kazi. Miradi inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na ununuzi wa vifaa vya kuhudumia mizigo kwa bandari zote, ujenzi wa eneo la kuhudumia makontena Mtwara, upanuzi wa eneo la bandari ya Mtwara, ujenzi wa kituo cha kuongozea meli - Dar es Salaam. Miradi mingine ni uboreshaji wa eneo la matishari katika bandari ya Tanga, ukarabati wa sakafu za mabohari ya kuhifadhi mizigo, uboreshaji wa gati la mafuta la Kurasini *(KOJ),* matengenezo ya kingo za gati la kontena na maeneo ya kuhifadhia mizigo katika bandari ya Dar es Salaam, kuzuia mchanga kujaa katika bandari ya Lindi na upembuzi yakinifu wa gati la Mafia.

Mheshimiwa Spika, mafanikio haya ya Mamlaka ya Bandari Tanzania yameweza kufikiwa pamoja na kuwapo mazingira magumu ya biashara ya bandari. Mamlaka inakabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na kuzorota kwa hali ya kisiasa katika nchi zitumiazo bandari za Mamlaka hususan, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Burundi; na uwezo mdogo wa vyombo vya usafirishaji wa nchi kavu vya uondoshaji na uletaji wa bidhaa bandarini. Aidha, kuongezeka kwa ushindani wa kibiashara katika bandari za ukanda wa mashariki na kusini mwa Afrika, uchache wa maeneo huru ya

biashara *(EPZ)* na ukosefu wa karakana za kuhudumia meli, ni baadhi ya changamoto ambazo zinaendelea kuikabili Mamlaka.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka imechukua hatua za kuboresha huduma kwa kuhakikisha kuwa zinatolewa kwa wakati muafaka, kwa ubora na gharama nafuu, na kwa kutumia teknolojia inayofaa. Mamlaka inaendelea kushirikiana na wadau mbalimbali. Wadau hao ni pamoja na Shirika la Reli Tanzania *(TRC), Tanzania International Container Terminal Services (TICTS),* Mamlaka ya Reli ya Tanzania na Zambia *(TAZARA),* Shirika la Reli la Uganda *(URC),* Mamlaka ya Mapato*(TRA),* Kampuni za Wakala wa mizigo *(Clearing and Forwarding Companies),* pamoja na Wakala wa Meli *(Shipping Agencies).*

Mheshimiwa Spika, Mamlaka inaendelea kushiriki kikamilifu katika kuanzisha maeneo huru ya biashara *(EPZ)* ili kuchochea maendeleo ya shughuli zenye kuongeza thamani ya maliasili zetu. Mamlaka pia inashirikiana na wadau wa nchi jirani na jumuiya nyingine kama vile Jumuiya ya Maendeleo ya nchi za Kusini mwa Afrika *(SADC),* Jumuiya ya Afrika Mashariki *(EAC)* na kushiriki kwenye mpango wa *NEPAD* katika kubuni na kutekeleza miradi kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, kwa kipindi cha 2004/2005, Mamlaka imejiwekea lengo la kuhudumia jumla ya tani za mizigo milioni 4.81 kupitia katika bandari zake zote nchini. Kitengo cha kontena kina lengo la kuhudumia makontena 204,243 ambayo ni zaidi ya asilimia 20.8 ikilinganishwa na lengo la mwaka jana. Aidha, Mamlaka inatarajia kuingiza pato la jumla la shilingi bilioni 86.417. Pato la shilingi bilioni 60.7 litatokana na shughuli zinazoendelea chini ya Mamlaka, shilingi bilioni 19.0 kama wharfage itakayokusanywa na *TICTS* kama wakala wa Mamlaka, na pato la shilingi bilioni 6.8 litatokana na kitengo cha Kontena kama ushuru wa pango na mrahaba.

Mheshimiwa Spika, mpango wa maendeleo wa Mamlaka kwa kipindi cha 2004/2005, unalenga katika kuboresha maeneo ya kazi, ili kulinda ubora na ufanisi wa rasilimali iliyopo. Aidha, Mamlaka inalenga kuinua uwezo wa bandari kwa kukarabati na kubadilisha vifaa na maeneo ya kuhudumia meli na mizigo na pia kuendeleza utekelezaji wa miradi iliyoanza, na ile ambayo ilitarajiwa kuanza katika kipindi cha mwaka 2003/2004. Mpango huu unatarajiwa kugharimu shilingi bilioni 19.2. Kati ya hizo shilingi bilioni 12.9 au asilimia 67.2 ni fedha za kigeni.

Mheshimiwa Spika, kutokana na umuhimu wa bandari kuwa katika mfumo unaowiana wa uchukuzi, katika kipindi cha 2004/2005, bandari zote zilizoko katika maziwa zitakabidhiwa kwa Mamlaka ya Bandari Tanzania ili kuziendeleza na kuziboresha. Mamlaka ya Bandari inatarajia kuziweka bandari hizi katika hali ya kisasa kwa kuboresha miundombinu na vitendea kazi vyake.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Meli ya Serikali ya China na Tanzania *(SINOTASHIP)* inamilikiwa kwa pamoja kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Jamhuri ya Watu wa China. Kampuni ina meli tatu zinazosafiri masafa

marefu baharini. Meli hizi kwa pamoja zina uwezo wa kubeba jumla ya tani 46,645 kwa wakati mmoja.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, meli za *SINOTASHIP* zilifanya safari 25 ikilinganishwa na safari 23 zilizokuwa zimepangwa. Katika safari hizo jumla za tani 253,241 za shehena zilisafirishwa, ambazo ni pungufu kwa asilimia 49.15 ikilinganishwa na tani 497,979 zilizosafirishwa mwaka 2002/2003. Kadhalika shehena hiyo inaonyesha ongezeko la asilimia 1.30 ikilinganishwa na lengo la tani 250,000 katika mwaka wa 2003. Mapato ya Kampuni kwa mwaka 2003 yalikuwa dola za kimarekeni milioni 6.4 ambapo Kampuni ilipata faida ya dola 310,000. Aidha, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Kampuni imejiwekea lengo la kusafirisha tani 300,000 kwa kufanya safari 24 na kupata faida ya dola 450,000. Malengo haya yanazingatia changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika kipindi kilichopita.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2003/2004, Kampuni ilikabiliana na changamoto mbali mbali. Hizi ni pamoja na; uhaba wa mizigo yenye kuingiza mapato makubwa kwa Kampuni; kushuka kwa nauli za usafirishaji; na ushindani mkubwa katika soko la dunia la shehena za meli. Aidha, hali duni kiuchumi ya Afrika ya Mashariki na Kati iliathiri upatikanaji wa shehena. Eneo hili ni muhimu sana kibiashara kwa *SINOTASHIP*. Gharama za kununua vipuri, mafuta ya kuendeshea meli pamoja na nyenzo nyingine, ziliendelea kupanda. Hali hii iliongeza gharama za uendeshaji. Ili kupunguza gharama hizi, juhudi mbalimbali zilifanyika zikiwa ni pamoja na kupeleka wawakilishi kwenda kwenye bandari zenye tija duni, ili kusimamia na kuhimiza kazi za upakiaji na upakuaji wa mizigo kwenye meli za Kampuni.

Aidha, kwa kipindi cha miezi sita iliyopita kampuni imefanya bidii kubwa kukamilisha maandalizi yatakayoiwezesha kukidhi kanuni na taratibu za mkataba wa kimataifa wa usalama wa meli na bandari ujulikanao kama *International Ship and Port Facility Security (ISPS) Code,* ambao unaanza kutumika mwezi Julai, 2004. Taratibu hizi zitaendelea kuimarisha biashara ya usafirishaji wa shehena.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2000, Bunge lako Tukufu lilibadilisha Sheria Na. 3 ya mwaka 1981 iliyoanzisha Shirika la Kudhibiti Shehena *(TCFB)* ili kulipa Shirika uwezo zaidi kiutendaji. Majukumu ya Shirika ni pamoja na kusimamia mwenendo wa soko huria la usafirishaji kwa njia ya maji. Katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Shirika liliendelea na uratibu, usimamizi na udhibiti wa gharama na mwenendo wa soko huria wa usafirishaji majini. Shirika liliendelea kuweka mazingira mazuri ya kuwavutia wafanyabiashara wa usafirishaji kwa njia ya maji. Hii ni pamoja na kufuatilia kwa karibu, taratibu na uharaka wa uondoaji shehena kutoka bandari za Dar es Salaam, Tanga, Mtwara na Malindi - Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa 2003/2004, Shirika kwa kushirikiana na wadau, lilisimamia majadiliano juu ya kusudio la makampuni ya uwakala wa meli kuongeza ada zao. Majadiliano yaliendeshwa kibiashara na kwa mafanikio makubwa kwa kuzingatia hali ya sasa ya uchumi wa soko. Lengo ni kuwavutia

wawekezaji, kutokuwabebesha gharama kubwa wasafirishaji wa shehena na vile vile kuziwezesha bandari zetu kumudu ushindani dhidi ya bandari za nchi nyingine.

Aidha, wadau wa sekta ya usafirishaji majini walikubaliana kuwepo kwa viwango vya juu vya ada *(Maximum Levels of Fees)* ili kuhimiza ushindani miongoni mwa makampuni ya uwakala wa meli. Mawakala watakuwa huru kutoza kiasi chochote ili mradi wasizidi kiwango kilichokubalika. Viwango vya ada vilivyotozwa hapo zamani vilikuwa ni dola za Kimarekani 25. Viwango vilivyopendekezwa na makampuni ya Uwakala wa Meli ni kati ya dola za Kimarekani 40 na 52. Makubaliano yaliyofikiwa ni kwamba, wakala wa meli watoze dola za kimarekani 36.

Mheshimiwa Spika, katika jukumu la kuratibu usafirishaji wa shehena za nchi Jirani zinazotumia bandari za Tanzania, Shirika lilihakikisha kwamba shehena zinasafirishwa kwa ufanisi na gharama nafuu na bila vikwazo visivyokuwa vya lazima. Shirika kwa kushirikiana na Baraza la Mawasiliano la Kisekta *(Shipping Industry Consultative Forum),* lilifanya utafiti wa kuboresha usafirishaji wa shehena. Utafiti huo umeonyesha kuwa wasafirishaji wa shehena walikuwa wakilalamikia utendaji kazi wa vituo vya mizani kwenye barabara zetu kuu. Ili kulipatia ufumbuzi suala hili, Shirika liliitisha kikao cha Wadau husika ili kutatua tatizo hili. Kikao cha wadau kilikubaliana kwamba Mamlaka Kuu ya Leseni za Usafirishaji *(Central Transport Licensing Authority)* wahakikishe kuwa wataalamu wao wanatoa mafunzo ya jinsi ya kusoma na kuhakiki uzito wa magari kabla ya kuyapa leseni za usafirishaji. Vile vile ilikubalika kuwa Wakala wa Barabara *(TANROADS)* waendelee kutangaza kwenye vyombo vya habari mambo ambayo muagizaji wa magari mazito anatakiwa kuzingatia kabla ya kuyaagiza. Ni matarajio yangu kwamba, kama utaratibu huu utafuatwa kwa makini, vituo vya mizani havitakuwa vikwazo tena kwa usafirishaji kwa njia ya barabara.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Kudhibiti Shehena *(TCFB)* linatarajia kupata Shilingi bilioni 2.23 kwa kipindi cha mwaka 2003/2004, ikilinganishwa na Shilingi bilioni 2.21 za mwaka 2002/2003, ikiwa ni ongezeko la asilimia 5. Kati ya hizo shilingi milioni 610.56 ni faida kabla ya kodi ya mwaka 2003/2004, ikilinganishwa na Shilingi milioni 539.78 kwa mwaka 2002/2003. Faida hii ni sawa na ongezeko la asilimia 13. Shilingi bilioni 2.45 zinatarajiwa kupatikana kama mapato kwa mwaka 2004/2005 ambalo ni ongezeko la asilimia 10. Katika kipindi hiki Shirika limo katika kipindi cha mpito kuelekea kuundwa kwa Mamlaka ya Udhibiti wa Usafirishaji wa Nchi Kavu na Majini *(SUMATRA)*. Majukumu ya *TCFB* na ya Mamlaka Kuu ya Leseni za Usafirishaji yanatarajiwa kuhamishiwa kwenye chombo hiki kipya. Wafanyakazi wa *TCFB* hawatapoteza ajira zao wala mafao. Ajira yao itaendelezwa katika *SUMATRA* na mafao yao kuhamishiwa *SUMATRA*.

Mheshimiwa Spika, usafiri katika mikoa ya kusini ya Lindi na Mtwara umeendelea kuimarika. Vile vile uboreshaji wa miundo mbinu ikiwa ni pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa Daraja la Mkapa, kumewezesha wananchi wa mikoa hiyo kuwa na uchaguzi wa kutumia usafiri wa meli, barabara au ndege. Hali hii imeongeza ushindani uliosababisha nauli kubakia kuwa za wastani. Aidha, uhaba wa shehena, idadi ndogo ya watumiaji wa usafiri wa meli pamoja na ushindani vimesababisha meli kubwa

ya *FB Santorini 3,* kushindwa kuendelea na utoaji huduma za usafiri katika mikoa ya kusini na hivyo kujiondoa. Hata hivyo Serikali itaendelea kuweka mazingira mazuri ili wenye meli wapeleke huduma katika maeneo ya kusini.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya Huduma za Meli *(Marine Services Company Limited - MSCL),* iliendelea katika kutoa huduma za uchukuzi kwenye maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Sekta binafsi nayo imeendelea kujiimarisha katika kutoa huduma kwenye maziwa haya. Mpaka sasa kuna zaidi ya meli 15 zinazomilikiwa na watu binafsi ambazo zinafanya kazi sambamba na meli za *MSCL.* Kampuni ya *Lake Fast Ferries* wamenunua na kuleta meli mbili za mwendo wa kasi zenye uwezo wa kubeba abiria 90 kwa kila meli ambazo zitasafiri kati ya Mwanza - Bukoba. Meli hizo ambazo zimeshafika Dar es Salaam zitasafirishwa hadi Mwanza. Natarajia meli hizi zitaanza kazi mwezi Julai, 2004. Serikali kwa upande wake itaendelea kuandaa mazingira mazuri yanayovutia wawekezaji katika sekta ya usafiri wa majini kwa nia ya kuboresha uchukuzi na mawasiliano ili wananchi waishio kandokando ya maziwa wapate fursa ya kujiendeleza kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, ili kuimarisha ubora wa huduma za uchukuzi hasa kwa wananchi waishio kando kando ya maziwa makuu, Wizara iliendelea na ujenzi wa magati kwenye maeneo muhimu kama Bukondo, Shirati, Nansio, Kinesi na maandalizi ya ujenzi wa bandari za Kasanga, na Mbamba bay. Tunaamini kwamba hatua hiyo itawawezesha wananchi katika maeneo hayo kuinua shughuli za kiuchumi ambazo ni pamoja na uvuvi, biashara na kilimo. Katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Serikali ilitoa jumla ya shilingi milioni 250 kwa ajili ya mradi wa magati ambao uliendelea kutekelezwa chini ya usimamizi wa Kampuni ya Huduma za Meli. Ukarabati wa Magati ya Bukondo, Shirati, Nansio (Ukerewe) na Kinesi ambayo yote yako katika Ziwa Victoria unaendelea vizuri. Matayarisho ya ukarabati wa gati la Kasanga katika Ziwa Tanganyika, yanaendelea. Ukarabati wa Gati la Shirati umekamilika kwa asilimia 95 na limeanza kutumika. Kazi ya ukarabati wa gati la Bukondo imekamilika kwa asilimia 85 na limeanza kutumika upande mmoja. Kuhusu gati la Kinesi, kazi imekamilika kwa asilimia 90 na limeanza kutumika pia.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2004/2005, Serikali inatarajia kukamilisha kazi zilizobakia za ujenzi wa magati ya Kinesi, Bukondo, Nansio (Ukerewe) na Shirati, na kuanza ukarabati wa gati la Kasanga na ujenzi wa gati za Karema katika Ziwa Tanganyika, Kiamkwikwi, Maisome na Nkome katika Ziwa Victoria. Aidha, maandalizi ya ujenzi wa gati la Manda na ujenzi wa gati la Mbamba Bay, katika Ziwa Nyasa yanafanyika. Jumla ya shilingi milioni 250 zimetengwa kwa kazi hizi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Kampuni ya huduma za Meli *(Marine Services Company Limited),* iliendelea kutoa huduma za uchukuzi wa abiria na mizigo katika maziwa ya Victoria, Tanganyika na Nyasa. Jumla ya tani 143,751 za mizigo zilisafirishwa. Abiria waliosafirishwa ni 347,564. Kiasi hiki ni kidogo ikilinganishwa na tani za mizigo 144,473 na abiria 370,588 waliosafirishwa mwaka 2002. Kiwango hicho cha utekelezaji kilikuwa chini kwa asilimia 6 kwa upande wa mizigo na asilimia 11 kwa upande wa abiria. Aidha, kampuni iliweza kukusanya jumla ya shilingi

bilioni 4.45 ukilinganisha na shilingi bilioni 4.0 zilizokusanywa mwaka 2002. Lengo lilikuwa ni kukusanya shilingi bilioni 4.75. Lengo halikufikiwa kwa asilimia 6.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ilikabiliwa na changamoto mbalimbali zilizosababisha kutofikiwa kwa malengo yaliyowekwa. Changamoto hizo ni pamoja na uchakavu wa meli, hali mbaya ya kisiasa inayoendelea katika nchi za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo *(DRC)* na Jamhuri ya Burundi. Hali hii imesababisha kupungua kwa shehena na abiria kupitia bandari zetu. Aidha, ajali ya *MV Victoria* iliyotokea eneo la Lubembe karibu na *Kemondo Bay* ilisababisha meli kusimama kwa muda mrefu kwa ajili ya matengenezo na hivyo kuathiri utendaji wa Kampuni. Uchunguzi uliofanywa kuhusiana na chanzo cha ajali hii ulibaini kuwa ajali hiyo ilisababishwa na uzembe wa wafanyakazi wa meli hiyo. Wafanyakazi waliohusika na ajali hiyo walichukuliwa hatua za kinidhamu ikiwa ni pamoja na kufukuzwa kazi na wengine kushushwa daraja au cheo.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *MSCL* inafanya kila jitihada katika kuendelea kuzifanyia matengenezo meli mara kwa mara ili kuongeza ufanisi. Kampuni inaendelea kuwaelimisha wafanyakazi wanaoendesha meli juu ya umuhimu wa kuwa waangalifu ili kuepukana na ajali zisizo za lazima. Katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Kampuni ya Huduma za Meli *(MSCL)* imelenga kusafirisha jumla ya tani 142,594 za mizigo na abiria 396,629. Kampuni inategemea kupata jumla ya shilingi bilioni 4.33 kwa kutoa huduma hizo.

Mheshimiwa Spika, ili kuongeza usalama kwa abiria pamoja na mizigo yao, Wizara inaendelea kusimamia usalama wa vyombo vya usafiri majini. Pamekuwepo na jitihada za kuweka tahadhari za uharibifu wa mazingira katika utoaji wa huduma hii. Tahadhari hizo ni pamoja na maandalizi ya kukabiliana na umwagikaji wa mafuta baharini. Katika kipindi cha mwaka 2002/2003, yalifanyika majaribio ya *Oil Spill Contigency Plan* na mafunzo ya namna ya kukabiliana na janga la uchafuzi wa mazingira unaotokana na kumwagika kwa mafuta. Wizara iliandaa mafunzo hayo kwa kushirikiana na wataalam wa Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Majini *(IMO).* Mafunzo hayo yalifanyika Bagamoyo, tarehe 15 hadi 19 Desemba, 2003. Washiriki wa mafunzo hayo walitoka katika makampuni ya mafuta, Mamlaka ya Bandari na Idara za Serikali.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kuwapongeza wananchi wanaopakana na maeneo ya maziwa na bahari kwa kuendelea kushirikiana na wakaguzi mbalimbali wa vyombo vya usafiri wa majini na hivyo kupunguza kiwango cha ajali. Aidha, kutokana na kuongezeka kwa vitendo viovu vya kigaidi na utekaji nyara vyombo vya uchukuzi na vitendo vinavyotishia usalama wa vyombo majini, Wizara yangu imejiandaa kutekeleza mikataba na taratibu mbalimbali zinazotolewa na Shirika la Kimataifa la Usafiri wa Majini *(The International Maritime Organization -IMO)*, ikiwa ni pamoja na suala la *International Ship and Port Security Facility Code (ISPS ).* Aidha, Wizara kwa kushirikiana na wataalamu wa *IMO*, tarehe 23 -27 Februari, 2004, iliendesha warsha Mjini Tanga, kwa lengo la kutafakari namna ambavyo Tanzania itaboresha huduma za ulinzi na usalama katika bandari zetu. Serikali inaendelea na taratibu za kumpata mfadhili wa kuwezesha utekelezaji wa mipango ya usalama *(Security Plan)* katika bandari ya Dar es Salaam, na bandari za Tanga, Mtwara na Zanzibar. Maandalizi

ya Kanuni *(Regulations)* za kusimamia utekelezaji wa *ISPS* yamekamilika na yatatangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, ili kuweza kusimamia suala zima la usalama wa vyombo vya majini, mwaka 2003/2004, nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Wizara inaendelea na maandalizi ya kuanzisha Mamlaka ya kusimamia usalama wa vyombo hivyo. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa sasa usimamizi wa usalama wa vyombo vya majini utafanywa na Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Nchi kavu na Majini *(SUMATRA).* Mapendekezo ya kurekebisha Sheria ya *SUMATRA* ili kuzingatia jukumu hilo yamepitishwa na Bunge lako Tukufu hivi karibuni. Aidha, Sheria ya mwaka 1967 iliyokuwa inasimamia Usafiri wa Majini *(The Merchant Shipping Act, 1967)* ilifutwa na Sheria mpya *(The Merchant Shipping Act, 2003)* ilipitishwa na Bunge lako Tukufu mwishoni mwa mwaka 2003. Sheria hii itaanza kutumika baada ya kutangazwa kwenye Gazeti la Serikali.

Mheshimiwa Spika, Sera ya Taifa ya Uchukuzi, inasisitiza umuhimu wa kuimarisha, kurahisisha, na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za usafiri nchini. Azma hii itafanikiwa kupitia mpango wa kanda za maendeleo *(Development Corridors).* Kanda hizi ni pamoja na Ukanda wa Maendeleo wa Mtwara *(Mtwara Development Corridor),* ambao unaanzia bandari ya Mtwara hadi Mbamba Bay na kuunganisha mikoa kadhaa ya kusini ambayo ni Mtwara, Lindi na Ruvuma na mikoa ya nyanda za juu kusini. Ukanda huu unazihusisha nchi za Tanzania, Msumbiji, Malawi na Zambia. Ukanda wa Dar es salaam unaanzia Bandari ya Dar es Salaam hadi Tunduma-Mbeya. Ukanda wa Kati unaanzia Bandari ya Dar es Salaam na kuishia Kigoma/Mwanza. Ukanda huu unaiunganisha Tanzania na nchi jirani za Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo *(DRC),* Rwanda, Burundi na Uganda. Ukanda wa Tanga unaanzia bandari ya Tanga na unaishia Ziwa Victoria na kuunganisha Tanzania na nchi za *DRC,* Rwanda, Burundi, Uganda na Kenya.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kuwa kanda hizi ni kiungo cha maeneo ya nchi yetu, pia zinaiunganisha Tanzania na majirani zake. Uwekezaji katika maeneo ya kanda hizi siyo tu utaendelea kuimarisha biashara kati ya nchi yetu na nchi jirani, bali pia utafanya wawekezaji kuvutiwa na soko kubwa la bidhaa na huduma zitakazozalishwa. Hatua za utekelezaji kwa sasa hivi ni kwamba kwa upande wa ukanda wa Mtwara mpango wa utekelezaji *(Business Plan)* unakamilishwa. Hatua nyingine ni kuwahamasisha wawekezaji kuwekeza katika maeneo mbali mbali kama vile barabara, reli, usafiri kwa njia ya maji, usafiri wa anga, kilimo, utalii na viwanda.

Mheshimiwa Spika, kuna mpango wa kuendeleza bandari ya Mtwara. Fidia imetolewa kwa wakazi waliokuwa kwenye maeneo yanayohitajika. Upo mpango wa kuanzisha Maeneo ya Biashara huru *(EPZ)* kwenye bandari na kiwanja cha ndege cha Mtwara. Upembuzi yakinifu wa awali unaendelea *(pre-feasibility study)* kabla ya kuendelea na hatua ya upembuzi yakinifu kuhusu mradi huo.

Mheshimiwa Spika, bandari za *Mbamba-bay* na *Nkata-bay* zitaendelezwa. Makubaliano ya awali *(MOU)* yalisainiwa mwezi Oktoba, 2003 kati ya Serikali za

Tanzania na Malawi kwa ajili ya kuweka kivuko *(Ferry)* kati ya bandari hizi. Maombi ya mkopo yalishapelekwa Benki ya Maendeleo ya Afrika Kusini *(Development Bank of Southern Africa- The African Partner Unit - (DBSA-APU)* na Saudi Arabia kwa ajili ya upembuzi yakinifu *(feasibility study)* wa mradi huo. Inatarajiwa kuwa baada ya upembuzi yakinifu kukamilika sekta binafsi itaachiwa jukumu la kuendesha kivuko hicho.

Mheshimiwa Spika, ukanda wa Dar es Salaam unalenga kuiunganisha bandari ya Dar es salaam na nchi za Malawi, Zambia na *DRC*. Aidha, ukanda huo unalenga kuboresha utumiaji wa reli ya *TAZARA* na barabara ya *TANZAM* na bomba la Mafuta la *TAZAMA* katika kusafirisha shehena ya nchi hizi. Kamati ya pamoja ya kuratibu utekelezaji wa shughuli za ukanda huo imeundwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu, ukanda wa maendeleo wa Kati, hatua za kumpata Meneja wa mradi zinakamilishwa kati ya Tanzania na Rwanda. Kwa ujumla uwekezaji katika kanda hizi kutaiwezesha Tanzania kutumia nafasi yake ya kijiografia na kuendeleza uchumi wake kwa kasi zaidi na kuendeleza wajibu wake wa kuzihudumia nchi zisizo na bandari.

Mheshimiwa Spika, sekta ndogo ya usafiri wa anga imeendelea kukua katika kipindi cha mwaka 2003/2004. Makampuni ya ndege ya *ATCL* na Precision Air yaliendelea kujiimarisha katika kutoa huduma ndani na nje ya nchi na hivyo kuwezesha abiria kusafiri kwa urahisi zaidi. Katika kipindi hicho, makampuni 29 ya ndege yalipewa leseni ikilinganishwa na makampuni 27 katika kipindi cha mwaka 2002/2003. Idadi ya abiria waliosafiri ndani na nje ya nchi iliongezeka kutoka abiria milioni 1.49 mwaka 2002/2003 hadi kufikia abiria milioni 1.88 mwaka 2003/2004 ambalo ni ongezeko la asilimia 25.3. Aidha, idadi ya abiria waliosafiri ndani na nje ya nchi kupitia Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Dar es Salaam iliongezeka kutoka abiria 707,997 mwaka 2002/2003 hadi kufikia abiria 898,864 mwaka 2003/2004, ongezeko ambalo ni asilimia 27. Idadi ya abiria waliosafiri ndani ya nchi katika kipindi cha mwaka 2003/2004 iliongezeka kwa asilimia 26.2, kutoka abiria 771,241 mwaka 2002/2003 hadi kufikia abiria 973,262. Safari za ndege za kimataifa kupitia viwanja vyetu zilipungua kutoka safari 20,341 mwaka 2002/2003 hadi kufikia safari 20,060 katika kipindi cha mwaka 2003/2004. Aidha, safari za ndege za kimataifa na za ndani ziliongezeka kutoka safari 136,975 mwaka 2002/2003 hadi kufikia safari 158,297, sawa na ongezeko la asilimia 15.6.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Mamlaka ya Usalama wa Usafiri wa Anga iliendelea kutoa huduma za uongozaji wa ndege katika viwanja 13. Ilitoa huduma kwa saa 24 katika viwanja vya Dar es Salaam, Kilimanjaro na Zanzibar; saa 17 katika kiwanja cha Mwanza na saa 12 katika viwanja vya Dodoma, Arusha, Kigoma, Tabora na Pemba. Viwanja vya Mtwara, Mbeya, Iringa, Tanga na Songea vilitoa huduma kwa saa 8.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana katika Bunge lako Tukufu nilieleza kuhusu kuanzishwa kwa kituo cha pamoja cha kuongozea ndege, utafutaji wa ndege zilizopotea

au kupata ajali *(Search and Rescue Co-ordination Services),* huduma za ramani *(AIS MAP facilities and services)* na matumizi ya pamoja ya vyuo vya mafunzo katika eneo la Afrika ya Mashariki *(East Africa Civil Aviation Safety Project)*. Mradi huu uko chini ya Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Sehemu ya kwanza ya mradi inahusu *Upper Air Space.* Sehemu ya pili ya mradi inahusu *Harmonized Safety Oversight.* Wakandarasi wanaohusika na utekelezaji wa mradi wanategemewa kuanza kazi rasmi mwezi huu wa Julai, 2004. Kazi hii itachukua miezi 12 kukamilika.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003/2004, Mamlaka iliendelea kuchangia Mfuko wa Usalama wa Usafiri wa Anga *(Aviation Security Fund).* Mfuko huu ulianzishwa mwaka 2002/2003, kwa nia ya kuboresha usalama katika viwanja vya ndege kwa lengo la kukabiliana na ugaidi. Vifaa vimenunuliwa na mafunzo kwa maofisa usalama wa viwanja na anga yamefanyika kupitia mfuko huu. Jumla ya maofisa 300 wamepata mafunzo mbalimbali. Uzio utajengwa kuzunguka viwanja vya ndege vya Mtwara na Kigoma.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Kimataifa la Usalama wa Anga *(ICAO)* wanashauri kuwepo mazoezi ya utafutaji na uokoaji *(Search and Rescue)* wa ndege iliyopotea na kuanguka kila baada ya miaka miwili. Kutokana na gharama kubwa za mazoezi hayo, utekelezaji wake unakuwa mgumu kwa nchi nyingi za Kiafrika. Katika mwaka 2003/2004, kwa mara ya kwanza, kwa msaada wa Shirika la Misaada la Marekani *(USAID)* kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu tuliweza kuendesha zoezi la utafutaji na uokoaji wa ndege. Zoezi la uokoaji mara nyingi linahitaji ushirikiano na nchi za jirani hasa inapobidi kutoa au kupata msaada wa vifaa vya uokoaji. Hata hivyo mipango inafanyika ili tuwe na mikataba ya ushirikiano na nchi zote tunazopakana nazo.

Mheshimiwa Spika, miradi itakayoendelea kutekelezwa katika kipindi cha 2004/2005 ni pamoja na ununuzi na ufungaji wa meza za kisasa za waongoza ndege *( ATC Consoles)* katika viwanja vya Songea, Mtwara na Kigoma na ununuzi na ufungaji wa vifaa vya redio vitakavyotumika kuchunguza hali ya utendaji wa mitambo ya kuongozea ndege katika viwanja vya Arusha, Kigoma na Tabora. Ununuzi na ufungaji wa vifaa vya redio za dharura katika viwanja vya Songea, Dodoma na Kigoma ni miongoni mwa miradi inayoendelea. Miradi mingine ni ile ya kufunga mtambo wa usambazaji wa mawimbi ya redio mkoa wa Ruvuma na kufunga mitambo ya nguvu ya mionzi ya jua kwa ajili ya umeme wa akiba katika viwanja vya Songwe na Tabora.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, wahitimu 12 wa Chuo Kikuu waliajiriwa kama waongoza ndege *(Air Traffic Controllers).* Wahitimu wengine 15 kutoka Chuo Kikuu wameanza mafunzo na wanatarajiwa kuajiriwa katika kipindi cha mwaka 2004/2005. Aidha, Mamlaka ilihuisha mpango wa mafunzo ya marubani ili kukabiliana na upungufu wa marubani nchini. Marubani watano akiwemo mwanamke mmoja wamepelekwa Afrika ya Kusini kwa mafunzo ya mwaka mmoja. Wahandisi wawili akiwemo pia mwanamke mmoja, wako Ethiopia kwa mafunzo ya miaka miwili katika fani ya matengenezo ya ndege *(Aircraft Maintenance Engineering).*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2003/2004, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania *(TAA)* iliendelea na kazi yake ya kuhudumia viwanja vya ndege hapa nchini. Matengenezo mbalimbali ya viwanja yalifanyika ili kuwezesha ndege kutua na kuruka kwa usalama. Aidha, matengenezo makubwa ya miundombinu na uboreshaji wa mitambo yanafanyika Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Dar es Salaam *(DIA).*

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imekamilisha mradi mkubwa wa ukarabati wa umeme *(Power Supply System)* katika kiwanja cha Kimataifa cha Dar es Salaam *(DIA).* Aidha, kiwanja hicho kilifanyiwa matengenezo katika sehemu za maegesho na barabara ya kuruka na kutua ndege pamoja na viungio vyake. Vivuko vitano vya abiria kutoka kwenye ndege hadi jengo la abiria vimekarabatiwa. Mamlaka inaendelea na awamu ya kwanza ya ukarabati mkubwa wa mitambo ya viyoyozi. Taratibu zinafanyika za ununuzi na usimikaji wa mtambo kwa ajili ya check in, boarding na kutoa taarifa za mizigo ili kuongeza ufanisi na usalama. Mtambo huu unaitwa *Common User Terminal Equipment (CUTE).*

Mheshimiwa Spika, Kiwanja cha ndege cha Mwanza kimefanyiwa matengenezo mbalimbali ikiwa ni pamoja na uwekaji taa kwenye viungio kuanzia kwenye barabara ya kurukia na kutua ndege kuelekea kwenye maegesho ya ndege. Hii ni kuwezesha ndege kutumia njia hizo usiku kwa usalama. Aidha, Mamlaka imekamilisha usanifu wa jengo jipya la abiria na mizigo pamoja na hangar ya kufanyia matengenezo ya ndege. Kiwanja cha Mwanza kinajengewa uzio kwa ajili ya kuimarisha usalama. Katika kipindi cha 2004/2005, kiwanja cha Ndege cha Mwanza kitafanyiwa ukarabati kwenye sehemu za maegesho kwa ajili ya ndege za mizigo na viungio vyake pamoja na sehemu za kugeuzia ndege.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kufanya ukarabati na uimarishaji wa njia ya kurukia na kutua ndege kwenye kiwanja cha ndege cha Arusha. Mamlaka inajenga uzio katika kiwanja hiki. Mamlaka pia imekamilisha ramani ya usanifu ya kiwanja cha Arusha *(Master Plan).* Aidha, Wizara imekamilisha taratibu za upatikanaji wa eneo kubwa zaidi kwa ajili ya uendelezaji wa kiwanja hicho.

Mheshimiwa Spika, kuhusu kiwanja cha ndege cha Mtwara, kazi iliyofanyika inahusu matayarisho ya ramani sanifu *(Master Plan),* usanifu wa jengo la kuongozea ndege na ukumbi wa watu mashuhuri *(VIP Lounge),* usanifu wa ukumbi wa kuondokea abiria na matengenezo ya kurukia na kutua ndege. Kipindi cha 2004/2005, Mamlaka imepanga kuendelea na matengenezo ya barabara ya kurukia na kutua ndege, ujenzi wa uzio na upanuzi wa ukumbi wa watu mashuhuri.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa kiwanja kipya cha ndege cha Songwe (Mbeya) unaendelea. Waliokuwa na nyumba na mashamba kwenye eneo la kiwanja wamefidiwa. Kazi ya kusawazisha eneo la kiwanja imekamilika. Ujenzi wa msingi, nguzo na paa la jengo la abiria umekamilika. Kazi za kutandaza mfumo wa maji pamoja na nguvu za umeme zinaendelea. Zabuni ya ujenzi wa awamu ya pili ya jengo la abiria, ujenzi wa kituo cha kuongozea ndege na kituo cha hali ya hewa, umetolewa kwa mkandarasi.

Zabuni nyingine ni ile ya ujenzi wa njia ya kuruka na kutua ndege. Zabuni hii nayo imetolewa. Mwaka 2004/2005, Mamlaka itaendeleza kiwanja cha Songwe kwa kusimamia ujenzi wa awamu ya pili ya jengo la abiria pamoja na majengo mengine ya huduma, na ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua ndege pamoja na viungio na maegesho yake.

Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha na kuboresha viwanja vingine, matengenezo yalifanyika kwenye viwanja vya Musoma, Tabora, Bukoba, Ziwa Manyara, Shinyanga, Lindi na Dodoma. Matengenezo hayo yalihusu barabara za kurukia na kutua ndege. Aidha, Mamlaka inaendelea na juhudi za kuimarisha usalama hasa katika viwanja vya *DIA,* Arusha, Mtwara, Mwanza, Bukoba, Tabora, Kigoma na Dodoma. Mamlaka pia inaendelea na ujenzi wa uzio katika viwanja vya Mtwara, Kigoma, Mafia, Moshi, Bukoba na Dodoma.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 nilitoa taarifa kwamba Wizara ilikuwa inafanya uchambuzi wa kubaini njia mbalimbali zinazofaa katika kushirikisha sekta binafsi katika uendeshaji wa viwanja vya ndege. Katika mwaka wa fedha 2004/2005, Serikali itakamilisha uchambuzi huu na kubaini njia bora na sahihi ya kufuata katika kushirikisha sekta binafsi. Kazi hiyo, itakwenda sambamba na kufanya mapitio ya Sheria ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege ili iweze kutoa fursa na kuvutia wawekezaji wa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, huduma za matengenezo na uendeshaji wa viwanja vya ndege zitaendelea kutolewa na Mamlaka kwa viwango bora zaidi, upatikanaji wa fedha ukizingatiwa. Viwanja vinavyohudumia ndege za abiria zenye ratiba *(Scheduled and Regular Flights)* kama vile Tabora, Kigoma, Bukoba, Ziwa Manyara, Mafia, Moshi, Shinyanga, Tanga na Lindi vitaendelea kufanyiwa matengenezo ili kuboresha utoaji huduma.

Mheshimiwa Spika, baada ya kubinafsishwa kwa Shirika la Ndege Tanzania na kuanzishwa kwa Kampuni ya Ndege Tanzania *(ATCL)* mwezi Desemba 2002, Kampuni hii imeendelea kutoa huduma za usafiri wa anga ambazo zimeleta mabadiliko makubwa ya kiutendaji. Mwaka 2003/2004 kampuni iliweza kusafirisha jumla wastani wa abiria 17,000 kwa mwezi ikilinganishwa na abiria 6,500 kwa mwezi ambao walisafirishwa katika mwaka 2002 kabla Shirika kubinafsishwa. Mapato kwa mwezi yalikua kwa zaidi ya mara mbili kutoka dola la Kimarekani milioni 1.2 mwezi Desemba, 2002 hadi milioni 2.8 mwezi Novemba, 2003. Vituo vya safari za ndege *(destinations)* viliongezeka zaidi ya mara mbili kutoka 7 mwaka 2002/2003 hadi 15 mwaka 2003/2004. Idadi ya safari kwa wiki iliongezeka zaidi ya mara tatu kutoka 28 hadi 97. Kiwango cha ndege kuondoka kwa wakati kilikuwa asilimia 90 badala ya asilimia 54.

Mheshimiwa Spika, idadi ya ndege iliongezeka kutoka ndege moja hadi tano, yaani *B737-200* tatu na *Dash 8* mbili. Hata hivyo, ndege hizo mbili za *Dash 8* zilirudishwa Afrika ya Kusini. Aidha, kuanzia Machi, 2004 *ATCL* imeongeza ndege moja aina ya *Jetstream*. Kampuni imekuwa na muundo mpya wa ajira ya wafanyakazi baada ya makubaliano kati ya Menejimenti mpya na Chama cha Wafanyakazi. Hata hivyo, kampuni ilikabiliwa na matatizo ya kibiashara na kiuendeshaji ambayo

yalisababisha kampuni kufanya kazi kwa hasara. Matatizo hayo yalikuwa ni pamoja na mtaji mdogo, madeni mengi yaliyosababishwa na gharama kubwa za uendeshaji ndege za zamani na gharama kubwa za bima. Katika kipindi cha 2004/2005, Kampuni inategemea kuongeza ndege moja kubwa kwa ajili ya kuanzisha safari za nchi za Ghuba, Asia na Ulaya. Lengo la Kampuni ni kuwa na mtandao madhubuti, na wenye faida, wa huduma ya usafiri wa anga katika soko la ndani ya nchi na pia katika masoko ya Kimataifa, kitovu kikuu kikiwa Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Ndege za Serikali umeingia kwenye mwaka wa pili wa utendaji baada ya kuzinduliwa rasmi mwezi Mei,2001. Katika kipindi hiki, Wakala uliendelea kufanya kazi kwa ufanisi zaidi kwa kutumia ndege tatu katika kutoa huduma kwa Viongozi Wakuu wa Serikali pamoja na kutoa huduma za kibiashara pale ilipowezekana. Wakala umefanikiwa kufuatilia malipo ya huduma za ukodishaji wa ndege toka kwa wateja wake wakuu kwa asilimia 95. Wameweza kulipa madeni yote ya vipuri na kuwa na uwezo wa kukopeshwa *(Credit Worth)* na watoaji huduma *(Manufacturers and Suppliers)*. Hali hii imewezesha kupunguka kwa ukaaji wa ndege chini bila kuruka kwa asilimia 75.Vile vile Wakala unategemea kupata ndege mpya ya Serikali aina ya *Gulfstream G50* mwezi Septemba, 2004. Ndege hiyo inategemea kuongeza uwezo wa Wakala kwa kuweza kuwasafirisha viongozi wakuu wa Serikali kwenye safari za masafa marefu.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza majukumu yake Wakala uliendelea kukabiliwa na changamoto ya ushindani wa biashara ambao umetokana na ubia wa kampuni mpya zilizoanzishwa ambazo zimekuwa na asilimia kubwa ya biashara. Katika kukabiliana na changamoto hiyo Wakala imeweka mikakati madhubuti ya kubadilisha mfumo wa ukodishaji ndege kwa wateja wasio wa kiSerikali kwa kusisitiza kuwa malipo yafanyike kabla ya safari na mikataba yake iwe madhubuti zaidi.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kukuza biashara na mapato, katika mwaka wa 2004/2005, wakala utaendelea kutoa huduma kwa viongozi wakuu wa Serikali kwa ndege mpya ya *Gulfstream* kwa safari za masafa marefu. Ndege hiyo aina ya *Gulfstream G550* inatarajiwa kupatikana mwezi Septemba, 2004. Ndege ya *F28* itaendelea kutoa huduma kwa viongozi wa Serikali na vile vile kukodishwa kwa watu binafsi. Ndege ndogo ya *Piper Navajo* itaendelea kukodishwa. Aidha, mpango wa kununua ndege ndogo tegemezi kwa ajili ya safari fupi na za dharura za viongozi wa Serikali pamoja na kupanua wigo wa biashara utatekelezwa ili wakala uimarike zaidi.

Mheshimiwa Spika, sekta ya mawasiliano ni kati ya sekta ambazo huduma zake zimepanuka kwa haraka sana hapa nchini. Hali hii imesababishwa na ongezeko la wawekezaji katika sekta hii. Sekta hii inajumuisha huduma za simu za msingi na zile za mkononi. Sekta vile vile inahusu huduma za mawasiliano kwa njia ya posta; na mawasiliano kutumia teknolojia ya habari na mawasiliano *(ICT).*

Mheshimiwa Spika, kuundwa kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania kumetokana na kukua na kuunganika kwa teknolojia za mawasiliano na habari. Mamlaka, ambayo imeanza kazi tarehe 1 Novemba, 2003, imeendeleza jukumu la kusimamia

shughuli za mawasiliano nchini kwa ufanisi baada ya kuchukua majukumu haya kutoka kwa iliyokuwa Tume ya Mawasiliano Tanzania *(TCC)* na Tume ya Utangazaji *(TBC).*

Katika kipindi cha 2003/2004, jumla ya vituo 60 vya redio na vituo 28 vya televisheni vimeanzishwa nchini kote. Vituo 32 vinavyotoa matangazo ya televisheni kwa njia ya kuunganishwa moja kwa moja *(cable)* vimepewa leseni na vinafanya kazi. Mamlaka, kupitia Shirika la Umoja wa Simu Duniani *(ITU)*, imepokea kompyuta na vifaa vya mawasiliano kwa ajili ya miradi mitatu ya kuwaendeleza wanawake katika biashara ya mawasiliano huko Mtwara, Kinampanda na Mpwapwa.

Mheshimiwa Spika, Mamlaka imeendelea kuboresha, kupanga na kusimamia matumizi ya masafa ya mawasiliano. Mamlaka imekamilisha ujenzi wa jengo la mtambo wa kuthibiti masafa *(Fixed Frequency Monitoring Station)* eneo la Mikocheni, Dar es Salaam. Idadi ya makampuni yaliyopewa leseni ya kutoa huduma za kusafirisha vifurushi na vipeto *(Courier Companies)* imeongezeka na kufikia 16, likiwemo Shirika la Posta Tanzania.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kuundwa kwa *TCRA,* Tume ya Mawasiliano Tanzania ilitoa zabuni kwa Kampuni ya *Analysys* ya Uingereza kuchunguza gharama halisi za mawasiliano nchini ili kuweka msingi wa kufanya makadirio ya gharama za maunganisho *(interconnection).* Kampuni hiyo imekamilisha kazi yake na itatoa taarifa yake katika Bodi ya *TCRA* kwa hatua zaidi. Mamlaka pia imeshiriki katika shughuli za Kitaifa na Kimataifa kama vile kuandaa uwakilishi wa nchi kwenye mkutano wa Wakuu wa nchi uliohusu uanzishwaji wa Jamii Habari *(World Summit on the Information Society - WSIS)* uliofanyika mjini Geneva mwezi Desemba, 2003. Mamlaka inaiwakilisha Tanzania katika Mashirika ya Kimataifa yafuatayo:-

(a) Shirika la Kimataifa la Simu Duniani *(International Telecommunication Union - ITU)* lenye Makao Makuu Geneva.

(b) Shirika la Mawasiliano ya Simu Jumuiya ya Madola *(Commonwealth Telecommunications Organization - CTO),* lenye Makao Makuu London.

(c) Umoja wa Posta Ulimwenguni *(Universal Postal Union - UPU)* lenye Makao Makuu Berne, Uswisi.

(d) Shirika la Mawasiliano ya Simu Afrika *(African Telecommunication Union - ATU)* lenye Makao Makuu Nairobi.

(e) Umoja wa Posta Barani Afrika *(Pan African Postal Union - PAPU)* lenye Makao Makuu Arusha.

(f) Chama cha wasimamizi wa mawasiliano Kusini mwa Afrika (Telecommunications Regulators Association of Southern Africa - TRASA) lenye Makao Makuu Gaborone, Botswana.

(g) Umoja wa Wasimamizi wa Mawasiliano na Watoa Huduma ya Mawasiliano ya Simu na Posta Afrika Mashariki *(East Africa Regulatory, Postal and Telecommunications Organization - EARPTO).*

Mheshimiwa Spika, katika awamu ya kwanza ya mpango wake wa maendeleo wa mwaka 2003/2004, Kampuni ya Simu Tanzania ilifanikiwa kujenga mtambo wa kisasa wenye uwezo wa kupokea malipo kabla ya huduma *(Pre-paid System)* katika Mikoa ya Dar es Salaam na Arusha. Aidha, mtambo kama huo utajengwa katika Miji ya Mwanza, Dodoma na Zanzibar ifikapo Desemba, 2004.

Mheshimiwa Spika, Kampuni pia ilitekeleza mradi wa upanuzi wa huduma ya simu kufikia maeneo muhimu ya uchumi kama vile migodi ya dhahabu ya Kahama na Buhemba, Kiwanda cha Saruji cha Tanga; Kiwanda cha Sukari cha Kagera na kwenye Mashamba ya Chai ya Kibena na Mufindi. Mitambo hii ilianza kazi Machi, 2004. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi mingine iliyotekelezwa ni pamoja na ubadilishaji wa mitambo ya zamani aina ya analogue ambayo ina zaidi ya miaka 20 sasa kwa kuweka mitambo ya kisasa aina ya, *digital* katika baadhi ya miji ili kuboresha huduma na kuwezesha utoaji wa huduma za internet na simu za mkononi. Njia na mtambo wa kisasa umejengwa kuunganisha mji wa Songea na Nyololo. Kampuni pia imeboresha njia za simu katika maeneo mbalimbali. Maeneo yanayohusika ni pamoja na Mtwara - Tandahimba - Newala - Masasi, Tandahimba inapatiwa huduma ya simu kwa mara ya kwanza, Dodoma - Kondoa, ambapo simu za kukoroga zimeondolewa Kondoa. Maeneo mengine ni Mbeya - Sumbawanga - Mpanda - Namanyere, ambapo simu za kukoroga zinaondolewa Namanyere. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Kampuni ya Simu Tanzania imepanga kutumia shilingi bilioni 20 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kuboresha mtandao na ubora wa huduma za Kampuni hiyo. Mbali na kuendelezwa kwa mradi wa upanuzi wa mtambo wa malipo kabla ya huduma *(Pre-paid System)* . Miradi mingine ni pamoja na uimarishaji wa njia za simu kwa wateja kwa kutumia teknolojia ya *Asynchronous Digital Subscriber Line - ADSL (Broad Band)* ili kuwezesha upatikanaji wa huduma za Internet. Aidha, *TTCL* itaweka mitambo ya kuzuia wizi na hujuma *(Fraud Management)*. Uboreshaji utafanyika wa njia *(Transimission Links)* za *digital* za Dar es Salaam - Zanzibar - Tanga, Dar es Salaam - Lugoba - Tanga na Tanga - Moshi - Arusha na njia za *digital microwave* za Dodoma - Mwanza na Dar es Salaam - Dodoma na Kondoa - Babati.

Mheshimiwa Spika, miradi mingine iliyopangwa kutekelezwa ni ya kubadilisha mitambo ya zamani ya njia za *analogue* kati ya Dodoma - Arusha na Mwanza - Kigoma na ubadilishaji na kuweka mitambo mipya inayotumia masafa yanayotakiwa kati ya Mwanza - Musoma. Kampuni itaweka njia kuu kuzunguka Dar es Salaam *(Dar es Salaam Optical Fibre Ring)* ili kuhakikisha kuwa mawasiliano kati ya vituo muhimu vya Dar es Salaam hayakatiki. Awamu ya kwanza ya mzunguko huo itahusu uunganishaji wa

vituo *(exchanges)* vya *Telephone House, Oysterbay,* Kijitonyama, Ubungo, na Barabara ya Nyerere. Mradi huu utaanza kutekelezwa mwaka 2005.

Mheshimiwa Spika, inatarajiwa kuwa mafanikio ya utekelezaji wa miradi hii yataboresha kwa kiasi kikubwa hali ya mtandao na huduma za simu pote nchini na hivyo kutoa mchango unaostahili katika jitihada za Taifa za kuboresha uchumi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Kampuni za simu za mkononi zimeendelea kupanua huduma zao katika sehemu mbalimbali nchini. Kampuni hizi ni *Vodacom, Celtel, Mobitel* na *Zantel*. Kampuni ya *Vodacom* imepanua mtandao wao kufikia sehemu zifuataz: Jiji la Dar es Salaam, Pwani, Kisarawe, Bagamoyo, Mkuranga, Kibaha, Chalinze, Kinyerezi, Tanga Mjini, Muheza, Lushoto, Segera, Korogwe, Morogoro Mjini, Morogoro Vijijini, Kilosa, Mvomero, *Mtibwa Sugar,* Dodoma Mjini, Kongwa, Dodoma Vijijini, Singida Mjini, Singida Vijijini, Manyoni, Iramba, Arusha Mjini, Arumeru, Monduli, Makuyuni, Ngorongoro, Karatu, Namanga, Moshi Mjini, Hai, Rombo, Marangu, Moshi Vijijini, Mwanga, Same na *Kilimanjaro Airport*, Mererani, Ngorongoro, Babati, Hanang, Mbulu, Musoma Mjini, Musoma Vijijini, Bunda, Sirari, Serengeti, Mwanza Mjini, Nyamagana, Magu, Misungwi, Ilemela, Sengerema na Geita, Bukoba Mjini, Karagwe, Bukoba Vijijini, Muleba, Ngara, Biharamulo, Shinyanga Mjini, Shinyanga Vijijini, Mwadui, Maswa, Bariadi, Isaka na Kahama, Meatu.

Mheshimiwa Spika, sehemu nyingine ni Tabora Mjini, Igunga na Nzega, Kigoma Mjini, Kigoma Vijijini, Rukwa, Sumbawanga, Lindi Mjini, Nachingwea, Mtwara Mjini, Masasi, Newala, Songea Mjini, Tunduru, Songea Vijijini, Mbinga, Mbeya Mjini, Rujewa, Mbalizi, Chimala, Vwawa, Mlima Nyoka, Songwe, Kyela,Tunduma, Bulyaga,Uyole, Kiwira, Igurusi, Iringa Mjini, Tanangozi, Ifunda, Mafinga, Ludewa, Makambako, Njombe, Unguja Kaskazini A, Unguja Kaskazini B, Magharibi, Kusini, Wete, Micheweni, Chakechake, Mkoani.

Aidha, mtandao wa *Vodacom* uko katika barabara kuu zifuatazo: Arusha - Makuyuni - Monduli - Ngorongoro; Moshi - Arusha - Namanga; Dar es Salaam - Kibaha - Chalinze - Morogoro - Ifakara; Chalinze - Segera - Tanga; Segera - Same - Moshi - Mwika - Marangu; Iringa - Makambako - Njombe; Makambako - Mbeya - Tunduma; Mbeya - Tukuyu - Kyela; Nzega - Shinyanga - Mwadui; Shinyanga - Isaka - Kahama - Sengerema; Mwanza - Sengerema - Geita - Muleba - Bukoba.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Vodacom* imepanua mtandao wake katika Mikoa yote ya Tanzania. Hadi Juni, 2004 *Vodacom* ilikuwa na wateja wa simu za mkononi 700,000.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Celtel* imeeneza huduma zake katika sehemu zifuatazo: Arusha Mjini, Tengeru, *Usa-River, KIA*, Makuyuni, Ngorongoro, Namanga, Lengijabe, Moshi Mjini, Moshi Vijini, Hai, Machame, *Arusha-Moshi Road, TPC*, Marangu, Moshi-Tanga Road, Himo, Mwika, Rombo, Mwanga, Same,Tanga Mjini, Pongwe, Muheza, Pangani, Mombo, Lushoto, Handeni, Kilindi, Korogwe, *Tanga-Segera Road, Segera-Chalinze Road,* Kibaha, Kisarawe, Mkuranga, Chalinze, Mlandizi,

Bagamoyo, barabara ya Dar es Salaam- Chalinze-Segera na ya Dar es Salaam- Morogoro, Dar es Salaam, Morogoro Mjini, Morogoro Vijijini, Kilombero, Kilosa, Mvomero, Turiani, *IDM - Mzumbe*, Mikumi, *Dar es Salaam-Mikumi Road (Mikumi National Park)*, Kilombero na Ifakara, Iringa Mjini, Mafinga, Makambako, Songea Mjini, Songea Vijijini, Mbeya Mjini, Chunya, Mbarali, Mbeya Vijijini (Songwe na Mbalizi), Mlowo, Vwawa, Tunduma, Mbozi, Tukuyu na Kyela, Sumbawanga Mjini, Sumbawanga Vijijini na Mpanda, Kigoma Mjini na Kigoma Vijijini (Ujiji), Kibondo na Kasulu.

Mheshimiwa Spika,vile vile katika maeneo ya Tabora Mjini, Igunga, Urambo, Nzega, Singida Mjini, Singida Vijijini, Iramba na Manyoni, Dodoma Mjini, Dodoma Vijijini, Kongwa, Mpwapwa, Kondoa, Shinyanga Mjini, Shinyanga Vijijini, Bariadi, Isaka, Meatu, Maswa Kahama Mjini, *Kahama Mining*, Bukombe, Mwanza Mjini, Magu, Sengerema, Misungwi, Ilemela, Nyamagana, Geita, Katoro, Buseresere, Bukoba Mjini, Bukoba Vijijini, Muleba, Biharamulo, Karagwe, Ngara, Musoma Mjini, Musoma Vijijini, Bunda, Tarime, Sirari, Serengeti, *Bunda - Musoma Road*, Lindi Mjini, Kilwa Masoko, Kilwa Kivinje, Songosongo, Mtwara Mjini, Tandahimba, Newala, Masasi, Mererani, Lake Manyara, Karatu, Babati, Hanang, Mbulu, Mjini Magharibi, Unguja Kusini, Unguja Kaskazini, Unguja Mashariki na Magharibi, Wete, Mkoani, Chake Chake na Micheweni. Hadi Juni, 2004 Kampuni ya *Celtel* ilikuwa na wateja 350,000.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Mobitel* imepanua mtandao na sasa ina wateja 220,000 nchini. Sehemu ambazo mtandao huu umefika ni pamoja na Kinondoni, Temeke, Ilala, Kibaha, Kisarawe, Bagamoyo, Chalinze, Mlandizi, Morogoro Mjini, Mikumi, Kihonda, Tanga Mjini, Muheza, Korogwe, Segera, Dodoma Mjini, Msalato, Arusha Mjini, Ngorongoro, Tengeru, Mererani, Moshi Mjini, Moshi Vijijini, Rombo, Hai,Sanya Juu, Marangu, Iringa Mjini, Makambako, Mafinga na Njombe, Mbeya Mjini, Meta, Sengerema, Geita, Ukerewe, Nyamagana, Isaka, Shinyanga Mjini, Kahama, Mwadui, Muganza, Bunda, Musoma, Tarime, Kigoma Mjini, Garaganza, Kibondo, Kasulu, Songea Mjini, Mtwara Mjini, Sumbawanga, Bukoba, Ngara, Kaskazini A, Kaskazini B, Mjini Madharibi, Mjini Magharibi, Magharibi na Kusini.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *Zantel* inatoa huduma za simu za mkononi katika Mikoa yote ya Zanzibar. Imepanua mtandao wake katika sehemu zifuatazo: Nungwi, Mtoni, Makunduchi, Tumekuja, Madema, Matemwe, Mkwajuni, Mahonda, Tunguu, Kizimkazi, Hamamni, Lumumba, Michamvi, Kitongani, Kiwengwa, Chwaka, Amani, Kisiwandui, Bububu, Masingini, Fumba, Mazizini, Jambiani, Chake Chake, Mkoani, Wete, Konde, Kichunjuu, Micheweni na Bhanasa. Asilimia 60 ya wateja wa *Zantel* wako Unguja na asilimia 40 wako Pemba. Hadi Juni, 2004 *Zantel* ilikuwa na wateja wapatao 70,000.

Mheshimiwa Spika, wateja wa simu za mkononi wameongezeka na kufikia milioni 1.4 mwezi Juni, 2004 ikilinganishwa na wateja 850,000 waliokuwa na simu za mkononi Juni, 2003. Aidha, kumekuwa na idadi kubwa ya watumiaji wa huduma za tovuti *(internet)* hasa sehemu za mijini. Tanzania sasa ina *internet services providers* 25 na *internet cafes* 272. Haya ni mafanikio makubwa ya Sera zetu ambayo hatuna budi kujivunia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 Shirika la Posta liliweza kutoa huduma kwa kiwango cha kuridhisha. Katika kipindi hiki Shirika lilisambaza na kutuma barua kwa kupitia mtandao wa posta ndani na nje ya nchi. Barua za ndani ya nchi zilikuwa milioni 18.2, zikiwa pungufu kwa asilimia 4.2 ikilinganishwa na barua milioni 19.0 zilizotumwa mwaka 2002. Aidha, barua zilizotumwa nje ya nchi zilifikia milioni 6.5 ambalo ni ongezeko la asilimia 6.6 ikilinganishwa na barua milioni 6.1 zilizotumwa mwaka 2002. Utumaji na usambazaji wa vifurushi katika soko la ndani ulipungua kwa asilimia 7.6 kutoka vifurushi 31,862 mwaka 2002 hadi kufikia vifurushi 29,422 mwaka 2003. Hata hivyo idadi ya vifurushi vilivyotumwa nje ya nchi iliongezeka kutoka vifurushi 5,789 mwaka 2002 hadi kufikia vifurushi 6,699 mwaka 2003 hii ikiwa ni sawa na ongezeko la asilimia 15.7. Wakati huo huo idadi ya barua zilizosajiliwa posta (rejista) na kutumwa katika soko la ndani katika kipindi hicho iliongezeka kwa asilimia 32.5 kutoka 324,214 mwaka 2002 na kufikia 429,688 mwaka 2003. Rejista zilizotumwa katika soko la nje ziliongezeka kwa asilimia 45 hadi kufikia 46,218 ikilinganishwa na rejista 31,814 zilizotumwa mwaka 2002.

Mheshimiwa Spika, Hawala za Posta *(Express Money Orders-EMS)* zilizotumwa zilipungua kwa asilimia 8.2 kutoka 280,798 mwaka 2002 hadi 257,685 mwaka 2003. Kwa upande wa utumaji fedha katika ya nchi za Afrika Mashariki *(Interstate Money Orders),* idadi ilipungua kwa asilimia 39.9 kutoka 2,320 mwaka 2002 hadi kufikia 1,393 mwaka 2003. Vile vile hundi za Posta *(Postal Orders)* zilipungua kwa asilimia 42 kutoka hundi 28,374 mwaka 2002 hadi 16,445 mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, huduma ya *EMS* inayohusisha ukusanyaji na usambazaji wa nyaraka na vipeto ilitolewa kwa ufanisi katika kipindi hicho. Usambazaji wa nyaraka na vipeto vya haraka ndani ya nchi uliongezeka kwa asilimia 7.8 na vya kimataifa uliongezeka kwa asilimia 1.7. Aidha, utumaji fedha kwa njia ya haraka *(Money Fax)* ulikuwa 216,700 ikiwa ni ongezeko la asilimia 16 ikilinganishwa na 186,360 kwa mwaka 2002. Huduma ya utumaji wa taarifa za haraka *(EMS fax Messages)* iliongezeka kwa asilimia 93 ambapo ilifikia 19,164 ikilinganishwa na 9,904 kwa mwaka 2002. Shirika liliongeza vibali vya kuuza stempu kutoka 3651 kwa mwaka 2002 hadi kufikia 3715 kwa mwaka 2003. Idadi ya vituo vya kusambazia barua *(Mail Delivery Centres)* iliongezeka kutoka 21 kwa mwaka 2002 hadi 27 kwa mwaka 2003.

Mheshimiwa Spika, utendaji wa Shirika katika kipindi cha mwaka 2003, ulikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na ufanisi mdogo wa kusambaza barua kwa wateja hasa katika maeneo ya vijijini. Hii ni kutokana na ubovu na uhaba wa miundombinu ya mawasiliano na usafirishaji kwa baadhi ya njia, mtaji hasi, madeni makubwa na kuongezeka kwa ushindani. Hata hivyo, Shirika liliendelea kubuni na kutekeleza mikakati na mbinu mbalimbali za kuliwezesha kuimarisha utendaji wake.

Aidha, katika kipindi cha mwaka 2003 Shirika limekamilisha ujenzi wa jengo la Posta Isaka na Wilaya ya Kilindi. Michoro ya majengo ya Posta ya Mpanda, Katesh, Orkesumet na Namanyere pia imekamilika. Wakati huo huo majengo kadhaa ya kutolea huduma yalifanyiwa ukarabati ili kuyaweka katika hali nzuri.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Shirika limepanga kutatua matatizo yaliyopo na kukabiliana na hali ya ushindani kwa kuongeza na kuboresha bidhaa na huduma zake na kuwapatia wafanyakazi wake mafunzo katika ngazi mbali mbali ili kuwaongezea uwezo na ujuzi. Aidha, Shirika lina mpango wa kutafuta mikopo na misaada ya kiufundi kutoka taasisi na mashirika yanayojihusisha na maendeleo ya sekta ya posta ili kuimarisha hali ya ukwasi, kuimarisha mradi wa kusafirisha barua, nyaraka na vifurushi usiku *(Overnight Mail Delivery)* toka Dar es Salaam kwenda mikoa ya Kaskazini, Kati na Nyanda za juu Kusini. Hii itasaidia kuongeza kasi ya usambazaji barua nchini, kuimarisha na kuboresha mfumo mpya wa mawasiliano unaotumia teknolojia ya kompyuta.

Mheshimiwa Spika, katika jitihada za kuboresha Shirika la Posta Tanzania, wataalamu waelekezi wanaendelea na kazi ya kulifanyia uchambuzi ili kutoa mapendekezo yao juu ya jinsi ya kulirekebisha. Katika kipindi hiki cha mpito Shirika litaendelea kufanya kazi zake chini ya mkataba wa utendaji kama ilivyokuwa miaka iliyopita. Vile vile Shirika linaandaa mkakati wa kibiashara ambao utaliongoza katika kipindi cha mpito cha miaka mitatu. Katika kipindi cha 2004/2005, Shirika linatarajia kutumia kiasi cha shilingi milioni 658.7 kwa shughuli za maendeleo kwa kujenga majengo mapya ya Posta ya Namanyere, Mpanda, Katesh na Orkesumet, kukarabati majengo yaliyopo ili yawe ya kuvutia kwa huduma za Posta, kununua magari na pikipiki kwa ajili ya kusafirisha na kusambaza barua za kawaida na za *EMS* na kununua vifaa mbalimbali kama vile kompyuta, *fax machines,* mashine za kudurufu *(photocopiers)*, vifaa vitakavyosaidia katika kutoa huduma za Posta.

Mheshimiwa Spika, Teknolojia ya habari na mawasiliano *(ICT)* inagusa kila mmoja wetu. Umuhimu wake ni mkubwa sana katika kuharakisha ujenzi na uendelezaji wa Jamii yenye maarifa na uelewa wa masuala na mazingira yanayoizunguka, jamii yenye uwezo wa kupata habari kutoka vyanzo na sehemu mbalimbali kwa kutumia teknolojia mpya. Jamii iliyo na uwezo na ufahamu na uelewa huo inaitwa Jamii Habari. Kwa kifupi, Jamii Habari ni mfumo wa maisha ambapo jamii ina haki na uwezo wa kuwasiliana, kujifunza, kupashana habari bila vikwazo katika kupokea na kutoa habari kupitia mtandao wa mawasiliano kama nyenzo ya kufanikisha, kurahisisha na kuharakisha utekelezaji wa shughuli za kila siku za maendeleo.

Mfumo huu wa Jamii Habari hutumia fursa mbali mbali zilizopo popote pale katika kujijengea mazingira mazuri ya kukuza uchumi. Jamii ya aina hii ina uhuru wa kutafuta, kupata na kutumia (kwa manufaa ya Taifa) taarifa bila kipingamizi chochote. Kigezo kimojawapo cha Jamii Habari ni utawala bora, demokrasia na haki ya kujiendeleza. Teknolojia ya Habari na Mawasiliano *(Information and Communications Technologies - ICT)* ni nyenzo muhimu ya kufanikisha kufikiwa kwa Jamii Habari. Kuongezeka kwa kasi ya kukua kwa teknolojia hii kumewezesha kasi ya ukuaji wa ustawi wa jamii. Matokeo ya matumizi ya huduma za *ICT* yamesababisha makutano makubwa ya matumizi ya huduma za kompyuta, simu, na za utangazaji katika kuleta maendeleo. Huduma hizi zinazigusa sekta zote za kijamii na kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, kwa kubaini umuhimu wa Huduma za *ICT* katika kujenga Jamii Habari, lengo likiwa ni kuharakisha maendeleo, Wakuu wa Nchi Duniani walikutana Geneva, Uswisi tarehe 10 - 12 Desemba, 2003 kujadili masuala mbali mbali yanayohusu matumizi ya ICT kwa ujenzi wa Jamii Habari *(World Summit on Information Society-WSIS).* Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi alipata heshima ya kumwakilisha Rais katika mkutano huo. Viongozi wa nchi Duniani walisisitiza umuhimu wa *ICT* katika ujenzi wa Jamii Habari ili kuweza kufikia malengo ya *UN Millenium Development Goals (UN MDGs).* Malengo hayo yanaendena na yale yaliyoainishwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025 ambayo yanalenga kupunguza umaskini hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, *WSIS* ilitilia mkazo kuongeza kiwango cha matumizi ya *ICT* kama njia mojawapo ya kufanyika yafuatayo:-

(a) Kutoa msukumo katika utekelezaji wa demokrasia na utawala bora.

(b) Kuendeleza, kuimarisha na kutekeleza dhana ya ushirikiano miongoni mwa watu, taasisi, nchi, na mabara kwa kutumia mfumo wa kubadilishana taarifa na upashanaji habari zinazozingatia maadili, mila na desituri zinazokubalika.

(c) Kutumia rasilimali zilizopo kwa ufanisi na kwa ushirikiano ili kutoa mafunzo bora yatakayowezesha kupatikana kwa wataalam wa kutosha katika kuendeleza matumizi ya huduma *ICT*.

(d) Kuweza kutumia huduma za *ICT* kikamilifu katika mipango ya maendeleo ya miundombinu na huduma, mfano, kutumia *ICT* katika kubaini, kuainisha, kutathimini na kuzikusanya rasilimali zilizopo na kuzitumia katika kuwekeza na kuendeleza sekta zote za kijamii na kiuchumi zikiwemo za biashara, fedha, utawala bora, kilimo, elimu, afya na kadhalika ili kuchangia katika kuongeza Pato la Taifa.

Mheshimiwa Spika, mkutano wa *WSIS* ulipitisha Maazimio ya Msingi na Mpango wa Kazi ambao kwa pamoja kila nchi inawajibu wa kuhakikisha unatekelezwa kwa ukamilifu. Maazimio hayo ni pamoja na:-

(a) Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi zitayarishe, sera na kutekeleza mikakati inayohusu teknolojia ya habari na mawasiliano. Masuala ya mafunzo yazingatiwe.

(b) Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine zijihusishe kikamilifu kufanikisha azma nzima ya Jamii-habari.

(c) Serikali zinazoendelea zitoe kipaumbele miradi inayohusu teknolojia ya habari na mawasiliano na ikibidi kuwe na ushirikiano na nchi zilizoendelea na mashirika ya fedha katika utekelezaji wa miundombinu inayoendana na teknolojia hiyo.

(d) Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine zitayarishe na kutekeleza mikakati ya kufikisha vijijini huduma za simu na mawasiliano yanayohusika *(Rural Access).*

Mheshimiwa Spika, Wakuu hao watakutana tena mjini Tunis, Tunisia, mwezi Novemba, 2005 ili kutathimini utekelezaji wa Maazimio ya *WSIS,* kujadili mafanikio na matatizo na ikibidi kuzidi kubuni mbinu zaidi ya jinsi ya kuendeleza matumizi ya *ICT* kwa maendeleo ya jamii. Hivi sasa, Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi inaendelea kukamilisha Mkakati wa utekelezaji wa Maazimio na Mpango wa Kazi wa *WSIS.*

Mhesimiwa Spika, Tanzania imeendelea kuwa mshiriki mzuri wa shughuli za Kimataifa. Ushiriki wa Mikutano inayohusu *ICT* na Jamii Habari umekuwa wa manufaa kwetu kama nchi na Kanda pia. Mfano, Tanzania iliweza kushiriki katika mikutano ya kujadili mikakati ya kutekeleza Mpango wa Kazi na Maazimio ya *WSIS* huko, Nairobi, Kenya, tarehe 23 - 25 Machi, 2004 na Cairo, Misri, tarehe 4 - 8 Mei, 2004, na mkutano wa matayarisho ya *WSIS* (awamu ya pili), Tunis 24 - 26 Juni, 2004.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia kwamba, *ICT* ni nyenzo muhimu katika kufikia malengo ya Wizara na Dira ya Taifa ya 2025 hatua za makusudi za Sera na mikakati zinahitajika kuwekwa na Serikali kwa kushirikiana na Wadau mbalimbali yaani sekta binafsi, mashirika yasiyo ya Kiserikali *(NGOs)* na Jamii kwa ujumla. Kwa misingi hiyo, Serikali imeanza hatua za kupunguza na kuondoa kabisa kodi kwa baadhi ya bidhaa na mitambo ya kutolea huduma za *ICT*. Matokeo yake ni kwamba huduma za simu za mkononi na vituo vya huduma za Tovuti *(Internet Cafes)*, barua pepe *(e-mail)* ziliongezeka wakati bei za vifaa vya kompyuta ziliendelea kushuka ingawa si kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Serikali kwa kushirikiana na wadau wote, itaelekeza nguvu zake katika kujenga uwezo wake wa kuratibu na kuimarisha mfumo wenye ufanisi mkubwa katika kutekeleza shughuli za *ICT* nchini. Sambamba na masuala mengine Serikali katika kipindi cha miaka minne kuanzia sasa itatekeleza shughuli za kuratibu Programu ya Taifa kuhusu utekelezaji wa shughuli za *ICT.* Aidha, Serikali itashirikiana na wadau husika katika kuwekeza kwenye mitandao ya mawasiliano ya shughuli za Serikali *(e-government)*, Utawala Bora *(e-governance),* Kilimo *(e-agriculture),* ya Biashara *(e-commerce)*, ya elimu *(e-education),* ya afya *(e-medicine)*, ya utalii *(e-tourism)* na mingineyo. Nafurahi kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, sasa Serikali imefanya uamuzi wa kutekeleza mpango wa Serikali elektroniki *(e-government)*. Mpango huo utasimamiwa na Ofisi ya Rais; Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Mpango mwingine utakaopewa msukumo ni ule wa kuanzisha mfuko maalum wenye lengo la kupeleka huduma za simu na internet hadi vijijini *(Rural Telecommunication Fund).*

Mheshimiwa Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba Tanzania sasa ina *Internet Exchange Point (IXP)* yake. Habari zetu na barua pepe sasa zinatumia njia ya hapa nchini badala ya kwenda nje ya nchi. *IXP* hiyo ambayo iko Dar es Salaam inasimamiwa na *Tanzania Internet Service Providers Association.* Ilianza kutumika tangu

Januari, 2004. Hatua hiyo inaleta pungufu la gharama, usiri wa habari, na matumizi mazuri ya mtandao kwenda nje ya nchi. Tunalishukuru Shirika la Maendeleo la Umoja wa mataifa *(UNDP)* na Idara ya Maendeleo ya Kimataifa ya Uingereza, *(DFID)* kwa msaada uliowezesha kuanzisha *IXP* nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mamlaka ya Hali ya Hewa *(TMA)* imeendelea kutoa huduma kwa kiwango cha kuridhisha. Katika kipindi cha 2003/2004, Mamlaka imepata vifaa vya kisasa ikiwemo mtambo wa kisasa wa utabiri *(Forecasting System)* kutoka Uingereza na mtambo mpya wa kupimia hali ya hewa katika anga za juu *(Upper Air System)* kutoka Marekani, kupitia Shirika la Hali ya Hewa Duniani *(WMO).* Mitambo yote hiyo imefungwa kwenye kituo chake kikuu cha Dar es Salaam. Mitambo hii imeboresha kwa kiasi kikubwa huduma zinazotolewa na Mamlaka. Kituo cha kupimia hali ya hewa anga za juu kilichopo Kigoma kimeanza kufanyiwa ukarabati ili kiweze kutoa huduma ipasavyo. Jengo jipya la ofisi lililoko Zanzibar lilizinduliwa wakati wa sherehe za miaka 40 ya Zanzibar na huduma za hali ya hewa zinatolewa katika jengo hilo.

Mheshimiwa Spika, vituo vya kupimia hali ya hewa vya Singida na Handeni vimezinduliwa rasmi na vimeanza kazi. Mamlaka imeanza taratibu za kujenga vituo vya Kilwa, Tukuyu na Mpanda ambavyo vitaboresha mtandao wa vituo na ongezeko la upatikanaji wa taarifa za hali ya hewa.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2004/2005, Mamlaka itafanya matayarisho ya ujenzi wa vituo Babati, Kibondo, Liwale na Mafia. Aidha, Mamlaka imeboresha Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma ambacho kimeendelea kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa Mamlaka na kwa asasi mbali mbali. Mamlaka inatarajia kuongeza madarasa, vitendea kazi na kukarabati mabweni ya chuo. Mamlaka itaendelea kuwapa mafunzo wafanyakazi na wataalam wake katika vyuo vya hapa nchini na nje ya nchi. Aidha, Mamlaka imepata ofisi mpya katika jengo la Ubungo Plaza na Serikali imeipa Mamlaka kiwanja kwa ajili ya kujenga ofisi zake za kudumu.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2004/2005, Serikali inakusudia kurekebisha Sheria Na.6 ya mwaka 1978 iliyounda Idara Kuu ya Hali ya Hewa baada ya kuvunjika kwa iliyokuwa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Juni 1977. Marekebisho haya yanatokana na mabadiliko mbali mbali yaliyotokea nchini na duniani pamoja na yale yanayotokana na sheria ya Wakala wa Serikali, Sheria Na 30. ya 1997 na Sheria Na.3 ya 2001 inayohusu kanuni za Fedha na Ununuzi.

Mheshimiwa Spika, huduma za hali ya hewa zimeendelea kutoa mchango mkubwa kwa sekta mbali mbali hapa nchini. Huduma za Mamlaka hii zimetumika katika sekta ya kilimo na hifadhi ya chakula, nishati, maji na usafiri wa anga. Aidha, Mamlaka ya Hali ya Hewa inashiriki kikamilifu katika mikakati ya Kitaifa ya kupambana na majanga kama vile ukame, mafuriko, mvua kubwa na upepo mkali. Mamlaka imeendelea kusambaza taarifa za hali ya hewa kupitia vyombo mbalimbali vya habari nchini na kwenye tovuti. Aidha, katika kuelimisha wanachi juu ya umuhimu wa kutumia huduma za hali ya hewa, Mamlaka, inaendelea kushiriki katika maonyesho ya Nane Nane.

Mheshimiwa Spika, pamoja na changamoto zinazoikabili; Mamlaka bado ni mfano bora katika Afrika katika kujiendesha kwa utaratibu wa wakala. Kutokana na hali hiyo Taasisi za Hali ya Hewa za nchi nyingi zimetembelea Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania ili kupata uzoefu. Katika kipindi cha 2003/2004, Mamlaka imetembelewa na taasisi za hali ya hewa kutoka Malawi, Zimbabwe, Afrika Kusini na Kenya ili kuona maendeleo tuliyofikia hapa nchini na jinsi huduma zinavyotolewa.

Mheshimiwa Spika, Serikali imeamua kuwauzia wafanyakazi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania *(THA)*, Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* na Kampuni ya Huduma za Meli *(MSCL),* nyumba ambamo wafanyakazi hao wanakaa. Wafanyakazi hao watauziwa nyumba hizo kwa bei ambayo itatokana na tathmini itakayofanywa kwa msingi ule ule uliotumiwa katika kuwauzia nyumba wafanyakazi wa Serikali. Ili kufanikisha uuzaji wa nyumba hizo Wizara ya Ujenzi na Wakala wa Nyumba za Serikali wanasimamia zoezi hilo. Sababu kubwa zilisababisha Serikali kukubali kuwauzia nyumba wafanyakazi hao ni kuwapatia wafanyakazi mahali pa kuishi kwa maana hiyo kuhifadhi heshima na utu wa mfanyakazi na kuwawezesha *(empower)* wafanyakazi kwa vile kama watapatiwa hati miliki za kisheria baada ya kulipia nyumba hizo, wanaweza kuzitumia kwa shughuli za kiuchumi na kijamii. Hati ya nyumba inamuwezesha mfanyakazi, kwa mfano, kwenda Benki na kukopa kwa ajili ya uzalishaji, elimu, afya na ujenzi, pamoja na mambo mengine.

Nyumba zinazohusika ziko sehemu zifuatazo: *THA*: Dar es Salaam, Tanga na Mtwara, *TRC:* Dar es Salaam, Morogoro, Tanga, Moshi, Arusha, Dodoma, Tabora, Mwanza, Kigoma na *MSC:* Mwanza, Kigoma, Kyela, Bukoba na Musoma.

Ni matarajio ya Serikali kwamba wafanyakazi, Menejimenti na Bodi za *THA, TRC* na *MSC*, pamoja na mabadiliko ya mfumo na muundo wa Mashirika hayo, wataongeza tija na kushirikiana na Serikali kuhakikisha tunakamilisha zoezi la kukodisha mashirika hayo.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Taifa cha Usafirishaji *(NIT),* kimeendelea na juhudi za kuboresha miundo mbinu na mazingira yake na kutimiza jukumu lake la msingi la kutoa mafunzo, kufanya utafiti na kutoa uelekezi katika sekta ya usafirishaji na uchukuzi nchini. Idadi ya wanafunzi wanaochukua masomo ya Stashahada ya Juu ya Uongozi katika Usafirishaji pamoja na wale wa stashahada ya Ufundi wa Magari imeongezeka kutoka wanafunzi 229 mwaka 2002/2003 hadi kufikia wanafunzi 351 mwaka 2003/2004. Idadi hiyo ni pamoja na ongezeko la wanafunzi wa kike, kutoka wanafunzi 26 mwaka 2002/03 hadi 48 mwaka 2003/2004.

Hali kadhalika, wamiliki wa magari ya abiria na mizigo, Wizara na idara mbalimbali za Serikali pamoja na asasi za umma na za watu binafsi nchini, zimeendelea kufaidika na mafunzo ya kozi fupi yanayoandaliwa na kutolewa na *NIT*.

Mheshimiwa Spika, utayarishaji wa mpango-mkakati wa Chuo *(NIT Rolling Strategic Plan*) sasa umekamilika. Mpango-mkakati huu una malengo yafuatayo:-

(a) Kufanikisha na kutekeleza Dira ya Chuo ambayo ni : kuwa kituo cha ufanisi katika utoaji wa mafunzo ya elimu ya juu katika sekta za uchukuzi na mawasiliano hapa nchini na nje ya nchi.

(b) Kufanikisha na kutekeleza Dhamira ya chuo ambayo ni kutoa mafunzo ya elimu ya juu na endelevu kwa viongozi na watendaji katika sekta za uchukuzi na mawasiliano.

Katika kufanikisha hayo, mpango unaelekeza yafuatayo kufanyika kati ya 2004 - 2009:-

(a) Kupitia na kuboresha sera, na sheria iliyounda Chuo pamoja na muundo wa utawala wa Chuo.

(b) Kufanya utafiti na uelekezi.

(c) Kujenga uwezo katika mafunzo ya teknolojia ya habari na mawasiliano *(ICT),* kutayarisha na kuhifadhi takwimu katika nyanja za usafirishaji na uchukuzi.

(d) Kuboresha ufundishaji kwa kutumia teknolojia ya Kompyuta.

(e) Kuongeza idadi ya wanafunzi na kuongeza programu zinazofundishwa na pia kuboresha mitaala.

(f) Kutangaza chuo ndani na nje ya nchi.

(g) Kujenga uwezo wa Chuo kwa maana ya nguvu kazi na miundombinu.

(h) Kuanzisha Bodi ya Taaluma *(Professional Board)* ya usafirishaji na uchukuzi.

Mpango mkakati unakuwa ndio msingi wa marekebisho yanayokusudiwa ya sheria iliyoanzisha Chuo.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana nilielezea juhudi za Wizara katika kurasimisha taaluma *(professionalism)* katika sekta ya usafirishaji na uchukuzi nchini, azma hiyo ilikabidhiwa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji. Ninafurahi kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba taasisi ya wataalamu wa sekta ya usafirishaji na uchukuzi nchini, yaani *The Tanzania Institute of Logistics and Transport (TILT)* imeanzishwa. Ni tegemeo langu kuwa uanzishwaji wa taasisi hiyo utaongeza chachu ya maendeleo ya taaluma katika sekta ya usafirishaji na uchukuzi nchini. Bado chuo hakijatumia kikamilifu nafasi yake kama chuo cha pekee na cha aina yake mashariki na kusini mwa Afrika. Hii ni changamoto inayotukabili.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha Mwaka wa 2003/2004, Chuo cha Mabaharia cha Dar es Salaam *(DMI)* kilijishughulisha na uimarishaji wa mitaala ili kukidhi mahitaji ya Mkataba wa standards of training, *certification and watch keeping of seafarers (STCW - 78)* kama ulivyorejewa mwaka 1995. Katika kipindi hiki pia Chuo kiliendesha mafunzo kwa mabaharia katika kozi ndefu 16 zilizohusisha wanafunzi 170 na kozi fupi 82 zilizohusisha wanafunzi 1,538. Kituo cha ukarabati *(servicing)* wa vifaa vya kujiokolea *(Life Rafts)* cha Chuo kimepewa hadhi ya kimataifa. Aidha, katika mwaka huu chuo kilihudumia meli 33 za Kitanzania na vifaa 85 vya kujiokolea, meli 13 za kigeni na vifaa 22 vya kujiokolea.

Mheshimiwa Spika, baada ya mabadiliko ya mitaala ya Chuo mwaka 2001 ambayo yametokana na mahitaji ya kutimiza masharti ya Mkataba wa Kimataifa wa *STCW - 78* kama ulivyorejewa mwaka 1995, kumekuwepo na changamoto mbalimbali zikiwemo ongezeko kubwa la wanafunzi wa ndani na nje ya nchi na hivyo kusababisha upungufu wa madarasa unaotokana na ufinyu wa eneo la Chuo, mahitaji zaidi ya walimu pamoja na vifaa vya kufundishia. Aidha, juhudi zinaendelea kupata eneo kubwa kwa ajili ya kukabiliana na ongezeko hilo. Chuo hiki nacho ni cha kipekee kwa Afrika ya Mashariki. Mwezi Juni, 2004, Kenya na Tanzania tumetiliana saini makubaliano ya kufundisha mabaharia wa Kenya na kutambua vyeti vyao kwa niaba ya Kenya. Hii imetokana na kwamba Kenya hawana Chuo cha Mabaharia kinachotambuliwa na Shirika la Kimataifa la Usafiri Majini *(IMO).* Kwa kutumia Chuo chetu mabaharia wa Kenya watatambuliwa na *IMO. (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Usalama wa Usafiri wa anga kilianzishwa mwaka 1985 na kinatoa mafunzo katika kiwango cha kimataifa katika sekta ya usalama wa usafiri wa anga kwa Watanzania, nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi Kusini mwa Afrika *(SADC)* na nchi jirani za Uganda na Rwanda. Mafunzo hayo ni katika fani za uongozaji ndege, mawasiliano, uhandisi wa mitambo na mawasiliano; usambazaji wa taarifa za safari za ndege; usalama wa viwanja vya ndege *(Aviation Security),* pamoja na utafiti na ushauri katika nyanja za usalama wa usafiri wa anga.

Mheshimiwa Spika, katika kipinidi cha mwaka wa fedha wa 2003/2004, Chuo kimetoa mafunzo kwa Watanzania 446 na wageni wapatao 46 kwa kuendesha kozi 32. Hadi kufikia Juni, 2004, Chuo cha Usalama wa Usafiri wa Anga kimeweza kutoa wahitimu 1,847. Kati ya hao 1,687 ni Watanzania na 160 ni kutoka katika nchi za jirani.

Aidha, Chuo kinakabiliwa na changamoto mbalimbali ambazo ni pamoja na miundo mbinu ambayo kwa sasa haikidhi mahitaji halisi, umuhimu wa kuboresha taaluma ya ufundishaji kwa Waalimu ili kuinua viwango vya ufundishaji kulingana na mabadiliko ya teknolojia katika fani za Anga na umuhimu wa kujitangaza ili kushawishi matumizi zaidi ya Chuo kwa wadau nchini na nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005, Chuo kina mipango ya kuongeza idadi ya wanafunzi wa ndani na nje ya nchi na kushirikiana na taasisi nyingine

ndani na nje ya nchi katika kuendesha mafunzo maalum na kuinua viwango vya ubora wa ufundishaji. Pia Chuo kina mpango wa kujenga ofisi zake.

Mheshimiwa Spika, Chuo cha Hali ya Hewa Kigoma kilianzishwa mwaka 1978 kwa madhumuni ya kufundisha mafunzo ya awali ya fani ya hali ya hewa na mafunzo ya kujiendeleza *(Refresher Courses).* Aidha, Chuo kimekuwa kikipokea maafisa wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) kwa ajili ya mafunzo ya hali ya hewa. Katika mwaka 2003/2004, Chuo kiliendesha mafunzo kwa maofisa ishirini na saba ambao miongoni mwao saba ni maafisa mawasiliano Wasaidizi na ishirini ni maafisa waangazi, wakiwemo wawili toka JWTZ. Aidha, Chuo kilianza mafunzo kwa wanafunzi ishirini na wanne kuanzia mwezi Mei, 2004 ambayo yataendelea hadi mwezi Juni, 2005.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha 2004/2005 chuo kina mipango ya kujenga madarasa mawili na kuimarisha uzio kuzunguka eneo la chuo, kukamilisha mafunzo kwa wanafunzi 24, kuendesha mafunzo kwa maofisa wa hali ya hewa daraja la III, kuongeza idadi ya walimu kwa lengo la kukiwezesha Chuo kuanzisha mafunzo ya juu ya maafisa wa hali ya hewa daraja la II ili kukidhi mahitaji ya hapa nchini pamoja na nchi jirani hususan nchi za *SADC* na kuongeza juhudi za kuelimisha na kuhamasisha jamii ya chuo ili kupunguza kasi ya maambukizi ya ugonjwa wa ukimwi kupitia semina, makongamano na vipeperushi.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2003 nililieleza Bunge lako Tukufu kuwa Wizara kwa kushirikiana na Idara Kuu ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma imetoa mafunzo ya kuboresha mfumo wa utendaji kazi Serikalini *(Performance Management System)*. Aidha, Wizara kwa kushirikiana na Idara Kuu ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma imekamilisha mkataba wa huduma kwa wateja *(Client Services Charter).* Mfumo huu umeanza kufanya kazi kuanzia nusu ya pili ya mwaka wa fedha 2003/2004.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2003/2004, Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya Taifa ya Kudhibiti Ukimwi *(TACAIDS),* iliendesha semina mbalimbali kwa nia ya kuwahamasisha watumishi wote toka ngazi ya chini hadi ya juu kuhusu jinsi ya kujikinga na maambukizi ya ugonjwa huu hatari wa Ukimwi.

Mheshimiwa Spika katika mwaka 2003/2004, Wizara iliendelea na jitihada za kuwapatia taaluma muhimu za kuwaongezea ujuzi watumishi wake. Taaluma hizo zilihusu utunzaji wa kumbukumbu *(records),* uhasibu na biashara. Katika kipindi hicho, watumishi kumi na nne walihudhuria mafunzo ya utunzaji kumbukumbu na kati yao tisa walisoma ngazi ya cheti na wengine watano wanasoma ngazi ya diploma. Katika kipindi hicho pia Wizara iliwapa fursa watumishi 11 kusoma shahada ya kwanza na shahada ya uzamili (ya pili). Kati ya hao watatu wanachukua shahada ya kwanza Chuo Kikuu huria cha Dar es Salaam, watumishi saba wanachukua shahada ya uzamili *(MBA)* katika vyuo vya hapa nchini na mmoja anachukua shahada ya uzamili huko Uingereza. Aidha, maafisa wawili walihudhuria kozi inchini Afrika ya Kusini *(Railway Safety Management)* na Sweden *(Maritime Safety Management).* Wizara inaandaa programu ya mafunzo kwa lengo la kuwa na mpango endelevu wa utoaji wa mafunzo mbalimbali kwa wataalam wa sekta kwa kutumia vyuo vya taasisi zake.

Mheshimiwa Spika, maelezo niliyotoa ni muhtasari tu wa mambo muhimu ya utendaji wa sekta za mawasiliano na uchukuzi. Hata hivyo, naamini yanatosha katika kuliarifu Bunge lako Tukufu pamoja na wananchi kwa ujumla kuhusu utendaji wa sekta za Mawasiliano, Uchukuzi na Hali ya Hewa kwa kipindi kilichopita na mipango ya mwaka ujao. Aidha, Wizara inaendelea na juhudi zake za kutafuta ufumbuzi wa changamoto zinazozikabilii sekta hizi hapa nchini. Lengo la Serikali ni kuona kwamba sekta hizi zinaimarika na hivyo kuleta maendeleo tuliyokusudia na kuwajengea wananchi imani ya utekelezaji wa majukumu yetu na dhamana tuliyopewa ya kuongoza vyombo vya umma kulingana na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, ni matarajio yangu kuwa Waheshimiwa Wabunge wenzangu watakuwa tayari kutukosoa pale tulipokosea, kutuweka sawa pale tulipoteleza na bila shaka kuwapongeza wafanyakazi wa sekta hii pale walipofanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kwa niaba ya Wizara kutoa shukrani zetu za dhati kwa wale wote walioshirikiana nasi kipindi hiki cha mwaka 2003/2004, katika kufanikisha malengo tuliyojiwekea. Shukrani hizi ziwaendee wahisani mbalimbali waliotusaidia katika kukamilisha programu na mipango yetu ya sekta za Mawasiliano, Uchukuzi na Hali ya Hewa katika kipindi kilichopita. Aidha, hatuna budi kutoa shukrani zetu za dhati kwa Mashirika na taasisi za kimataifa zilizochangia katika kuboresha huduma mbalimbali na miundombinu ya sekta hizi. Nchi na Mashirika hayo ni pamoja na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa *(UNDP),* Shirika la Kimataifa linalosimamia Usafiri wa Majini *(IMO)*, Shirika la Kimataifa linalosimamia Usalama wa Usafiri wa Anga *(ICAO),* Shirika la Kimataifa linalosimamia masuala ya Simu *(ITU),* Jumuia ya Kimataifa inayosimamia masuala ya huduma za Posta *(IPU),* Shirika la Hali ya Hewa Duniani *(WMO),* Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB),* Benki ya Dunia, Benki ya Rasilimali ya Ulaya, Benki ya Kiarabu inayoshughulikia maendeleo ya Afrika *(BADEA),* Benki ya Maendeleo ya Afrika Kusini *(DBSA),* Umoja wa nchi za Ulaya, Nchi za Uholanzi, Sweden, Kuwait, Finland, Denmark, Ujerumani, Uingereza, Japan, China,Ubelgiji, Ufaransa, Italia, Urusi na wengine wengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, namalizia hotuba yangu kwa kutoa shukrani zangu kwa viongozi wenzangu katika Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi nikianza na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, Katibu Mkuu, Ndugu Salim Himidi Msoma, Wakuu wa Idara, Viongozi wa Asasi na Taasisi zilizo chini ya Wizara yangu, pamoja na Watendaji wote wa Wizara yangu. Ushirikiano wao mkubwa walionipa umenisaidia katika kutekeleza majukumu ya Serikali na hasa lile la kuendeleza sekta za mawasiliano na uchukuzi. Ni dhahiri kwamba, bila mchango wao ingeniwia vigumu na hakika tusingeweza kupata mafanikio yote haya niliyoyaeleza. Nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili Wizara yangu iweze kutekeleza majukumu na malengo yake ipasavyo katika kipindi cha mwaka 2004/2005, naomba Bunge lako Tukufu, liidhinishe jumla ya Shilingi 42,324,336,000. Kati ya fedha hizo, Shilingi 22,613,104,500 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, shilingi 445,689,600 kwa ajili ya mishahara ya

watumishi wa Wizara na Shilingi 19,265,541,900 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za Miradi ya Maendeleo, Shilingi 1,850,000,000 ni za hapa nchini na Shilingi 17,415,541,900 ni fedha za kigeni kutoka kwa Wahisani mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi, pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kwa kunisikiliza wakati nikiwasilisha hotuba yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge wanne, watakaochangia mwanzo katika hoja hii ni Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga na Mheshimiwa Halima Kimbau wajiandae. Sasa namwita Mwenyekiti au Makamu Mwenyekiti wa Kamati iliyochambua Makadirio ya Wizara hii, atoe maoni ya Kamati.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 103b(1), Toleo la 2003 na kwa heshima kubwa, napenda nitumie fursa hii kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, taarifa ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi katika mwaka wa fedha uliopita, pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, kabla ya kutoa maoni ya Kamati kuhusu Fungu 62 la Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, naomba kuchukua fursa hii kwa niaba ya Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Miundombinu, kutoa pole kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, pamoja na wapiga kura wake wa Jimbo la Mbeya Vijijini, kwa kuondokewa na mpendwa wao, Marehemu Mheshimiwa Yete S. Mwalyego, ambaye alikuwa Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, alikuwa ni mtu mwenye busara, hekima, upendo, aliyeshirikiana na kila mtu na asiyependa makuu. Kifo chake cha ghafla kimeacha pengo kwa wote waliokuwa wakimfahamu vizuri. Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati yangu, naomba kutoa salamu za rambirambi kwa familia ya Mheshimiwa Dr. Lawrence M. Gama, kwa kufiwa na mwanaye. Tunawaombea Mwenyezi Mungu, awape faraja na kumwomba Mwenyezi Mungu ailaze roho yake mahali pema peponi. *Amina.*

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Miundombinu imeundwa kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Kanuni ya 103b(1), Toleo la 2003. Majina ya Wajumbe wa Kamati hii ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Prof. Henry R. Mgombelo, Mwenyekiti, Mheshimiwa Henry D. Shekiffu, Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Lydia T. Boma, Mheshimiwa Zamda S. Bozzen, Mheshimiwa Dr. Batilda S. Buriani, Mheshimiwa Robert J. Buzuka, Mheshimiwa Bakar S. Faki, Mheshimiwa Abdallah K. Feruzi, Mheshimiwa Dr. Amani W. Kabourou, Mheshimiwa Ally A. Karavina, Mheshimiwa Mohammed Juma Khatib, Mheshimiwa Dr. Thadeus M. Luoga, Mheshimiwa Ibrahimu W. Marwa, Mheshimiwa Mohammed H. Missanga, Mheshimiwa Dr. James A. Msekela, Mheshimiwa James P. Musalika, Mheshimiwa Frank M. Mussati, Mheshimiwa Prof. Daimon M. Mwaga, Mheshimiwa Ludovick J. Mwananzila, Mheshimiwa Karim S. Othman, Mheshimiwa Sijamini M. Shaame na Mheshimiwa Maria D. Watondoha.

Mheshimiwa Spika, Mawasilisho ya Mpango na Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka 2004/2005, yamefanywa kwa kina na kwa ufasaha na Kamati yangu imeridhika na maandalizi yaliyofanywa. Kamati inampongeza Mheshimiwa Prof. Mark J. Mwandosya, Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Mheshimiwa Dr. Maua A. Daftari, Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi na Ndugu Salim Msoma, Katibu Mkuu wa Wizara hiyo pamoja na watendaji wote, kwa kazi nzuri iliyofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu pia ilipokea taarifa ya mapato na matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa kipindi cha mwaka 2003/2004, pamoja na mafanikio na matatizo yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji wa mpango huo. Aidha, Kamati ilipata maelezo kuhusu kazi zilizopangwa kufanywa na Wizara katika kipindi cha mwaka wa fedha cha 2004/2005 na maombi ya fedha kwa kazi hizo.

Mheshimiwa Spika, Wizara imeyapa umuhimu maelekezo yaliyotolewa na Kamati yangu wakati wa kujadili bajeti ya mwaka 2003/2004 na kwa kiwango kikubwa, mengi yamefanyiwa kazi na mengine yapo katika hatua ya utekelezaji. Aidha, Kamati inashauri jitihada hizo ziendelezwe pia kwa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi kilichopita cha mwaka 2003/2004, Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi katika utekelezaji wa mipango yake imepata mafanikio lakini pia imekumbana na changamoto. Hii nisingependa kuirudia kwa sababu Mheshimiwa Waziri ameyaeleza kwa kirefu, naomba wajumbe warejee katika mafanikio na utendaji kwa mwaka 2003 pamoja na changamoto ambazo ziliikabili Wizara.

Mheshimiwa Spika, Wizara inatarajia kukusanya jumla ya shilingi bilioni 1.937 kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005, kutoka katika vyanzo vyake vya mapato, ambavyo ni Idara ya Utawala, Idara ya Uchukuzi na Mamlaka Kuu ya Leseni za usafirishaji.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2004/2005 Wizara huenda ikakabiliwa na hali ngumu hasa katika utekelezaji wa mipango na bajeti kutokana na kutengewa fedha kidogo ikilinganishwa na mahitaji halisi. Hivyo Wizara imedhamiria kutoa kipaumbele katika kutekeleza kazi muhimu tu.

Mheshimiwa Spika, Kamati inapenda ushauri yafuatayo:-

1. Kwa vile Chuo cha Posta kilicho chini ya Kampuni ya Simu Tanzania *(TTCL)* hakitumiwi kwa muda mrefu, Kamati inashauri Serikali, *TTCL* na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wafanye mazungumzo yatakayowezesha Chuo hicho kumilikiwa na *UDSM.* Mazungumzo hayo yaharakishwe ili rasilimali hiyo iwanufaishe Watanzania na Serikali iwape Chuo Kikuu cha Dar es Salaam bila malipo yoyote, kama ilivyofanyika kwa Chuo cha *TANESCO* Morogoro;

2. Kamati inaishauri Serikali kuwa makini katika zoezi la ubinafsishaji wa Shirika la Reli Tanzania *(TRC)* na Mamlaka ya Bandari Tanzania *(THA).* Aidha, Kamati inashauri kuwa zoezi hilo lifanyike kwa uangalifu mkubwa kwa kuzingatia maslahi ya Taifa;

3. Mheshimiwa Spika, kutokana na baadhi ya bandari kutokuwa na uwezo wa kujiendesha zenyewe kama Kilwa, Lindi, Mtwara na Tanga, Kamati inashauri zisibinafsishwe kwa sasa na badala yake Serikali iziimarishe ili ziweze kujiendesha na hatimaye zinaweza kubinafsishwa baada ya kuonekana zina faida;

4. Kuhusu Nembo ya Twiga kwenye ndege za *ATCL* Kamati inapongeza hatua ya Serikali kurudisha nembo hiyo, lakini bado hairidhishi kwa namna ilivyowekwa sehemu ya mlangoni, ambapo haionekani vizuri. Kamati inashauri upungufu huo urekebishwe ili nembo ionekane wazi wazi;

5. Kamati inaishauri Serikali kuwa na uratibu mzuri na udhibiti wa kutosha wa mapato ya *ATCL* kupitia Afrika ya Kusini. Pia Kamati inasisitiza uwekwe muda maalum wa kurekebisha utaratibu huo ili mahesabu ya Kampuni yaandikiwe hapa hapa nchini bila kutegemea mtandao wa Shirika la ndege la Afrika ya Kusini hasa tukibaini yanayotokea sasa hivi;

6. Kamati inashauri kuwa Serikali ifanye kila linalowezekana ili *Rural Telecommunication Fund* ianze mapema;

7. Kuhusu suala la kuanzishwa kwa *SUMATRA, TCRA* na *TCAA,* Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua iliyofikiwa. Hata hivyo, Kamati inashauri zoezi hilo liharakishwe kwani ucheleweshaji zaidi utaathiri shughuli nyingi, kwa mfano, kuchelewa kuanza kazi *TCRA* kumesababisha kuchelewa kuanza kwa vituo vya Redio na Televisheni za watu binafsi katika kupewa leseni;

8. Kamati imesikitishwa kwa Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania *(TMA)* kutopata fedha zilizopitishwa katika bajeti ya mwaka uliopita na hivyo basi inashauri kuwa katika bajeti hii *TMA* wapewe fedha za kutosha kutokana na unyeti wa Mamlaka hiyo ya hali ya hewa ni muhimu sana;

9. Kamati inapongeza juhudi za *TTCL* kwa kuanzisha huduma ya *Prepaid Card. TTCL* waendelee kupanua mtandao huo ili wananchi wengi wafaidike na huduma hiyo;

10. Pamoja na kuendelea kupanua huduma za mawasiliano, *TTCL* ifanye jitihada za kufikisha mtandao wa simu za kawaida za kisasa *(Landlines)* katika Wilaya zote za Tanzania ambazo bado zinatumia mitambo ya kizamani, simu za kukoroga zifutwe;

11. Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha kuwa *TTCL* wanalipa faini waliyotozwa na Tume ya Mawasiliano kwa kushindwa kutekeleza mkataba kwani iwapo watasamehewa kulipa faini hiyo wawekezaji wengine watabweteka na wananchi watakosa huduma muhimu kwa maendeleo yao;

12. Kamati inasisitiza kuwa juhudi madhubuti zifanyike za kupunguza gharama za simu za mikononi. Aidha, matokeo ya utafiti uliofanywa kuhusu gharama za simu za mikononi na Kampuni ya *Analysis* uwekwe wazi na mapendekezo yenye manufaa kwa umma yatekelezwe mara moja. Katika hili napenda kusema kuwa, pamoja na habari kuwa mamlaka ya udhibiti wa mawasiliano imerekebisha gharama za muingiliano wa simu *(Inter-connection)* kati ya *operators,* kuna habari kwamba, utaratibu uliotumika kufikia uamuzi huo haukuzingatia sheria na taratibu za kibiashara. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ikae na wadau kwa maana ya Makampuni ya simu yote na wafanye mazungumzo ili kufikia muafaka kwa manufaa ya pande zote husika ili kuendeleza na kuhakikisha sekta hii muhimu inaendelea kushamiri kwa manufaa ya pande zote wakiwemo watumiaji wa simu.

13. Fedha zilizotengwa kwa ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Songwe hazitoshi kulingana na kazi zinazotakiwa kufanywa. Kamati inashauri kuwa Serikali ifanye juhudi za makusudi ili mradi huo uliokwishaanza uweze kukamilika katika mwaka huu wa fedha;

14. Kwa kuwa nchi yetu ipo katika nafasi nzuri sana kijiografia *(Geographical Position),* Kamati inapendekeza Serikali iandae semina kwa Wabunge na Wadau kuhusu umuhimu wa Uchumi wa Kijiografia ili kutoa fursa ya kukusanya maoni kutoka kwa wadau katika kujenga mpango kabambe wa kuibua uchumi wetu kwa kutumia barabara, reli na bandari, ambavyo ni viungo muhimu sana kati yetu na nchi jirani na ni kitega uchumi muhimu ambacho kama kingeibuliwa kwa nguvu kingeweza kutuletea mafanikio makubwa siku za usoni;

15. Kamati inaishauri Serikali kutoa kipaumbele katika ujenzi wa viwanja vya ndege kwa maeneo ambayo yana matatizo sugu ya usafiri na yana vivutio vya kiuchumi na kiutalii kama Mafia, ambako uwanja uliopo haufai na ni hatari kwa maisha ya wasafiri. Aidha, Serikali iangalie pia viwanja vingine vya ndege kama Tabora, Dodoma, Singida na kwingineko na pawepo na mpango bayana na mikakati dhahiri ya kufikia lengo hilo bila kusahau kiwanja cha Mombo;

16. Bandari ya Itungi iliyopo Kyela ni muhimu sana kwa wananchi wa maeneo hayo. Kamati inashauri Serikali iwekeze katika Bandari hiyo ili huduma hiyo isisimame na iendelee kutoa huduma kwa wakazi wa mwambao wa Ziwa Nyasa ambao kwao ni tegemeo na mkombozi katika shughuli zao za kila siku;

17. Serikali iharakishe ujenzi wa gati la Mafia ili kuwaondolea kero ya usafiri wakazi wa eneo la kisiwa hicho, ambao kwa muda mrefu hawana usafiri wa kuaminika wa anga wala wa majini;

18. Kamati inapendekeza kuwa Serikali iwakumbuke wafanyakazi wa Wakala wa Ndege za Serikali na kuboresha maslahi yao ili wataalam wazalendo wasishawishike kukimbilia Mashirika mengine ya ndege yanayolipa vizuri;

19. Ukarabati wa kiwanja cha ndege cha Arusha usizuie Serikali kutoa kipaumbele kwa viwanja vingine vya ndege. Aidha, Kamati inashauri kuwa uwanja wa ndege wa *KIA* utumike ipasavyo;

20. Kamati inashauri Serikali kutoa kipaumbele kwa bandari na reli kama ilivyo katika barabara. Serikali iendeleze miradi hiyo kuliko kuitelekeza na kusubiri wawekezaji wa kutoka nje. Hii Wajumbe wana maana ya kwamba, bila kuwekeza wapangaji wazuri, waaminifu, hawatapatikana hatimaye reli itaharibika kabisa na tutapata hasara Kitaifa;

21. Kutokana na kutokuwa na watendaji wa kutosha wa Mamlaka za Leseni wa Mikoa, kazi ya kukusanya mapato haifanyiki inavyotakiwa. Kamati inaishauri Serikali ifanye jitihada za kupata watendaji wa kutosha katika ofisi hizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya mawasilisho ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kuhusu mpango na makadirio ya bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka 2004/2005 na kwa niaba ya Bunge lako Tukufu, Kamati yangu ilipitia na kujadili kwa kina taarifa hizo, ninaliomba Bunge lako Tukufu lijadili na likubali kupitisha kiasi cha fedha kilichoombwa na Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa Teknolojia ya Mawasiliano na Habari *(ICT),* napenda kulieleza Bunge lako Tukufu kuwa, Kamati yangu imeshaanzisha Kikundi cha Wabunge wenye hamasa na sekta hii kinachoitwa *Tanzania Parliamentarian Network on ICT4D* na Wajumbe wote wa Kamati ya Miundombinu ni wanachama waanzilishi. Napenda kutoa wito kwa Waheshimiwa Wabunge wengine, kujiunga nasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa mara nyingine tena napenda kukushukuru wewe binafsi, Waheshimiwa Wabunge, Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu, kwa kukamilisha zoezi la kuichambua Bajeti ya Wizara hii kwa ufanisi. Pia napenda kuwashukuru tena Mheshimiwa Prof. Mark J. Mwandosya, Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi na Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Ndugu Salim Msoma, Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, pamoja na wasaidizi wao wote, kwa mawasilisho ya mpango na bajeti ya Wizara yao kwa ufasaha mkubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Makamu Mwenyekiti wa Kamati hii, Mheshimiwa Henry D. Shekiffu, kwa busara zake zilizonisaidia kuiongoza Kamati. Namshukuru pia Ndugu Kipenka Msemembo Mussa, Katibu wa Bunge na Watendaji

wote wa Ofisi ya Bunge, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake. Aidha, nampongeza Ndugu Justina Shauri, Katibu wa Kamati hii, kwa kuihudumia Kamati ya Miundombinu kwa ufanisi na kukamilisha kazi za Kamati kwa muda uliopangwa.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee ninaishukuru tena Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, pamoja na Mashirika, Taasisi na Asasi zilizo chini ya Wizara hiyo, kwa ushirikiano waliouonyesha na kazi nzuri waliyoifanya kwa mwaka 2003/2004 kwa Kamati yangu kila ilipokutana au kutembelea miradi yao kwa nia ya kujifunza na kupata hali halisi ya utendaji wao. Ziara na mikutano hiyo imeielimisha Kamati yetu kwa kiwango kikubwa sana na kuiwezesha kuishauri Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. BAKARI SHAMIS FAKI - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, ningependa kukushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kuwasilisha maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Mpango wa Maendeleo na makadirio ya matumizi ya fedha kwa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka 2004/2005, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 43(5)(b)(c), Toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, kwa niaba yangu na Wananchi wa Jimbo la Ole, ninapenda kuwapa pole, familia ya Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, aliyekuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini, kutokana na msiba uliowakumba kwa kifo cha Mheshimiwa huyo wiki iliyopita. Vile vile ninawapa pole Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda, kwa kufiwa na baba yao hivi karibuni. Aidha, ninawapa pole Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama, Mbunge wa Songea Mjini na Mheshimia Parmukh Sing Hoogan, Mbunge wa Kikwajuni, kwa kufiwa na watoto wao. Ninawapa pole pia wale wote waliofikwa na masahibu mbalimbali kama vile ajali na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mizozo kadhaa katika Shirika la Reli inayohusisha wafanyakazi na Menejimenti kuhusiana na zaidi, maslahi ya wafanyakazi. Wafanyakazi wamewahi kugoma, kujitahidi kushinikiza kufanyiwa kazi madai yao. *TRC* ni Shirika nyeti kwa uchumi na hata umoja wa Taifa letu na chochote kinacholitikisa Shirika hili kinagusa maslahi ya Watanzania wote. Serikali na Menejimenti ya *TRC* ni lazima sasa watafute kisayansi na siyo kijazba, chanzo sahihi cha migogoro inayolipuka mara kwa mara ndani ya Shirika hili.

Mheshimiwa Spika, wafanyakazi kugoma si uhaini, bali ni haki yao ya kidemokrasia. Kugoma ni dalili tu ya tatizo la msingi lililojificha na kujichimbia mahali fulani, ndani ya *TRC*. Kutumia nguvu ya Kiserikali na kuwatisha wafanyakazi ni kitendo cha kukwamisha demokrasia na Utawala Bora. Serikali irejeshe ari ya wafanyakazi wa *TRC* kwa kushughulikia matatizo yao ya msingi, ambayo kimsingi Serikali inayafahamu vyema. Matatizo yashughulikiwe badala ya kurundikwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala la kuwafukuza baadhi ya wafanyakazi wa *TRC* si ufumbuzi mzuri na pengine inaweza kusababisha madhara zaidi yasiyotarajiwa.

Mheshimiwa Spika, hujuma za kimakusudi kabisa zimekuwa zikiendelea dhidi ya njia za reli, hasa zile za *TRC*. Pamoja na ushawishi wa hujuma unaotokana na kuibuka kwa wimbi la wizi wa vyuma chakavu, upo uwezekano wa watu wenye hasira ndani ya *TRC* kufuatia kutosikilizwa au kutofanyiwa kazi kwa kero zao zilizojikusanya kwa muda mrefu, kuhusika kwa njia moja au nyingine katika hujuma hizo. Matatizo ya ajali kadhaa za treni ikiwa ni pamoja na kugongana kwa injini yawezekana kabisa yakawa yanatokana na hujuma za watu wenye hisia za kuonewa, kunyimwa haki zao, kukandamizwa na kutosikilizwa kikamilifu ndani ya *TRC*.

Kambi ya Upinzani inashauri kwamba, huu ni wakati muafaka sasa hivi kwa Serikali kulitazama kwa kina tatizo zima la ongezeko la ajali za treni na vitendo mbalimbali vyenye mwelekeo wa kihujuma. Uchunguzi uhusishe zaidi wataalamu wa saikolojia ya wafanyakazi katika maeneo ya kazi na wataalamu wa sosholojia katika maeneo ya kazi vilevile kuliko vyombo vya dola kama Polisi na kadhalika na kadhalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, simu za mikononi ni hatua muhimu katika maendeleo ya kimawasiliano katika dunia ya sasa. Hata hivyo, Kambi ya Upinzani inaona yapo matatizo makubwa yanayostahili kupatiwa ufumbuzi na Serikali ambayo ni pamoja na:-

(a) Gharama kubwa sana za ununuzi wa muda wa maongezi. Mshahara mzima wa mfanyakazi wa kima cha chini cha mshahara katika Serikali uko sawa na dakika kama 35 mpaka 40 za muda wa maongezi. Gharama kubwa za muda wa maongezi zinaonekana kuchochea umaskini wa Watanzania badala ya kurahisisha mawasiliano kati yao na kwa hali hiyo kuchochea maendeleo ya kiuchumi na kijamii.

(b) Simu za mkononi zinapatikana kwa bei kubwa sana hasa kwa mtu wa kipato cha chini na kodi kubwa ya Serikali inachangia sana ukali wa bei ya simu hizo. Kama Serikali ilivyojitahidi kurahisisha upatikanaji wa Kompyuta na vifaa vyake kwa wananchi, inaweza pia ikatoa unafuu katika kodi ili kuwafanya Watanzania wengi zaidi wamiliki na watumie simu za mkononi, simu hizo si anasa, ni nyenzo muhimu katika kuchochea maendeleo ya Taifa. *(Makofi)*

(c) Pamoja na kuwepo kwa teknolojia ya simu za mikononi, Serikali isisahau kwamba bado wapo wananchi wengi ambao hawatafikiwa na teknolojia hiyo haraka. Simu za kawaida ikiwa ni pamoja na zile za SIWAYA, pamoja na kuimarisha mawasiliano ya barua kupitia Shirika la Posta bado ni mambo yanayostahili kupewa angalizo maalum. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo bado hayajakaa sawa ndani ya Shirika la Simu *TTCL*. Bado lipo fukuto la wafanyakazi kutokubaliana sana na sera za wawekezaji wa nje wanaoendesha Kampuni hiyo. Ni wawekezaji hao hao katika *TTCL* ambao pia wanaendesha na kwa kiasi kikubwa kumiliki Kampuni ya *Celtel* Tunashindwa kuelewa

wale waliokuwa wafanyakazi wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki mpaka sasa hawajalipwa maslahi yao na wengine wanaamini kwamba Mtaji wa *Celtel* wa kununua Kampuni ya Simu za Mikononi ya Kenya *(KENCELL),* unatokana na *TTCL.* Kwa hili Kambi ya Upinzani inaomba ufafanuzi toka kwa Waziri.

Bado wananchi wengi katika nchi hii wanaamini ubinafsishaji wa *TTCL* haujakaa sawasawa na inawezekana maslahi ya Taifa hayajalindwa ipasavyo katika Ubinafsishaji huo. Maelezo ya Serikali kuhusu ubinafsishaji huo wa *TTCL* si ya kuridhisha sana na hayatoi ufafanuzi toshelevu na ndiyo maana malalamiko ya wananchi na hata wafanyakazi hayaishi. Ubinafsishaji wa *TTCL* unaelekea kuwa ni donda ndugu la Taifa na wananchi wanayo kila sababu ya kuhoji kilichopo ndani ya ubinafsishaji huo, kwa lengo la kuona kama maslahi yao kama wenye nchi yamelindwa au hapana.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Posta *(TPC)* limeendelea kudorora kwa kutokarabati ofisi zake za Posta Mikoani na Wilayani na kadhalika. Huduma zake kama *Money Fax,* pamoja na kupendwa na watu wengi, bado si imara sana na muda mwingi wa wateja unaendelea kupotezwa katika Posta mbalimbali ikiwa ni pamoja na Posta Kuu Dar es Salaam ili kusubiri watu wa Posta kukamilisha mawasiliano, Katika Posta za Wilayani matatizo ni mengi zaidi ikiwa ni pamoja na Matawi ya Posta Wilayani kutokuwa na pesa za kuwalipa wateja.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri kwamba, Shirika la Posta liimarishe huduma zake za msingi na hasa zile zinazowagusa watu wengi wa kawaida. Huduma ya *EMS,* pamoja na gharama zake kubwa sana, bado si kila mara inafanywa kwa uharaka unaostahili. Uharaka na usahihi ni mambo ya msingi sana katika *EMS* ambayo ni lazima Shirika la Posta liyazingatie.

Mheshimiwa Spika, bado Watanzania wengi wanajiuliza kama kuna lolote la maana limefanyika na linaendelea kufanyika kuimarisha usalama wa vyombo vya majini na hasa katika Ziwa Victoria kufuatia ajali mbaya ya meli ya *M.V. Bukoba* katika Ziwa hilo mwaka 1999. Wananchi hawako tayari kusikia Taifa linapata hasara kiuzembe kama ilivyojitokeza katika janga la meli ya *M.V. Bukoba*. Ripoti na michanganuo huwa si haba kutoka Serikalini lakini wananchi wanachohitaji ni hakikisho la usalama wao majini kwa kutopata ajali za aina ile na si vinginevyo.

Ni lazima ajali ile itoe funzo chungu kwa Taifa letu, ni jambo la lazima Watanzania wote wanaojali maisha ya Watanzania wenzao, waihoji Serikali kuhusu hakikisho la usalama wa vyombo vya majini, hasa vile vinavyobeba abiria. Vyombo imara ni vile vinavyokaguliwa mara kwa mara. Tunapenda kujua kutoka kwa Waziri ni mara ngapi vyombo hivyo vimekaguliwa na hatua gani zimechukuliwa kwa wamiliki wa vyombo hivyo iwapo vimepatikana na hitilafu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba miji mingi ya Tanzania inao ugumu wa usafiri wa mijini na hasa jiji la Dar es Salaam, kutokana na hasa idadi kubwa ya wakazi katika miji, bado zipo sababu za kudhibiti aina ya magari yanayoweza kutoa huduma mijini kwa lengo la kupunguza ajali, kupunguza misongamano ya magari barabarani,

kuwawezesha abiria kusafiri kwa raha, amani  na utulivu na pia kulinda afya zao kwa kuepusha kubanana na kuinama bila ya sababu za msingi.  Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inashauri kwamba, tutilie mkazo juu ya matumizi ya *minibuses* na *micro-buses* na  huku tukiendelea kutumia magari aina ya vipanya, ambayo yanasaidia sana katika usafirishaji abiria hasa Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Spika, hatua hizi ni za muda tu, kuelekea kwenye utatuzi wa kudumu wa tatizo hili.  Kambi ya Upinzani inaona matumizi ya treni na mabasi makubwa ingekuwa ni jibu la tatizo hili. Tunaelewa kwamba, Jiji  na Mamlaka ya Usafirishaji wangependa kutumia treni na magari makubwa kwa usafirishaji mijini.  Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam imeshatoa taarifa kuwa mwezi Juni, 2004, mradi wa mabasi makubwa ungeanza.  Tungependa kujua kimetokea nini au kuna kikwazo gani kwani vigogo nao wanayo magari kama hayo jijini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika,  Chuo cha Taifa cha Usafirishaji *(NIT),* kinayo nafasi muhimu katika kuimarisha sekta ya usafirishaji katika Taifa letu.  Changamoto za msingi kwa Chuo hicho ni pamoja na:-

(a) Kutafiti chanzo halisi cha ongezeko la ajali katika barabara kuu na miji yetu;

(b) Kubuni mbinu za kisasa za kupunguza msongamano wa magari barabarani, hasa Jijini Dar es Salaam na Arusha na kadhalika.

(c) Kufanya utafiti kuhusu namna bora zaidi za kuboresha na kuimarisha usafiri katika miji ya Tanzania;

(d) Kutathmini zoezi la matumizi ya vidhibiti mwendo katika magari ya abiria ili kuona kama malengo ya msingi ya zoezi hilo yamefanikiwa.

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na mjadala miongoni mwa wananchi kuhusiana na agizo la Serikali linalozuia magari ya abiria *(Upcountry Buses),* kufanya safari usiku unaozidi saa 4.30.  Yawezekana malengo yalikuwa mazuri na bado ni mazuri tu, lakini je, Serikali haiwezi kuangalia upya uamuzi huo na hata ikibidi kutoa ruhusa ya kusafiri usiku?  Kule Kenya na Uganda mabasi yanatembea usiku na ukweli huo unawafaidisha wafanyabiashara wa nchi hizo kwa kuwaokolea muda wa mchana ambao ungetumika kusafiri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na uchungu tulionao kufuatia ajali mbaya zilizowahi kutokea katika barabara zetu, inaeleweka wazi kwamba, kuvunjika kwa koleo kuwa siyo mwisho wa uhunzi na kwa hali hiyo, maamuzi yenye lengo la kuogopa kutazamana uso kwa uso na ukweli mpya hayatusaidii kwenda mbele.  Ni wakati muafaka sasa wa kufanya tathmini ya kina kuona kama ni kweli uamuzi huo bado unazo sababu za kuendelea kutumika au hapana.  Kama hoja ni ajali kwa kuwa madreva wanasinzia, pamoja na ujambazi, basi hilo bado linaendelea kushamiri pamoja na kwamba mabasi yanatembea mchana.  Kwa hiyo, sasa hilo la kusafiri usiku si hoja ya msingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufuatia ubinafsishaji wa Shirika la Ndege la Tanzania *(ATC)* na kuibuka kwa *ATCL,* sasa ni wakati muafaka kwa Watanzania kujua shirika hilo limeimarika na kufufuka kwa kiasi gani. Je, Shirika hilo linazo ndege mpya na za kisasa lilizozinunua au linazokusudia kuzinunua? Je, lile tishio la kumezwa na kugubikwa kabisa na Shirika la Ndege la Afrika ya Kusini *(SAA)* sasa halipo?

Mheshimiwa Spika, kuhusu kuundwa kwa Shirika la *Air Tanzania Holding Corporation (ATHCO),* kwa mujibu wa Sheria Na. 6 ya Mwaka 2002, *(The Air Tanzania Corporation (Re-organisation and Vesting of Assets and Liabilities) Act)* lilikuwa na majukumu yaliyoainishwa ndani ya sheria hiyo. Tunashukuru wamejitahidi kufanyakazi zao kwa mujibu wa sheria kutokana na uwajibikaji wa Watendaji wake, inaonyesha kuwa wanakumbwa na vikwazo ambavyo pengine vinaweza kupoteza uhai wao kutoka kwa wale waliokuwa wamejihalalishia mali za *ATC* na kufanya ni shirika lao binafsi. Mfano wa madeni yanayoshughulikiwa ni *ATC Vs Muscat Travel Agency LLC* anadaiwa *USD* 1,526,254.24 na *ATC Vs Archipl* (Comoro) ni *USD* 185,000 na kadhalika.

Inaonekana kuwa lipo wingu la kuzuia *ATHCO* wasiendelee kufuatilia hayo madeni. Kitendo hiki ni kinyume na madhumuni ya uanzishwaji wa *ATHCO.* Hivyo basi, Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya Serikali, atoe tamko hapa Bungeni, Serikali isijaribu kwa namna yoyote ile kuingilia utendaji kazi wa *ATHCO* katika kudai madeni ya ndani na nje ya iliyokuwa *ATC*. Aidha, iwape watendaji hao ushirikiano ili kutimiza lengo la uanzishwaji wake kabla ya kipindi chake kumalizika na ikibidi iongezewe muda mpaka kesi zote za Madai ya walioihujumu *ATC* zipatiwe muafaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa miaka mingi kumekuwa na habari za kuwepo kwa mipango ya kujengwa Uwanja wa Kimataifa wa Ndege Mjini Dodoma eneo la Msalato. Uwanja huo ni muhimu katika kuunga mkono harakati za kuifanya Dodoma kuwa Makao Makuu ya Serikali. Uwanja huo pia umekuwa ukitazamiwa kusisimua maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika kanda nzima ya kati. Uwanja wa sasa wa Dodoma unatumika zaidi mchana kwa sababu hauna taa maalum za kuwezesha ndege kutua usiku. Uwanja huo pia ni mdogo na kwa hali hiyo ndege kubwa kabisa za Kimataifa haziwezi kutua kiwanjani hapo. Kambi ya Upinzani inashauri kwamba, kama kweli Serikali inayo nia ya kuifanya Dodoma kuwa Makao Makuu ya nchi hii na sio danganya toto, kama wengi tunavyoamini, basi tuone juhudi ya kuanzisha Mradi huo zinafanywa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kufuatia ubinafsishaji wa *TTCL* na mabadiliko kadhaa ndani ya *TTCL,* Chuo cha Simu kilichopo Kijitonyama, Dar es Salaam, Chuo hicho sasa yaelekea kimekufa kabisa, ili angalu kuwa na matumizi bora ya mali hiyo ya Taifa, Serikali iseme wazi na kiuhakika kwamba, hatima ya Chuo hicho ni nini? Majengo ya Chuo hicho na vifaa vingine vilivyopo ni muhimu kwa Taifa na atafutwe mwendelezaji aliye makini au taasisi nyingine inayoweza kujiimarisha kupitia majengo na mali nyingine za chuo mfu cha simu.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inashauri kuwa, Kijiografia, Taasisi ya Ustawi wa Jamii na Taasisi ya Mawasiliano ya Umma ya Chuo Kikuu cha Dar es

Salaam, zinaweza kuyatumia majengo ya Chuo cha Simu kwa manufaa makubwa bila ya kukisahau Chuo cha Kodi.

Mheshimiwa Spika, kama ilivyowahi kusemwa katika hotuba zetu za miaka ya nyuma kwamba, pamoja na Shirika la Viwango la Taifa *(TBS),* kuanzisha viwango vya mabodi ya mabasi, bado lipo wimbi la kuyabadilisha mabasi chakavu (malori ya mtumba), hasa yale ya *Scania* na *Fuso* kuwa mabasi kwa kuyajengea bodi. Uhakika wa mabodi ya mabasi hayo hasa kwa maana ya kulinda maisha ya abiria si mkubwa. Kwa hiyo, Kambi ya Upinzani inashauri kwamba, Serikali ifuatilie kwa ukaribu sana suala hili kabla ya kusababisha zahama kwa abiria.

Mheshimiwa Spika, dunia ya sasa ni mawasiliano, habari nzima ya utandawazi ni mawasiliano. Siasa ni mawasiliano *(e-democracy, e-governance, e-administration)* na kadhalika. Uchumi na biashara pia ni mawasiliano *e-commerce, e-business, e-trade* na kadhalika. Maisha ya kisasa si nje ya mawasiliano. Serikali yetu iwekeze zaidi katika kufanikisha mawasiliano na uchukuzi kwa lengo la kukuza uchumi wa Taifa.

Mheshimiwa Spika, nakupongeza wewe binafsi kwa kuliongoza Bunge hili tukufu kwa ufanisi mkubwa, pia ninampongeza Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Naibu Waziri wake, dada yangu mpendwa, Mheshimiwa Maua Abeid Daftari, Katibu Mkuu wa Wizara hii na Watendaji wote, kwa kazi yao nzuri na ushirikiano wao katika kutekeleza wajibu wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi ya awali asubuhi hii katika kuchangia hoja iliyoko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, napenda nianze kwa kutoa pole kwa familia ya Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, aliyetutoka yapata wiki moja hivi. Kwa kweli Mheshimiwa Yete Mwalyego, alikuwa ni sehemu ya kukamilisha timu yetu katika Kamati yetu ya Miundombinu na busara zake hakika tutazikosa kama ambavyo nina uhakika pia zitakumbukwa sana katika ukumbi wako Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, nianze pia kwa kuwapongeza Wizara, Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote wa Wizara hii, kwanza kabisa, kwa kazi nzuri ambayo wameifanya kupitia wasilisho hili la bajeti, lakini pia kwa ushirikiano mzuri sana ambao wamekuwa wakitupatia sisi kwenye Kamati ya Miundombinu na kufanya kazi yetu ya kusimamia Serikali iwe ya kufurahisha na rahisi.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli niseme moja kwa moja naunga mkono hoja hii na ningependa nisemee kidogo kwenye haya yafuatayo:-

La kwanza, ningependa niongelee *TCRA* au *TC* wanavyoita kwa kifupi. Utakumbuka hivi karibuni na ilikuwa ni tarehe 16 Juni, 2004 alitangazwa Mkurugenzi Mwendeshaji Mpya *(DG)* wa *TCRA*. Kwa mujibu wa sheria iliyoanzisha hii *Tanzania*

*Communication Regulatory Authority* kwenye kifungu cha 13(1), ni Waziri mwenye dhamana ndiyo ambaye ana mamlaka ya kumteua huyu mtu baada ya kuwasilishiwa mapendekezo na Kamati ya Mapendekezo. Lakini pia kwenye kifungu cha 13(2), zimetolewa sifa za mtu ambaye anastahili kuchukua nafasi hii ya *DG* wa *TCRA*. Sasa mimi nisome tu kipengele (c) pale mwanzo tu kinasema: *"Person shall not be qualified for appointment as a DG unless he ..."*. Sasa kwenye kipengele (c) kinasema: *"has knowledge and experience of the communication sector"*. Halafu (d) inasema: *"he is willing to serve as DG"*. *Of course* hizo zingine mbili pia ni muhimu lakini nimetaka niweke *emphasis* kwenye hizi mbili za mwisho kwa sababu nataka ni-*drive* kwenye *point* ambayo nitaisema baadaye.

Mheshimiwa Spika, kwenye kifungu hicho hicho au ibara ya 13(4) kinasema: *"The Director General shall also be the Chief Executive Officer of the authority and shall not engage in any other paid employment". That is* wakati anapopewa kazi hii hatakiwi kuwa mwajiriwa sehemu nyingine yoyote ambapo anapata mshahara.

Mheshimiwa Spika, mkononi hapa ninayo *CV* ya huyu ndugu aliyeteuliwa, jina lake ni Prof. J. S. Nkoma. Yeye anasema kwa mujibu wa hii *CV* ni Profesa wa *Physics.* Sasa kuna *qualification* ambazo zimetajwa hapa kwenye 13(2). Nataka *to bear in mind.* Halafu simu yake *extension* ni namba 2470, hii ni ya *University of Botswana.* Nafikiri huyu bwana sina uhakika sana lakini hili pia nitataka sasa Mheshimiwa Waziri atuthibitishie. Nafikiri huyu bwana bado ni mwajiriwa wa Chuo Kikuu cha Botswana kwenye Idara ya *Physics.* Ninavyosikia, sina uhakika, pia itabidi anisaidie Mheshimiwa Waziri kwamba, mkataba wa huyu Professa kwenye hiyo *University of Botswana* una-*run* mpaka mwaka 2007. Sasa *I don't know* kama ameachia ngazi kule au vipi? Lakini tunafahamu kwamba, *according to 13(4) of the Act, this guy is not supposed to hold any other job* ambayo anapata mshahara.

Kwenye *brief biography* ya huyu Profesa anasema yeye amezaliwa Tanzania. Sasa nataka niamini kwamba, huyu ni mzoefu sana wa kusafiri duniani hapa. Unapotoa *particulars* zako kwamba wewe umezaliwa wapi, *usually* unasema umezaliwa mahali fulani kwenye nchi fulani. Sasa yeye amekusanya hapa akasema *born in Tanzania. Now I am asking Mr. Honourable Speaker, where was this guy born in Tanzania?* Napenda nijue alizaliwa wapi, Tanzania? Ni Mtanzania huyu kweli, maana yake mtu anaweza kuzaliwa Tanzania hapa lakini sio lazima awe Mtanzania?

Nafahamu kwamba, kwenye sheria hii iliyoanzisha *TCRA* haijatamkwa mahali popote na mimi nilijaribu kutafuta kwa kweli sikuona. Haijatamkwa mahali popote kwamba, *DG* wa *TCRA* anatakiwa kuwa Mtanzania, *there is nothing like that.* Lakini pamoja na hayo nataka niseme kwamba, nafikiri *Tanzania has come of age* kiasi cha kuanza kutokujali kwamba, anayeajiriwa kwenye nafasi muhimu kama hiyo anaweza kuwa *just anybody else* isipokuwa Mtanzania. Hapana. Mimi nafikiri lazima tuwe na uhakika wa Utaifa wa huyu ndugu. Ni *simple logic* tu inaniambia kwamba, huyu mtu lazima tufahamu Utaifa wake.

Mheshimiwa Spika, hii *CV* ninayo hapa kama Mheshimiwa Waziri atataka nitampatia kama kiambatanisho. Lakini nataka niulize tu kwa kujumuisha hili suala la huyu *DG*, je, Mheshimiwa Waziri anaweza kuthibitisha kwamba huyu *DG* ni Mtanzania na anakidhi sifa zote ikiwa ni pamoja na ile ya kifungu cha 13(4) wakati anamteua? Hilo nataka niliachie hapo niendelee mbele kidogo.

Mheshimiwa Spika, suala la *interconnection fees* limetajwa kwenye mawasilisho ya Kamati yetu na mimi nikiwa Mjumbe. Kwa kweli nataka niseme siku zote ukiwa mtumiaji huwa inakupa faraja unapopata punguzo la kile unachokitumia. Lakini saa nyingine mapunguzo mengine unaweza ukajua pia yanaweza yasiwe ya msaada sana kama unataka huduma hiyo iwe *sustainable.*

Sasa nataka niseme kwa taarifa niliyonayo inaelekea kwamba, utaratibu wa ku-*determine* hii *interconnection fees* ya hizi *rates* haikufuatwa sawa sawa. Sasa atatusaidia Mheshimiwa Waziri kama ulifuatwa na ulitimizwa. Kwa sababu ile ripoti kwa mujibu wa taarifa niliyonayo, ile ripoti ambayo ilitokana na *study* iliyokuwa *carried out* na *Analysis* hii, Kampuni ya Waingereza ilikuwa *presented* kwa *stakeholders* tarehe 29 Septemba. *And then determination* ikafanywa tarehe 30 Juni.

Sasa sidhani kama watu wanao-*invest* pesa nyingi kiasi hicho kama unawapatia *benefit* kupitia hiyo *presentation* halafu una-*ignore* kabisa *input* zao. Kwa sababu *I don't think* kama hawa watu baada ya kupewa hiyo *submission* hiyo tarehe 29 walipata muda wa kutosha kwenda kuketi huko na kupitia hii *study* na kutoa *comments* zao. Siamini kabisa kwa sababu *these are serious people* ambao wana pesa nyingi walizowekeza pale lazima wazilinde pamoja na kuwa na sisi tunataka huduma kwa kweli lazima tuhakikishe kwamba, hawa watu wanapata nafasi ya kusikilizwa kama sheria inavyotaka. Mimi nafahamu kwa uzoefu nilionao kidogo naona kuna nchi, kwa mfano, Marekani, wanatoa muda wa kutosha sana kwenye vitu vya namna hii ambavyo *regulator* anavyotaka kuingilia maslahi ya watu kwa kiwango kikubwa namna hiyo, lazima atoe muda wa kutosha. Hilo napenda tusaidiwe.

Mheshimiwa Spika, niseme haraka haraka sasa kwenye hii *TTCL.* Nataka niseme kwamba, *PSTN* bado naamini kwa muda mrefu sana ujao, yaani huduma za simu kutumia hii waya *(copper),* bado itaendelea kuwa ni kitu *very practical* kwa muda mrefu sana ujao. Hawa watu waliokuja kuingia ubia na Serikali yetu nataka niseme kwa kweli mimi sijafurahishwa sana na mambo yote ambayo yame-*evolve* tangu wamekuja hawa mabwana mpaka hatimaye tukapata hizo dola milioni tano. Lakini pia kuna matatizo mengine ambayo sasa hivi yapo kwenye hii Kampuni. Kwa mfano, nasikia kuna tofauti kubwa sana kwenye hili Shirika. *This is supposed to be one company* lakini nasikia kuna *segregation* pale kwamba, wale wageni na ambao wako kwenye *upper echelon, actually* wanapata mishahara mikubwa sana *several times* ukilinganisha na mishahara ya hata viongozi lakini ambao ni Watanzania.

Kwa mfano, *I am made to understand* kwamba, kuna mtu huko anapata shilingi milioni 24 lakini Mkurugenzi ambaye hatimaye anakaa naye lakini ni Mtanzania anaweza kuwa anapata kama shilingi milioni mbili tu mpaka Sh. 700,000/=. *This is not fair.*

Hii ni nchi yetu, hatuwezi sisi kuwa *discriminated.* Kazi wanafanya wote, *after all this guy have only 35%* halafu Watanzania ndio wanaanza ku-*suffer.* Ninasikia pia kwamba, sasa hivi hata kwa kazi ambazo zinaweza kufanywa na mafundi ambao wako *TTCL,* wamekuwa *trained,* wana ujuzi na wanalipwa mshahara na *TTCL,* nasikia sasa wana *acquire services* kutoka nje na wanaleta mafundi ambao saa nyingine si lazima wawe wazuri sana. *What is this, is this capital flight?* Hii ni *capital flight* au ndiyo njia nyingine pia ya kusaidia kuhamisha fedha kama ambavyo wanahamisha kupitia kwenye hiyo *ATC? (Makofi)*

Mimi nafahamu kwamba, hawa mabwana wakati wanasaini kuingia ubia walitakiwa kuweka simu 810,000 wakati ule zilikuwepo simu laki mbili lakini hadi sasa hawajafanya kitu. Mheshimiwa Spika, *I am made to understand* kwamba, sasa hivi simu zenyewe hizi zimeshapungua ziko 140,000 tu. Kitu gani kinatokea huku, wanataka kuua hii Kampuni? Kila kitu unachokiangalia inaonekana kama kuna mpango wa muda mrefu wa ku-*suffocate* hii Kampuni hatimaye ife kabisa. Kama ambavyo unaona kabisa kwenye *Air Tanzania* inakuwa *suffocated* hatimaye ife kabisa. Vitendo vinaonyesha moja kwa moja utaratibu wa namna hiyo.

Sasa mimi nasema atoe tamko tena kwa sababu kwenye Kamati tulimwuliza hakusema *straight* Mheshimiwa Waziri kwamba, hii faini italipwa. Mheshimiwa Waziri, naweza nikamwelewa kwamba, yeye ni msimamizi wa sekta zote hizi. Lakini nataka nipate *statement* yake watalipa faini hawa watu, *they have to pay?*

Mheshimiwa Spika, nasikia huku kwenye *TTCL* kuna mtindo umeanzishwa. Nafikiri ndiyo njama ya kuua hii Kampuni wanadhoofisha wafanyakazi. Kwa mfano, kawaida mtu ukitumwa kwenda kufanya kazi mahali fulani, utapewa viposho vyako kawaida unakwenda unachagua mwenyewe mahali pa kulala, kula na vitu kama hivyo. Sasa nasikia wamewanyima hata hiyo. Hata *subsistence allowance* nasikia ni viongozi tu ndiyowanaopewa, hawa watu wa kawaida hawapewi. Badala yake wanaambiwa wawapatie *full board.*

Sasa ukipelekwa kwenye Kijiji changu cha Ibili ambako hata hoteli hakuna utapewa *full board* wapi, kama sisi pia wanataka watuwekee si waya pale. Nasikia hata kama ukipelekwa sehemu ambayo pana hoteli *genuine,* wanapelekwa kwenye hoteli kubwa kweli kweli. Badala ya kumlipa, kwa mfano, mahali ambapo ungemlipa mfanyakazi *total allowance* labda kwa muda atakaokaa hapa labda shilingi laki moja, sasa *full board* utakuta unalipa mpaka shilingi laki sita na hizi hoteli nasikia nazo ziko kwenye *chain. Again is this capital flight? (Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nataka nisemee kidogo kwenye hotuba yake moja kwa moja kwenye ukurasa wa 12. Nataka niseme kuwa, nimefurahishwa sasa hivi naanza kuona kuna *co-ordination* kwenye hii Wizara na Wizara ya Ujenzi. Nataka niseme kwamba, nimefurahishwa na ile *approach* yake kwenye ile aya ya 17, anaongelea *Development Corridor.*

Lakini nafikiri bado *definition* hapa ni tatizo kama ambavyo kule kwenye Wizara ya Ujenzi ile *Central Corridor* inakuwa *defined* si ambavyo watu wengine tumekuwa tunafahamu siku zote. Hapa inaonekana hii ni hivyo hivyo. Sasa *is this a common mistake?*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana naunga hoja mkono. *(Makofi)*

**MHE. ABDULARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii na mimi niweze kutoa maoni yangu machache kuhusu sekta hii au Wizara hii ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Kwanza kabisa, nami niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kwa niaba ya wananchi wa Mafia, kutoa pole kwa Mbunge mwenzetu, Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, kwa msiba uliotokea na tunatoa pole kwa familia, Mwenyezi Mungu awape subira kwa sababu hii ni njia mojawapo ya wote kule tunakokwenda. Kwa sababu tumetamkiwa kwenye vitabu kuwa kila mtu ataonja umauti. Kwa hiyo, yeye ametangulia na sisi tunafuatia huko nyuma.

Mheshimiwa Spika, naomba nitoe shukrani zangu kwa Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, Mkurugenzi Mkuu wa Wizara, Wakurugenzi wote katika Wizara, pamoja na Mheshimiwa Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti pamoja na Wajumbe wake wa Kamati ya Miundombinu, ambao wamesaidia katika kuandaa taarifa ya Kamati na kuona wao wenyewe kwa macho yao ni hali gani jinsi ya nchi yetu ilivyokuwa inahitaji au inavyoona umuhimu wa sekta hii ya mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, kuna hadithi ya Mtume Muhammad *(S.A.W)* inasema: "Mtu asiyeweza kumshukuru binadamu mwenzake japo kwa kidogo kile ambacho anampa, basi hata Mwenyezi Mungu hawezi kumshukuru kwa sababu hamwoni". *(Makofi)*

Sasa naomba nitoe shukrani zangu nyingi sana kwa Mheshimiwa Waziri, nirudie tena kwa jitihada kubwa ambayo wanaifanya pamoja na Wakurugenzi haswa wa Mamlaka ya Bandari na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege.

Naomba nitoe shukrani zangu nyingi sana kwa jitihada ambayo wanaionyesha juu ya kuhakikisha kwamba, Mafia tunaondokana na tatizo la usafiri. Hakika Kitabu cha Mheshimiwa Waziri kimezungumza katika ukurasa wa 39 kwamba, upembuzi yakinifu wa gati ya Mafia unafanyika. Ni kweli unafanyika. Mimi mwenyewe nimeshuhudia. Mpaka Makampuni ambayo yanashughulika na mambo hayo tunashirikiana nao na kufuatilia. Ilikuwa Mungu akipenda mwezi Desemba mkandarasi awepo kwenye *site* kwa maana awepo Kilindoni. Sisi tumeshawaambia wananchi wa Mafia wanaokaa lile eneo ambalo linategemewa kujengwa gati kwamba, wajitayarishe kuhama kwa ajili ya kupisha ujenzi wa gati na wao wako tayari bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Spika, lakini inaelekea kuna kitu ambacho kinasababisha kusuasua kwa ujenzi huu wa gati. Juu ya jitihada zote za Wizara ya Mawasiliano na Mamlaka ya Bandari na sina haja ya kusema nini tukifanye.

Lakini kikubwa kinajulikana kwamba, Serikali ilitoa shilingi 1,690,000,000 mwaka 2002 lakini ujenzi bado haujaanza na mwaka huu wa 2004, Mamlaka ya Bandari pia ilikuwa imetenga shilingi 2,000,000,000 kwa ajili ya kuongezea mfuko ule ambao ulikuwa tegemeo la kuweza kwenda na kukamilisha fedha ambazo zitaweza kujenga gati la Mafia, lakini kwa bahati mbaya Wizara ya Fedha ikawa imezichukua zile fedha.

Mheshimiwa Spika, Waziri wa Fedha anatusikia, kwa hiyo, nimesimama hapa kwa heshima zote kuomba Wizara ya Fedha, iikubalie Mamlaka ya Bandari kama ilivyokuwa kutenga Shilingi 1,960,000,000/= basi iwape tena kibali Mamlaka ya Bandari iweze kutenga tena shilingi bilioni 1.54 ili iweze kukamilisha bilioni 3.5 za ujenzi wa Bandari ya Mafia na ujenzi uanze kama ilivyopangwa, hata kama si mwezi wa 12 na kwa sababu nimesikia kwamba bado wale watu wa survey wanaendelea na utafiti wao kuona zile piles zitakwenda kina gani baharini inawezekana ikachelewa hadi mwezi nne nimesikia.

Lakini si mbaya nia na madhumuni kwamba, nia yenu Serikali tunaifahamu tunaipenda yote imechukuliwa inapokelewa mikono miwili. Lakini basi naamini fedha zikiwa tayari basi hata shughuli zitaanza haraka na mamlaka nayo itapata nguvu ya kuweza kufanya shughuli hii iweze kufanikisha. Kwa hiyo, nasimama hapa sisemi kwa niaba ya mamlaka ya bandari, lakini nasimama kwa niaba ya wananchi wa Mafia kuomba Wizara ya Fedha, iikubalie Mamlaka ya Bandari, kuweza kutenga zile fedha, kuwapa kibali cha kutoa zile fedha bilioni 3.5 ili ujenzi uanze mara moja. Kama si mwezi wa 12 basi mwezi wa nne kama ilivyotarajiwa ujenzi huu uanze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuhusu *gate* sina haja kuendelea sana kwa sababu linazungumzwa mara nyingi. Naamini wapo Waheshimiwa Wabunge, ambao watachangia na watanisaidia katika kuzidi kuomba Serikali iweze kutukubalia maombi yetu haya kwa sababu ni miaka mingi jamani tunateseka kule Mafia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakwenda sasa katika uwanja wa ndege. Bahati nzuri Mheshimiwa Waziri, mwenyewe alishuhudia jinsi wakati ndege ilipokuwa inatua katika Uwanja wa Ndege wa Mafia, jinsi tulivyotaka kupata ajali. Ndege ilikuwa inaseleleka kama vile inapanda milima ya Kitonga, Kitonga sasa hivi ni lami tupu sembuse uwanja wa Mafia.

Labda milima ya sehemu za Ngara au Matumbini au Rufiji, jinsi ilivyokuwa inakuwa inaseleleka. Lakini kikubwa naamini yeye anafahamu na ana nia hiyo Mheshimiwa Naibu Waziri, amekuja Kamati ya Miundombinu imefika imejionea hali halisi. Sasa basi Mamlaka ya Viwanja vya Ndege imetenga shilingi milioni 200 kwa ajili ya ukarabati wa Uwanja wa Ndege wa Mafia, ikaiomba Serikali shilingi milioni 350 yaani Wizara ya Fedha ili waweze kutimiza shilingi milioni 550 zikipatikana fedha hizi kwa wingi ziende Mafia angalau pale sehemu *(touch down)* ile sehemu pale inapogusa

ndege paweze kuimarishwa kwa sababu pale ndiyo hatari. Watalaam wa viwanja labda nimtaje kwa jina *Engineer Suleiman* aliweza kutoa maelezo mbele ya Kamati ya Miundombinu, mbele ya Waheshimiwa Mawaziri wote kwamba katika yale mashimo yaliyokuwepo lile tairi la mbele kama linatua likipiga kwenye *anger* ya shimo linaweza likasababisha maafa makubwa sana. Sasa tusingojee yatokee maafa makubwa kwa sababu ya pesa ndogo ambazo wao wameziomba. *(Makofi)*

Kwa hiyo, narejea tena kuiomba Wizara ya Fedha, ikubali kutoe fedha shilingi milioni 300 badala ya shilingi milioni 50 ilizotenga kwa kukarabati wa Uwanja wa Ndege wa Mafia ili zitimie shilingi milioni 550 ziweze kufanya kazi nzuri ambayo itakuwa ya uhakika na huenda kelele zitakuwa zimepungua kabisa kuzungumzia suala la Uwanja wa Ndege wa Mafia. Shilingi milioni 550 kwa Bajeti ambayo Serikali hii tumeipitishia ni fedha ndogo sana. *(Makofi)*

Kwa hiyo, tunaomba sana kwa heshima zote jambo hilo. Leo naomba na wala sina nia nyingine kusema kwamba siku nyingine nikikosa nitafanyaje, lakini tunaendelea kuomba kila siku. Tunaomba tusaidiwe. Wizara ya Fedha itoe shilingi milioni hizi 350 ilizoombwa ikichanganyishwa na shilingi milioni 200 ambazo tayari mamlaka imeweza kutenga basi kazi nzuri itafanyika na yenye uhakika kuliko usumbufu huu ambao kila siku wa kuomba milioni tano, milioni hamsini, kila mwaka zinapotea. Chokaa na udongo haiwezi kufanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho upande wa simu za mkononi. Tuna matatizo ya mawasiliano, lakini naomba nitumie fursa hii japokuwa Mheshimiwa Waziri hakulizungumzia, sasa sisi tuliokuwa kule vijijini ndiyo tunaona. Mheshimiwa Waziri ninaomba nikushukuru kwa jitihada zako na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa jinsi mlivyolifuatilia na kuona tatizo sugu la mawasiliano katika Wilaya ya Mafia. Hivi sasa Ndugu zetu wa *Vodacom* wanafunga mitambo Mafia na wamesema kwamba huenda watakamilisha mapema leo hii. Sasa hivi wakati niko ndani ya ukumbi nilitoka nje kwenda kuwasiliana nao jamani kukoje huko? Wanasema tunakamilisha ujenzi wa dishi lile ambalo litakuwa linasukuma *satellite* moja kwa moja. Kwa hiyo, wakati wowote ule sisi wananchi wa Mafia tutaweza kutumia mtandao huo wa *Vodacom* naamini hata kabla ya Bunge hili kumalizika. Naomba nitoe shukrani za dhati kabisa pia kwa kampuni ya *Vodacom* kwa kazi hii muhimu na nzuri kwetu sisi wa Mafia. *(Makofi)*

Lakini kuna jamaa zetu hawa wa *Celtel* hawa bwana kwa taarifa zao hata kwenye vikabrasha vyao wanachekesha. Wametuandikia kwamba hapa kabla ya mwezi wa saba huduma hii, itakuwepo katika Wilaya ya Mafia. Lakini sasa hivi nimeongea na mmoja wa Mameneja wao, *(Celtel Manager)* anaitwa Kiwali Exaudi sasa hivi kama dakika 20 tu zilizopita anasema ohoo! unajua Mafia bwana bado kidogo tulikuwa tunatumia sijui mtambo, sijui tuwaombe watu wa Songosongo tutumie laini zao lakini imekuwa matatizo. Kwa hiyo, tunaomba tumeshapata *Vodacom* wakija, Kheri wasije basi. Lakini tunataka huduma yao kwa sababu, sidhani kama *Vodacom* wataweza. Wakija sawa, lakini tunataka yawe masharika mengi. Kila mashirika yakija yakiwa mengi naamini huduma zitaweza kuenea na zitakuwa nafuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo sina haja ya kupoteza muda mrefu kengele ya pili isinikute, naomba nirudie tena kutoa shukrani kwa Wizara na kuwatakieni kila la kheri wakuu wote wa idara, wewe mwenyewe Mheshimiwa Spika na hasa kwa kunikubalia wageni wangu hawa kuja kuingia ndani bila tatizo lolote. Kwa jinsi hii wataona kwamba Tanzania, kuna demokrasia hakuna tatizo lolote. Huu ndiyo mwelekeo aliotuachia mwenyewe baba yetu Marehemu Mzee mwalimu Nyerere, Mungu amuweke mahali pema peponi na naamini juhudi hizi zitaendelezwa na kila atakayekuja katika nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niseme naunga mkono hoja hii sijui niseme mara milioni ngapi, siyo mara mia, mara milioni kuweza kufanikisha na wewe mwenyewe nakutakia kila la kheri. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. FETEH SAAD MGENI:** Mheshimiwa Spika, kwanza sina budi nikushukuru na mimi kwa kunipa nafasi asubuhi nikatoa mchango wangu mdogo katika Wizara hii kubwa, Wizara nene, Wizara iliyoenea maeneo yote.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote na mimi kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kupata nafasi katika session hii basi nitoe pole kwa marehemu Mbunge mwenzetu Mheshimiwa Yete Mwalyego, ambaye tulikuwa naye wiki iliyopita tu, lakini Mwenyezi Mungu, kamwita na kaitika. Huyu mjaa alikuwa maeneo ya pembeni pembeni hapa, basi akiondoka hapa atasogea wapi, lakini atatusailia *Inshallah* ataturejesha tuwahi kipindi kijacho.

Mheshimiwa Spika, niendelee pia kutoa pole kwa Ndugu zetu pia waliofiwa na watoto wao kama Mheshimiwa Parmukh Singh Hoogan, kwa kufiwa na mwanae binti yake, Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama, kwa kufiwa na binti yake na dada yangu Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda na Mheshimiwa Dr. Abdallah Kigoda , kwa kufiwa na baba yao mpendwa. Mwenyezi Mungu awalaze wote mahali pema peponi. *Amin.*

Wale ambao waliopata matatizo mbalimbali wakiwa wanakuja huku Bungeni, basi nao pia tunawapa pole hizo pamoja na kuomba kwa yule aliyekuwa kabakia kule hospitali apone haraka aje aungane nasi katika kuwatumikia wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sina budi kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, yeye mwenyewe binafsi, Naibu wake, Katibu Mkuu wake, pamoja na watendaji wote watalaam ambao wanamsaidia katika Wizara hii. Wizara hii kubwa mno, Wizara ambayo inahitaji utalaam mwingi, Wizara ambayo imeshika kila pembe ya Tanzania. Kwa hiyo, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri. Pia ninawashukuru watu wake kwa juhudi ambazo wanazomsaidia, wanamsaidia kweli na sisi tunakubali kwamba wanamsaidia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nianze kutoa mchango wangu mdogo tu katika baadhi ya maeneo, maana hotuba ya Mheshimiwa Waziri, imefunga maeneo yote. Ni kweli Wizara aliyopewa Profesa anaimudu vizuri na namtakia kila la heri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi ninazungumzia hasa sehemu za bandari kwanza. Mheshimiwa Waziri kaeleza katika hotuba yake, namna gani alivyojidhatiti katika kuimarisha uchumi kupitia katika bandari zetu. Kwa kweli bandari ni sehemu moja kubwa katika kutuletea uchumi wa taifa letu na naamini tukizishughulikia ipasavyo kufuatana na taratibu zake za kimataifa, naamini tutapata nafasi kubwa sana kuongeza uchumi kupitia katika bandari zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Bandari ya Dar es Salaam, pia inahitaji maangalizi mazuri pamoja na hali iliyoko sasa siyo mbaya lakini inahitaji maangalizi mazuri hasa katika vifaa vya upakuaji mizigo katika meli yaani winji na kadhalika na vifaa vyote vya kitaalam. Ndiyo hivyo hivyo ninavyomshauri Waziri katika Bandari ya Tanga, hizi ni bandari zetu kubwa na ndizo zitaweza kutusaidia zaidi katika uchumi.

Lakini pia tusisahau bandari zetu ndogo ndogo kama bandari ya Mtwara, Bandari ya Lindi, Bandari Kilwa na zingine. Lakini pia siwezi kuisahau Zanzibar, kwa sababu tunazungumzia masuala haya ya uchumi kwa Tanzania hatuzungumzii uchumi Tanganyika, tunazungumza uchumi kwa Tanzania. Kama ni Tanzania tuna wajibu kuiangalia Zanzibar ili kunyanyua katika hali ambayo iliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Zanzibar kibandari, si suala la Kimuungano, lakini yanazungumzika haya katika masuala ya Kimuungano. Naamini yataendelea kuzungumzika kwa sababu naamini kwamba kwa juhudi ya Waziri, anakuwa karibu kila wakati na Waziri mwenzake katika kubadilishana mawazo fikra na namna gani kunyanyua uchumi wa Taifa letu. Kwa hiyo, ningemwomba Waziri aliangalie kwa sababu niliona jana hotuba ya Mheshimiwa Waziri Magufuli jinsi aliyoigusia Zanzibar kaigusia kweli kweli Zanzibar jana. Kaikamata kama kweli mdogo wake hasa ambaye hataki kumwacha njiani. Vile vile ndivyo tunavyotakiwa kufanya. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nafikiri Waziri sikusahau maana umegusa pia *airport* ya Zanzibar imeelezwa pia kwamba Zanzibar nayo umeiona. Kwa hiyo, mfano ule wa Mheshimiwa Magufuli ndiyo mfano ambao ninaamini na wewe unakwenda nao na naamini utaendelea kwenda nao. Zanzibar haina nafasi ya kujitegemea zaidi kuliko ilivyokuwa ikijitegemea zamani katika uchumi wake. Ilikuwa ni *spices* tu Zanzibar ndiyo uchumi wake. Uondoke kwenye karafuu, mbata, pilipili nani anataka *spices* sasa hivi? Hata Indonesia walikuwa wakinunua karafu Zanzibar sasa hawataki wamepanda mikarafu kama mwitu wa porini ingawaje karafu yao siyo kama *quality* ya kwetu, lakini wananunua kidogo tu wanachanganyia mle wanafanya mambo yao. Sasa ukitazama Zanzibar iende wapi, kweli Zanzibar itajiimarisha kwa *tourism* peke yake ndiyo itaweza kuongoza taifa la Zanzibar? Nadhani kuna haja sana Mheshimiwa Waziri uliangalie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tukizungumzia juu ya hizo hizo bandari sasa tukubali kwamba wakati umefika pia tunapoimarisha bandari zetu, basi tuimarishe na hali ya usalama wa bandari zenyewe. Kama inatokea janga Mungu atuepushe salama pasitokee moto kwa zile *tanker* zinazokuja kutia mafuta hapa kwetu. Kama inatokea ajali naamini hatuna *fire fighting boat* za kuwenda kushambulia hali ile iliyoko kule. Kwa maana hiyo, ile tunayoita bandari ya kimataifa tutakuwa tumeipunguzia hadhi yake. Kwa hiyo,

Mheshimiwa Waziri, tuone hilo, tusibaki na vyombo vya kubaki na *fire fighting* za nchi kavu lakini tufikirie sasa *fire fighting* za kwenda kupambana na janga linaloweza kutokea baharini. Vyombo vyetu vimejaa pale inaweza ajali yoyote ya bandari kutokea pale. Panatokea *tank* moja kushika moto pale basi tuhakikishe kwamba bandari yetu yote iko katika hali ya hatari. Kwa hiyo, lazima tuwe wepesina vyombo vya kwenda kuvamia moto. Vile vile kupatikana vyombo vya uokozi *rescue board* ambazo hizi ni muhimu kulingana na mambo yote ya baharini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, labda niendelee kwenye viwanja vyetu vya ndege japo kwamba ndugu yangu amezungumza sana, lakini mimi nazungumzia usalama hasa wa pale kwenye viwanja vyetu. Viwanja vikubwa ni cha Dar es Salaam na kule Kilimanjaro.

Lakini sisi Kamati ya Ulinzi na Usalama tulifanya ziara si kipindi kirefu sana na tuliona kuna haja ya kuimarishwa baadhi ya mambo hasa katika mambo ya *fire fighting* tuimarishe. Sitaki kuzungumza hali tulivyoikuta kule jinsi ilivyo, tumekaa tumejadili tumezungumza. Lakini nakuomba sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na kwamba kuna nia ya kununuliwa vyombo vipya vya kusaidia mambo haya lakini naomba sana tujitahidi ile ule mpango wake uliopangiwa katika *category* yake iliyowekwa basi isiteremke ibaki pale pale au izidi zaidi ya Kimataifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nizungumzie juu ya Chuo cha *DMI.* Kwanza nampongeza Waziri kama nilivyompongeza mwanzo na Naibu wake kwa juhudi kubwa wanazokiimarisha chuo hiki. Chuo hiki ni sehemu kubwa ya maendeleo ya taifa letu kwa sababu pale ndipo tunapopata hawa wote tunaozungumzia kwa mambo yetu ya mwambao wa bahari. Namshukuru sana Waziri kukifanya chuo hiki sasa hivi kuwa Chuo cha Kimataifa. Lakini nimshukuru *principal* wa chuo kile na nimpongeze kwa kazi yake yeye na wataalam wake, maana yeye hakai kitako katika kutafuta maendeleo ya chuo kile, anajitahidi kwa uwezo wake wote katika kukitafutia maendeleo, halali katika kukiimarisha chuo. Nampongeza sana na kumsifu huku nataka aendelee na juhudi zaidi. *(Makofi)*

Lakini chuo kinahitaji misaada kadhaa. Hivi sasa chuo kina mpango wa kuimarisha mpaka mambo ya *training* za *diving* (Uzamiaji). Sasa hivi zinahitaji vifaa. Nashukuru wamepata msaada wa kulipata *D compression chamber* ambalo hili ndiyo hili linaweza kuwafundisha ma-*drivers.* Lakini tukitazama eneo lenyewe lile pale haliwezi kututosheleza. Kwa hiyo, naomba sana Waziri kuna sehemu ilishazungumzwa ili kukipatia nafasi chuo na kuweza kukipanua kutokana na nafasi ndogo iliyoko pale, kwa nafasi hiyo, Mheshimiwa Waziri, nakuomba kupitia kwa Mheshimiwa Spika, ulisimamie ili lile eneo tulipate ili liweze kuimarisha Chuo chetu cha *DMI. (Makofi)*

Aidha ningeliomba vile vile tukipe nafasi chuo hiki katika kukiimarisha zaidi kwa sababu tunatoa mabaharia wazuri, tunapata ma-*able seaman* ambao wanakubalika kufanya kazi wote kimataifa. Kwa hiyo, lazima kiimarishwe katika kuwapata hao. Pia kuwapata manahodha wazuri tunawapata kutoka pale yaani waongozi wa meli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho ningeomba kumshauri Waziri umefika wakati sasa Mheshimiwa Waziri ukaunda chombo kinachoweza kusaidia katika hali ya *emergency.* Panapotokea *emergency* katika taifa lazima tuwe tuna kikundi kinachoweza kukabili hali hiyo, mfano nchi yetu ikiingia janga la vita lazima vijana wawe tayari kuziweza kuzidhibiti boti na kusafirisha meli za pale, kuzisafirisha vizuri, kuweza kupakia na kupakua mizigo kama kawaida, pamoja na mambo mengineyo kama hayo.

Vile vile kunapotokea matatizo ya migomo, hatusemi kwamba watu wasigome, kugoma ni moja katika demokrasia na kukua kwa demokrasia, lakini kunaweza kutokea migomo mingine ya ovyo ovyo tu. Sasa ikitokea kama ile lazima tuwe na vijana wanaoweza kuzisafirisha zile treni zetu, waweze kuikabili hali ile mpaka tatizo lao wanalogoma likamilishwe. Likishakamilishwa wataendelea na kazi zao, lakini isiwe nchi ime-*collapse* kwa sababu ya kugoma kwa kikundi fulani. Hiyo nakushauri sana Waziri umefika wakati sasa hivi ufanye kitu kama hicho ili kuhimili yanapotokea madhara na matatizo kama hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa dakika zilizobakia ni chache, napenda kutoa kauli ya kupongeza hotuba ya Waziri pamoja na kuiunga mkono kwa asilimia mia kwa mia. Lakini mwisho kabisa nampongeza sana Mheshimiwa Danhi Makanga kwa kuingia na yeye katika ukumbi huu tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, narejea kusema naipongeza hotuba hii mimi na wana jimbo wangu wote wanaipongeza na wanaiunga mkono *speech* yako. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. THADEUS LUOGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie machache kwenye hotuba nzuri ya Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi. *(Makofi)*

Kabla sijaanza kuchangia na mimi nitumie nafasi hii kutoa pole nyingi sana kwa familia na wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini, kwa kifo cha Mheshimiwa Yete Mwalyeko. Naomba Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema peponi. *Amen.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, natoa pole nyingi sana kwa Waheshimiwa Wabunge wote waliofiwa na waliopata matatizo mbalimbali naomba Mwenyezi Mungu, awape nguvu ya kuweza kuvumilia matatizo yote waliyopata.

Mheshimiwa Spika, kwanza natoa pongezi nyingi sana kwa hotuba ya Mheshimiwa Waziri, hotuba ambayo imechambuliwa kwa kina, kila vipengele imechambua na kutokana na uchambuzi wake mzuri, inatupa nafasi sisi kujadili. Mimi natoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watalaam wote wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ina majukumu mazito na muhimu katika maendeleo ya nchi yetu. Wizara ina wachapakazi wazuri, inaongozwa na kiongozi

mwenye upeo wa hali ya juu sana. Lakini ni nini kinachokwamisha Wizara kutekeleza majukumu yake ipasavyo? Tatizo kubwa Wizara hii inakosa uwezo. Ukiangalia katika Bajeti ya mwaka huu Wizara iliomba bilioni 30 ili iweze kutekeleza mipango yake ya maendeleo kamili, lakini nini hazina imetoa? Hazina imetoa asilimia 6.3. Sasa angalia kutoka bilioni 30 unapewa shilingi bilioni 1.9 utafanya nini? Mimi naishauri hazina itoe fedha za kutosha ili Wizara iweze kukamilisha majukumu yake. Huwezi kufanya chochote kizuri kama hujawezeshwa. Ni hatua moja ya kwanza muhimu na inatakiwa ifanyike kwa makini ili Wizara iweze kutekeleza majukumu yake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jingine nataka kuchangia juu ya ubinafsishaji wa Shirika la *TRC,* pamoja na Shirika la *Marine Service Company Limited* nianze na shirika la railway *TRC.* Shirika la *TRC* litakodishwa na yeyote anayetaka kukodi anataka kufanya biashara hataki kutoa sadaka na huwezi kukodisha kitu ama mradi utakaokuletea hasara. Sasa shirika baada ya kuweka kwenye *PSRC* hakuna uwekezaji wowote unaokwenda huko.

Shirika liko katika hali ngumu, shirika halina mabehewa, shirika *engine* zake ni mbovu, njia (reli) ni mbovu. Sasa nani atakayeweza kukubali kukodi shirika hilo ili aweze kupata hasara? *(Makofi)*

Kwa kuwa Serikali inakodisha hilo shirika haiuzi inakodisha, inakuwa miundombinu yote bado ni mali ya Serikali. Kwa hiyo, kwa nini sasa Serikali haiwekezi? Mimi naishauri sana Serikali iwekeze katika Shirika la *Railway,* iwekeze kwenye mabehewa, iwekeze kwenye *engine* itengeneze reli ili mwekazaji atakapokuja hapo akute miundombinu imekamilika na hata kama atakodisha, miundo mbinu itakuwa bado ni mali ya Serikali, bado ni mali ya nchi hii, kwa hiyo, ili zoezi hili liweze kwenda vizuri Serikali iwekeze. *(Makofi)*

Ni ajabu kabisa ukiangalia mwaka wa fedha uliopita Serikali ilitenga shilingi milioni 300 kwa ajili ya Shirika. Mimi nilitegemea mwaka huu shirika lingepewa fedha nyingi zaidi badala ya kupata fedha nyingi Serikali imetenga shilingi milioni 200 kutoka milioni 300 inashuka, sijui mwakani Serikali itatenga sijui milioni 100. Ni vema tusitegemee huyu mkodishaji ndiyo atakayekuja kuleta ukombozi katika shirika hili, hakuna mtu yeyote ama mfanyabiashara yoyote anakodi kitu, lengo la kupata hasara, anakodisha apate faida, siyo apate hasara. Kwa hiyo, Serikali iwekeze kwenye shirika hili. Ifanye juu chini iimarishe miundombinu, iimarishe mabehewa, iimarishe injili za *TRC* ili liweze kupata mwekezaji atakayeweza kuliendesha shirika kadri ya mkataba utakavyokuwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la pili niongelee juu ya *Marine Service Company. Marine Service Company* nayo iko katika utaratibu wa kubinafsishwa, meli zote zinazotoa huduma katika maziwa yote matatu zitabinafsishwa. Sipingi zoezi la kubinafsisha, lakini ninachosema inategemea sasa hizo meli zinafanya kazi katika mazingira gani. nikitoa mfano meli zinazotoa huduma katika Ziwa Nyasa tuna meli mbili *MV Songea* na *MV Iringa.* Hizi meli hazifanyi biashara, hizi meli zinatoa huduma. Sasa hakuna mwekezaji atakayekubali achukue hizo meli ili atoe huduma katika ziwa hili. Mwekezaji lengo lake kubwa anataka afanye biashara na bahati mbaya meli hizo zote sasa hivi zimechakaa na

mbaya zaidi hatuna mahali pa kutengeneza hizo meli katika ziwa nyasa. Kwa sababu zimechakaa tunapata huduma ya matengenezo Malawi. Ili tupate nafasi ya kuzitengeneza meli kama sehemu yao inatumika muda mwingi unapita kupata nafasi. *(Makofi)*

Sasa katika hali hiyo ningeiomba sana Serikali iwadhamini *Marine Service Company,* inunue meli moja walau kubwa kuimarisha huduma katika Ziwa Nyasa badala ya kutegemea hizi meli mbili. Ni meli ambazo zimechakaa na mara kwa mara huwa zinaharibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni kwamba, hizi meli zinatoa huduma Mwambao wa Ziwa Nyasa na kuna bandari moja. Hizi meli zamani zilikuwa zinasimama, lakini sasa hazisimami. Hiyo bandari ni ya Ndumi. Ni kweli Wizara ilituma wataalam kukagua hiyo bandari na wakaona kuna matatizo, lakini naiomba sana Serikali iwapeleke wataalam wanaoweza kufanya kazi ya kusafirisha hiyo bandari ili Wananchi wa sehemu hiyo waweze kuendelea kupata huduma ya meli hizo zinazotoa huduma Ziwa Nyasa. Vile vile, natoa shukrani nyingi sana, pia pongezi nyingi sana kwa Waziri kwa kuanza kutengeneza magati katika Ziwa Nyasa. Gati la *Mbamba Bay* na gati la Manda. Jambo ninaloweza kusema hapa ni kwamba, shughuli yenyewe kwa kweli inakwenda polepole sana. Kwa mfano toka mwaka jana wameanza ile gati ya *Mbamba Bay* hadi leo hii hali bado haijakamilika, sielewi itakamilika lini. Kwa hiyo, ningeomba shughuli hizi zingefanywa kwa haraka. *(Makofi)*

Pia, napenda niongelee juu ya Kiwanja cha Ndege cha Songea. Tuna kiwanja cha ndege kizuri, kimegharimiwa pesa nyingi, lakini hakuna ndege inayotua hapo! Tumeomba mara nyingi *route* ya Mtwara, badala ya ile ndege kuishia Mtwara ingefika moja kwa moja hadi Songea. Kama abiria wa Mkoa wa Ruvuma peke yao hawawezi kutumia *route* yao moja kwa moja kutoka Dar es Salaam hadi Songea, basi walau ile ndege inayofika Mtwara badala ya kuishia Mtwara ikafika hadi Songea ili Wananchi wa Ruvuma nao wakaweza kupata huduma ya ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ombi lingine la pili ni juu ya simu. *TTCL* tunashukuru tumepata *digital system* Mjini Mbinga, lakini simu za mkorogo bado zinatumika *Mbamba Bay,* Liuli na Litembo. Tungeomba tupate simu za kisasa katika sehemu hizo. Vile vile, katika hizi simu za mkononi tunapata huduma ya *Celtel,* lakini tungeomba pia Makampuni mengine yangekuja kutoa huduma Mbinga na yakaweza kutoa huduma katika Vijiji vyote hasa *centre* zote za biashara katika Wilaya yetu ya Mbinga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naunga mkono hotuba ya Mheshimiwa Waziri kwa asilimia mia moja. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA O. KIMBAU:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii iliyo mbele yetu ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Lakini pia, ningependa kutoa pole kwa wale wote ambao wamefiwa. Aidha, ningependa kutoa pole nyingi sana kwa ndugu zetu wa Wilaya ya Mbeya Vijijini kwa kumpoteza Mbunge wao au mwenzetu Mheshimiwa Yete Mwalyego.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Yete Mwalyego nitamkumbuka sana hasa kwa kipindi hiki alipokuwa mmoja kati ya Wajumbe wa Kamati ya Miundombinu. Mheshimiwa huyu alifika Mafia na alitoa ushauri wake wa kitaalam. Pamoja na kwamba walikuwepo Wataalam wa Viwanja vya Ndege, lakini na yeye alijaribu kusaidia kwani kutokana na maelezo yake Marehemu alisema kwamba alishiriki katika ujenzi wa Kiwanja cha Songo Songo. Kwa hiyo, alitoa ushauri wa kuona kwamba Kiwanja cha Mafia hakiwezi kutengenezwa katika ile hali ambayo sisi tunajaribu kukitengeneza kwa kutumia udongo ule, kwa kutumia chokaa na kwa kutumia *cement* ambayo tulikuwa tunajaribu kuchanganya. Kwa hiyo, kila siku nasema nitamkumbuka Mheshimiwa huyu baada ya kuona wataalam wa Wizara hiyo husika na wale Wajenzi wa Kiwanja cha Mafia kama watafuata mawazo ya Mheshimiwa na kuona kwamba Mafia tunapata kiwanja kinachofanana na cha Songo Songo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia ningependa kutoa pole kwa wenzetu wote ambao wamepata matatizo barabarani akiwemo Mheshimiwa Kilango ambaye amenusurika kupata matatizo yaliyosababishwa na majambazi, Mheshimiwa Makongoro Nyerere ambaye amepata matatizo ya ajali pamoja na Mheshimiwa Kilasi. Mungu awajaalie wote wanusurike na balaa hizo na nyinginezo.

Mheshimiwa Spika, ningependa kutoa pongezi nyingi sana kwa Mheshimiwa Makanga na hususan kwa Chama cha CCM kwa kupata ushindi wa kishindo katika Wilaya ya Bariadi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia, kwa masikitiko makubwa napenda kutoa pole kwa ndugu zangu wa Mkoa wa Tanga kwa kumpoteza Mwenyekiti Mahiri wa Chama cha Mapinduzi (Mkoa). Mungu amlaze mahali pema peponi, Mheshimiwa Mwenyekiti wetu wa Mkoa wa Tanga.

Mheshimiwa Spika, napenda kuungana na Mheshimiwa Mbunge wa Mafia kwa kuwashukuru sana, sana, sana, Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na wale wenzetu wote kutoka *THA* na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege. Kwa kweli jitihada yao ya kuona kwamba Mafia tunapatiwa gati na tunapatiwa kiwanja imeonekana wazi kabisa kwamba sasa hivi wako mbioni kuona kuwa na sisi watu wa Mafia tunaondoka katika umaskini, kwani wote kama tunavyofahamu kwamba miundombinu ni njia moja ya kuondoa umaskini. Kwa hiyo, najua haya yakikamilika basi Wananchi wa Mafia na sisi tutaondokana na umaskini kwa kutumia miundombinu ambayo wenzetu wamefaidika nayo kwa miaka mingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nisingependa kurudia yale ambayo mwenzangu Mheshimiwa Mbunge wa Mafia, ambaye bahati nzuri tunaishi wote Mafia ameyasema. Kwa kuokoa muda, ningependa kuongelea juu ya suala la simu za mkorogo. Tunawashukuru sana watu wa *Celtel* kwa kujaribu kutuwekea simu. Maana mtu akijaribu halafu akishindwa kama alivyosema Mheshimiwa Shah kuwa, mtu naye akikupa kidogo basi mshukuru kwamba angalau alikuja kujaribu. Watu wa *Celtel* walikuja kujaribu kuona wangewezaje kutusaidia kutuwekea simu za *Celtel.*

Mheshimiwa Spika, wenzetu wa *Vodacom* wamejaribu na wamefanikiwa. Kwa hiyo, nawashukuru sana na ninawapongeza, lakini nina imani na wengine nao watachukua ujasiri kama wa *Vodacom* kuja kutuwekea simu za *Celtel* na simu za *Mobitel.* Lakini na Mheshimiwa Waziri kupitia *TTCL* hebu aone basi kwamba hizi simu za mkorogo nazo zinaondoka Mafia. Sasa hivi wenzetu wanaongelea habari ya *pre-paid,* sisi bado tunaongelea kuondoshewa simu ya mkorogo. Kwakuwa wanakuja kufanya shughuli zao za Bandari kuweza kututayarishia ujenzi wa gati, tutoe ushirikiano kikamilifu. Tunajua ujenzi wa gati utawasaidia wengi, lakini pia utawaathiri wachache na ninasema hili wote tukiwa makini kabisa kwamba sasa hivi kuna baadhi ya vyombo ambavyo vinatoa huduma ya usafirishaji kati ya Mafia na Dar es Salaam na vyombo hivi havina *insurance,* si vyombo vya uhakika, lakini bado wenzetu ambao wanamiliki vyombo hivyo wanapata maisha yao kwa ajili ya biashara hiyo. Sasa tuone basi kwamba, pamoja na kwamba wao wanafaidika na biashara hiyo, lakini bado sisi watu wa Mafia tunaathirika na usafiri kwa kutumia vyombo hivyo ambavyo havina *insurance* wala havina hakika, vingine vinatumia tu upepo. Basi wote tuwe pamoja kwa kushirikiana na wenzetu ambao watakuja kutujengea gati kuwapa ushirikiano na kuona kwamba kweli gati linajengwa ili tuweze kupata vyombo vya uhakika, vyombo vya usalama na vyombo ambavyo vitatusaidia sisi kiuchumi na kimaendeleo katika Wilaya yetu.

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda kurudia kusema nawashukuru sana, sana, wenzetu wa Kamati ya Miundombinu kwa kutoa pia na wao ushauri kwa Serikali yetu juu ya gati la Mafia na juu ya Kiwanja cha Ndege cha Mafia. Ninaamini sasa hivi Mafia haitaongelewa tena na sisi tunaoishi Mafia, lakini itaongelewa pamoja na wale wenzetu waliotoka Mbeya Vijijini, waliotoka Lushoto, maana Mheshimiwa Makamu wa Mwenyekiti wa Kamati hiyo naye alifika Mafia, Mheshimiwa Watondoha, watu wa Lindi huko nao wataongelea juu ya Mafia. Kwa hiyo, kwa umoja wetu huo, basi nina hakika ushauri wetu sisi pamoja na ushauri wa Kamati utazingatiwa na Serikali yetu kuhakikisha kwamba Mafia tunaondokana na matatizo ambayo yamekuwa sugu kwa muda mrefu na ni kero kubwa kwa Wananchi wa Mafia.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, kwa heshima na taadhima naendelea kuwashukuru wale wote ambao wameshiriki katika kuchangia juu ya Mafia. Lakini pia, napenda kutamka kwamba naunga mkono hoja hii ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi na kuwatakia kila la kheri kwenye kazi zao ili waweze kukamilisha yale yote ambayo wameyapanga. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja na ninakushukuru sana kwa nafasi ya kuchangia uliyonipa. *(Makofi)*

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, nami naomba nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa fursa ya kuweza kuchangia katika hoja hii.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa ni mara yangu ya kwanza kuzungumza katika Bunge hili, basi naomba niende moja kwa moja kutoa salam za rambirambi na pole kwa wenzetu Wananchi wa Jimbo la Mbeya Vijijini, pamoja na familia ya aliyekuwa

Mheshimiwa Mbunge, Marehemu Mwalyego, kwa kufariki dunia ghafla akiwa katika kikao hiki cha Bajeti. Nimesimama kwa lengo la kutaka kuunga mkono hoja na ninampongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara husika pamoja na wasaidizi wake wote kwa kazi nzuri ambayo wameifanya ikiwa imejiashiria katika hotuba aliyoiwasilisha kwa ufasaha Mheshimiwa Waziri Profesa Mwandosya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ninapenda kwanza nianze kwa kuipongeza Wizara kwa kazi kubwa ambayo imeifanya katika kuboresha usafiri wa vyombo vya majini na nitazungumzia kuhusu Ziwa Victoria. Katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri ametueleza kwamba, sasa hivi miongoni mwa harakati ambazo alikuwa amezianza miaka mitatu tangu tumeingia Bungeni za kuboresha usafiri katika Ziwa Victoria, sasa amefanikiwa kuzipata meli mbili ambazo wawekezaji wameishakubali, zimeishafika Dar es Salaam na zitasafirishwa wakati wowote mwezi huu kuelekea Mwanza ili zikaanze kufanya kazi katika Ziwa Victoria ambapo zitakuwa zinatoa usafiri wa kutoka Mwanza kuelekea Bukoba na uwezo wake utakuwa ni wa kuchukua abiria 90 na vile vile zitakuwa zinachukua mizigo. Huu ni ukombozi mkubwa kwa Wananchi wanaoishi kando kando ya Ziwa Victoria, lakini vile vile na wale waishio katika visiwa vya ndani ya Ziwa Victoria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika maeneo ya Jimbo la Muleba Kaskazini, mojawapo ya eneo kubwa la Jimbo lile limemilikiwa na maji. Eneo hilo kwa kipindi kirefu sana limekuwa na matatizo ya usafiri wa Wananchi waishio kule ndani ya visiwa, wavuvi wanaofanya kazi zao kule, lakini kwa msingi huo uchumi wao umekuwa haukui ipasavyo kwa sababu ya kutokuwa na usafiri wa uhakika kutoka nchi kavu kwenda katika visiwa na kutoka katika visiwa kwenda nchi kavu. Lakini vile vile, kumekuwa na matatizo ya mawasiliano katika Mikoa iliyo jirani na hata nchi jirani hasa kwa wavuvi wadogo ukizingatia kwamba meli iliyokuwa inafanya kazi katika ziwa ni ile ya *MV Victoria.*

Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo, meli hizi zinakuja kwa wakati ambao ni muafaka na kweli Wananchi na mimi tunashangilia na tunafurahia. Tunachoomba sasa ni kwamba, Julai 2004 mwishoni bado siku 29, basi uwezekano uwepo hizo meli zije zifanye kazi na sisi tutakuwa tayari kushirikiana nao. Nami nawahamasisha Wananchi wa maeneo hayo kutumia meli hizi vizuri kwa sababu baada ya mipaka ya nchi yetu kufunguliwa sasa katika Afrika Mashariki, kama Wananchi wa nchi yetu hawatachangamkia huduma nzuri kama hizi, basi watakuwa wanatoa nafasi kwa wale Wananchi wa nchi nyingine, nchi jirani ambazo tunashirikiana nazo kuja kubeba kwa sehemu kubwa uchumi hasa wa ziwa kwa Mikoa inayozunguka ziwa. Nashukuru pia kwa kitu kingine ambacho nakiona ni muujiza. Ni muujiza kuona kwamba gati la Kyamkwikwi katika Jimbo la Muleba Kaskazini nalo limo katika Bajeti ya kutengenezwa mwaka huu 2004! Kwa kweli ni muujiza kwa sababu ni eneo ambalo lilikuwa limekaa tu, linaweza kuwa na watu wengi, lakini lilikuwa linaonekana kwamba halikuwa rahisi kuweza kuingia katika Bajeti ya kipindi cha miaka hii mitano.

Kwa hiyo, nampongeza Mheshimiwa Waziri na ninaomba sasa watakapoanza ujenzi ushirikiano wa karibu na TAMISEMI pamoja na Wizara ya Ardhi uwepo ili mazingira ya Kyamkwikwi yafanane ili kupata uwezo wa kuweza kuhudumia watu

ambao wanaweza kuwa kati ya 180 na 360 au zaidi kulingana na kwa kiasi gani zile meli zitakuwa zinaweza kufanya safari zake katika lile gati la Kyamkwikwi, kwa maana kwamba mwelekeo siyo kuishia kupata gati, ila uelekeo ni kuandaa bandari nzuri itakayoweza kutoa huduma nzuri zitakazoweza kuboresha uchumi wa Wananchi, lakini na kubadilisha mazingira.

Pia, meli hizi zitasaidia sana kwa sababu kwa sasa hivi Mkoa wa Kagera umeanzisha kivutio cha utalii na kuna Wananchi wameanzisha niseme Kampuni inaitwa Kiroyela ambayo imejulikana kwa haraka na kazi yake inaendelea vizuri na ndani ya Ziwa Victoria kuna vituo vingine ambavyo itakuwa ni rahisi kuvifikia na vitaboreshwa baada ya kuwa na usafiri wa uhakika wa vyombo hivi. Baada ya hapo, nitamwomba Waziri kwa kipindi kijacho pia aiangalie gati ya Rwazi ambayo nayo ni nzuri, imekwishapata barabara inafika mpaka kwenye ziwa kabisa na ina wavuvi. Watu wa eneo lile ni wavuvi wazuri, lakini gati lao si la kisasa, halijaendelezwa. Basi umefika wakati muafaka atume wataalam wake pia waangalie ili kuweza kutusaidia kuboresha eneo hilo tena, kwani itaharakisha kukua kwa uchumi wa Wananchi wa eneo husika na majirani.

Mheshimiwa Spika, labda jambo dogo ambalo napenda nilizungumze kuhusu usafiri wa majini ni kwamba, sijasikia vizuri ama labda sijasoma, sikulikuta hilo eneo linaloelezea usalama wa watu wanaosafiri ndani ya vyombo vya majini pamoja na mali zao. Kwa vipindi mbalimbali tumekuwa tukipatwa na majanga ya Kitaifa kwa kupoteza abiria wanaosafiri ndani ya vyombo kama meli zikiwemo pia hata treni, lakini kwa mara zote wamekuwa wakipata fidia inavyoitwa 'kifuta machozi' kitu ambacho sifahamu ni kifungu gani kinachosema kifuta machozi. Pengine ilikuwa ni hali tu ya kuona ubinadamu utendekekama hivi ulivyo uwanja ule ni mgumu kuupanua na hivyo kama uwanja hauwezi kupanuka, ndege zile zinazoweza kubeba mizigo mikubwa na zinazoingizia Taifa pesa nyingi haziwezi kufanya kazi kwani haziwezi kutua pale kwa sababu uwanja unakuwa ni mfupi na siyo imara. Ninaamini kwamba hayo yakishakuwa yamewekwa vizuri basi mambo mengi yatakwenda vizuri, uchumi wa Wananchi wa Kagera utaboreka na mawasiliano yatakuwa ni mazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa nimechangia katikati bado najua na wenzangu wataendelea kuchangia. Basi kwa hayo ambayo nimeyazungumza ninarudia kuipa shukrani Serikali na nawatakia utekelezaji mwema wa Bajeti hii Wizara nzima wakiongozwa na Waziri, Mheshimiwa Prof. Mwandosya, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari na wote wanaoshiriki katika utendaji kazi katika Wizara husika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, narudia kwa kusema ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Spika, na mimi ninashukuru kwa kunipa nafasi hii kwani ni mara ya pili sasa ili niweze kuchangia hoja iliyopo mbele yetu ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa kweli Kamati yetu ya Miundombinu imempoteza mpiganaji na msemaji mkuu wa Wilaya ya Mbeya Vijijini, Yete Sintemule Mwalyego na ni mtu ambaye amesemea sana masuala ya msingi kama kiwanja cha ndege cha Songwe. Mimi nina uhakika alikuwa amezungumza na Mheshimiwa Waziri masuala fulani kuhusu uwanja huu na alikuwa amezungumza na Waziri wa Fedha kuhusu suala hili. Naomba Wizara hii ili kumuenzi basi yale aliyokuwa ameyaomba Wizara hii ikae ione ni jinsi gani ya kutekeleza yale mawazo aliyokuwa anayabeba, yale aliyokuwa anayazungumzia waone jinsi ya kuweza kuyatekeleza ili kumpa heshima na kumuenzi kwa kazi nzuri aliyokuwa anaifanya kutoa ushauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kalambo Mkoa wa Rukwa kwa kweli tunapeleka salamu za pole kwa familia ya Marehemu ya Mwalyego na tunasema Mungu aipumzishe roho yake mahali pema Peponi, *Amina.*

Mheshimiwa Spika, nikija katika masuala ya Jimbo langu la Kalambo nazungumzia juu gati ya Kasanga. Nashukuru sana Serikali ambayo imeingiza katika mpango wake kuweza kuikarabati gati ya Kasanga. Gati hii ni muhimu sana hasa tunapozungumzia uchumi wa kijiografia. Tunapozungumzia uchumi wa kijiografia ni kwamba Tanzania kama nchi tumekaa mahali ambapo tunaweza kutumia nchi jirani zinazotuzunguka tukaweza kutumia miundombinu tunayokuwanayo kuweza kupata fedha nyingi sana kutoka kwa majirani zetu. Mawasiliano ya reli, barabara, simu, posta na vitu vingine. Vinatuweka katika mazingira ya kuweza kutumia nafasi hii ya kuwepo katika eneo hili kupata uchumi wa *DRC,* Zambia, Malawi, Rwanda, Burundi, Uganda kwa urahisi sana tukaweza kupata fedha nyingi sana.

Mheshimiwa Spika, mzigo uliopo Kongo wala hautoshelezi kupitishwa katika reli ya Kati-Kigoma kwenda Dar es Salaam. Tukifungua gati ya Kasanga tukaijenga vizuri, tukajenga barabara kutoka Kasanga-Sumbawanga-Tunduma tukafika mpaka kwenye *TAZARA* ili tuweze kuunganishia pale, nina uhakika kwamba uchumi wa nchi hii utaanza kukua haraka sana. Pamoja na hali ya gati ya Kasanga ilivyo, ni mbovu ni mbaya lakini ukienda leo pale uone mzigo unaoteremka pale, na mzigo unaopandishwa katika meli hasa *cement* kutoka Kiwanda cha Saruji Mbeya kwenda kuuzwa Burundi na *DRC* utashangaa kwamba kwa nini muda wote tulikuwa tunapuuzia mambo haya. Mheshimiwa Waziri nakuomba kwa juhudi zako zote hebu fungua uchumi wa kijiografia katika gati hii ya Kasanga. Maajabu mtayaona na nchi hii itapata fedha nyingi sana kutoka nchi zetu jirani kwa sababu tumekaa mahali pazuri na tukichelewa wapo maadui zetu ambao wanataka kuifungua Ziwa Tanganyika waifunguie kwa njia nyingine ili waweze kuchukua uchumi wa nchi hizi na kuupeleka katika nchi ya Afrika Kusini kumbe sisi tukiwa wa kwanza kufungua uchumi huu wa kijiografia kwa mawasiliano haya nina uhakika kabisa mambo yatakuwa mazuri.

Mheshimiwa Spika, lakini gati ya Kasanga inahitaji huduma. Tunahitaji tupate umeme ili shughuli ziweze kwenda vizuri. Tunahitaji zana za kupakua na kupakulia pale ili shughuli ziweze kwenda haraka. Barabara inayounganisha pale iwe nzuri. Tupate majengo ya kuweza kuendeshea utawala wa gati pamoja na vifaa vinavyotelemshwa pale, bidhaa za biashara majengo yaweze kujengwa.

Mhehsimiwa Spika, lakini pia na pale papimwe ili majengo yaweze kujengwa sambamba na gati ili bidhaa ziweze kuwekwa mahali ambapo haziwezi kuharabika kama mvua na hali mbaya ya jua na kitu gani. Kumbe tunaomba vitu vyote hivi viende sambamba ili ujenzi wa gati uende sambamba na upanukaji wa biashara ambayo inategemewa kuwa inaweza kupatikana.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Ziwa Tanganyika kwa ujumla. Ziwa Tanganyika ina gati mbili, ni Kigoma na Kasanga ambayo bado imewekwa katika mpango huu. Tunaomba Serikali pamoja na kuzungumza kuhusu suala la Gati ya Kalema, lakini ipo pia Nanikipili. Sehemu hizi zingeweza kujengwa gati, zingeweza kusaidia sana kufungua uchumi wa kijiografia tunaouzungumza ili nchi ya *DRC* iweze kuwa na *outlet* nyingi yaani sehemu nyingi za kuweza kuingizia mizigo yake ili kuweza kuiongezea Bandari ya Dar es Salaam uwezo wa kupata mizigo mingi zaidi. Kumbe kufungua gati pale ni kuiongezea Bandari ya Dar es Salaam uwezo wa kupata mizigo mingi zaidi ili iweze kufanya kazi ya kibiashara vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nizugumzie kuhusu suala la Reli ya *TAZARA*. Suala ya reli ya *TAZARA* ndiyo hilo ambalo tumekuwa tukilizungumzia kuhusu matatizo ya reli ile. Sasa Zambia majirani zetu taarifa tulizonazo ni kwamba wameshaiuza ile reli yao, wamekwishaikodisha kwa Afrika Kusini. Sasa mizigo tuliyokuwa tunategemea kutoka Zambia mingi sasa haipiti bandari ya Dar es Salaam inakwenda Durban Afrika Kusini. Ni kwamba tumepoteza biashara.

Sasa reli tunayoizungumza ya *TAZARA* ni kutoka Tunduma kuja Dar es Salaam. Sasa tuna mizigo gani itakayoweza kuingia katika bandari ya Dar es Salaam ili iweze kupata mzigo. Ni lazima tutafute njia nyingine ya kuweza kui-*feed* hii kuiwekea mizigo mingi zaidi ni pamoja na kufungua gati ya Kasanga pamoja na barabara yake ili mizigo iweze kutoka *DRC* moja kwa moja ije ipandishiwe katika reli ya pale Tunduma.

Mheshimiwa Spika, *DRC* walishaonyesha nia njema kabisa kwamba wako tayari kuweza kusaidia kuimarisha barabara au hata kujenga reli kutoka Tunduma kwenda Kasanga ili tuweze kupata mizigo mingi ya kutosha huko. Mimi nina uhakika kabisa kama umbali huu wa kilomita 270 au 300 reli ingeweza kujengwa katika urefu huu mfupi tungeweza kuwa na manufaa makubwa kuhakikisha kwamba reli yetu ya *TAZARA* kutoka Tunduma kwenda Dar es Salaam inapata mzigo wa kutosha basi baada ya Zambia kuacha kutumia reli hii.

Kumbe nadhani tutumie nafasi hii kuanza kufikiria ni jinsi gani ya kuweza kuimarisha gati hii ya Kasanga iwe bandari imara ya kuweza kubeba mizigo na kuimarisha reli ya *TAZARA* kwa sababu hatuwezi kwa gharama yoyote ile kuacha T*AZARA* kwa sababu ni chombo ambacho kipo ndani ya nchi yetu kina urefu mkubwa na kitatusaidia hata kwa chuma cha Liganga na makaa ya mawe kule Mchuchuma.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la viwanja vya ndege, kama nilivyotangulia kusema kuhusu msemaji aliyekuwa anatusaidia kuzungumza kuhusu kiwanja cha Songwe. Ukiangalia viwanja vya ndege vilivyokaa nchini, viwanja vingi viko Kaskazini. Kusini viwanja ni vichache na ukitoka Kigoma mpaka Songea kiwanja ambacho Mheshimiwa Dr. Luoga alikuwa anazungumzia hakuna kiwanja chochote cha ndege ambacho kinaweza kikatumika kwa dharura kwa ajili ya kulinda amani ya nchi hii. Kukitokea tafrani yoyote, ni hali mbaya sana.

Mheshimiwa Spika, Kigoma mpaka Songea hapa katikati hakuna kiwanja chochote. Sasa ni lazima tutafute jinsi ya kuweza kujenga viwanja *strategically* ili viweze kutusaidia katika matatizo yanayoweza kujitokeza ambayo hatuyategemei na wala hatuyataki lakini yanaweza yakatokea. Kumbe kuhimiza kiwanja cha Songwe ina umuhimu sana ni jambo la msingi sana lazima tuliangalie jinsi ya kuweza kulifanyia kazi haraka ili tuweze kuhakikisha kwamba kiwanja hiki kinakamilika mapema.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la Posta. Shirika hili linafanya kazi mzuri sana Shirika la Posta linafanya kazi nzuri sana. Serikali haiwezi ikafanya kazi bila Posta. Kwa sababu nyaraka za Serikali hii nyingi zinatumika kusafirishwa na Shirika hili la Posta, vifurushi na mambo mengine.

Lakini shirika hili ukiangalia Sheria yake iliyoanzisha Shirika la Posta kuna matatizo mengi ambayo yanahitaji kutatuliwa. Mheshimiwa Waziri anafahamu. Mheshimiwa Waziri wa Fedha anafahamu suala hili. Naomba washirikiane ili kuweza kusaidia kuondoa matatizo yaliyopo katika Shirika hili hasa ya mtaji. Kwa sababu bila mtaji shirika litaendelea kuyumba na kushindwa kutekeleza wajibu wake.

Mheshimiwa Spika, lakini pamoja na hiyo, naomba pia Shirika liweze kuona jinsi ya kuweza kutujengea Posta mzuri pale Mpanda. Kwa kweli ni jambo la kusikitisha Mpanda kuna konteina tu. Nimekwenda kutembelea juzi juzi pale. Nkansi ndiyo kabisa kuna jengo bovu sana sana ni aibu tupu, ni aibu tupu kwa Serikali. Serikali itafute jinsi ya kuweza kutusaidia. Jengo la Sumbawanga ndiyo lenyewe limepasukasuka halafu limekwisha wekwa (X) na Mheshimiwa Magufuli.

Sasa sijui tutafanyaje na wakilibomoa lile na kusema fedha zimepatikana akilibomoa sijui tutafanyaje tutaendelea kukaa hivi. Naomba Mheshimiwa Waziri hebu liwekee manani kwa sababu ile imeshawekwa (X) ikibomolewa itakuwa tena tafrani kwako tutakuja tena kwako tuanze kufanya mipango mingine. Naomba ujue hilo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mambo ya usalama wa anga. Mimi nashukuru sana kwamba kwa kweli Shirika au Taasisi hii imekuwa na rekodi nzuri hatujawahi kusikia mambo mabaya yanayotokea katika nchi yetu. Nawapongeza sana kwa juhudi hizo. *(Makofi)*

Kuhusu hali ya hewa tunawapongeza kwa sababu sasa takwimu wanazozitoa ni zile za kuaminika na wewe ukiziona kwenye vyombo vya habari unaridhika kwamba walau mvua kweli itanyesha. Nadhani sasa wamepata vyombo. Lakini Serikali ione jinsi

ya kuwaongezea vyombo na tunawapongeza watu wote wanaotumikia katika maeneo hayo pamoja na mashirika mengine.

Kuhusu suala la Simu. Naomba niseme kwamba Mji wa Sumbawanga ambao una Halmashauri na ni Makao Makuu ya Mkoa wa Rukwa. Hapo huduma za simu zipo. Wilaya ya Sumbawanga haina kijiji chochote ndani ya Wilaya ambacho kina simu ya aina yoyote. Hili suala labda pengine halikufahamika. Vijiji vyetu vya Matai, Ulumi, Laela, Kasanga na sehemu nyingine zote hakuna simu. Kumbe Wilaya yote ya Sumbawanga vijijini hatuna simu mahali popote. Naomba muweke hili katika rekodi. Kwa sababu mkisema Sumbawanga mnasema wote wanayo lakini Wilaya ya Sumbawanga jimbo la Kalambo ambako niko hakuna simu wala jimbo la Kwela, hakuna simu. Kumbe naomba na sisi mtuingize katika mpango hata tukitumia *Rural Open Communication Fund* naomba sasa ianze hapa mfikirie ni jinsi gani ya kuweza kutupatia na sisi katika vijiji vyetu ili na sisi kuwa katika dunia ya mawasiliano ya kisasa.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, mimi niwashukuru Watendaji wote wa Wizara hii, Katibu Mkuu na Wakurugenzi katika Wizara pamoja na Wakurugenzi wa Mashirika yote yaliyoko chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri mnayofanya Mungu atawasaidia ili muweze kufaniwa zaidi. Baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. EDSON M. HALINGA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Mimi nilikwishatoa rambi rambi kwa hiyo naomba niendelee. Kwanza kabisa naomba sote tukubali kwa mtu aliyefanya kazi tumpe shukrani zake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Wizara hii ilipoanza nchi hii ilikuwa na simu nyingi za mkorogo. Lakini sasa zimekwisha. Na hii ninawashukuru sana Wizara hii wamekuwa ni wazungukaji sana kwa kila Mkoa kufuatilia na kuzingatia yale wanayoyaona kwa wananchi. Nawashukuru na kuwapongeza sana, tangu Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na hata uongozi wa Ofisi yake, nawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kitu kingine ambacho ni cha msingi katika sehemu zile za Kusini sisi hatuna kiwanja cha ndege. Kwa kweli kile cha Mbeya kilikuwa ni cha wana jeshi tu kupitia pale. Kile kiwanja hakina uhai wowote. Hiki kiwanja cha Songwe ndiyo pekee ambacho kingeweza kuondoa tatizo la usafiri wa ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Mbeya kwa wengine ambao hawajaiona kwa kusikia tu kuwa ni milimani huko, Mbeya kwanza kuna utalii wa kutosha. Mbeya kuna mazao mengi ya mboga mboga na matunda na wale ambao mnapenda mananasi yasiyo na chachu, basi utayapata Mbeya kutokea Ileje, kutokea Kyela, acha haya ya Chalinze haya, kule ni mananasi mazuri sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, yote haya bado yanahitaji, huwa wanafika wenzetu kwa njia za uchochoro kutoka Afrika Kusini wanayachukua kwa hamu sana na kama usafiri ungekuweko wangeweza kununua na biashara hii ingeweza kwenda mbele zaidi.

Na kama kiwanja hiki kitakamilika basi biashara yetu na wenzetu wa *SADC* itakuwa ni bora zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa nilikuwa ninaiomba Serikali ilione jambo hili kama alivyosema mwenzangu Mheshimiwa Mwananzila pia Mbeya hakuna kiwanja ambacho kwa kweli kwa usalama wa nchi unaweza ukasemea. Chukua Sumbawanga, Mbeya mpaka Ruvuma hakuna. Tuwe angalau na mahali ambapo watu mna uhakika wa maisha na usalama endapo vurugu zitatokea. Tunapopakana na nchi hizi tusindhani daima tutakuwa na amani na utulivu. Lazima tuwe tunajiandaa. Fedha zilizotengwa naomba sana Wizara iangalie na itafute tafute iongeze angalau ile njia watengeneze ianze kufanya kazi kama Mheshimiwa Rais alipofika kuweka jiwe la barabara ile ya Tunduma alisema kitu anachotazamia kwamba ataona kiwanja kile kinakamilika kabla ya mwisho wa uongozi wake. Basi hili alilisema mbele na watu wengi walikuweko basi tunaomba uongozi wa Serikali ulione hili na uzingatie kwamba Mheshimiwa Rais ana hamu ya kukizindua kiwanja hicho yeye mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili ni suala la reli. Reli hii ya *TAZARA* kwa kweli ilijengwa kwa kusudi kuzindua sehemu za mabonde kama Ifakara, kilimo humu katikati. Lakini sasa inaonekana kwamba hii reli haina namna au utaratibu wowote wa kuzindua kilimo katika maeneo hayo. Ilikuwa pamoja na viwanda vya mbao, lakini sasa viwanda hivyo vimekwisha kufa. Sasa kitu kikubwa kama tunategemea Zambia tushirikiane, ilikuwa inasaidia sana wakati Afrika Kusini ilikuwa haina mwelekeo wa kuelewana na sisi huku na upande wa Zambia.

Lakini sasa inaonekana wenzetu wa Afrika Kusini wanazidi kuvuta sehemu yao na tutakosa hata mizigo na kwa namna hii reli hii itakufa. Hatutakwenda mbali na reli hii. Sasa nilikuwa naomba tatizo letu kubwa ni nini? Ni kutokufanya ukarabati. Si kazi hizo tu, hata magari yetu haya usipofanya ukarabati huishi nalo hata miaka miwili. Lazima ulikarabati mara kwa mara na ulipeleke *service.* Sasa sisi vipi?

Mheshimiwa Spika, sasa sisi tangu imejengwa reli hiyo hakuna ukarabati wa maana tunabaki kuangalia tu, utafikiri ni kitu ambacho kimewekwa cha kudumu. Na ndiyo ubovu ambao unatupata katika reli hii ya Kati. Tangu Mjerumani amejenga sasa hii mitalimbo ipo mpaka leo. Hivi kweli tutadumu na usafiri wa reli hii? Juzi ameniambia jamaa mmoja kuwa ng'ombe walikuwa wasafirishwe kutoka Manyoni sasa hakuna behewa, wameteremshwa hapo Manyoni, sasa wamekondeana hata biashara yenyewe hawana sasa.

Mheshimiwa Spika, sasa hasara yote hii tunaipata kwa nini? Na kama watu wanasema wasafirishe mifugo kwa magari, malori, gharama itakuwa kubwa mno. Na bei ya nyama itabidi ipande na kwa watu wengi hawatakuwa na uwezo wa kula nyama. Tunarudi kule kule kwenye tatizo la kwashakoo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu na kuanza mikutano ooh! Tuondoe kwashakoo, tuombe misaada. Sasa tutaishije kwa misaada namna hii. Lakini tungekuwa kila tunachopata tunakarabati, tunaweka hii reli ingetusaidia sana. Na hata hivi inachechemea

basi tuione hii tuikomboe, tuiache angalau inatembea kama yupo mtu atakayekuja kuwekeza basi awekeze kwa kitu kinachoonekana kina manufaa. Sio katika hali hii iliyopo kwa kweli.

Sasa sioni fedha zinazowekwa hapa kuwa zinaweza zikaiwezesha hii reli kuchechemea kama tunavyojali. Barabara ni sawa tumeziangalia. Lakini reli hii inachukua watu mikoa karibu minane. Sasa ni kitu cha msingi sana na bei ni nafuu sana kuliko kwenda kwa barabara hata hii inayojengwa mpaka huko Mwanza. Lakini reli ni nafuu kwa nauli na kwa watu wetu katika usafiri. Ipo haja ya kuliona hili suala Serikali ijaribu kuwekeza angalau kidogo hasa wakati huu ambao hatutegemei kuwa watakuja haraka hawa wawekezaji.

Mheshimiwa Spika, mwekezaji yeyote anayeweka ana nia ya faida. Sasa unafikiri aje awekeze wewe ufaidike. Kwa kweli hii tutapata matatizo sana huko tunakokwenda.

Mheshimiwa Spika, la tatu, ni Idara hii ya Hali ya Hewa. Mambo yetu ya kufanya vitu vya kienyeji enyeji ndiyo yanayotuua. Maana mtangazaji wa hali ya hewa leo anakuambia kesho kuna manyunyu manyunyu ya hapa na pale. Unasubiri hakuna. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, au kesho ni jua kali. Mvua inaanguka ya mawe. Sasa tatizo letu ni kwamba hatuna vifaa vya kutabiri hali halisi iliyopo. Sasa tunakuwa wabanifu tu na hii mikono ya Serikali yetu kuwa na mkono wa korosho. Mkono huu wa birika wa Serikali hatuwezi kwenda. Ni afadhali kununua vifaa ambavyo kweli vitatuletea manufaa na mafanikio tunayotarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tuwape wanunue vifaa, ili watuambie. Wenzetu Ulaya akikuambia kesho kuna baridi chukua koti. Usipochukua koti utakiona kwa kweli. Lakini sasa sisi mara aah! Pepo hizi zimebadilika ghafla mvua mnazoziona zimekuja kutokana na upepo umebadilika baharini. Sasa hii hatuwezi kuendesha maendeleo ya kilimo kwa utabiri wa hewa wa namna hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, halafu lingine ni vidhibiti mwendo wa magari haya. Mimi nadhani vitu vingine ni vizuri tuwe tunaangalia. Magari haya hayana vidhibiti mwendo. Ukisafiri pale walipo askari ndipo unaona anapunguza mwendo. Akisha pita tu anakwenda mwendo hata gari ndogo ukiweka *speed* mpaka 130 linakupita kama upepo. *(Kicheko)*

Na haya ndiyo matokeo kama hii gari ya *Air Bus* iliyoanguka njia hii ya kwenda Sumbawanga. Hii gari siyo leo tu, muda wote na miaka yote wanakimbia utafikiri dereva ana kichaa. Matokeo ndiyo hayo watu wanakufa. Kwa nini wasiyafanyie ratiba kwa vipande vidogo vidogo hata ufike saa hizi hapa, ingeweza kudhibiti zaidi kuliko hii ya kusema vidhibiti mwendo. Vidhibiti mwendo kwa kweli havisaidii na watu watazidi kufa na kuumia kwa sababu hii haisaidii kitu. Hili Serikali iliangalie sana.

Mheshimiwa Spika, mwisho, hizi simu tunashukuru sana zimeenea sehemu zote. Sijui tatizo hili ni langu mwenyewe au na wenzangu. Ukishapiga simu *Voda* kutaka upate kuunganishiwa, unapomaliza tu kupiga kubonyeza zile namba wanakuambia ooh! Tunasikitika haiko hiyo simu subiri. Wakati huo yule mtu naye ndiye anaichukua ili asikilize.

Mheshimiwa Spika, sasa imekuwa mchezo huu ni wa kawaida wa siku zote. Sasa namna hii inakuwa kama ni kuchezea. Yuko mama mmoja sijui amesomea masuala haya ya namna ya kuchelewesha watu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, tunaomba Wizara iende imwambie kwamba sisi tunachoka na maneno yake ya udanganyifu. Maana mtu unapiga simu anakuambia hayupo, usubiri baadaye. Dakika mbili mtu yule anakuambia aah! Bwana na mimi nashangaa. Imelia mara moja tu na mimi nachukua ile simu sipati majibu.

Sasa huyu mama pamoja na jinsia lakini kazi ya namna hiyo ya jinsia haina heshima wala hadhi ya kuheshimika. *(Kicheko)*

Ni afadhali waweke muda wa kuona inaita kwa mara ngapi. Lakini kwa hali hii Mheshimiwa Spika, tutakuwa tunapoteza muda na kukatishana tamaa.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na napenda niwaombe wenzangu kwamba haya Makadirio ya Wizara hii tuyapitishe kwa kweli na tuombe Serikali kama yanapatikana mahali pengine wakokotoe waiongezee maana tuna mambo mengi sana. Nakushuru sana ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumefikia mwisho wa kipindi cha asubuhi. Msemaji wa kwanza kipindi cha mchana atakuwa Mheshimiwa Ali Karavina.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11 jioni.

*(Saa 06.56 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

*Hapa Mwenyekiti (Mhe. Eliachim J. Simpasa) Alikalia Kiti*

**MWENYEKITI:** Kabla sijamwita Mheshimiwa Ally Karavina kuchangia, Mheshimiwa Waziri amefanya marekebisho fulani katika Kitabu kile cha Nne. Marekebisho yale mtagawiwa ili yaingie pale tutakapokuwa tunapitisha vifungu, natoa taarifa hiyo.

**MHE. ALLY A. KARAVINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwanza nakushukuru kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia kidogo kwenye Bajeti hii ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.

Awali ya yote, kwa sababu nilikwishatoa rambirambi zangu na salaam zangu, nitaendelea moja kwa moja kwa kuanza kuchangia

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa leo sina mengi, nianze kwa kusema kwamba nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri pamoja na wafanyakazi wao wote kwa jinsi ambavyo wamekuwa na ushirikiano mzuri sana na Bunge hili kupitia Kamati ya Miundombinu na kwa jinsi ambavyo kwa kweli wameiendesha Wizara hususan katika kipindi hiki cha miaka hii tunayomalizia ngwe, miaka minne mpaka sasa hasa sekta ya mawasiliano kwa kweli imepiga hatua sana na mimi nawapa hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja nianze kwenye Kitabu cha Bajeti ukurasa ule wa 12 kuanzia *paragraph* ya 17,18 maelezo yale yanaashiria nini? Maelezo yale bado yanarudia kosa lile la kutafsiri *central corridor* maana yake na maelezo yote yaliyofuata pale kwa Mheshimiwa Waziri alivyokutana na Waziri mwenzake wa Burundi, yamekwenda kufuatana na tafsiri hiyo hiyo, ukiyasoma vizuri unashindwa kuelewa huu uzito utakaokwenda Burundi unafikaje Kigoma? Nafikiri ni vizuri kwa Wizara ingekuwa mara nyingi inapoeleza masuala haya iwe inafanya kwa upana zaidi. Maelezo yale kidogo yanaoonyesha kwamba ilikuwa ni kueleza ile *cement* ya Mbeya itakwendaje Burundi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini napenda kueleza kwamba na ndio hapo mimi nitaingilia kuielezea yote jumla mpaka kufika kwenye *TAZARA.* Jana nilipokuwa nachangia Wizara ya Ujenzi, napenda nirudie kitu hicho kwa sababu ni muhimu sana kwa Wizara hii vile vile kwamba katika mapambano yetu ya kujaribu kuchuma uchumi wa Jiografia *time is of a essence* kwa kweli, kwa sababu utandawazi sasa hivi unafanya mambo yote yanakwenda haraka sana. Kinachotokea sasa hivi, nieleze kweli tu Afrika Kusini wanatengeneza mikakati ya kuhakikisha ukilianganisha na sisi wote hapa wanakuwa na *competitive advantage* pamoja na kwamba sisi tuna *comparative advantage* lakini wanatumia *elements* nyingi tu sasa hivi na uwezo wao mkubwa kuweza ku-*erode comparative advantage* yetu kwenye uchumi wa jiografia kwa kutumia *competitive advantage* hiyo waliyonayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli *time is of essence* namna gani sisi tunaweza kuikamata hii biashara ya Soko la Maziwa Makuu? Biashara ya mzigo wa *transit* ni biashara kubwa kama Tanzania kila siku tunalalamika kwamba pato letu ni dogo, basi Mwenyezi Mungu katujalia kwa sehemu hiyo ya jiografia pato ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikinukuu tu alichosema kwa mfano Waziri wa Ujenzi jana zile tani milioni 12 *potential* iliyoko kwenye Maziwa Makuu. Nataka nifanye hesabu kidogo, chukua kwa *conservative rate* tu ambayo *TRC* sasa hivi ina-*charge,* ina-*charge* zaidi ya dola 60 kwa tani, hivi tani milioni 12 maana yake nini zaidi ya dola milioni 600.

Sasa kila siku katika nchi hii tunazungumzia biashara, tunazungumzia nini? Kweli mtu una *potential* namna hiyo na kinachotakiwa hapo ni miundombinu ulioujenga kwa *priority* tu na huo muundombinu utajilipa wenyewe halafu bado unalalamika kwamba nchi hii ni maskini! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndio maana nasema *definition* nimeona kwenye maelezo yale (i)-(v) yanakwenda kinamna ile kwa sababu *wrong definition* yenyewe ya *central corridor.* Nirudie tena *central corridor* ni kutoka Dar es Salaam - Morogoro - Dodoma - Tabora - Kigoma, *branch* yake ya Kaskazini ndio hiyo inayokwenda Lusaka, huendi Kongo unakwenda Rwanda na *branch* nyingine unakwenda Burundi na siku hawa wakichachamaa mzigo wa Kongo huupati hata kama umejenga reli.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachosema katika *priorities* zetu ndio maana lazima tuelewe tuna *advantage* yetu *maximum* wapi? Kwa nini tunasema ujenge na barabara sasa isaidiane na reli kwenda Kigoma? *Capacity* ya reli ndugu zangu ndio hiyo aliyoeleza Waziri hapo milioni 1.45 hapa walijitahidi sana hawawezi kwenda zaidi ya hapo, wana *constraints* nyingi mno, hawawezi kwenda zaidi ya hapo mpaka ufanye *fundamental changes.* Inabidi ubadilishe vidaraja vyote vile ulete *engine* zenye uwezo mkubwa, sasa hivi hata huyo atakayebinafsishiwa sijui namna gani hizo *special made engines* atafanyaje bila kubadilisha madaraja hayo ni kazi kubwa. Katika hiyo milioni moja ndugu zangu *transit traffic* jamani ni hiyo *point 45* anayosema, hii nyingine yote ni sukari, pamba, tumbaku ya Tanzania. Katika milioni 10 hii *transit traffic* tunayosema tunayobeba kule ni *point 45* sasa siku tukinyang'anywa na hao wenye *competitive age* zaidi ya sisi tutafanyaje? Mtu akishachukua mzigo huurudishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina haya ya kusema ndugu zangu *TAZARA,* sasa hivi kuna fedha zimetolewa za kujenga ile *branch* ya kutoka Kasama - Mpulungu sasa hivi sio mzigo wote wa Burundi unakuja kupitia Bandari za Tanzania mwingi unapita Afrika Kusini kupitia Bandari ya Mpulungu, tumeshanyang'anywa kiwango kikubwa tu. *TAZARA* pale inawekwa tena *extension* nyingine ya kwenda Nchinji, Malawi kule kwa ajili ya ku-*serve Nakala Corridor. Zambia Railways Management* inatawaliwa na Afrika Kusini, Mwafrika Kusini anaitumia *Zambia Railways* kubeba mzigo wa Kongo kama *transit,* sio kama kuendesha reli ya Zambia kama *transit* tu ya kupeleka mzigo Afrika Kusini na wataiendesha kwa muda wa miaka 20 sijui soko letu litakuwa wapi kwa wakati huo?

Mheshimiwa Waziri sasa unapoita ile *Ministerial Meeting* ya *TAZARA* siku hizi wale Mawaziri wa Zambia hawaji, *they will not come,* waje kufanya nini? Wamesha-*direct* biashara *elsewhere.* Mkakati ambao Wizara sasa hivi inatakiwa uwe nao ni namna gani wataifanya *TAZARA* ku-*survive* katika mazingira hayo mapya ya soko *originally* ambalo lilifikiriwa la *TAZARA* la kubeba shaba ambalo sasa hivi halipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *structure* ya soko la *TAZARA* imebadilika na huwezi kwenda mpaka Kongo moja kwa moja kwa urahisi kwa sababu pale katikati sasa *Zambia Railways* inatawaliwa na M-*South Africa!*

Jamani hebu tuwe *careful* tuelewe haya, ile *TAZARA* ni yetu, tunafanya nini? Ndio maana jana tulikuwa tunaeleza na mwenzangu kaeleza leo kujenga ile *corridor* ya kutoka Kasanga kule *Bismark point* aliyoweka Mjerumani kule ujenge hiyo Barabara ya Tunduma sehemu ya huo mzigo unakuja kwenye *TAZARA*. *TAZARA* hiyo *installed*

*capacity* yake ni zaidi ya milioni nne, jamani *critical density* peke yake, mzigo ambao unatakiwa uupitishe ili ipate faida ni zaidi ya milioni mbili sasa hivi *TAZARA* kwa ule mzigo wanaobeba wanakula *capital* tu *they are eating capital there is nothing there. (Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ndugu zangu nilikuwa naona haya niyaeleze wazi kwa sababu sio mazuri kwa kweli. Lakini lazima tuelewe sasa hivi ndani ya kitabu chake Waziri kasema kwamba Bandari ina *efficiency* kubwa sana, Bandari ya Dar es Salaam tunai-*feed* na nini? Mzigo unaopita kwenye Bandari ya Dar es Salaam ni kidogo sana tunafanya nini sasa ku-*expand* Bandari zetu hizi kwa ku-*increase output* itakayokuwa inapita kwenye bandari hizi? Ni *hinterland routes* zile lazima ziwe *clear* na lazima ziongezwe. Tusiwe na *colonial mentality* ile ya kufikiria eti *central line* kwa sababu kuna reli basi ukiweka barabara ita-*compete* jamani lazima muangalie *complementarity* hii uta-*compete* nini kwa kubeba mzigo milioni 1.4 mahali ambapo una *potential* ya milioni 12? Ni lazima upate na barabara ya kuwa *complementary.*

Mimi naomba *definition* za *corridor,* zimeelezwa vizuri sana na Serikali, ninyi wenyewe kule Wizara ya Biashara na Viwanda, *NDC* wana *proper definition* ya hizi *corridor,* hebu tuwe na *uniform definition,* Serikali nzima tafadhalini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niingie kidogo kwenye suala la *Telecom.* Tumetangaziwa kwamba *connection fees* zimeshuka lakini na sisi kwenye Kamati tulikuwa tunataka tuone mchanganuo mzima wa gharama zile. Lakini hii ina maana kwa kuwatangazia kwamba *connection fees* zimeshuka, umewatangazia Watanzania kwamba bei za matumizi ya simu yatashuka. Sasa tusione tena hayashuki asije mtu akafanya kampeni mpya kama gharama zimeshuka maana yake gharama zi- *treacle down* kwa wananchi wenyewe wanaotumia zishuke kweli. Naomba hili liwe *clear* sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Urambo bado natumia simu ya kukoroga. Mheshimiwa Waziri ulitoa ahadi mwaka 2001 mpaka leo haijatekelezwa bado tuna zile simu za Marehemu George za mwaka 1947. Mheshimiwa Waziri una deni kule la kudumu na la muda mrefu. Pamoja na kwamba tumepata mtandao, nashukuru, *Celtel* tumepata lakini ule sasa hau-*cover* wale waliokuwa wanatumia zile *line* hatuwezi kuendelea na zile za kunyonga na mkakati ulikuwepo sijui mpaka sasa tumefikia wapi mimi sielewi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo nilivyoeleza, napenda nieleze kitu kimoja kidogo pia kwa kipindi hiki ni lazima nieleze wazi kwa bahati mbaya mimi nina utaalam kidogo kwenye sekta hii lakini naona kama Wizara imekuwa inaendesha sana masuala ya *Telecommunication* zaidi ya uchukuzi na usafirishaji. Naomba kuwa na *balance* kati ya *Telecommunications* na mambo ya uchukuzi. *However much* tunafanya kwenye mambo ya mawasiliano *final delivery* ya *physical goods from points of production to point of consumption* ni kitu muhimu sana kama tunataka tuendelee. Hicho ni cha muhimu na naomba kuongezwe nguvu kidogo kwenye sehemu ya uchukuzi, ile sehemu ya uchukuzi ya Wizara kidogo inaonekana inalegalega ni pamoja na shule yao na kufundisha wataalam wale wa usafirishaji, tumesahau, kuna shule hapa sijui tunalifanyia nini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema na-*support* kwa asilimia mia moja, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi kuchangia hoja hii na kwa kuwa nilishasimama na kuzungumza katika Bunge lako Tukufu, wakati huu sitarudia niliyotangulia kusema kuhusu kutoa rambirambi na pole kwa baadhi ya watu waliopatwa na matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara ya mwisho, Mheshimiwa Rais alipokuwa anahutubia Bunge hili alituambia kwamba kama mtu amefanya kazi yake nzuri, alikuwa anachukua kazi ambazo zinafanywa na Chama cha Mapinduzi kutokana na Ilani ya Uchaguzi, akasema hata kama watu hawakukusifu, wewe unaweza ukajisifu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hoja iliyo mbele yetu kwa kweli Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, anastahili sifa zote na wala hakuna sababu yake yeye kujisifu zaidi kwa sababu anaonekana kama anavyojiona kwenye kioo yeye mwenyewe. Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya ni Askari wa Mwavuli kweli kweli. *(Makofi)*

Napenda nimpongeze na kuwashukuru wote waliomsaidia kufanya kazi nzuri kwa kipindi cha miaka hii mitatu na nusu na hasa hasa Msaidizi wake Mkuu, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Katibu wa Wizara husika na wataalam wote wa ngazi zote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri akubali kupokea shukrani za wananchi wa Ngara, katikati ya mwaka 2002 alitembelea Wilaya ile pamoja na Mkoa mzima na kwa Wilaya ya Ngara ambayo kwa muda mrefu ina matatizo mengi tu ambayo Serikali inayafahamu, aliyasikia na akaweza kuishawishi kampuni za *Celtel* na *Vodacom* na haikuchukua muda mrefu simu zote hizi ziko Ngara na zinafanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ile ameiunganisha na nchi nzima na Wilaya ile sasa inafanya kazi kwa njia za mawasiliano ulimwengu mzima kwa sababu karibu mahitaji yote ya mawasiliano tunayo hadi kufikia kuwa na redio ambayo inasaidia katika Wilaya za Ngara, Kibondo, Karagwe na sehemu kubwa ya Biharamulo, Redio Kwizela ambayo inamilikiwa na Shirika la Wakimbizi. Redio hii ilikuwa iondolewe baada ya wakimbizi wa Rwanda kuondoka mwaka 1996 lakini kwa kweli ilisimama kidete akishirikiana na uongozi wa Wilaya ya Ngara, Ofisi ya Waziri Mkuu basi tukajaaliwa kuendelea kuwa na redio hii ambayo kwa kweli imekuwa ni kichocheo kikubwa kwa maendeleo ya Wilaya ile na Mkoa mzima wa Kagera. Nampongeza na namshukuru sana kwa niaba ya wananchi wa Ngara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine nimwombe atazame zaidi upande wa kampuni ya simu ya *TTCL* kwa sababu kuna matatizo kule. Kampuni hii katika Wilaya ya Ngara na kwa bahati nzuri niseme kwa nchi nzima ina matatizo ya kurundikiza madeni kwa watu ambao hawakutumia huduma za simu hii. Kwa Ngara nafikiri ni zaidi na watu wengi wameikimbia baada ya kupata simu hizi za mkono.

Malalamiko hayo kwa bahati nzuri nimeshamfikishia. Nashukuru alisema atayashughulikia kwa wale ambao watakuwa wamemfikishia malalamiko yao lakini ukweli unabaki pale pale kwamba kutokutumia chombo hiki cha Serikali na chombo ambacho kinafahamika ndio kinazaa vyombo vingine vinavyokuja, itakuwa sio vizuri. Kwa hiyo, ni vizuri kikatazamwa kusudi kama kuna kurekebisha basi yafanyike marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kubwa ni kwamba watumishi wa kampuni hii wako pale kwa muda mrefu sana tangu ilipoanza karibu miaka 20 iliyopita. Wanayoyatenda sidhani kama yanapendeza. Wanalalamikiwa na kila mtu, wengine wamekuwa hata wakihamishwa lakini wanarudishwa, sasa wadau hawana raha na huduma za kampuni hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna sehemu nyingi tu za kushauri lakini muda hautoshi. Nataka nizungumzie usafiri wa anga kwa Mkoa wa Kagera. Mkoa wa Kagera unazalisha kwa wingi mazao ya chakula na biashara. Mkoa wa Kagera unapakana na nchi za Rwanda na Burundi ambazo kwa miaka mingi zina matatizo ya ndani kwa ndani na Serikali inafahamu. Mkoa wa Kagera sasa utakuwa ni mlango kwa sababu ya *East African Community* iwapo tutaruhusu Rwanda na Burundi kuingia. Ni mlango kwa sababu ya Tanzania yenyewe na Uganda na mlango huu unafunguka kuelekea Kongo. Mkoa huu una maeneo mazuri ya kulima, una vivutio vingi vya utalii na kwa hakika ni Mkoa ambao katika Mikoa ya Tanzania unajulikana kwamba unachangia pato kubwa la Taifa lakini hatuna uwanja wa ndege. Wakazi wa Mkoa wa Kagera wanahitaji Serikali iwajengee uwanja wa ndege wa kisasa.

Wakati wa vita ya Iddi Amini, ndege ambazo zingetua Makao Makuu ya Mkoa zilikuwa zinatua kilometa 320 mpaka 330 Wilayani Ngara ambako ndio kuna uwanja mzuri. Hali hii haipendezi.

Naomba iwezekane kabisa Wizara hii ione umuhimu huo, ujengwe uwanja wa kisasa kwa sababu nilizozitoa na kwa sababu kubwa hasa ya ulinzi wa mipaka yetu, wananchi wa Mkoa wa Kagera na nchi nzima pia mali zao. Ni muda mrefu tuna malalamiko ya namna hiyo na kila mara Serikali inaahidi kwamba itajenga uwanja lakini haijatokea dalili ya kuonyesha kwamba kuna matumaini. Naomba sana Mheshimiwa Waziri kwa uwezo ninaoufahamu anao atazame suala hili kwa undani zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mkoa wa Kagera kuna uwanja katika Wilaya Ngara. Mheshimiwa Waziri anaufahamu ni uwanja mzuri sana, mrefu mno, mpana sana, udongo wake ni mgumu mno. Inafahamika wazi pengine ukiondoa uwanja wa Ibadakuli, Shinyanga, pengine huu ni wa kwanza katika Kanda ya Ziwa kwa uzuri wake, lakini kwa bahati mbaya uko mahali ambapo umejificha na uko katika eneo ambalo limekuwa katika matatizo na vurugu nyingi za Kimataifa inawezekana kuwa haujulikani vizuri. Kwa kuwa vurugu hizo zimekwisha, wakazi wa Mkoa wa Kagera hasa Wilaya ya Ngara, wataishikuru Serikali na Wizara yenye dhamana kwa uwanja huu ukaanza kutumika tena.

Mwaka 1977 na mwaka 1978 mimi nikiwa humu Bungeni uwanja huu ulikuwa unatumika. *ATC* walishaanza safari zao kwa sababu ya nchi za Rwanda, Burundi, Kongo na Wilaya za Biharamulo, Ngara, Kibondo na Karagwe. Wakati wa vita ya Kagera ndio uwanja uliotumika sana. Tangu mwaka 1993 wakimbizi wa Burundi walipomiminika kule, wakimbizi wa Rwanda walipokuja kwa maelfu uwanja huu ndio umekuwa ukitumiwa na Shirika la Wakimbizi la Kimataifa. Kwa bahati kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ameuona uwanja huo, naomba aufanyie *promotion.* Wananchi wa Ngara wako tayari kusafiri, Wanyarwanda, Warundi wako tayari kusafiri na kwa sababu ya ujambazi ambao umezidi wa kuteka magari ni dhahiri kwamba tatizo lililopo la wafanyabiashara kutoka sehemu zote hizo wanapata matatizo kutembea na fedha wanapokuwa wakija katika vituo ambapo bidhaa zinapatikana kufanya biashara zao utasaidia. Kwa hiyo, nina hakika kwamba kama kutakuwa na mawasiliano mazuri kati ya Tanzania, Rwanda na Burundi, uwanja huu ni muhimu sana kwa kuendeleza uchumi wetu na kulinda mali za wananchi wa Tanzania. Naomba Mheshimiwa Waziri hilo alichukue na ni maombi ya Mkoa kwamba iwezekane uwanja huo utumike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie ujenzi wa reli mpya alioutangaza katika Ibara ya 17 ya hotuba yake. Kwa Mkoa wa Kagera tendo hili litakapokuwa limefanikiwa ni mkombozi, kwa Ngara ni zaidi kwa sababu reli hii itapita Wilayani Ngara. Kinachohitajika tu ni kuwe na ushirikiano wa wazi kabisa kati ya Wizara hii, Wizara ya Kilimo na Chakula na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo, ili kusudi kuweka vitega uchumi vya uhakika, kusudi reli hii itakapokuwa imejengwa basi isionekane ya kufanya kazi kutoka hizo nchi zilizoko Magharibi. Reli hii itatufungulia nafasi nzuri kwa sababu ya utalii, kuna vivutio vingi katika Mkoa wa Kagera lakini hasa Wilaya ya Ngara. Kulikuwa na mpango wa *Kagera Basin Organization* ambao ulikufa wa kutoa umeme katika maporomoko ya Rusumo kwenye Mto Kagera, maporomoko yanayotegemewa kwamba yanaweza kuzalisha *megawatt 23.* Kulikuwa na *projects* za umwagiliaji nyingi tu chini ya mpango huo.

Kwa hiyo, naamini kabisa kwamba kwa mafanikio haya ambayo Wizara hii inayashughulikia eneo hilo litakuwa limechochewa vizuri kwa uchumi wake na kwa hiyo, umaskini utakuwa umepunguzwa. Lakini kusema kweli inahitaji ushirikiano kati ya Wizara hii na Wizara nilizozitaja kwa sababu ya kilimo cha hakika, ufugaji wa hakika ili kusudi iweze kutumika vyema, iwapo mipango ya Wizara hii kwa miaka ijayo itafanikiwa. Naomba kusema kwamba kwa vyovyote vile nchi ikiwa na mawasiliano mazuri, uchukuzi mzuri, ikawa na amani haiwezi kushindwa kuendelea na kwa njia hii ninaamini tutasonga mbele.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja hii na naomba niseme kwamba Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, ategemee hakika kwamba wakazi wa Mkoa wa Kagera na Wilaya ya Ngara watamsaidia sana pale atakapohitaji msaada wao kufanikisha shughuli za Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi jioni hii nami nichangie katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa

Mawasiliano na Uchukuzi. Naomba niseme kwamba naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Naomba pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri mwenyewe, Naibu wake, pamoja na Wakurugenzi wote wa Mashirika yaliyo chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya ya kumsaidia Mheshimiwa Waziri. Naomba waendelee hivyo hivyo, bidii iongezeke ili Taifa letu liweze kusonga mbele. Wao ndio tunaowategemea kama wataalam. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizungumzia mawasiliano, basi unamgusa kila mtu na uchumi wetu hauwezi kupiga hatua kama mawasiliano kwa ujumla hayako katika utaratibu mzuri. Kama barabara zetu ni mbovu, hatutakuwa na uchumi mzuri, reli *engine* zake kama ziko katika hali mbaya na ni za zamani, msitegemee kama uchumi utaboreka. Lakini Viwanja vya Ndege pamoja na ndege zenyewe kama zina matatizo, basi maendeleo hakuna. Lakini pia kwa sababu wananchi wanasafiri kila kukicha, mabasi yanayoweza kuwasafirisha wananchi kama nayo yatakuwa na matatizo kila siku yanaua watu, basi nalo ni tatizo, kwa hiyo uchumi wetu utasimama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili uchumi wetu utengemae ni lazima barabara zetu ziwe nzuri zaidi, reli iwe imara, viwanja vya ndege viwe imara, bandari na kadhalika. Kwa hiyo, wasimamizi wa kusimamia haya ni wale ambao leo wapo kwenye *gallery* na wataalam. Nawaomba na kuwasihi, nchi yetu inawategemea sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa baada ya hayo nizungumzie simu za mkononi. Ni kweli tunashukuru katika Wilaya yetu ya Kwimba, mnara umewekwa pale Hungumarwa lakini bahati mbaya ule mnara haufanyi kazi vizuri. Ukitaka kupiga simu, ili upate mawasiliano mazuri ni lazima upande juu ya mti. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sio kichekesho, ni kweli. Kama sio kwenye mti, kuna sehemu moja ambayo hata ukimpigia simu *DC* wangu Bwana Muhua, ukimpigia simu *DED* wangu Bwana Bremo, Afisa Elimu wangu Bwana Itule, Bwai, kuna sehemu yao ambayo huwa nakwenda kusikilizia simu kwenye kichuguu. Hili wala sio uwongo ni ukweli kabisa. Sasa ukizungumzia utandawazi, mpaka uende kwenye mti, uende kwenye kichuguu, sio vizuri. Naomba sana Mheshimiwa Waziri na yeye bahati nzuri ametajwa kabisa kwamba ni askari wa mwavuli na akishuka anashuka wala hatetereki, hebu awashukie hawa *Vodacom!* Ule mnara waliofunga pale Hungumarwa ni kuurekebisha tu, kuna *buster* ambazo hawajaweka. Tunaomba sana wananchi wangu wa Jimbo la Sumve na Kwimba, maeneo ya Sumve, Inara, Nyambiti, Malya, Hungumarwa na sehemu nyingine, wanazo *handset* zao mikononi lakini mawasiliano ni taabu. Naomba sana Mheshimiwa Waziri hili alichukue na alifanyie kazi. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia *TTCL* ni miaka nenda rudi, tumeshaandika barua kwa Waziri, mimi na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu na Utamaduni lakini utekelezaji ni mdogo. Namkusihi na kumwomba kwamba hili Shirika liko chini yake, hebu awaambie wale wenzetu, Watanzania wa leo wanataka mawasiliano. Bila mawasiliano hatuwezi kwenda mbele. Unamtoa mtu Nyambiti, Malya anakwenda mpaka

Mwanza wakati kama kungekuwa na simu pale Malya, Ngudu, Sumve ingemrahisishia angepiga tu simu mara moja bila kuwa na gharama kubwa zaidi. Utandawazi ndio huo, tunaomba sana Mheshimiwa Waziri hili alichukue ili kusudi simu za Wilaya ya Kwimba kwa maana ya *Vodacom, TTCL* lakini si vibaya hata hawa wenzetu wa *Celtel, Mobitel* nao tunawakaribisha katika Wilaya ya Kwimba ili waje kusaidia kupeleka maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nizungumzie Shirika la Ndege Tanzania. Lile ni Shirika letu lakini matatizo yaliyopo unayafahamu. Lakini nimwombe tu Mheshimiwa Waziri, kuna karatasi ambazo nilimletea yeye mwenyewe, wale wafanyakazi ni Watanzania wenzetu, wazalendo, sio vizuri sana kupuuza kilio cha wazalendo. Kama kuna mapungufu, basi mapungufu hayo utaratibu upo yanaweza kushughulikiwa. Hili sipendi niliseme sana kwa sababu karatasi nimeshampa na kwa sababu najua yeye ni muungwana, suala hili atalishughulikia na hata kwenye kitabu chake ametaja kabisa kwamba Shirika lile sasa linajiendesha kwa hasara.

Sasa hiyo hasara ukijiuliza inatokana na nini? Uongozi inawezekana sio mzuri! Mambo ya *undungunization,* ukabila, si vizuri yakaendelea kukaa kwenye Mashirika yetu, sote ni Watanzania. Naomba Mheshimiwa Waziri hili alisimamie. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine, nizungumzie Shirika la Reli Tanzania. Shirika hili naomba kabisa niwape pongezi ndugu zangu kwa kufanya kazi katika mazingira magumu kweli kweli. Shirika hili sijui lina mabehewa mangapi, lakini *engine* zake zimechoka na mabehewa yale ya abiria yamechoka. Hivi leo watu wenye mizigo inawabidi wasafirishe mizigo yao kutoka Dar es Salaam walete Dodoma. Dodoma ndio wanapata eti unafuu kwa sababu *engine* zimechoka haziwezi kutoka Dar es Salaam kuja hapa. Lakini mwisho, kwa ile bidhaa inayosafirishwa anayekwenda kuumia ni yule mlaji. Naomba kama kuna pesa zimetengwa, kwa kweli zipelekwe *TRC* ili iweze kufanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika vitu ambavyo nimefurahi ni kusikia kwamba ndege ya Serikali inakuja mwezi wa tisa. Wale waliokuwa wanasema sio kweli sasa ndege inakuja mwezi wa tisa. Nimwombe Mheshimiwa Waziri, kwa sababu picha yake iko pale nimeinusanusa, wakati ana-*windup* ni vizuri akaichukua, akaionesha ili kila mtu aone kwamba sio mzaha ni kweli. Naomba sana hilo kwa sababu lilizungumzwa sana hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie Kiwanja cha Ndege cha Mwanza na kila siku nimekuwa nikiomba kwamba tafadhali sana kiwanja hiki ni cha muhimu sana, naomba kiongezwe au kipanuliwe kwa sababu ni kidogo hasa ukizingatia kwamba Mwanza ni sehemu kubwa kwa uchumi, kwa biashara kwa sasa hivi, hata mapato ya Shirika la *ATC* nafikiri Mwanza ni ya pili. Sasa kama ni ya pili, ni vizuri sasa ule muundombinu wa pale tukauboresha zaidi. Lakini pia kwa maana ya Kiwanja cha Ndege cha Dar es Salaam, niombe tu, pale wasafiri wanapopumzikia kuna joto sio la kawaida, viyoyozi havipo.

Naomba viyoyozi viwekwe kwa sababu ule ni uwanja wa Kimataifa, kwa hiyo, ni vizuri ukafanana na Uwaja wa Kimataifa, sio kwa kutumia feni maana pale utakuta zimewekwa feni. Naomba sana viwanja vyetu vifanane na hali halisi jinsi vilivyo. *(Makofi)*

Baada ya kusema hayo, kwa sababu kengele ya pili iko jirani kulia, niseme kwa mara ya pili kwamba yale ambayo nimemwomba Mheshimiwa Waziri, lakini hasa la simu Wilaya ya Kwimba pamoja na Kilolo na sehemu nyingine, kweli kabisa simu hizo zitengenezwe na hawa wenye kumiliki simu *Vodacom, Celtel, Mobitel,* basi waombwe wafanye hivyo ili wananchi wetu waweze kufaidika na huduma hiyo. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. MARIA D. WATONDOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri ambayo wanaifanya. Utendaji unadhihirisha nidhamu na mshikamano wa watumishi wote. Pamoja na pongezi, nina ushauri katika maeneo yafuatayo ambayo nimeyabaini baada ya Vikao vya Kamati:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, yapo malalamiko dhidi ya uongozi wa *ATCL.* Hii niliipata nilipofika Ofisi ya *ATCL* kutaka huduma ya tiketi. Watumishi walionyesha dhahiri wana mgomo baridi. Nilipofuatilia, nikaambiwa kuwa *ATCL* imekithiri kwa ukabila, ulaji na kubagua watumishi wa zamani. Nashauri Serikali iunde Tume na kufuatilia suala hili, maana ina asilimia 51 ya hisa zote. *SAA* isiachiwe kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lipo pia lalamiko la kuondoa Kampuni ya Ulinzi ya Kitanzania na kuiweka ya Afrika ya Kusini ambayo gharama zake ni mara kumi ya ile ya Tanzania. Serikali itambue kuwa Watanzania siku hizi wako makini sana katika kufuatilia matatizo ya nchi yao. Nashauri Serikali isifumbie macho tatizo hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uwanja wa ndege wa Lindi ni mkubwa, lakini haupati huduma za ndege. Naomba Serikali iendelee kuuhudumia uwanja huu ili usiharibike na kusahauliwa. Huduma ya Zimamoto iliopo ipatiwe gari la uhakika ili ndege zitakapokuja zisikwame.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *ATC Holdings* haijakamilisha kazi zake za kudai madeni yaliyoachwa na *ATC.* Nashauri *ATC Holdings* waongezewe muda ili wakamilishe kazi iliyoanza. Kazi wanayofanya ni ngumu na ina umuhimu wa kufichua waovu na kurudisha mali za Watanzania. Yapo mambo mengi ambayo yameanza kufichuliwa, hivyo tusiachie njiani ama sivyo, Serikali yetu nayo itakuwa inawalinda wadaiwa na wale waliopoteza mali ya umma. Nashauri mitambo ya simu ya Lindi na Mtwara irekebishwe, maana simu hazipatikani kwa urahisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ELIACHIM J. SIMPASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jitihada ni kubwa sana imefanywa kusambaza mtandao wa simu za mkono nchini. Hongera. Bado bei za simu hizo C, V na B, ni za juu mno ukilinganisha na nchi nyingine zinazotuzunguka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *TTCL* na uendeshaji wake, na makubaliano utumishi, hisa na mafao, ingefaa vipitiwe upya *(revisited)* kuondoa kero.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinzi wa njia za Reli ya Kati na *TAZARA* ufanyiwe mkakati mahsusi kwa kuhusisha vijiji jirani na njia hizo. Wanaoishi katika maeneo yaliyofanyiwa uharibifu, wapate adhabu kubwa. Napongeza hatua za hivi karibuni za kushirikisha mikoa ipitayo *TAZARA* kwa *RCS* kukutana Mbeya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafirishaji wa abiria Jijini Dar es Salaam ni hatari kwa sababu nidhamu ya madreva ni mbovu. Wanaacha barabara na kupita pembeni mwa barabara na hivyo kuendelea kubomoa barabara na kuunda njia mpya zenye mashimo mengi. Ni vyema vyombo na Mamlaka zinazohusika ziweke vizingiti kando ya barabara hizo ili kwazuia wapasua njia hizo na kuwafanya wafuate mstari *(queue).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado Tunduma tuna majengo ya *TTCL* yaliyojengwa miaka zaidi ya mitano iliyopita, lakini mtambo haujawekwa. Jambo hilo limetupa taabu sana sisi wasiwasi. Pengine tuendelee kuomba Wizara ituonee huruma, iweke mtambo huo haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, umahiri wa kazi ndani ya Wizara unafurahisha sana. Tuendelee kukumbea ili uendeleze kasi njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaiomba Serikali itoe fedha ya kutosha kwa ajili ya ujenzi wa uwanja wa ndege wa Songwe, uweze kukamilika kama ilivyopangwa na kukusudiwa. Nawatakia kila la kheri.

**MHE. SHAMIM P. KHAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kuwapongeza Waziri Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Naibu Waziri mwenzangu, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Katibu Mkuu, Ndugu Salum Msoma, pamoja na Wataalam wote kwa kazi nzuri wanayofanya kuliendeleza gurudumu la Mawasiliano na Uchukuzi. Ninaunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *ICT,* nashukuru sana kwamba Wizara imeweza kutayarisha Sera ya *ICT.* Tanzania ni nchi mojawapo katika Bara la Afrika kuwa na sera hiyo. Hongereni! Kwa bahati nzuri nilipata bahati kuhudhuria mikutano uliohusu *ICT* - Kampala, Uganda. Msisitizo ulikuwa kama ufuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuwe na mipango ya makusudi kuwaelimisha akinamama (wanawake) wote walioko mijini na vijijini, fani hii ambayo ni muhimu sana katika kuukabili utandawazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile vitendea kazi kama vile *computers* ni ghali, nashauri tuendelee kuongezea *Tele-Centres* vijijini. Hii itasaidia watu wanaoishi vijijini kushitiki katika suala la kuukabili utandawazi, na siyo tu kuwa watazamaji kama ilivyo hivi sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri takwimu zetu ziwe *disaggregated* yaani zionyeshe idadi ya wanawake na wanaume na siyo kutupatia jumla tu. Tunaposhiriki mikutano ya Kimataifa, huwa tunaadhirika tunaposhindwa kutoa taarifa hizo. Hii inawezekana kabisa, kwani kila Wizara sasa ina *Gender Focal Point* na Wizara yenu tayari imemteua Afisa anayesimamia kitengo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sekta binafsi nao hawako nyuma. Nashukuru tuna *Internet Café* nyingi mijini, bado vijijini. Nashauri waombe wajaribu kwenda vijijini *(Rural).*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipata fursa ya kuhudhuria Mikutano wa Wanawake, *Seoul - South Korea.* Asilimia 60 ya wanawake wa Korea wana uwezo wa kutumia *computer* kwa sababu *programmes* zao ziko katika lugha yao (Kikorea). Nashukuru wameanza kutayarisha *programmes* za Kiswahili. Hii itatusaidia sisi Watanzania wenye kutumia huduma za *Internet.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho nampongeza sana tena sana Ndugu Kowero, ni hazina kubwa. Alinisaidia sana kunipatia *information* ya *ICT* tulipokwenda Kampala. Namshukuru pia Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, kunisaidia kufanikisha mikutano huo muhimu.

**MHE. ARIDI M. ULEDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kupeleka huduma za Posta katika Mji Mdogo wa Mangaka. Mangaka ndiyo Makao Makuu ya Jimbo la Nanyumbu na kwa hivi sasa hakuna huduma yoyote ya Posta, hivyo, kupeleka huduma hii muhimu, itawasaidia sana wananchi na taasisi mbalimbali zilizoko katika mji huo na maeneo yanayozunguma mji huo mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taasisi ambazo zipo katika maeneo ya Mji Mdogo wa Mangaka ni pamoja na Kituo cha Polisi, Shule za Sekondari, Vituo vya Afya, Shule za Msingi, Wafanya biashara mbalimbali, *Mission* mbalimbali na Misikiti na Makanisa mengi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano ya simu ni muhimu kwa sasa. Naomba mitandao ya simu ambayo sasa imefika Masasi Mjini, ielekezwe ifike katika Mji Mdogo wa Mangaka na kuendelea hadi Tunduru, ili barabara yote ya Masasi - Tunduru, ipate huduma za simu. Mitandao ya simu ambayo hadi sasa imefika Masasi Mjini ni *TTCL,*

*Celtel* na *Vodacom.* Naomba mitandao hiyo yote sasa ielekeze nguvu zao kupeleka simu Mangaka ambapo ni kilometa 50 tu kutoka Masasi Mjini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano ya Simu na Posta ni muhimu sana kwa Jimbo la Nanyumbu kutokana na kuongezeka kwa shughuli mbalimbali za kiuchumi. Ieleweke kuwa hivi sasa kuna Hifadhi ya Lukwika - Lumesule ndani ya Jimbo la Nanyumbu, ambapo watalii mbalimbali hutembelea na kuja kuwinda. Hivyo, mawasiliano mazuri ya Simu na Posta ni muhimu sana katika kukuza utalii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa barabara ya Mtwara - Masasi - Tunduru - Songea - Mbamba Bay na ujenzi wa Daraja la Umoja kuanza kwa hatua mbalimbali, kunahitaji mawasiliano kama ya Simu na Posta. Kwa sababu shughuli zote hizo zinafanyika kupitia Jimbo la Nanyumbu, ni muhimu kukawepo mawasiliano mazuri na ya kutosha. Kwa hiyo, naomba mawasiliano hayo yakapelekwa Jimboni Nanyumbu mapema sana.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nitumie nafasi hii kwa njia ya maandishi, kuwapongeza Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wa Idara zote ndani ya Wizara hii, pamoja na Watendaji wote walioshiriki kuandaa Bajeti hii nzuri yenye mtazamo wa kuleta mawasiliano ya kisasa na uchukuzi wenye kulenga kuinua uchumi wa nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizi, sasa nitamke rasmi kuwa naunga mkono Bajeti kwa asilimia mia moja na ninawatakia utekelezaji wenye ushirikiano na ufanisi wa kiwango cha juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda niipongeze Serikali kwa kujenga Kituo cha Utabairi wa Hali ya Hewa Mkoani Singida, ambao sasa unasaidia sana kutoa utabiri wa mambo mbalimbali, kwa mfano hewa, mvua, joto na kadhalika ambao unasaidia wananchi katika shughuli zao za uzalishaji mali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza pia Serikali kwa kununua *Radar* ambayo sasa inasaidia sana utabiri wa anga kwa ajili ya usafiri wa anga. Naiomba Serikali itazame uwezekano wa kununua *Radar* kwa ajili ya Utabiri wa Hali ya Hewa ili uanze kufanana na ukweli kuliko ilivyo sasa kwani inakuwa kama wanapiga ramli, siyo utabiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu kuwa endapo Serikali itatekeleza, utabiri utakuwa wa kisasa na wenye kuwasaidia Watanzania kutimiza majukumu yao barabara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kuwapatia Ofisi ya kudumu Kitengo cha Hali ya Hewa. Hii inaonyesha ni jinsi gani Serikali inajali maoni ya Waheshimiwa Wabunge, nikiwa miongoni mwa walioomba wapewe ofisi kuwaletea ufanisi katika utendaji wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru Serikali kwa kuunga mkono ujenzi na upanuzi wa uwanja wa ndege Mkoani Singida. Naiomba Serikali kwamba jitihada hizi ziendelee ili uwanja huu ukamilike.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile nitakuwa mchoyo kama sitapongeza juhudi za makampuni ya *Celtel, Vodacom, Mobitel* na kadhalika kwa kusaidia kwa kiwango kikubwa mawasiliano sasa hadi vijijini. Naiomba Serikali isaidie makampuni haya kuona ni tatizo gani mawasiliano yanatofautiana hata kati ya chumba na chumba katika nyumba moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kusema kwamba naunga mkono hoja.

**MHE. LEPHY B. GEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kuunga mkono hotuba hii ya Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa kazi nzuri anayofanya. Juhudi anazoendelea nazo zinaleta matumaini makubwa ya maendeleo kwa nchi yetu yote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Waziri kwa kazi nzuri aliyoifanya katika Jimbo langu kwa kubadilisha mataluma ya reli yenye uzito wa Lb. 45 na kuweka Lb. 56. Bado namwomba Waziri aendelee kubadilisha reli hiyo ifikie Lb. 80 ili usafiri wa reli hiyo uwe wa raha na haraka kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru kwa kutuletea huduma ya simu za mkononi. Kwa Mpanda, huo ni ukombozi mkubwa kwa maendeleo ya Wilaya yetu kwa ujumla. Mungu akujalie Mheshimiwa Waziri katika hilo. Tunaomba makampuni mengine ya *Vodacom,* yaje kuwekeza, *Celtel* wametangulia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kuhusu mambo mawili. Kwanza, ni ujenzi wa nyumba ya kupumzikia wageni wanaposhuka kwenye uwanja wa ndege wa Mpanda. Kibanda kilichopo hivi sasa hakifai na hakikidhi hadhi ya mji na uwanja wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni ujenzi wa nyumba ya Posta. Nyumba iliyopo ni *container.* Huduma za Posta ni muhimu sana kwa Wilaya yetu hususan mji wetu wa Mpanda. Hivyo, inatakiwa nyumba inayolingana na hadhi ya mji wetu wa Mpanda na ongezeko la idadi ya watu ambao watahitaji huduma hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaomba kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ni mfuatiliaji mzuri na mchapakazi, ni imani yangu kwamba katika haya mawili angalau atatoa maelezo ya kuwapa imani wapigakura na wananchi kwa ujumla wa Jimbo la Mpanda Kati kuwa yote hayo mawili, utaratibu wake wa kuyatekeleza utakuwaje. Asante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena kukushukuru na ninaunga mkono hotuba hii.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri kwa hotuba nzuri na yenye kuweka matumaini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napongeza jitihada nyingi za kiutendaji zinazofanywa na Wizara hii. Naomba Waziri asaidie kuweka wazi au kutoa ufafanuzi kwa mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na tatizo la kutowekwa lami uwanja wa ndege wa Bukoba, jambo ambalo hivi sasa linasababisha wakati wa mvua, ndege zisitishe safari zake za kuruka na kutua Bukoba. Ikizingatiwa kuwa tayari tatizo hili, mimi pamoja na uongozi wa Mkoa, tulishaliwasilisha kwa Mheshsimiwa Waziri, naomba Mheshimiwa Waziri aeleze iwapo Bajeti hii itawezesha uwanja wa Bukoba kuwekwa lami.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kufikia hatua ya kufanikisha suala la kuanzisha huduma ya *speed boat* kati ya Mwanza na Bukoba. Tunaamini kwamba meli hizo zitawezeshwa kutumia huduma ya gati zinazomilikiwa na *Marine Services* pale Mwanza na Bukoba, badala ya utaratibu wa sasa ambapo kila anayeanzisha huduma hulazimika kuwa na gati yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri kwa kuweka utaratibu wa kutumia gati kwa pamoja, utawezesha kupungua kwa gharama na hivyo kuwa na nauli yenye unafuu kwa abiria na pia njia hiyo itawezesha taratibu nzuri za matumizi ya maeneo yetu ya ufukoni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ipo haja ya Serikali kuwasilisha haraka Bungeni marekebisho ya sheria inayosimamia utoaji *TLB* itakayowezesha zitolewe mikoani moja kwa moja badala ya Dar es Salaam. Urasimu uliopo hivi sasa umepitwa na wakati, na ni kero kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Kanda ya Ziwa na hasa Bukoba na ambao hutegemea huduma ya usafirishaji mizigo kwa njia ya treni, wangeomba njia ya reli ya kati ishughulikiwe haraka ili mizigo yote inayokwenda Kanda ya Ziwa, yote ipakiwe Dar es Salaam badala ya Dodoma. Kwani husababisha bei za bidhaa kupanda maradufu kutokana na hali hiyo pindi inapojitokeza. Nawasilisha.

**MHE. PROF. PIUS P. MBAWALA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja mia kwa mia, hoja ya Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naunga mkono hoja ya Waziri kuhusu matumizi ya fedha kwa mwaka 2004/2005. Nianze kwa kushukuru sana kwa dhati kabisa kwa Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi kwa kuhakikisha pale anapozaliwa Mbunge Kijijini Namabengo, Wilaya ya Namtumbo, pamefungwa *TTCL Phone* 025 - 2600959 ili itumike kwa umma kwa kukodisha. Ahsante sana sana. Wananchi wanafurahi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naleta maombi mapya mengine kuwa Kijijini Mkongo Nakawale au Mkongo Gulioni, Vijiji viwili vinavyopakana, wanahitaji pia *Public Telephone* kupitia mwekezaji. Hapa ndipo anaishi Ndugu Nchimbi, Mwenyekiti wangu wa CCM Wilaya ya Namtumbo. *He is a former TTCL employee.* Hivyo, ukifunga simu hii ninayoomba, italipa kwa sababu ipo *Secondary School* jirani kijijini, ipo *Catholic Parish Headquarters* ya Mkongo jirani, ipo *Health Centre* kijijini, zipo Shule za Msingi nyingi, lipo gulio ya Tumbaku/Ushirika na wapo wakazi wengi sana jirani hapo katika Vijiji vya Mkongo Nakawale na Njalamatata Mkongo Gulioni, Litete na Mwangaza. Hivyo, ikifungwa simu hiyo ya kulipia, hapatakosekana mapato ya kuiendesha simu hiyo kwa faida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natanguliza shukrani. Simu za mkononi kwa sasa hazifai vijijini, Wilayani Namtumbo kwa sababu ya kukosekana kwa *Rural Electrification.* Hivyo, *landline* ndilo jawabu Wilayani kwangu.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa makadirio mazuri ya mwaka 2004/2005, yaliyotayarishwa kwa ufanisi mzuri sana. Naunga mkono kwa 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri ahadi za muda mrefu zitekelezwe mapema ili kuondoa matatizo kwa wananchi. Wizara iliahidi kuweka simu katika Mji Mdogo wa Iguguno, Nkengi, Kinampanda, Shelui na ahadi hii ilikuwa simu zifungwe mwaka 2000. Inasikitisha sana kuona mpaka leo 2005 ahadi hiyo haijatekelezwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo *TTCL* inashindwa, basi namwomba Mheshimiwa Waziri kwa niaba ya wananchi wa Iramba Mashariki, awaombe wenzetu wa *Celtel* watuwekee mnara wa Nkungi, ambapo kuna wateja wengi na utahudumia Iramba Mashariki, Singida Kaskazini, Hanang, Mbulu na sehemu ya Wilaya ya Karatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natanguliza shukrani zangu nyingi kwa Mheshimiwa Waziri kwa msaada atakaotoa kwetu.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze moja kwa moja kwa kutoa pongezi kubwa kwa Mheshimiwa Waziri Profesa Mark Mwandosya na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, kwa jinsi ambavyo wameandaa hoja au hotuba hii nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara hii imefanya kazi zake kwa uhakika na mipango inayoeleweka. Sasa hivi tunaingia kwenye dunia mpya ya utandawazi. Unaposema utandawazi maana yake ni mawasiliano ya uhakika. Hivyo, ni mategemeo yangu kuwa kama kweli tumedhamiria kuingia kwenye dunia mpya, basi tuimarishe mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii nitoe pongezi kubwa sana kwa Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa jinsi ambavyo wanatoa ushirikiano mzuri kwa Waheshimiwa Wabunge. Mimi binafsi nimepewa ushirikiano mzuri katika suala la kupeleka huduma za simu za mikononi katika Miji Midogo ya Ilula na Kilolo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nategemea kabisa kwamba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anajibu hoja za Wabunge, atalitolea ufafanuzi suala hili la simu Ilula na Kilolo, ili wananchi waelewe jinsi Serikali yao inavyowajali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pale katika Mji Mdogo wa Ilula kuna majengo ambayo yalijengwa kwa ajili ya simu za kawaida. Pia ningeomba Wizara hii itoe tamko kuhusu mipango yake, kwani majengo yanaendelea kulindwa na kuangaliwa na Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kutoa pongezi kubwa kwa Uongozi wa Chuo cha Usafirishaji *(NIT)* kwa kazi kubwa wanayoifanya, kwani kwa kiasi kikubwa imechangia kupunguza ajali kwa mafunzo mazuri wanayoyatoa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Katibu Mkuu, *DAP,* Wakuu wa Idara na Wakuu wa Mashirika ndani ya Wizara kwa kazi nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu simu za mkononi, kuna matatizo ya usikivu katika maeneo ya Ngerengere Mjini, Vikosini na kadhalika. Niliandika barua *Vodacom* ili kuweka mnara pale Ngerengere au Kizuka au Sangasanga, wapo wateja zaidi ya 3,000 lakini wanapotaka mawasiliano, watembee umbali hadi uwanja wa shule au hadi wapande juu ya paa la nyumba, hali hii si nzuri. Naomba kampuni mojawapo ya simu iweke mnara Ngerengere, Kidugalo au Diguzi. Naomba sana Waziri unisaidie sana kwa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu gharama za simu, naomba Wizara itoe mchanganuo wa bei halisi ya mawasiliano kwa dakika, *Vodacom* kwenda *Vodacom, Vodacom* kwenda *TTCL, Celtel* kwenda *TTCL, TTCL* kwenda *Celtel* na *Celtel* kwenda *Mobitel.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni nini kilichotokea *Tritel? Code number 0742* ni ya simu gani hivi sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi na Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, kwa usimamizi mzuri katika Wizara yao. Hongera sana.

**MHE. HALIMENSHI K. R. MAYONGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika suala zima la miundombinu ya kuongeza ujenzi wa reli mpya inayotoka Tanzania - Rwanda, Tanzania - Kenya na Tanzania - Uganda. Hii ni kwa sababu ili kuongeza Pato la Taifa. Nadhani reli hutoa mchango mkubwa na pengine kuzidi hata barabara ambayo kila baada ya miaka mitano huharibika yote kuliko reli ambayo haiwezi kuharibika katika kipindi hicho cha miaka mitano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo 2 Julai, 2005 vyombo vya habari vimesikika vikisema kuwa simu za mkononi ni gharama sana kuliko nchi nyingine yoyote ile Barani Afrika. Ni vema ada hizo zitazamwe upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba vituo vya meli ya Mwongozo na Liemba katika Ziwa Tanganyika viongezwe, kwani vile vilivyopo havikidhi mahitaji ya wananchi waishio mwambao wa Ziwa Tanganyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba uwanja wa ndege Kigoma uongezwe, kwani ndege zinazotua ni ndogo sana. Hivyo tunahitaji aina ya *Boeing 707,* ambazo hubeba abiria wengi zaidi na mwendo wa haraka.

**MHE. CHARLES H. KAGONJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Naibu wake, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, pamoja na Watendaji wote wa Wizara hiyo wakiongozwa na Ndugu Salum Msoma, Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri sana inayofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Wizara kwa jitihada zake za kusambaza huduma ya simu nchini. Pia nafurahi na kupongeza utaratibu mpya wa *TTCL* kuanzisha utaratibu wa *Prepaid Cards.* Hata hivyo, *TTCL* imekuwa ikitoa ankara za malipo za ajabu na za kutisha kwa wateja wake. Hivi sasa wateja wengi hasa kule vijijini katika Jimbo langu, wameshindwa kabisa kulipa madeni hayo. Inawezekana vipi kwa miezi miwili au mitatu, mtu aletewe *bill* ya shilingi 300,000/= mpaka 800,000/=? Kwa sababu hiyo, simu nyingi hivi sasa hazitumiki tena. Hayo ni matumizi ya nyumbani tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuelewa kwamba wale wateja ambao wanaamini kuwa *bill* walizopewa siyo sahihi, wafanye nini kabla hawajaingia katika mpango mpya?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeambiwa katika hotuba ya Waziri kwamba yako Mashirika ambayo yatapewa muundo mpya, vema. Naomba kupewa ufafanuzi kwa nini yaundwe upya, ziko faida na hasara kiasi gani katika mpango huo? Wala siyo katika Wizara hii peke yake, nadhani ni mtindo mpya. Ninachoomba ni ufafanuzi wa sababu za Mashirika hayo kuundwa upya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nishukuru kwa juhudi ya usambazaji wa simu za mikononi hadi vijijini. Nimemwomba Mheshimiwa Waziri na Wizara hii mara kadhaa kwamba *Celtel* hawajafika Jimboni kwangu, ingawa wamefika Wilayani. Licha

tu kwamba Jimbo langu litakuwa na biashara nzuri kwa kampuni hiyo ya simu za mikononi kwa sababu ya uzalishaji wa kushoto na wafanyabiashara wengi, simu hizo kuishia ukingoni mwa Jimbo langu pia ni mgogoro wa kisiasa.

Pamoja na maombi hayo, nashauri pia gharama ya matumizi ya simu hizo za mikononi ni ghali sana. Utaratibu ufanyike, gharama hizo ziangaliwe upya. Simu siyo kitu cha anasa. Hivi leo, simu kwa sasa ni nyenzo muhimu sana ya maendeleo. Hivyo, jitihada zilizokwusha anza zisikome, bali ziongezwe nchi nzima na vijiji vyote viweze kufika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu yote ya Wataalam wakiongozwa na Katibu Mkuu, kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara. Napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi napenda kutoa shukrani za dhati kwa makampuni ya simu za mikononi ya *Mobitel, Celtel* na *Vodacom,* ambazo zote zimefika Karatu na zinapatikana karibu katika vijiji vyote vya Karatu, japo mahali pengine *network* inakuwa na matatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Tarafa nzima ya Eyasi, ambako vinazalishwa vitunguu 25% ya Tanzania na pia wanunuzi wa vitunguu wanatokea nje ya nchi ikiwa ni pamoja na Nairobi na Mombasa, hakuna kabisa mawasiliano. Je, Wizara itakubali kushauri na kushawishi makampuni hayo kuongeza nguvu mitambo iliyoko maeneo ya Maratu kwa kusogeza mnara angalau mmoja kwa ajili ya miji midogo ya Mangola Barabarani na Qanded ili iweze kutumika kuhudumia wateja katika eneo hilo muhimu kwa biashara ya vitunguu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, siku za hivi karibuni kuna taarifa katika vyombo vya habari kuwa kuna hujuma dhidi ya *ATCL* inayofanywa na kampuni ya *SAA.* Je, Serikali ina taarifa hiyo? Na kwa kuwa Serikali ya Tanzania inamiliki 51% za hisa za kampuni hiyo, je, ni hatua gani inachukuliwa kuzuia kufilisika kabisa kwa kampuni hiyo, jambo ambalo litaathiri kwa kiasi kikubwa wafanyakazi na hata maslahi ya nchi yetu?

Kwa vile kuna mgogoro wa muda mrefu kati ya uongozi na wafanyakazi wa *TTCL* kuhusu mkataba wa hiari na kwa vile taarifa iliyoko ni kuwa uongozi unajilipa viwango vikubwa vya mshahara wakati wafanyakazi wanaomenyeka wanaumia, Serikali inafanya nini ili mgogoro huo umalizike mapema, hasa kwa kulinda maslahi ya wafanyakazi wa Tanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, natanguliza shukrani za dhati.

**MHE. TATU M. NTIMIZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza hotuba na kuunga mkono hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wahudumu wa Reli katika Magenge, bado ni kitendawili katika kuwahudumia. Nyumba zao bado ni duni, hazifanyiwi ukarabati. Nge, nyoka na tandu ni washiriki wenzao katika kuishi ndani. Kama nyumba hazitengenezwi, basi hata kuwaondolea wadudu hao? Afya na mazingira mazuri ya nyumba, kiakili watafanya kazi kwa ari, kwa nia na kwa uwezo wao wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika magenge hayo, maji ni tatizo. Matenki ya kuhifadhia maji ni mabovu na kutu nyingi. Pia hawapelekewi maji kwa wakati, ni watu sawa na sisi, tuwaenzi na kuona kuwa wanapata stahili za kibinadamu. Wataishi vipi ikiwa hata maji kwao ni mzigo kwa Shirika la Reli na Wizara kwa ujumla. Kutokana na kutokuwa na mahali pazuri pa kukaa na kutokana na kutokuwa na maji ndiyo maana maradhi hayatoki katika magenge yao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifaa vya kufanyia kazi ya kuhudumia Reli, havitolewi kwa wakati muafaka na vikitolewa havitoshi na nyakati zingine visivyoenea kwa wote au kupeleka *size* moja bila kujali umbile la mtu. Hii ni kuwadhalilisha. Hivi hawa watu mnawaonaje? Kama si wa muhimu, basi tuwaondoe ili lisiwe kero. Pengine mtapata namna iliyo bora kuhudumia Reli hii ka Kati? Inasikitisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tazameni vema kuhusu watoto wanaopelekwa Shule ya Msingi ya Reli huko Itigi. Kuna malalamiko jinsi ya uchaguzi unavyofanyika. Wapelekeni watoto zaidi, na wazazi wafanye kazi kwa magenge ambayo maeneo yao hayana vijiji ambako shule zipo. Inasemekana watoto wasiokuwa na matatizo ya Shule ya Msingi, ndiyo wanachukuliwa kwa kufahamiana. Waoneeni imani watoto walioko katika magenge maporini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niliomba kuwekewa *halt* kati ya Stesheni ya Malongue na Tura. Eneo hili nilitoa maelezo ya kutosha na ya msingi kwa nini niliomba niwekewe *halt* hiyo. Barua ya maelezo hayo anayo *DTM* Tabora, Mkurugenzi Mkuu wa Reli na Mkuu wa Mkoa Tabora. Nashukuru wataalam walifika kwenye eneo hilo linaloitwa Ipulanilo. Baada ya kupima, imekuwa *Assalaam Aleikum,* hawajaonekana tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa ujenzi wa shule umeanza, wananchi wanapata taabu namna ya kusafirisha vifaa vya ujenzi na wahudumu wa kusaidia ujenzi. Wanakwama kufika mara kwa mara. Mvua zikianza na shule itashindikana kumalizika kwa shida ya usafiri. Viduka vya huduma, vinapata shida ya kupata vitu kutokana na usafiri. Sifa zote za kuwa *halt* zinafahamika na kukubalika kwa asilimia kubwa. Waoneeni huruma wakazi wa Ipulanilo ambao ni wengi na wanahitaji huduma za maendeleo.

Kuhusu huduma ya simu za mikononi. Nitaishukuru Wizara kama itawashawishi wawekezaji wa huduma za simu hizo ili watuwekee mtandao mmoja katika Stesheni ya Ugalula, hasa wa *Vodacom* na *Celtel,* hapo ni Makao Makuu ya Jimbo, lakini pia kuna vijiji karibu vya Goweka, Kigwa, Kawekapina na Ipululu. Vijiji hivi nimevitembelea hivi karibuni na kuona wakazi wengi kwa ujumla katika vijiji vyote ni takriban 500.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitashukuru kama huduma hii itapatikana kwani vitaendeshwa kifaida kutokana na watumiaji kuwa wengi hasa kipindi hiki cha kukaribia uchaguzi kuliko miaka hii miwili. Nawasilisha.

**MHE. D. PIUS Y. NG'WANDU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hongera kwa hotuba nzuri yenye mipango thabiti na endelevu. Sina la kuongeza, ila kuwatakia utekelezaji bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi langu ni kwamba Chuo cha *TTCL* Kijitonyama kipewe *UDSM* au *DIT* kwa ajili ya kuendeleza kwa ukamilifu fani ya *Tele-Communications.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna mpango wa *Rationalization of Tertiary Education and Training* wa *World Bank* ambao unalenga katika kupata *allocative efficiency of scarce resources.* Ni vema tukashirikiana ili kupunguza *unit costs* na *in built inefficiencies* katika *institution* zetu. *NIT, Bandari College, DMI, CATC* na Vyuo vinavyofundisha *ICT* viimarishwe kutoa elimu bora zaidi nchini na Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa taarifa *Vodacom* bado hawajaanza shughuli Wilayani Maswa.

**MHE. KHALID S. SURU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sina tatizo la kukataa kuunga mkono hoja hii yaani naiunga mkono hoja kwa kiwango cha 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachangia kuhitaji maelezo ya wazi zaidi kuhusu ahadi ya Serikali kupanua huduma za simu kwenye maeneo yafuatayo chini:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Tarafa ya Pahi, Makao Makuu ya Kata za Pahi, Busi, Haubi, Kwadelo, Bumbuta na Kalamba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, simu za mkononi ni rahisi sana kufika maeneo hayo ili mradi madishi au *buster* kusimikwa kwenye vilima vilivyo karibu na maeneo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sana tena sana ufafanue majibu hayo. Pia za *TTCL* zifikishwe huko haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarafa ya Bereko katika Makao Makuu ya Kata za Masange, Mnenia, Kisese, Kikilo, Bereko na Kikore. Wananchi hawa wanataka simu hizo za mkononi haraka sana. Uwezo wanao wa kununua, mradi mtandao ufikishwe huko. Madishi au *buster* zifungwe ili zifike huko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na *Celtel,* naomba *Vodacom* na *Mobitel* watoe huduma hii huko kiushindani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tarafa ya Kolo katika Makao Makuu ya Kata za Kolo, Changaa, Thawi na Soera, maelezo ya hapa ni kama nilivyoeleza katika hizo Tarafa zingine za Pahi na Bereko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa mtandao wa *STD* na *Celtel* umekamilishwa pale Mjini Kondoa, kwa nini sasa simu hizo zisipelekwe maeneo hayo ya vijijini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kuimarishwa kwa Posta Jimboni. Nashukuru Posta ya Bareko imeboreshwa vizuri kuliko zamani. Sasa uhai wake unaonekana upo na ziko dalili za kuboreka zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba itengewe fedha za kuiboresha zaidi. Mhudumu apewe kima cha chini cha mshahara ili wakati wote awepo kazini, kujengwe simu ya *Call Box Telephone* nje ya Posta ili kuvutia watu zaidi. Pale Bereko ziko simu za zisiz na waya, jambo hili ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Posta ya Pahi nayo iimarishwe ili itoe huduma vizuri zaidi. Ikarabatiwe kama ya Bereko. Pia ifungwe simu. Simu ni kichocheo kikubwa sana katika huduma hizi. Mhudumu naye afikiriwe chini ya Shirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante sana.

**MHE. JUMA S. KIDUNDA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Katibu Mkuu na watumishi wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya kama timu moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Wilaya mpya ya Kilindi, naomba niishukuru Wizara kwa mambo mawili makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kuhusu uamuzi wa kuanzisha Posta kamili Makao Makuu ya Wilaya pale Mjini Songe. Huduma hii ni muhimu sana kwetu maana njia ya mawasiliano ya barua na vifurushi, ilikuwa haipo kabisa.

Aidha, huduma ya Benki itakuwa ndiyo huduma pekee ya kibenki katika Wilaya yote na maeneo ya Wilaya jirani kama vile Kilosa, Mvomero Kaskazini, Kiteto, Simanjiro na Handeni. Tunaomba huduma hii ianze mapema maana maandalizi yote ya majengo yamekamilika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba ya Waziri ukurasa wa 75, imeonyesha kuwa Kilindi ni miongoni mwa Wilaya zilizo na huduma ya simu za mkononi za *Celtel.* Kwa kuwa tumekuwa na mawasiliano yenye matumaini makubwa na Waziri Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya pamoja na Naibu wake na Meneja Mkuu wa *Celtel* kuhusu uanzishwaji wa huduma za simu za mkononi za *Celtel,* Wilayani Kilindi pale Makao Makuu Songe, naamini mipango yote ya kazi hii imekamilika na huduma kupatikana muda mfupi mwaka huu. Naishukuru sana Serikali na Kampuni ya *Celtel.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wananchi wa Wilaya ya Kilindi, wanaendelea kukumbushia ombi lao la muda mrefu kuwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, atafute muda wa kuitembelea Wilaya yetu ili tupate fursa ya kupokea nasaha zake nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuunga mkono hoja hii ili Wizara ipate fedha za kuanzisha Posta ya Songe (Kilindi) na simu za mkononi za *Celtel* Makao Makuu ya Wilaya pale Songe.

**MHE. SOPHIA M. SIMBA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia katika kutilia mkazo tatizo kubwa la ujenzi wa gati kule Mafia. Nimekuwa nikisikia kuhusu shida hii ya gati tokea nilipoingia hapa Bungeni mwaka 1995.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kisiwa cha Mafia ni eneo zuri la utalii. Hebu waoneeni huruma ili wapate gati na pia ile *Airport* yao iboreshwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Waziri alitupie jicho Shirika la Ndege la *ATCL. SAA* ya Afrika ya Kusini haina nia nzuri na maendeleo ya Shirika hili pamoja na wafanyakazi. Wenzetu wa *SAA* wataiua *ATCL* kama zilivyokufa *Uganda Airways, Zambia Airways* na hata *Air Mozambique.* Hofu hii ilionekana tokea wakati wa majadiliano ya ubinafsishwaji na sasa ni dhahiri utendaji wao unaonyesha kutonufaisha nchi yetu. Ni kwa nini tiketi zitumike za *SAA* na si za *ATCL?* Hii inaikosesha mapato makubwa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi waliyopewa *ATHCO* ni kubwa na jinsi siku zinavyoendelea, ndivyo umuhimu wake kuonekana. Yapo madeni makubwa ambayo yanawahusu baadhi ya watendaji wa *ATCL.* Hii imedhihirika kwani *Legal Officer* ambaye ndiye aliyakabidhiwa *files* za kesi hizo amekataa kuzikabidhi *ATHCO* na *ATCL* hawaonyeshi kujali kuhusu suala hili, kwani huyu *Legal Officer* anajaribu kuwalinda watendaji wenziwe. Huyu *Legal Officer* wa *ATCL* anastahili kuchukuliwa hatua za kinidhamu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza sana Wizara kwa kazi nzuri inayofanya hususan katika shughuli za usafiri wa reli, maji na mtandao wa simu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri kwa hotuba nzuri aliyoiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wa Wizara na Mashirika yote yaliyo chini ya Wizara hii, kwa kazi zote zilizofanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usafiri wa reli na meli, vitaendelea kuwa njia nyepesi, rahisi na salama kwa ajili ya watu na mizigo. Lakini yaelekea huduma za usafiri huo zinadidimia siku hata siku, na watu wanaotegememea huduma hizo wanaanza kukata tamaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi sasa na ni muda mrefu sana mizigo inayokwenda Bara huletwa na magari toka Dar es Salaam na kupakiliwa ndani ya mabehewa hapa Dodoma. Hii inafanya bei ya bidhaa mbalimbali kupanda bei zinapofika Ngara, Bukoba na Wilaya zote za Mkoa wa Kagera. Mikoa yote ya Ziwa, Tabora na Kigoma yote pia huathiriwa na hali hii. Hivi kuna nini? Tutaendelea hivi mpaka lini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupanda kwa nauli ya meli (Mwanza - Bukoba) kwa asilimia zaidi ya hamsini, nalo limeshtua wananchi wanaohusika. Gharama ya usafiri inapanda, lakini huduma zimeboreshwa vipi? Je, uzembe wa wafanyakazi umerekebishwa? Je, ratiba ya kuondoka na kuwasili kituo hadi kituo kwa meli ya *MV Victoria* imeboreshwa na itakuwa ni ya uhakika? Je, meli *MV Victoria* iko imara?

Mheshimiwa *Spika*, naomba nizungumzie hali ya uwanja wa ndege wa Bukoba. Katika Bajeti ya Wizara, sikuona fungu lolote kwa ajili ya kukarabati uwanja huo. Hivi ni lini uwanja huu utaboreshwa kwa kuweka lami na kuwekewa uzio ili ndege zitue na kuondoka kwa uhakika na usalama zaidi? Nisingependa kueleza mengi maana Mheshimiwa Waziri hata Naibu Waziri, anauelewa uwanja huu. Je, mnasubiri ajali zitokee? Naomba wakati wa kufanya majumuisho, Mheshimiwa Waziri anipe ufafanuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE.TALALA B. MBISE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na timu nzima ya watendaji wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, ikiongozwa na Katibu Mkuu, kwa kuandaa na kutoa hotuba nzuri ya Bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, taarifa ya Kamati ya Bunge ya Miundombinu, katika ukurasa wa 7, aya ya 58, imebaini kwamba Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania *(TMA)* haikupata fedha zilizopitishwa katika Bajeti ya mwaka 2003/2004. Kwa hili, itakuwa vizuri kama Wizara itatoa ufafanuzi na maelezo. Je, *TMA* ilipata *budgetary allocation* kwenye *vote* yake, halafu hiyo ikawa hewa au ilipelekwa kwingine? Je, *behavior* ya namna hii inaweza kuwa ndiyo sababu ufanisi wa *TMA* haujawa wa kuridhisha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, bila ku-allo*cate resources* za kutosha kwa *TMA,* itakuwa ni ndoto kuweza kuboresha huduma za *TMA* na bila kuboresha huduma za *TMA,* itakuwa vigumu kuboresha utabiri wa mwelekeo wa kilimo na maafa yatokanayo na mwenendo wa hali ya hewa. Teknolojia ipo, lakini ni gharama na inahitaji utaalam wa hali ya juu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine linahusu uchukuzi na usafiri vijijini. Huenda hili limeachiwa Serikali za Mitaa kupitia TAMISEMI. Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ndiyo yenye utaalam na uwezo wa ku-*formulate policy guidance.* Mikokoteni, *carts* na vitu vingine vinavyotumika vijijini kwa kutumia nguvu ya wanyama na watu, havifanyiwi utafiti kuboresha kupunguza nguvukazi inayotumika kuvuta.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna wakati masuala kama haya yalikuwa yakifanyika *under the overall supervision of the Ministry of Agriculture.* Kwa sasa ni vigumu kutambua ni nani atoe *leadership* hasa kwenye masuala ya utafiti unaolenga kuboresha vifaa vya uchukuzi vijijini. Naomba Wizara ifikirie hili, itoe kauli yake kuhusu role ambayo wanaweza kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. GIDEON A. CHEYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kuwapongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya Wizara, kwa kazi yao nzuri ya kuimarisha na kuboresha huduma za Mawasiliano na Uchukuzi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Jimbo langu la Ileje na kwa niaba yangu mwenyewe, tunatoa shukrani kwa Wizara kuiwezesha Wilaya yetu kupata mawasiliano ya kuaminika ya siku kati ya Makao Makuu ya Wilaya na sehemu nyingine hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mawasiliano ya simu yaliyopo Wilayani ni ya *TTCL.* Hatuna huduma za simu za mkononi. Upo mnara uliojengwa na *Celtel,* Makao Makuu ya Wilaya. Ni muda mrefu umepita na wananchi wengi wamekwisha nunua simu za mkononi lakini haieleweki uzinduzi wa huduma hiyo ya *Celtel* utafanyika lini. Naomba nifahamishwe mipango ya *Celtel* ikoje.

Aidha, Kampuni ya *Vodacom* nayo iliahidi kufika Ileje na kujenga mnara au minara na wakaonyeshwa mya kujenga minara yao. Lakini kumekuwa kimya. Tunajiuliza kulikoni? Tunaomba Wizara isaidie kutoa msukumo ili huduma ya simu za mkononi iweze kufika Ileje ili tuweze kuunganika na maeneo mengine ndani na nje ya nchi yetu katika mtandao wa simu wa kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho napenda kuishukuru Wizara na Serikali kwa jumla, kwa mradi wa uwanja wa ndege Songwe, Mbeya. Tunaomba kila jitihada ziendelee kufanywa ili uwanja huo ujengwe na kuboresha huduma za mawasiliano ya anga kwa ukanda wa Kusini Nyanda za Juu, pamoja na nchi jirani za kuzini mwa Tanzania. Nawatakieni mafanikio mema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. ROBERT J. BUZUKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze kwa kumpongeza Waziri, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Naibu Waziri,

Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Katibu Mkuu, Ndugu Salum Msoma na Watendaji wengine wote, kwa juhudi zao za pamoja katika kufanikisha majukumu yaliyo mbele ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kimsingi naomba kuchangia maeneo kadhaa ili kuboresha huduma na kufikia malengo yanayokusudiwa kwa Wizara na ili kuwafanya Watanzania wafaidi matunda ya Uhuru wa nchi yao kupitia nyenzo bora za mawasiliano ya kisasa na uchukuzi wa uhakika kwa bidhaa mbalimbali zinazoingia na kutoka nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mawasiliano ya simu Jimboni Solwa, napenda kuiomba Serikali kujitahidi kuweka uwiano wa mawasiliano ya simu katika nchi kwa kugusa Wilaya mbalimbali. Katika jimbo langu la Solwa, nilikwisha iandikia Serikali kupitia Wizara hii mara nyingi kuhusu kupatiwa simu katika vituo *(centers)* au Miji Midogo ya Iselamagazi, ambapo ndipo panakusudiwa kuwa Makao Makuu ya Wilaya ya Shinyanga Vijijini.

Aidha, maeneo mengine ni Solwa, Ikonongo, Zunzuli Sekondari, Salawe na Kakola. Huduma hii ifikishwe kwa kutumia mitambo ya simu za mkononi *(Celtel, Mobitel, Vodacom)* au siwaya kwa simu za mezani, tutakuwa tumewafanya wananchi wa maeneo haya kurahisisha mawasiliano yao ya kibiashara na kijamii na hivyo kuweka katika ramani ya dunia ya mawasiliano ya kisasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uwanja wa ndege wa Mwanza. Uwanja huu ni muhimu sana kwa uchumi na huduma ya nchi yetu. Abiria wengi wanaotumia uwanja huu karibu unashindana na *DIA.* Aidha, usafirishwaji wa minofu ya samaki unafanyika kwa kiwango kikubwa na kuipatia nchi yetu fedha nyingi za kigeni. Uwanja huu pia uko katika eneo la nchi za Maziwa Makuu na kati ya nchi za Afrika Mashariki (Kenya, Uganda na Tanzania). Pamoja na huduma zote hizo, lakini bado yaelekea Serikali haijaupa hadhi inayostahili uwanja huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napendekeza kuwa uwanja huu upewe hadhi na kujengwa katika kiwango cha Kimataifa ili uitwe *Mwanza International Aiarport.* Hii itavutia pia watalii wanaohitaji kuja *Serengeti National Park,* watatumia moja kwa moja uwanja huu badala ya kupitia Nairobi, Kenya na *KIA.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shirika la Ndege la Tanzania. Kumekuwapo mafanikio mazuri ya kuongezeka kwa ndege na huduma zake tangu liingie ubia na Shirika lingine la Afrika ya Kusini. Hata hivyo, hivi karibuni kumekuwako na malalamiko ya watumishi pengine juu ya uongozi kadhaa. Nashauri Serikali ifuatilie mambo haya ili kutatua mapema. *Ambilecho* Waswahili, kuzuia ni bora kuliko kuponya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Shirika la Reli *(TRC),* napenda kushauri kuwa ni vyema hatua zote muhimu zizingatiwe katika kufikia hatua ya ama kubinafsisha au kuweka ubia na kadhalika. Watumishi waelimishwe vya kutosha juu ya kila hatua zinazochukuliwa na Serikali ili waweze kushirikishwa. Aidha, suala la maslahi yao yawekwe bayana baada ya Shirika kukodiwa, kuwekewa wakezaji au kubinafsishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho narudia kuitakia kila la kheri Serikali kupitia Wizara, juu ya azma wanayoikusudia kuwafanyia wananchi na moyo wa kujituma na kujitolea pamoja na kuitumia vyema Kamati ya Kudumu ya Bunge kama walivyofanya kipindi kilichopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante sana.

**MHE. SHOKA KHAMIS JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukushukuru wewe mwenyewe binafsi kwa kuliongoza Bunge letu vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile namshukuru Mheshimiwa Waziri, amejitahidi kuwasilisha vizuri na sitamsahau mama yangu mpenzi Naibu Waziri , Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari pamoja na wafanyakazi wao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pongezi pekee zimfikie Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Bakari Shamis Faki, Mbunge wa Ole, alivyowasilisha. Mimi sitakuwa na mengi katika hoja hii, ila nina machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nitachangia kuhusu simu za mikononi. Katika hotuba yake Mheshimiwa Waziri, alisema kuwa simu za *Vodacom* zimeshafika mpaka Wete na Micheweni, ila napenda kumwambia Waziri kuwa huko bado au zimefika lini? Mpaka naondoka, bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili ni kuhusu simu za *Celtel,* nazo amesema hivyo hivyo. Ni kweli, lakini katika Wilaya ya Micheweni, sehemu kubwa *Celtel* haina *network.*

Tatu ni kuhusu *Zantel,* wao tayari wameshafanya kazi nzuri, lakini tatizo lao kubwa hawatumi ujumbe. Kwa hiyo, nakuomba Mheshimiwa Waziri awaambie wahusika wajitahidi wafanye hivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne ni kwamba napenda kuchangia kidogo kuhusu Posta. Shirika hili liko katika hali mbaya sana, kwani nakumbuka siku za nyuma Shirika hili likuweko mpaka Micheweni, lakini nasikitika katika Makao Makuu ya Wilaya ya Micheweni, Shirika hili limekufa kabisa. Kwa hiyo, naomba lifufuliwe tena.

Kuhusu usafiri wa majini, napenda kushukurukwa kurudi kwa *M. Sepideh* ambayo tayari imeshaanza kusafirisha abiria wa Dar es Salaam - Zanzibar - Pemba na Tanga. Mheshimiwa Waziri kama unakumbuka kipindi cha Bunge la mwezi Februari, niliulizia usafiri huu. Kwa kweli sisi watu wa Visiwani, unatusaidia sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usafiri wa anga, bei zimepanda sana , kwa hiyo, naomba Serikali iangalie kidogo, tupunguziwe bei ingawa ni soko huria. Lakini wenzetu wamezidi.

**MHE. MBARUK K. MWANDORO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Naibu wake, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Katibu Mkuu pamoja na Wataalam Wizarani na kwenye taasisi zinazosimamiwa na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, kwa hotuba nzuri na kazi nzuri zinazofanywa na zinatarajiwa kufanywa na Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pia uniruhusu kuchukua fursa hii kutoa rambirambi na pole za dhati kwa Waheshimiwa Wabunge na familia ya Marehemu Yete Mwalyego, kwa msiba mkubwa wa kuondokewa ghafla na marehemu mpendwa wetu. Namwomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu huyo mahali pema peponi na kuwapa ndugu na marafiki wa marehemu moyo wa subira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inastahili pongezi kubwa kutokana na mafanikio mengi waliyopata na waliyopanga kutekeleza katika sekta ndogo inayosimamia na pia katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kuchukua fursa hii kukumbushia masuala ambayo yanahitaji kupewa kipaumbele maalum, baadhi yake yakiwa ni Bandari ya Tanga. Kwa kuzingatia mwelekeo wa uimarishaji wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, utandawazi na azma za kujenga *EPZ,* Tanga na *Northern Corridor,* ipo haja kubwa ya kujenga bandari mpya na kubwa zaidi huko Mwambani kama ilivyokuwa azma ya siku nyingi.

Pia Reli ya Tanga - Musoma, kutokana na maendeleo na mwelekeo kama nilivyotaja hapo juu, sasa ni wakati muafaka kufikiria upya na kuamua kuhusu kujenga Reli ya Tanga - Musoma na kuhusu mawasiliano Jimboni Mkinga, kama nilivyowasiliana na Wizara pamoja na taasisi na ama asasi zinazohusika, mawasiliano kwa sehemu kubwa ya Jimbo la Mkinga bado hayapo. Naomba Wizara iongeze jitihada ya kusukuma taasisi na asasi zake mbalimbali ili kuondoa kero hii kubwa katika Jimbo la Mkinga.

Kuhusu usafiri kati ya Tanga na miji mingine, usafiri wa anga, meli na reli kati ya Manispaa ya Tanga na miji mingine, bado ni hafifu sana. Ipo haja na kuhamasisha wahusika kuboresha usafiri huu ili wananchi hasa watalii waweze kupata huduma bora zaidi na mwisho ni kuhusu taasisi za udhibiti na usimamiaji, *SUMATRA* kama vile ilivyo *EWURA*, hazina budi kuanzishwa mapema na kuimarishwa ili ziweze kutekeleza wajibu wake ipasavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja 100% na kuitakia Wizara hii utekelezaji mwema. Ahsante.

**MHE. MARIAM S. MFAKI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Watendaji wao wote kwa kazi nzuri inayofanywa na Wizara yake kwani kazi yao inaonekana katika maeneo mengi nchini. Hii inaonyesha mshikamano uliopo katika Wizara pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii. Nawashauri waendelee kushirikiana ili kueneza huduma hizi katika Vijiji vyote nchini ikiwepo Kijiji cha Pahi, Kondoa na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba niseme haya yafuatayo: -

(i) Huduma za simu ni muhimu sana na hasa zikifika vijijini ili ziwasaidie wakulima katika kutafuta masoko ya mazao yao na hii itawasaidia kupunguza gharama za kutafuta soko.

(ii) Naomba Serikali iwasaidie *TRC* kufanya usafi katika treni na kuwa na uhakika wa treni za abiria.

(iii) Naomba Serikali iangalie uwezekano wa kujenga kiwanja kipya cha ndege hapa Dodoma katika eneo la Msalato kwani ndicho kina nafasi ya kutosha badala ya maendeleo kutumia kiwanja kilichopo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu wake na ninawatakia ushindi wao kwa uchaguzi ujao ili waje wafanye kazi.

**MHE. RAPHAEL N. MLOLWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Naibu wake, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara na Mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri wanazofanya kuiboresha sekta hii muhimu ya Mawasiliano na Uchukuzi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu kuhusiana na sekta hii ya Mawasiliano na Uchukuzi ni wa masuala matatu ambayo ni Reli ya Kati, mawasiliano vijijini na kuendeleza Bandari zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Reli ya Kati ni sehemu ya Ukanda wa Kati wa Maendeleo *(Central Economic Development Corridor).* Kwa maana na mtazamo huo, reli hii ni chombo muhimu sana katika kukuza na kuendeleza shughuli za kiuchumi na kijamii kwa nchi yetu na nchi jirani hususan Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, Zambia na Burundi. Wakati Taifa linajitahidi kuboresha huduma za barabara na wakati tayari kuna jitihada za kuboresha uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam, inabidi pawepo juhudi sawia kuboresha Reli ya Kati. Vinginevyo, *carrying efficiency* ya reli itaathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni mapendekezo yangu ya dhati kwamba Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ione umuhimu wa kuiboresha Reli ya Kati kwa kuzingatia: -

(a) Msukumo wa utandawazi hasa hasa hoja ya ku-*maximize on transit trade and to rap on the economic potential of Eastern Democratic Republic of Congo.*

(b) Kuibua uwezo wa kiuchumi na kijamii uliomo katika Ukanda wa Maendeleo wa Kati wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mawasiliano vijijini, napenda kuhimiza kwamba huduma za mawasiliano zienezwe haraka vijijini. Katika ulimwengu wa leo wenye changamoto za utandawazi, wakulima vijijini wanakabiliwa na masuala ya kujua maendeleo na bei za mazao ya Tumbaku, pamba na kadhalika katika masoko.

(c) Ulinzi na usalama wao na mali zao.

(d) Kupata huduma za afya za uhakika.

(e) Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kujielimisha juu ya masuala mbalimbali ya dunia ya leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Wilaya ya Kahama yapo maeneo mengi ambayo wananchi wanataka huduma za mawasiliano ya kisasa kama:-

(a) Wakulima wa tumbaku wa Kata ya Uyogo, Ushetu, Ulowa na Bulungwa wanataka simu za mikononi kuweza kusimamia vizuri zaidi uchumi wa zao hili ambalo kwa msimu wa 2003/2004 peke yake linatarajiwa kuwapatia zaidi ya shilingi bilioni 6;

(b) Wakulima wa pamba wa Tarafa za Dakawa na Mweli nao wanataka kusimamia vizuri kilimo cha pamba hususan upatikanaji wa pembejeo na mwenendo wa bei za pamba katika masoko ya ndani na nje na utaratibu mzima wa ununuzi wa uchambuaji wa pamba; na

(c) Wakulima wa mpunga nao wana hamu kubwa kuwezeshwa kimawasiliano waweze kujue mwenendo wa ununuzi na uuzaji wa zao hili ambalo linalimwa kwa wingi Wilayani Kahama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla, wananchi walioko vijijini wanataka kuwezeshwa kimawasiliano ili kusaidia maisha yao ya kiuchumi na kijamii kutabirika zaidi. Kwa mantiki hii, Wananchi wa Jimbo la Kahama wamenituma nimuombe Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, atume wataalam Kahama kutathmini uwezekano wa kusambaza huduma za simu za mikononi katika Tarafa za Dakawa na Mweli ili hatimaye wananchi walio katika maeneo hayo nao wafaidike na teknolojia hii ya mawasiliano katika karne hii ya 21 ya Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande mwingine, bandari zetu zilikoko Bahari ya Hindi inabidi ziimarishwe ili kuweza kuhimili changamoto za biashara ya utandawazi. Hata hivyo, uboreshaji wa bandari hizo ni budi uendane na mwelekeo wa mahitaji halisi

ya kibiashara. Nionavyo mimi, kipaumbele cha uboreshaji wa bandari hizi uendane na matarajio ya maendeleo ya kanda husika za maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hii kwa mwaka wa fedha wa 2004/2005.

**MHE. HAMZA A. MWENEGOHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wake wote kwa ushirikiano wao mkubwa wa kazi na hatimaye utayarishaji wa hotuba nzuri sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia maombi yangu ya kila mwaka, naomba simu kwa Tarafa ya Mvuha na Bwakila. Naomba simu hizo zijengwe Mvuha, Duthumi na *Kisaki Station.* Naamini kuwa *TTCL* mwaka huu watatukumbuka katika Jimbo la Morogoro Kusini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ombi hili ni muhimu sana kwa vile Jimbo la Morogoro Kusini lipo mbali sana na Mji wa Morogoro.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sina budi kuishukuru *TTCL* kwa kuweka simu Mji mdogo wa Matombo (Mtamba). Hapa bado maombi ya simu ni makubwa, naomba simu zifungwe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Ahsante.

**MHE. JOEL N. BENDERA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze kwa kuwapongeza Waziri, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Katibu Mkuu, Wakurugenzi wote na Wataalam wa Wizara hii kwa kazi nzuri sana wanayofanya katika Wizara hii. ninawapongeza sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwapongeza, naomba kuchangia machache ambayo ni kero sugu kwenye Mkoa wetu wa Tanga na Jimbo langu la Korogwe Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bandari ya Tanga ni moja ya bandari muhimu zinazotegemewa na Taifa na pia kwa uchumi wa Mkoa wa Tanga. Lakini lazima tukubali hali yake ya miundombinu inahitaji kuboreshwa ili iweze kutoa tija sahihi. Bandari hii ikiboreshwa vizuri itaweza kutumiwa na wafanyabiashara wengi wa humu humu nchini na nje ya nchi kuliko ilivyo sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo la kusikitisha kwa nchi za Uganda, Burundi, Rwanda na Kongo kwa kushindwa kutumia Bandari ya Tanga. Nchi yetu ingeweza kupata Pato la Taifa kubwa kama miundombinu ya Bandari ya Tanga ingeboreshwa na kuwa ya kisasa. Pia, kipo kikwazo cha muda mrefu kwa *documents* kupelekwa Dar es Salaam ambapo ndipo kwenye mashine ya kupitia *(process) documents* hizo ndio

zirudishwe Tanga. Tendo hili limesababisha wafanyabiashara wengi kuihama Bandari ya Tanga. Hivi kuna sababu gani ya kuwa na urasimu huo? Ninaomba maelezo. Yapo maneno Mjini Tanga yanayosemwa kwamba eti huo ni uamuzi wa makusudi ili kuwakomoa wananchi wa Tanga na Bandari ya Tanga kwa ujumla. Hii yote imefanyika baada ya kuona kazi nzuri inayofanywa na Bandari ya Tanga. Tanga mzigo umekaa sana ni siku tatu. Ninaomba sana suala hili lipatiwe ufumbuzi wa haraka.

**MHE. PROF. DAIMON M. MWAGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa pongezi kwa hotuba nzuri, naiunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu uanzishaji wa Jamii Habari Tanzania, mpango huu ni mzuri, naunga mkono. Lakini sharti la msingi ni kuwepo kwa mawasiliano vijijini. Wazo la kuanzisha Mfuko wa Kupeleka Huduma za Simu Vijijini *(Rural Telecom Fund)* ni wazo na mpango mzuri. Lakini hotuba ya Waziri iko kimya juu ya lini Mfuko huu utaanza na utaanza kwa utaratibu gani na kwa awamu zipi. Je, utahitaji sheria kufikishwa Bungeni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ikumbukwe mabadiliko yanakwenda kasi duniani. Hatuwezi kusubiri hisa za wadau kuchangia *fund* hii. Sasa hivi Serikali inafanya makusanyo ya mapato makubwa na kinachotakiwa ni *political will* kuelekeza fedha za kutosha kwenye hiyo *fund* kama tunahitaji kwenda na wakati na nchi nyingine duniani katika mfumo huu wa utandawazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TTCL* ya sasa imerithi madeni mengi ya simu *(bill* za simu) bandia na za kubambikiziwa. Nashauri menejimenti ifanye *cleaning up* ya kumbukumbu hizi ili wale waliobambikiziwa bill hizo wafikie muafaka na hivyo kuendelea kupata huduma za *TTCL.* Kwa kuwa tatizo hili menejimenti ya sasa inalifahamu na kwa kuwa *TTCL* imeanzisha *Prepaid system,* ipo haja ya kulitazama suala hili na kufikia muafaka na wale walioathirika na bill za udanganyifu wa kipindi kilichopita.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Naibu wake, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa 100%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kukumbushia ombi langu la tangu mwaka 2003 kuhusu matatizo ya Jimbo pamoja Mkoa kwa ujumla: -

(i) Uwanja wa ndege wa Sumbawanga bado hali yake siyo nzuri, je, mipango iliyotangazwa mwaka 2003 ya kuimarisha uwanja huo umeishia wapi?

(ii) Ombi la ujenzi wa ofisi yenye hadhi ya Mkoa kwa Posta na Simu, je, kuna maelezo yoyote?

(iii) Ombi la kuimarisha gati ya Kasanga ili iwe bandari kamili kwa ajili ya kuimarisha biashara na nchi jirani kwa faida ya Mkoa na Taifa zima kwa ujumla.

(iv) Napendekeza Waziri aandae Kamati Maalum ya Kupembua Njia ya Kuimarisha *TAZARA* kutoka Tunduma hadi Sumbawanga - Kasanga ili mizigo ya kusafirisha hadi Kongo *(DRC)* ipitie huko badala ya kupitia Mpulungu, Zambia.

(v) Gharama za simu za mikononi ziangaliwe upya, huu ni wakati wa ushindani, wasijenge *cartel* yao. Pia, Waziri afuatilie mbinu za wafanyabiashara wa *handsets* mitumba ambazo zimeanza kuingizwa. Kwa nini wasitengeneze *handsets* za bei nafuu zenye mitambo rahisi na ya muhimu kwa mpiga simu na mpokeaji? Je, *computers* zilizomo kwenye *handsets* ni wangapi wanazitumia?

(vi) Suala la Watumishi wa Reli *(TRC)* lipewe kipaumbele ili hujuma zisitumike. Naelewa jitihada za Waziri katika mambo yote hayo, lakini *TRC, TTCL* limalizwe kwa muafaka. Jitihada ziendelee. Tutafanikiwa tu chini ya uongozi wa Mheshimiwa Waziri na Watendaji wake mahiri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii na kuendelea kumtamkia kheri Waziri na watumishi wa Wizara yake.

**MHE. BUJIKU K. P. SAKILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii kwa hotuba nzuri na shughuli zao kwa kipindi chote cha mwaka uliopita. Mwaka uliopita nchi imeendelea kujionea maendeleo mazuri katika mtandao wa mawasiliano ya simu za mikononi. Hivyo hivyo, katika mawasiliano ya nyanja zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kutumia fursa hii kuendeleza maombi yangu kwa niaba ya wakazi wa Kwimba hususan Ngudu ambapo ndipo Makao Makuu ya Wilaya. Ngudu bado tuna simu za kukoroga. Mtambo uliopo una uwezo wa wateja 200. Hata hivyo, kutokana au na ubovu wa mtandao wa mawasiliano yasiyo ya kuaminika na huduma inayoishia kati ya saa 2 usiku na kuiacha Wilaya nzima ikiwa kama kisiwa, wateja wameshuka kutoka 120 waliokuwa wamefikiwa mwaka 2002 hadi 53 mwaka 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maombi yangu yamekuwa daima kubadilishiwa mtambo ili nasi tuweze kutoka *landline* na za kukoroga kwani kwa simu za aina hii huwezi kufanya mengi katika hali ya sasa. Pia, *line 028 2500917* ifufuliwe kwani sasa *line* moja tu ndiyo inayotumika tangu mwaka 1995/1906 nayo ni 028 2500916. Vile vile, mnara wa *Vodacom* uliowekwa na jengwa Hungumalwa uongezwe nguvu ili kuboresha usikivu Ngudu wanakotegemea mnara wa Misungwi ambao nao kutokana na umbali (kilometa 50) usikivu kwa Ngudu ni hafifu sana. Maeneo yaliyotengwa na Halmashauri ya Wilaya kwa ajili ya kujenga minara ya *Vodacom* na *Celtel* yajengwe ili kuboresha mawasiliano katika Makao Makuu hayo ya Wilaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuendelea kwangu kuililia Wizara hii ni kwa kuwa natambua umuhimu wa mchango katika maendeleo kwa jamii wakiwemo wakazi wa Kwimba. Naomba wasinichoke, bali mara uwezo utakapopatikana watuwezeshe katika yale yote yatakayowezekana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. OMAR S. KWAANGW':** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza sana Waziri, Naibu wake na Watendaji wote wa Wizara hii kwa kazi muhimu wanayoifanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mawasiliano na Uchukuzi ndiyo silaha muhimu sana ya maendeleo. Hivyo, umuhimu wa Sekta hii ni lazima upewe nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa juhudi zake za kutaka kusaidia Mkoa wa Manyara kupata huduma za usafiri wa anga hasa pale alipofanya ziara Mkoani Manyara na Makao Makuu ya Mkoa (Babati). Lakini nasikitika kuwa kwenye hotuba hii hakueleza mipango yoyote ya ujenzi wa uwanja wa ndege Makao Makuu ya Mkoa (Babati). Ni muhimu Mheshimiwa Waziri akasema neno kwenye eneo hili ili tuone na sisi wa Manyara hasa Babati tupo kwenye mipango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafurahi kuwa Babati ipo kwenye mipango ya ujenzi wa Kituo cha Hali ya Hewa. Nakaribisha sana kituo hiki kwa sababu Babati ni eneo la kilimo hivyo kituo hicho kitasaidia sana kuinua kiwango cha uzalishaji. Namtakia kazi njema Mheshimiwa Waziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na naunga mkono hoja.

**MHE. KARIM SAID OTHMAN:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri yenye mwelekeo mkubwa wa kuleta maendeleo ya nchi yetu. Shukrani nyingi zimwendee pia Naibu Waziri pamoja na Watendaji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani sina cha kusema kwa sababu Waziri ameiwezesha Kamati yetu ya Miundombinu kuona na kukagua shughuli zote zilizomo katika Wizara hii pamoja na vitengo vilivyo chini yake, ila kuna mambo mawili ambayo ningeomba ayawekee mkazo katika kuondoa kero hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu Uwanja wa Ndege wa Mafia, Kamati yetu imekwenda na kuona uwanja huo wa ndege. Kwa kweli tusipoziba ufa, tutajenga ukuta, uwanja ni wa udongo mbaya, una misingi mikubwa, unateleza wakati wa mvua, kwa kweli ni hatari sana ingawa kuna jitihada za Wizara kuziba misingi hiyo kwa chokaa na mchanga, nashauri kwa hali ilivyo ni bora ufungwe kabisa, lakini nikakumbuka ukifungwa watafanyaje na wao kako kwenye kisiwa? Taarifa niliyopokea ni kwamba marubani ambao wanaweza kutua uwanja huo ni watatu tu, wakikosekana hao basi rubani yeyote hawezi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naleta ombi maalum kwa Serikali ifanye juhudi za makusudi za kuepuka ajali ya ndege ambayo wakati wowote inaweze kutokea Mafia. Serikali isione kwamba ni hasara kutengeneza kiwanja ambacho hakifanyi biashara, ijali zaidi kutoa huduma kwa raia wake. Mafia kuna hifadhi ya mazalio ya samaki na hoteli za kitalii, itoshe kwamba hiyo ni faida ya kujenga kiwanja hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo lilinivunja moyo ni kuona wanawake, watoto na wagonjwa wakiteremka kwenye mashua umbali wa mita 500 kutoka ufukweni tena maji yakiwa yanawafikia kwenye kitovu. Nilipouliza niliambiwa huingia wasafiri hao kwenye mashua kutoka Kisiju, Rufiji kwa kuvuka mkondo mkali hadi Mafia kwa kutumia tanga wala siyo mashine. La kusikitisha zaidi niliambiwa haimalizi mwezi mashua nyingine huzama na kupoteza roho na mali za raia wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuliona hilo na imeanza mpango madhubuti wa kuliondoa balaa hilo kwa kujenga gati ya uhakika waweze kuhamasika kupeleka vyombo vyao Mafia. La muhimu kwa Serikali ni kufanya hili jambo kwa haraka kabla ya mwaka 2005 iwe matumaini ya Wamafia kwa Serikali yao yawepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Dodoma ni Mji mkubwa sana na ni Mji wetu Mkuu, lakini inasikitisha kwamba hakuna ndege hata moja ya abiria wa kawaida. Mashirika yote ya watu binafsi na hata hili liitwalo la Tanzania *(ATCL)* nalo haliwezi kushawishiwa likaanza njia ya kuja Dodoma angalau ya kupitia, japo wiki mara moja. Kwa nini Serikali imefikia hapa? Ukitaka kuja Dodoma mpaka ukodi ndege kitu ambacho ni gharama mara tatu zaidi kama kungekuwa na ndege ya kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa bidii yake ya kupanua mawasiliano kwa nchi nzima, lakini bado kilio cha wateja ni bei ya simu zenyewe pamoja na huduma kuwa ghali sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi binafsi nilinunua kadi moja ya dola tano Marekani nikatumia dakika ishirini na tisa kupiga Afrika na nikanunua dola tano nikatumia dakika 52 kupiga Uingereza. Sisi Tanzania dola tano kupiga Marekani ni dakika mbili tu, hivi ndivyo jinsi simu zetu zilivyo ghali. Nashauri Mheshimiwa Waziri ajitahidi kwa hili kuzungumza na wenye Makampuni ya Simu ili unafuu upatikane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue fursa hii nimpongeze Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, kwa hotuba nzuri ya Bajeti na malengo mazuri katika sekta zote mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nikichangia hoja ya Wizara hii, napenda kwa niaba ya wananchi wote wa Mwanga nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Naibu

Waziri kwa kazi kubwa waliyoifanya kuwezedha Kampuni ya *Celtel* kuwekeza na kuweza kupokelewa katika Tarafa zote za Wilaya ya Mwanga. Ahsanteni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengi tunaopongeza uwekezaji katika barabara tunafarijika sana kuwa baada ya mipango hii kukamilika, sekta ya uchukuzi itakua na kuiletea nchi mapato mengi. Hili litaongeza pia mapato ya fedha za kigeni kwa kuongeza uchukuzi na nchi za Zaire, Rwanda na Burundi na Uganda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na pongezi hizi, tunaona uimarishaji wa Reli ya Kati na Reli ya Tanga umekuwa hafifu. Tungependa Serikali iongeze uwekezaji katika usafirishaji wa reli kama ifuatavyo: -

(i) Kuimarisha umadhubuti wa reli na kukarabati miundombinu yake ikiwa ni pamoja na mawasiliano.

(ii) Tununue *engine* na mabehewa ya abiria ya kisasa yatakayoongeza *speed* na kupunguza muda wa kusafiri kwenye Reli ya Kati na Reli ya Tanga.

(iii) Tujenge reli mpya ya kuunganisha reli ya *TAZARA* kutoka Tunduma kwenda kwenye *Lake Tanganyika* katika Mkoa wa Rukwa ili kufungua Majimbo ya Katanga na Mashariki ya *DRC* kutumia Bandari ya Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii bila mashaka yoyote. Ahsante sana.

**MHE. GWASSA A. SEBABILI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitangulize kukushukuru kwa nafasi hii ya kuchangia hoja hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kusema kwamba naiunga mkono moja kwa moja hoja iliyoko mbele yetu na pia kumpongeza Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya na msaidizi wake Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, ni halali mno, bila kumsahau Katibu Mkuu na timu yote ya Wataalam Wizarani kwa kazi nzuri na endelevu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hakika Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, ameiratibu na kuisimamia vilivyo Wizara hii. Kweli ni askari wa mwavuli. Siri ya Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, kufanikisha kasi kubwa ya maendeleo katika Wizara yake ni kuifahamu nchi na jiografia yake. Anatembelea Mikoa, Wilaya, Vijiji na sehemu nyingine mpaka Vitongoji. Hongera Mheshimiwa Waziri na Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kazi nzuri ya kuwakomboa Watanzania toka katika umaskini. Kwa mfano, ni jana au juzi tu Naibu Waziri ametoka safari ya Mkoa wa Kigoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kutoa shukrani kwa *Celtel*. Wananchi wa Jimbo la Ngara wamenituma nilete shukrani zao kwa Mheshimiwa Waziri na Wizara yake kwa kuiunganisha Wilaya hii na nchi nzima pia ulimwengu wote. Ni shukrani za kuwahamasisha Kampuni ya *Celtel* ikaweka mitambo yake mwaka 2002 na leo *Vodacom*

imejenga mitambo yake Wilayani Ngara. Simu za kukoroga za *TTCL* hakuna tena. Wilaya ina *fax, telefax* na redio Kwizera inayohudumia Shirika la Wakimbizi na Wananchi wa Wilaya za Ngara, Kibondo na Biharamulo. Uchumi na maendeleo yanakua haraka kwa msaada huu wa Serikali ya Awamu ya Tatu na CCM. Kasoro ndogo za *Celtel* ni kutosikika sehemu za mabondeni na Kata za Rusumo, Ntobeye, Kirushya, Murusagamba na Muganza. Naiomba Wizara ifanye hima kuleta marekebisho kwa kasoro hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *TTCL,* naiomba Wizara iichunguze Kampuni ya Simu Wilayani Ngara. Wateja wake wanabambikizwa gharama kubwa kwa simu wasizotumia. Malalamiko ni makubwa sana. Wateja wengi wameamua kuachana na Kampuni hii na kukimbilia Kampuni za Simu za mikono *Celtel,* baadaye watakwenda wengine kama *Vodacom.*

Mheshimiwa Waziri, sababu ya haya ni watumishi wa *TTCL* kukaa sana katika kituo kimoja kwa miaka mingi sana. Wadau wengi wamekatiwa simu kwa sababu ya kulundukiwa madeni ya watumiaji wengine. Tafadhali saidia hapa na mapema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usafiri wa anga katika Ibara ya 19 na 89, Mkoa wa Kagera hauna kiwanja cha ndege cha uhakika licha ya kuwa Mkoa unaopakana na nchi za Rwanda, Burundi na hata Uganda na *DRC* zenye matatizo miaka yote. Usalama wa Mkoa huu ni wa mashaka na Serikali inafahamu hivyo. Tunahitaji kiwanja cha ndege cha kisasa kwa usafirishaji wa abiria, mazao na amani ya wakazi wa Kagera.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilaya ya Ngara inao uwanja mpya wa Ruganzo ni mpana, mgumu, mrefu na salama. Ulitumiwa na *ATC* miaka ya 1977 hadi 1978 ndipo vita ya Nduli Idd Amin, vita vya Kagera vikavuruga ratiba mpaka leo. Shirika la Wakimbizi linatumia uwanja huu. Baada ya amani kurejea nchini Rwanda na Burundi sasa ni salama na Uganda, *DRC* na hata Kenya wanaulizia matumizi ya uwanja huu. Sasa naomba Wizara iufanyie *promotion.* Wapo wasafiri wengi toka Ngara na Karagwe wanaosafiri kwa barabara wakiwa na wasiwasi waendapo kufuata bidhaa toka Bukoba, Mwanza na mbele zaidi wakiogopa kutekwa na majambazi.

Mheshimiwa Waziri, tafadhali fikiria *promotion* ya Uwanja wa Ruganzo, Ngara. Naamini kwamba *UNHCR* wakishawishiwa watasaidia maana miaka ya 1998 hadi 2000 walikuwa na wazo la kuweka lami barabara ifikayo uwanja huo kutoka barabara kuu ya lami kilometa nne tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usafiri wa reli katika Ibara ya 17, kwa niaba ya wakazi wa Mkoa wa Kagera na zaidi wakazi wa Wilaya ya Ngara, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri na Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa mategemeo ya ujenzi wa reli toka Isaka hadi Kigali. Reli hii itapitia Wilayani Ngara na hakika itachochea maendeleo kwa kiasi kikubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, giza la Kanda *(corridor)* ya Magharibi litatoka maana reli hii itakuwa mwanzo wa kujulikana maporomoko ya Rusumo kwenye Mto Kagera yanayokisiwa kutoa *megawatt 23* za umeme, hatimaye umeme huu nao utapatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, reli hii itakuwa mkombozi mkubwa kwa kuvuta wawekezaji na watalii kama Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii alivyoshuhudia vivutio vya utalii hapo tarehe 21 Aprili, 2004 alipotembelea Wilaya ya Ngara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na matumaini makubwa ya kuchimba madini mengi ya thamani Mkoani Kagera kama *Nickel,* bati, dhabati na kwa reli hii itaimarisha mahusiano mema ya umoja wa nchi za Maziwa Makuu pia Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namtakia utekelezaji mwema wa Bajeti hii Mheshimiwa Waziri na Wizara nzima kwa maendeleo ya Tanzania. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, kwamba ategemee ushirikiano wa hakika na wa wakati wote kutoka kwa wakazi wa Mkoa wa Kagera kwa dhamira ya kufanikisha program za Wizara yake. Ahsante.

**MHE. SIJAMINI MOHAMMED SHAAME:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wote waliotangulia pamoja na kuunga mkono maelezo au Taarifa ya Kamati ya Miundombinu kuhusu Utekelezaji wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi katika Mwaka wa Fedha uliopita pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadiiro yake kwa Mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nichukue nafasi hii maalum kukupa pole wewe mwenyewe pamoja na Bunge lako Tukufu kwa msiba mkubwa wa kufiwa na Mbunge mwenzetu Marehemu Yete Mwalyego, ambaye alikuwa Mbunge wa Mbeya Vijijini na pia Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu. Marehemu Yete Mwalyego alikuwa Mjumbe na Mbunge wa aina yake na aliyekuwa amejaaliwa busara na ukimya na saa zote alikuwa na michango ya utatuzi na uvumbuzi katika vikao vyetu vya Kamati na Bungeni. Naomba kuwapa pole sana familia yake, wapigakura wote wa Mbeya Mjini na Vijijini na pia uongozi wa Chama na Serikali wa Mkoa wa Mbeya, poleni sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kutoa pole kwa msiba wetu wote ambao kwa kiasi kikubwa kimempa taabu kubwa Waziri Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya na Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa ufupi nami nitoe mchango kuhusu hotuba hii. Hotuba hii kama zilivyo hotuba zake tokea mimi kuwa Mjumbe wa Kamati ya Miundombinu, imeniridhisha baada ya kuona kuwa matayarisho yake tokea mwanzo yameshirikisha ma mawazo ya wadau mbalimbali na hatimaye kuungana na Wataalam wa Wizara na Viongozi wao na kwa kuwa nimekuwa mshiriki katika hatua mbalimbali na kwa kuwa Wizara imetupa fursa kuyaona mengi yaliyotajwa humu, sina sababu hata kidogo ya kuwa na wasiwasi wa kuiunga mkono hotuba hi kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwapongeze sana Wataalam wa Wizara ya mawasiliano kwa kuonyesha uadilifu mkubwa kwa viongozi wao na kuonyesha kuwa tayari kwao kufanyakazi na Wajumbe wote wa Kamati ya Miundombinu kwa muda wote, saa yoyote. Aidha, sina budi kuwapa pongezi maalum Waziri, Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, kwa namna ambayo wanafanyakazi kwa kuheshimiana, kushaurina na kuwa muda wote wanaoonyesha kukubaliana jambo ambalo mimi limenipa faraja kubwa sana kwa kujua kuwa ushirikiano wao ukichanganyika na umahiri wa Katibu Mkuu wao, Ndugu Msoma, kwa kweli utazidi kurutubisha heba ya shughuli zetu kwa maslahi ya Zanzibar na Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa hizi siyo Wizara ya Muungano, lakini wenzetu hawa kwa muda wote wamekuwa wanafanya kazi wakitilia sana maanani maslahi ya nchi zetu mbili na hususan wanatambua kuwa uhai wa Zanzibar unategemea imani ya ndugu zetu wa Bara. Nani atashangaaa kuwaona wenzetu hawa kwa uangalifu mkubwa wametuachia na viongozi wetu Watendaji wa Mashirika ya Muungano wenye asili ya Zanzibar kule Zanzibar na hili linafanyika kwa makusudi kuwarahisishia wao na sisi utendaji wa kutotiliana mashaka kwani daima imani huzaa imani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa *terminal* ya *containers* kwa hakika nataka niwapongeze sana Mawaziri wetu wa Bara na Zanzibar kwa ujasiri walionao wa kuamua ujenzi huu kujengwa kule Malindi Zanzibar na kitendo hicho kitapunguza vijineno vya bughudha kwa wasiotutakia mema katika uhai wa matendo yetu yanayoimarisha Muungano wetu wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usalama wa anga, napenda kuwapongeza sana watendaji wa kitengo hiki kwa namna wanavyoendelea kutoa huduma za uongozi wa ndege katika kiwanja chetu kule Zanzibar na kwingine Tanzania Bara hususan kwa kuongeza muda wa saa 17 kwa Kilimanjaro, Mwanza na Zanzibar na saa 12 kwa viwanja vya Dodoma, Arusha na Pemba pamoja na viwanja vingine vya Tabora na Kigoma. Huduma ya Mamlaka hii kwa hakika inaonyesha kusudi lililokusudiwa la kuwa na huduma zinazothibitisha umuhimu wa kuvilinda viwanja vyetu vya ndege nchini Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa Wizara hii imetupatia nafasi ya kutembelea maeneo ambayo ni muhimu, ni muhimu pia kuyasemea kwa umuhimu wa uhai wake na maendeleo yao. Napenda sana kuiomba au kuishauri Wizara hii kuendeleza juhudi zake za matengenezo ya gati ya Kisiwani Mafia na kiwanja chake cha ndege. Kwa kuwa hatua za matengenezo ya dharura yamekuwa yanafanywa na bila ya mafanikio kutokana na mazingira ya visiwa, bado naishauri Wizara kuendeleza juhudi za kutafuta pesa kwa kuendeleza mapenzi hayo. Aidha, nawaomba sana na kuwashukuru Wananchi na Viongozi wao wa Mafia wasivunjike moyo na juhudi za Serikali yao zinavyochukuliwa kwa ajili ya maendeleo yao na wakae wakijua kuwa kila siku watu wanasema baada ya dhiki faraja. Nawaomba sana tuendeleze stahmala zetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ununuzi wa ndege mpya ya Serikali kwa Viongozi Wakuu, naomba nimalizie shukrani zangu kwa Serikali yetu Tukufu ya CCM

kwa kununua ndege hiyo ambayo tunaitarajia kufika baada ya muda ambao si mrefu sana. Naomba sana kwa wale wataalam wetu basi tuangalie sana kupata wafanyakazi wazuri, waadilifu pia kutoka Zanzibar ili kuonyesha kuwa hiki chombo ni chetu sote kwa faida ya Taifa hili la Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeza sana viongozi wa Wizara hii na narejea kuunga mkono hotuba hii kwa asilimia mia moja. Shukrani.

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, pamoja na watendaji wote wa Wizara hii, kwa kazi kubwa na nzuri ambayo imezifanya na kuzisimamia vizuri sana na kuleta mabadiliko na mafanikio makubwa ya maendeleo ambayo hayajawahi kuonekana tangu Taifa letu hili la Tanzania lilipopata uhuru wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii imedhihirisha juhudi za Wizara hii na Serikali yetu ya Tanzania ilivyoleta maendeleo makubwa katika sekta hii ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa nchi nzima, jambo ambalo linajenga matumaini makubwa ya Watanzania kufikia malengo ya maendeleo makubwa ya kiuchumi na kiteknolojia hapa nchini petu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni imani yangu kuwa Mheshimiwa Waziri na wahusika wote wa Wizara hii na Serikali Kuu, wataendeleza juhudi hizi kubwa za kujenga uchumi na maendeleo ya Tanzania. Napenda kuthibitisha kuwa katika kipindi cha mwaka 2003/2004, huduma za usafiri wa anga nchini zimeendelea kuimarishwa sana sana, kitu ambacho kinaleta faida na huduma karibu nchi nzima ikiwemo Zanzibar (Unguja na Pemba) ambapo kila siku kuna usafiri wa ndege zinazotoa huduma kuanzia Dar es Salaam, Zanzibar, Pemba Tanga na hata Mombasa na Mikoa mingine ya Tanzania. Pia katika kipindi hiki cha mwaka 2003/2004, usafiri na uchukuzi kwa njia ya barabara umeimarika sana ndani ya nchi yetu na hata nchi jirani kama vile Kenya, Uganda, Zambia, Kongo, Rwanda, Burundi na kadhalika, jambo ambalo linawapatia fursa wananchi mbalimbali kutembelea nchi hizi na kufanya biashara mbalimbali za kiuchumi na kimaendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na mafanikio haya ya huduma za usafiri na uchukuzi kwa njia za barabara umewezesha wananchi kufanya safari zao za kila siku bila ya usumbufu mkubwa ambao unawaweka katika vituo vya usafiri huu wa barabara kwa kusubiri usafiri. Tatizo hili limeondoka kwa asilimia kubwa sana. Kwa kweli mafanikio makubwa yameonekana na kwa kweli yamesimamiwa vizuri na kuendelezwa zaidi ili pia ziwepo huduma nzuri za usafiri kwa wananchi wanaoishi vijijini hapa nchini ili kuondoa vikwazo katika harakati za kuondoa umaskini nchini kutokana na kutokuwepo kwa miundombinu thabiti, jambo ambalo linawasababishia wananchi wa vijijini kuishi kwa gharama kubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kuwepo kwa matatizo madogo madogo lakini pia tumeshuhudia kuwa wananchi ambao safari zao wanatumia usafiri wa njia ya reli *(TRC),* wanapata huduma hii ya usafiri hapa nchini. Kwa hiyo, ninaiomba sana

Serikali kutokana na umuhimu wa safari hii ya njia ya reli, iangalie yale matatizo ambayo yanaonyesha kutoa usumbufu kwa wananchi wanaosafiri kwa kutumia reli na watumishi wa Shirika hili ili kujenga ufanisi zaidi wa kutoa huduma kwa wananchi wa Tanzania na kujenga misingi madhubuti ya maendeleo kwa wananchi wote wa Tanzania na nchi yetu ya Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri, imeelezea juu ya usafiri na uchukuzi kwa njia ya maji ambapo imeelezea kuwa katika mwaka 2003/2004, miundombinu na huduma za usafiri na uchukuzi kwa njia ya maji ziliendelea kukua na kuboreshwa zaidi kwa mwaka uliopita. Ninathibitisha hili kwa kusema kuwa ni kweli kabisa kuwa usafiri na uchukuzi kwa njia ya maji uliendelea kukua na kuboreka zaidi ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa mwaka uliopita. Hivi sasa usafiri baina ya Dar es Salaam na Zanzibar umeimarika sana na yale matatizo madogo madogo ya usafiri kwa vyombo (Boti) ya kupangiana umepungua na huduma zinakwenda vizuri na zinaridhisha. Pia usafiri kutoka Dar es Salaam, Zanzibar, Pemba kwa njia ya maji upo na unapatikana vizuri sana, kitu ambacho kinaleta mafanikio makubwa na mazuri katika kuwa hudumia wananchi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika ziwa letu la Victoria zipo meli zinazotoa huduma kwa wananchi wa kanda ya ziwa vizuri sana. Kwa hiyo, Serikali haina budi kuimarisha zaidi huduma hizi za usafiri katika maeneo hayo kwa maendeleo ya wananchi wa maeneo hayo na nchi kwa ujumla, sambamba na kuimarishwa kwa huduma hizi za usafiri katika maziwa na hata majini (baharini), suala la usalama wa vyombo vya usafiri majini ili kuongeza usalama kwa abiria pamoja na mizigo yao. Kwa hiyo, ni imani yangu kuwa suala hili la usalama litaendelea kusimamiwa vizuri ili kuendelea kuwepo kwa usalama madhubuti katika vyombo vyetu vyote vya usafiri wa majini na maziwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ambalo ninataka kulichangia ni juu ya usalama wa usafiri wa anga nchini, ni suala muhimu kusimamiwa vizuri ili kuepusha majanga ambayo yanaweza kuhatarisha usalama wa wasafiri wanaotumia anga na kadhalika. Suala la ndege kurushwa na rubani mmoja kwa masafa marefu linastahili kuangaliwa vizuri sana kwani huyu rubani ni binadamu anaweza kuwa amechoka, usingizi mwingi, ulevi kama alilewa usiku uliopita na kuamka nazo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wenye kumiliki vyombo vya anga wasijali gharama kama wataweka rubani wa pili au fundi katika ndege, hii ni faida ya wasafiri kuwa na uhakika wa safari yao pia kwa mwenye kumiliki ndege atakuwa na uhakika wa ndege yake kuruka salama zaidi na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, ninaunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia ahsante.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda kukupongeza kwa hotuba nzuri. Pili, naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100. Pamoja na kuunga mkono napenda kuchangia maeneo yafuatayo:-

Kwa kuwa Shirika la Reli Tanzania lilipunguza wafanyakazi, je, ni wafanyakazi wangapi walipunguzwa na kiasi gani cha fedha (mafao) walilipwa na je, kupunguza wafanyakazi hakutaathiri utendaji wa shirika ambalo lilikuwa linafanya kazi nzuri ya kuhudumia Watanzania? Pia ni sababu gani zilizofanya kupunguza wafanyakazi na sababu gani zilizofanya kuajiri/kuwarudisha *Station Masters* waliostaafu kazini na wapo wangapi waliorudishwa kazini?

Kwa kuwa hivi sasa kuna mgogoro mkubwa kati ya Serikali na wafanyakazi wa *TTCL*, je, chanzo/sababu gani zinazofanya mgogoro huo kuendelea na Serikali imejiandaa vipi kukabiliana na mgogoro huo na je, mgogoro huo hauathiri utendaji wa kazi katika kampuni hiyo (*TTCL*)? Je, Serikali ina mpango gani wa kupunguza gharama za simu ili kupata wateja wengi? Je ni nini uhusiano wa kampuni ya simu ya *TTCL* na *Celtel k*atika kutoka huduma kwa Watanzania?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ningependa kujua masuala yafuatayo kuhusiana na *TRC:-*

(i) Je, ni lini *Station* ya Reli ya Gulwe Wilayani Mpwapwa itapatiwa simu ili mawasiliano yaboreshwe kati ya *Railway Station* ya Gulwe na Makao Makuu ya Wilaya ya Mpwapa na maeneo mengine hapa nchini?

(ii) Je, ni lini R*ailway Station* ya Gulwe Wilayani Mpwawa itapatiwa umeme kwa ajili ya usalama, ulinzi na huduma ya wafanyakazi wa kituo hicho cha reli?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa 100%.

**MHE. IRENEUS N. NGWATURA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji walioshiriki katika kuandaa hotuba hii kwa umahiri mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nianze na kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Hata hivyo, naomba nichangie machache kama ifuatavyo:-

Idara ya Hali ya Hewa imezorota au kutekelezwa ukilinganisha na siku za nyuma licha ya kwamba karne hii ni ya sayansi na teknolojia ya kisasa. Utabiri mwingi unaotolewa na chombo hicho muhimu ni wa kubahatisha kiasi kwamba, hata wananchi wa kawaida wameanza kukosa imani. Vituo vingi vya takwimu za hali ya hewa ambavyo vilikuwa kwenye sehemu mbalimbali kama taasisi za elimu, vituo vya utafiti wa masuala ya mazingira (misitu), wanyamapori na kadhalika, ama vinapata huduma ndogo au havihudumiwi kabisa. Nashauri Serikali ichukue hatua za makusudi za kutenga fedha ili kufungua vituo hivyo.

Aidha, napongeza maamuzi ya kununua vifaa, mitambo ya kisasa kwa ajili ya Dar es Salaam, Handeni na Singida. Lakini vifaa/mitambo hiyo itasaidia maeneo yote ya Tanzania au ni mpango wa awamu kwa awamu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashirika yote ya umma yanayogusa ulinzi na usalama wa nchi hii yako chini ya Wizara hii, kwa mfano, bandari, reli, viwanja vya ndege na hata posta na simu. Sipingi usanii wa ubinafsishaji, lakini bado nina wasiwasi mkubwa na utaratibu huo kwani kama tutabinafsisha halafu nchi ikaingia vitani na nchi ambayo wawekezaji wanahisa itakuwa ni vigumu kushinda vita hivyo. Natoa tahadhari kuwa kama ni lazima kubinafsisha reli kama *TAZARA*, basi tuwasiliane na China ambao wataweza kufufua hata viwanda walivyojenga kwa lengo la kuimarisha reli hiyo hususan *Mang'ula Machine Tools.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri, aliwahi kutoa ahadi kuwa ndege zimeanza kutumia tena Uwanja wa Ndege wa Songea, naomba Mheshimiwa Waziri atuambie kulikoni, je, Uwanja wa Songea hauwezi kuwa Uwanja wa Kimataifa kwa lengo la kuunganisha Malawi na Kaskazini mwa Msumbiji?

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuipongeza kampuni ya *celtel* kwa kutekeleza ahadi yake ya kupeleka huduma zake Mbinga, hata hivyo, usikivu wake katika maeneo mengi ni hafifu kwa sababu mtambo uliowekwa Mjini Mbinga, ungewekwa kwenye mnara mkubwa uliopo Mlima wa Lupembe, ambao ungeweza kusikika katika maeneo mengi ya Wilaya hiyo na hivyo kupata wateja wengi na kampuni kunufaika. Mheshimiwa Naibu Waziri, alikwishatoa ahadi kuwa ifikapo mwaka 2004/2005, mitambo ya simu ya *digital* ingewekwa katika Miji Midogo ya Magu na Litembo. Ningependa nipewe maendeleo ya utekelezaji wa ahadi hiyo.

**MHE. MAJOR JESSE J. MAKUNDI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa ninakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia japo kwa maandishi hotuba hii muhimu ya Waziri mahiri wa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Ninampongeza sana kwa kazi yake nzuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii ikizingatiwa na wote wahusika Tanzania tutakuwa tumepiga hatua asilimia 75 kati ya 100 za safari yetu kukuza mawasiliano, uchukuzi na uchumi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, bajeti hii ilenge uimarishaji na ulinzi wa kisasa kwenye viwanja vya ndege. Matengenezo/ukarabati uwe ni kazi ya kila siku. Isingojewe *running way* ipasuke pasuke eneo kubwa ndipo matengenezo yafanywe. Viwanja vya ndege ni muhimu sana hapa Tanzania hasa kwa majeshi yetu wakati wa vita na wakati wa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, reli na bandari. Nchi yetu ina ukanda wa bahari ya Hindi na Maziwa Makuu. Njia zetu za reli kuanzia bandarini na kuzagaa nchi nzima na ni usafirishaji muhimu hasa maeneo magumu kupitisha barabara. Njia zetu za reli zikarabatiwe kila siku, ukaguzi uwe ni wa saa 24 kwa kuongeza viberenge na vibarua wa kudumu kwa kutumia wananchi wa maeneo hayo, hivyo, kuleta ajira na waajiriwa kulala kwao, bandari ziongezewe vifaa vya kisasa vya ulinzi na usalama na vitendea kazi. Tegemeo la usafiri wa majeshi yetu wakati wa amani na wakati wa vita ni reli na bandari

kwani ni mtandao mkubwa na wenye usiri mkubwa. Sifa za waajiriwa wengi wa maeneo haya iwe ni pamoja na kupitia mafunzo ya JKT, JWTZ, Polisi au Mgambo. Hawa ni wazalendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kuhusu simu, hongera sana Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, kwa kusheheneshа nchi hii kwa simu za mkononi na *TTCL*. Imerahisisha mno mawasiliano yote ya miundombinu ya uchukuzi na usafirishaji hivyo kuongeza ufanisi na uchumi wa nchi yetu kuboreka. Hakika kipaji alicho nacho Mheshimiwa Prof. Mark Mwandosya cha kuongoza Wizara hii ni zawadi ambayo Mwenyezi Mungu amewapa Watanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**MHE. BEATUS R. MAGAYANE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nampongeza Waziri kwa hotuba nzuri na taarifa ya utekelezaji ya bajeti ya mwaka uliopita. Kwa kuwa malumbano yaliyokuwa *TTCL* sasa yameisha ni vema sasa *program* ya kazi za awali itekelezwe kama ilivyokusudiwa katika makubaliano ya awali. Vibanda vya simu visambazwe hasa katika miji midogo ya Kasanda, Kakonko, Nyabibuye na Muhange kwa kuzingatia umbali wa huduma ya simu hupatikana Kibondo ambako wananchi hulazimika kulipa Sh. 6,000/= kama nauli. Badala ya kusambaza *tonnage* ya mizigo iendayo *BRZ*, kupitia Kigoma tu kwa kupeleka Sumbawanga na Bukoba, Reli ya Kati na Bandari ya Kigoma, viimarishwe kwa kuzingatia *advantage* ya kijiografia. Kiwanja cha Ndege cha Kigoma kipanuliwe kwa kuzingatia *traffic* iliyopo sasa kwani hutumiwa na ndege kubwa za *MONUC*. Pia utaunganisha kwa urahisi zaidi Burundi na *DRC*. *UN* wahusishwe kikamilifu.

Wizara iangalie kwa namna ya pekee kada ya *security officers* walioko viwanja vyetu vya ndege hasa *DIA* kwani hawa ndio hasa wanaoleta ufanisi kwani hata ukiwa na ndege nyingi na wahandisi wazuri bila ya kuwa na *security rating* nzuri mambo huharibika. Tunapoelekea kubinafsisha *TRC* ni vema kuwe na mazungumzo ya dhati na chama cha wafanyakazi kwani kutoridhika kwa wafanyakazi, kunaweza kusababisha hujuma na hasa kubwa kwa Taifa. Ripoti ya ajali ya treni iliyotokea mwaka 2002 Msagali Dodoma iwekwe wazi ili umma ujue ni nini hasa kilijili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja.

**MHE. FRANK M. MUSSATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote ninapenda kuwapongeza Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Bwana Msoma, Katibu Mkuu na wafanyakazi wote kwa kazi nzuri waliyoitenda mwaka 2003/2004, Mungu awape nguvu zaidi ili katika mwaka 2004/2005 wafanye vizuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaomba kuunga mkono hoja, pamoja na kufanya hivyo, tafadhali yafuatayo yafanyike:-

Kwanza, mawasiliano ya simu vijijini. Wizara ilishajiwekea lengo la kuweka mawasiliano ya simu kwenye maeneo yenye watu zaidi ya 3,000. Ninaomba Wizara isaidie ili Vijiji vya Kwaga, Rusesa, Kasangezi, Muzye, Bugaga, Nyamsha, Nyambare, Kidyama, Kamazi, Nyakitonto, Nyachenda, Kitagata, Makere na Mvugwe ambavyo viko katika Jimbo la Kasulu Mashariki na ambavyo vinainukia kibiashara kipate mawasiliano haya. Aidha, vijiji vya kibiashara vya Manyovu, Kifurua, Kasanda na Mabamba katika Wilaya za Kasulu na Kibondo viangaliwe kwa kupewa huduma ya simu.

Pili, ukodishaji wa *TRC* na matatizo ya *TAZARA,* ninaiomba Wizara isitishe lengo lake la kukodisha Shirika la Reli la Tanzania (*TRC*) kwani kufanya kutaleta matatizo makubwa. Serikali ifanye kila kile kinachowezekana kukopa fedha ili njia ya reli ambayo imechakaa sana ikarabatiwe kwa kiwango kikubwa au itandazwe upya kabisa. Umuhimu wa usafiri wa reli hauna mashaka yoyote. Aidha, Serikali isimamie kuhakikisha kuwa matatizo yote yanayoikabili *TAZARA* yanatatuliwa mara moja.

Tatu, ujenzi wa magati ya Kagunga, Mwangongo na Kalya. Ninaomba Wizara iangalie uwezekano wa kujenga gati katika Vijiji vya Kagunga, Rwamgongo na Kalya, kwenye mwambao wa Ziwa Tanganyika Mkoani Kigoma kwani vijiji hivi kiuchumi na kiusalama ni muhimu sana kwa Taifa letu. Aidha, wananchi wanapata tabu sana kupanda, kushuka, kupakia na kupakua mizigo melini kwenye maeneo haya. Maisha ya watu na mali vinaendelea kupotea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne, huduma ya simu mipakani, Mkoa wa Kigoma uko mpakani na unapakana na nchi ambazo ziko vitani na hivyo mara kwa mara hushambuliwa na waasi kutoka nchi hizo. Ni vyema basi, Wizara ikatoa kipaumbele kwa kuvipatia huduma ya simu vijiji vya mpakani hususan vile vya Manyovu (Mnanira), Muyama, Kilelema, Kitanga, Makere, Mabamba na Nyarunga katika Mkoa wa Kigoma. Ahsante.

**MHE. CAPT. THEODOS J. KASAPIRA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa Jimbo langu la Ulanga Mashariki, hasa kwa kazi nzuri anayoifanya Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Mheshimiwa Prof. Mark J. Mwandosya. Ninayo furaha kuunga mkono hoja. Nakutakia kazi njema, nakuheshimu jinsi unavyotetea Sera za CCM katika Wizara yako.

Nampongeza ndugu yangu, mwana-CCM mwenzangu, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, Naibu Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, amekuwa hodari na msikivu sana wa shida zetu sisi Wabunge. Pongezi kwa rafiki yangu Katibu Mkuu *Comrade* Salim H. Msoma na watalaamu wake. *Comrade* Msoma, amekuwa mshauri mzuri sana katika masuala mbalimbali ya Wizara hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri umekuwa msikivu sana kwa matatizo ya wananchi, katika ziara zako mbalimbali kwa wananchi umekuwa msikivu sana hadi kufikia kutatua shida za majimbo yetu, Wilaya yetu kwa usahihi bila kubahatisha. Toka mwaka 2002/2003 umekuwa muwazi katika kufuatilia simu ya *celtel* kufika Mahenge. Jitihada yako wananchi wa Ulanga wameiona, mimi mwenyewe nimeshaahidi, nitafika

kukusalimu ofisini kwako. Tumepokea vipeperushi vikionyesha utaratibu wa uongozi wa *celtel* utafikisha simu maeneo kadhaa katika Wilaya zetu na kazi hii itaanza na kukamilika mwezi Julai, 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili wananchi wapate hamasa wajue ukamilifu na utekelezaji wa Wizara, ipo haja wewe mwenyewe katika majumuisho ya Bajeti yako, utoe tamko ukamilifu wa kazi hii kukamilika mwezi huu. Kwa ushahidi nakutumia hapa kipeperushi hicho, kwa Mahenge vipeperushi zaidi ya 20 vimefika tayari kwa wananchi kwa matumaini makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii.

**MHE. LYDIA T. BOMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii ili niweze kuchangia machache kutokana na hoja iliyopo mbele yetu. Awali ya yote, nampongeza Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, Mheshimiwa Dr. Maua A. Daftari, Naibu Waziri, Ndugu Salim Msoma, Katibu Mkuu wa Wizara pamoja na Watendaji wote, kwa kazi nzuri waliyoifanya, hongera sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni miongoni mwa wanakamati, yote yaliyotolewa na taarifa ya Kamati ya Miundombinu nakubaliana nayo, nisingechangia ila nimelazimika kuonyesha umuhimu wa Wizara hii kwa Wananchi wa Tanzania na kwa Serikali kutekeleza Sera ya CCM na kuiweka Serikali mahali pazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mawasiliano na Serikali yake ina masikio sababu nililalamika Bungeni kuhusu vijiji vya Mkoa wa Mtwara kupatiwa simu za mkononi, ninayo furaha sana na kuipongeza sana Wizara kwa kuipatia simu za mkononi, *vodacom*, *celtel* hata Kijijini Nambunga tunaongea na Ulimwengu. Nawatakia kila la kheri watendaji wote na Mungu awabariki.

Pamoja na kushukuru bado nina kilio kwa vijiji ambavyo viko mbali na Makao Makuu ya Wilaya ikiwemo na shule zetu za sekondari kama Kitangari, Mnyambe zote ziko Wilaya ya Newala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule hizi nilizozitaja na nyingine ambazo sikuzitaja za Mkoa wa Mtwara, walimu hupata tabu kuwasiliana na Makao Makuu ya Wilaya wanapopata matukio ya ujambazi, moto na kadhalika. Hivyo, nashauri jitihada za makusudi zifanyike ili kuwapatia simu hasa sehemu nyeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TTCL* ipo lakini haijakidhi mahitaji ya kupeleka simu vijijini sawa na malengo. Nashauri shirika lijitahidi kupeleka simu vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usafiri majini, Dar es Salaam kwenda Mtwara, baada ya kuhama meli ya Santorini umekuwa hakuna meli ya uhakika, ile meli Mtwara inakumbukwa kwa sababu usafiri na usafirishaji mali ulikuwa wa uhakika na bidhaa

zilishuka bei kwa sababu wafanyabiashara hufuata bidhaa Dar es Salaam kwa uhakika na hata bila kwenda unapiga simu tu na unakwenda baharini kupokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, najua Serikali inafanya jitihada kutoa kero kwa wananchi na bado nashauri endeleeni kuwasiliana na matajiri wenye meli ili itoe huduma Dar es Salaam - Mtwara, wananchi kuipata barabara ya nchi kavu isiwe mbadala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *airport* ya Mtwara haina hadhi ya kiwanja kikubwa cha Mkoa, vifaa vya kupakulia mizigo, *VIP* ni ndogo, nashauri Serikali ijitahidi kuangalia hadhi ya kiwanja hiki. Mwisho, nawatakia kila la heri na ufanisi mzuri wa kazi zenu na kufuatilia malengo mliyojiwekea ili kuleta maendeleo kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia kwa mia.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wananchi wa Jimbo langu la Siha, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Profesa Mark Mwandosya, kwa hotuba yake nzuri na yenye mafanikio tele katika maeneo mbalimbali ya nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, nachukua fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri na Naibu wake, kwa kufanya ziara katika Jimbo langu la Siha. Kufika kwao jimboni kunaonyesha namna Serikali inavyotuthamini. Kupitia Wizara ya mawasiliano na uchukuzi na msukumo uliotolewa na watendaji wake, Mashirika ya *TTCL*, *Vodacom, Mobitel,* yamewaeleza katika jimbo langu na kwa msingi huo mawasiliano yameimarika sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nikumbushie ombi la wananchi wa *West Kilimanjaro* hususan Londrosi na Ngarenairobi la kupatiwa huduma za *celtel* kwani maeneo hayo bado hayana mawasiliano kabisa. Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, waliahidi kulifuatilia ombi hili kwa karibu zaidi.

Kwa upande wangu nimemwandikia Mwenyekiti wa *TTCL,* Mheshimiwa Freeman Mbowe na kuliweka ombi hili mbele yake. Nakala nilizipeleka kwa Waziri na Naibu wake. Mwenyekiti wa *TTCL* aliahidi kulipa uzito suala hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mara nyingine tena nampongeza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Uchukuzi, kwa hotuba yake na ninaunga mkono hoja hii bila tatizo. Nawaomba Wabunge wenzangu, waipitishe bila usumbufu. Ahsante.

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza, naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Naipongeza Wizara hususan Waziri, Naibu Waziri na Watendaji wote Wakuu na Taasisi zote katika Wizara hii, kwa kazi nzuri waliyofanya 2003/2004. Kuhusu simu za mkononi na *fixed lines* katika Jimbo langu la Lushoto nina maombi yafuatayo:-

(a) Kwa upande wa simu za mkononi, tunashukuru *celtel* kuweka mtandao Lushoto, tunaomba mtandao huo uimarishwe. Kwa kuwa Lushoto kuna milima, usikivu wa simu katika maeneo ya bondeni siyo mzuri. Tunaomba *receiver points* ziwekwe. Pia tunaomba maeneo ya Mkuzi, Kwemakame, Mlola na Kwekanga katika jimbo langu la uchaguzi yawekewe simu.

(b) Kwa upande wa *TTCL* naomba simu za *wireless local loop* zifanyiwe marekebisho maana bila umeme simu hizo hazifanyi kazi. Umeme unapokatika Mji wa Lushoto simu hazifanyi kazi kabisa, batteries waliozoweka zinakufa haraka sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, narudia tena kuipongeza Wizara kwa kazi nzuri.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia hoja iliyoko mbele yetu. Naomba radhi sitoweza kuwajibu Waheshimiwa Wabunge wote kwa sababu muda niliopewa ni mchache sana wa dakika 15, lakini nitajitahidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema na kuweza kukutana leo hii kujadili maendeleo na changamoto za Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Hivyo, napenda kwanza nitoe pole kwa ndugu zangu waliofiwa na ndugu, wahisani na marafiki wa karibu akiwemo Marehemu Mheshimiwa Yete Mwalyego, Mbunge wa Mbeya Vijijini, nawaombea pole wazazi na watoto na ninamwombea Marehemu Mungu amlaze mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapa pole ndugu zangu Wabunge wote waliofiwa na watoto wao, wazazi wao na wapendwa wao wa karibu. Hayo ndiyo matakwa ya Mola.

Baada ya kusema hayo, sasa nami naomba nitoe mchango wangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi inayo nafasi kubwa ya kuchangia uchumi wa nchi hii, kuondoa umaskini na kuongeza chachu ya ukuaji wa sekta nyingine iwapo tu itapata nyenzo thabiti za kutosha katika kukamilisha utekelezaji wa majukumu yake. Kwa mfano, kama hatutaweza kumsaidia mkulima aliyezalisha mazao yake Vijijini kuweza kuyafikisha sokoni kwa kumboreshea njia za uchukuzi za gati, usafiri wa majini, barabarani na kadhalika tukamsaidia vya kutosha ili asiache mazao yake yakaoza na kuongeza dimbwi la umaskini, hivyo uboreshaji wa magati, viwanja vya ndege, reli na kadhalika vinayo nafasi kubwa ya kusaidia hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kuwa tukiwekeza mara moja tu vya kutosha kwa kuboresha vyema njia za reli zetu, basi reli hizo zitadumu zaidi ya karne mbili au tatu zijazo bila matengenezo makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sekta ya Utalii, Madini, Biashara, Kilimo, Afya na nyingine zinaweza kutoa huduma zao kwa njia ya urahisi zaidi iwapo sekta yetu

itaboreshwa ipasavyo. Sipendi nijigambe na kusema mengi kuhusu ulimwengu wa kisasa wa sayansi na teknolojia ya Mawasiliano na Uchukuzi na yalivyoboreka, biashara ndogo ndogo na kubwa, imebadilisha mienendo na maisha ya wengi kati yetu. Tukiwezeshwa zaidi tunaweza kufanya mengi zaidi, ila umaskini au uhaba wa mapato unatufanya hatua zetu za kusonga mbele ziwe za taratibu kuliko matarajio yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge mbalimbali ni nzuri, nzito zenye busara na changamoto kubwa toka kwa wapigakura wao. Naungana nao na kusema yanayowagusa wenzangu Waheshimiwa Wabunge, nami yananigusa. Naahidi kuwa tutaendelea kushirikiana nao kama kawaida yetu katika kuwatafutia ufumbuzi matatizo yao. Sasa naomba nichangie katika Sekta ifuatayo:-

Kwa leo napenda nichangie Viwanja vya Ndege, Bandari na *Marine Services,* Mamlaka ya Hali ya Hewa, Mamlaka ya Usafiri wa Anga, Reli ya *TRC* na *TAZARA,* Usalama wa *Airports* na Bandari na mengineyo machache kama muda utaruhusu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikianza na *Airports,* kuhusu *Arusha Airport* yamezungumzwa mengi na Waheshimiwa Wabunge wengi. Ningependa niwataje lakini muda hauniruhusu, naomba leo mnivumilie, nitakwenda kinyume na kawaida yangu.

Mheshimiwa mwenyekiti, *Arusha Airport,* mimi nasema viwanja vingine tunavifikiria kwa kadri uwezo unavyoruhusu. *Mwanza Airport* itatengenezwa, *Bukoba Airport* iongezwe alisema Mheshimiwa Ruth Msafiri, ili ikidhi mahitaji ya uchukuzi au ujengwe uwanja mpya, tunamwambia Mheshimiwa Mbunge tunaboresha *Airport* hata walipokuwa na shughuli za Mwenge tuliwasaidia sana vya kutosha kikaweza angalau kuwa katika hali iliyoko hivi sasa na tutaendelea. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge tutaendelea kufanya hivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ni *Songwe Airport.* Ziongezwe fedha na umalizike kabla ya kipindi chake, tunamhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba tutajitahidi kadri fedha tutakavyozipata ili kiwanja hiki kiweze kumalizika. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge wa Kigoma kwamba tutaboresha Kiwanja cha Kigoma angalau ndege ziweze kutua na kuruka na ikiwezekana tutaendelea kuwasiliana na wenzetu wa *UNHCR* waweze kutusaidia kwa sababu na wao ndege zao zinatua pale mara kwa mara. *(Makofi)*

Kuhusu *Mafia Airport* najua hali ni mbaya, mimi mwenyewe nimetembelea, Mheshimiwa Waziri ametembelea, mawazo aliyoyatoa Mheshimiwa Mbunge ya kupata shilingi milioni 350 kutoka Hazina zisaidie na zile zetu milioni 200 ni busara kweli. Sisi tukipata sawa, lakini za kwetu tutaendelea kumsaidia Mheshimiwa Mbunge na anaelewa Naibu Waziri wa Fedha Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, analielewa hili na ameanza kulishughulikia, naamini ufumbuzi utapatikana. Namwomba Mheshimiwa Mbunge asikate tamaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu magari ya Zimamoto mara hii tutanunua matano na tuna nia ya kupeleka Mwanza magari mawili, Arusha moja, Mtwara moja na *DIA* moja. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kadri fedha zitakapopatikana tutahakikisha viwanja vyetu vinapata magari ya Zimamoto. Lakini tukumbuke magari haya ni gharama kubwa sana, sio sawasawa na kununua gari la kawaida. Lakini hali itakapoturuhusu tutaweza kufanya yote tunayoyahitaji kuyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwa na suala la *Dodoma Airport.* Kama tunaendelea na *Dodoma Airport* tuutanue basi ule uwanja au kama sivyo tuupeleke Msalato. Tunasema kujenga Msalato nia ipo pale pale, tatizo ni uwezo tu wa kifedha. Lakini fedha zikipatikana Msalato ni *priority number one.* Lakini kwa hivi sasa hatuwezi kukiongeza Kiwanja cha Ndege cha Dodoma kutokana na hali halisi ilivyo. Lakini tutaendelea kukiboresha kila wakati ili kiwe katika hali nzuri.

Kuhusu *Singida Airport* tutaendelea kuisaidia na kuiboresha na namuahidi Mheshimiwa Mbunge na viwanja vilivyobakia tutahikikisha ndege zinaweza kuruka na kutua wakati wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ulinzi na usalama wa Viwanja vya Ndege tutaendelea kuboresha na hatuna *compromise* katika hili. Mizigo yote itapita katika *screen,* wasafiri wote watakuwa *screened* na hata kama sehemu za ndege ndogo ndogo zile za mizigo, kwenye *charter* vile vile tumeshaweka sasa hivi *screen* na shughuli zinakwenda vizuri tu. Tunawahakikishia Waheshimiwa Wabunge waendelee kuvumilia pale watakapopita na kulia, basi tutawaiteni pembeni kwa uangalizi zaidi na kucheki mizigo yenu na mifuko yenu kama kawaida yetu. Tunakuombeni busara zenu muendelee kutuvumilia katika hilo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Bandari, kama kawaida Bandari zinaleta faida na zinaendelea kuleta changamoto sana katika uchumi wa nchi yetu na tunakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba Bandari ya Lindi, Mtwara na Mafia na zile zote ambazo ni ndogo ndogo na ambazo hazizalishi, basi zibakie zisibinafsishwe. Hilo ndilo lililokuwa wazo la Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi na ambalo limepitishwa na Baraza la Mawaziri. Kwa hiyo, sisi hatuwezi kubadilisha chochote hapo na tutaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu ujenzi wa Bandari ya Mafia, namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, kama tutapata hela Hazina sawa, hatukupata tutaendelea kufanya hiyo kazi. Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, pia anaendelea kutusaidia katika hili. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge tuko pamoja naye kwamba dhiki za wananchi wa Mafia ndio dhiki zetu na tutasaidiana naye katika kuhakikisha kwamba Bandari ya Mafia inajengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu usalama wa vyombo vya majini, tutaendelea kufuata *protocols* na *conventions* za *MO* katika kuhakikisha kwamba tunaendelea kufuata taratibu za usalama. Tutaendelea kukagua vyombo vyote kwa mujibu wa taratibu

tulizoziweka na hapo baadaye hali ikiruhusu tungependa kuona Bandari tunaweka angalau *screen* ya kuchunguza mizigo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ikituruhusu hapo baadaye tunaweza tukafanya hivyo. Tutaendelea kuwasihi wamiliki wa vyombo vya majini waendelee kufuata taratibu za kiusalama kwa kuwa na *lifejackets* za kutosha kulingana na idadi ya abiria walionao, kuwa na *life rafts* katika meli zao, kuendelea kuonyesha filamu za namna ya kujiokoa wakati panapotokea majanga na tutaendelea kutoa semina mbalimbali Mikoani kama tulivyokuwa tunafanya huko nyuma na ninahakikisha kwamba *SUMATRA* ikianza kazi vizuri sana, nina hakika masuala kama haya yote yatashughulikiwa ipasavyo. *(Makofi)*

Kuhusu magati ya Maziwa, wengi tu wameyazungumzia, kweli mwaka 2003 tuliweza kutenga fedha kidogo na tukaweza kufanya mambo mengi. Yako mengi tu yaliyofanywa. Mheshimiwa Mbunge aliuliza *Mbambabay Port,* alikuwa na wasiwasi sana, tunamhakikishia kwamba ile gati itajengwa na tunategemea Agosti, itakuwa katika hali nzuri. *(Makofi)*

Kulikuwa na suala la Bima wakati wa ajali aliuliza Mheshimiwa Ruth Msafiri katika kupitisha ile *Merchant Shipping Act,* yalikuwepo marekebisho kadhaa ambayo yameongezwa likiwemo hili suala la Bima. Namhakikishia Mheshimiwa Mbunge, hatuwezi kurudia kosa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *fire fighting boats* na *fire rescue boats* alilolitoa Mheshimiwa Mbunge, ningependa kumfahamisha Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, kwamba tutajitahidi tukipata fedha kuwasiliana na Serikali Kuu pale itakapowezekana, basi tupate hizi. Lakini kwa muda huu tutaendelea na kutumia *rescue boats* ambazo wanazo wenzetu na tutaendelea kutumia Kitengo cha Taifa cha kuzuia Maafa na vifaa vilivyopo katika suala zima la *rescue facilities.* Najua zipo *boats* za wanamaji, Maliasili na utalii na Bandari. Shughuli zote ziko *well coordinated* chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Bandari ya Tanga tutaipa uzito unaofaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la Hali ya Hewa, tutaendelea kufundisha wafanyakazi wetu kwa bidii zaidi na kuboresha huduma zetu ziwe za uhakika zaidi Mheshimiwa Edson Halinga, wala usiwe na wasiwasi. Vifaa tumepata na tumevifunga na sasa tunaendelea vizuri zaidi kuliko tulivyokuwa mwaka 2003. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vyuo vyetu vilivyo chini ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi vyote vinafanya kazi vizuri sana. Napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, Chuo cha *NIT* na *DMI* vimeshapita kwenye *NECTA,* vimesajiliwa rasmi na vinaeleweka rasmi. Vimeendelea na tutaendelea kuviboresha pamoja na kuboresha mitaala yake. Chuo cha *NIT* wanayo mashirikiano mazuri tu na *Leads Metropolitan University U.K* na wanafanya vizuri tu. Naamini tukiboresha Vyuo hivi tutakuwa tumewaboresha sana wafanyakazi wa sehemu hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naona kengele ya kwanza imelia, ya pili sitaki inifikie mbali, nina masuala ya Mamlaka ya ...

**MWENYEKITI:** Endelea, bado una dakika kumi.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Ahsante. Nina masuala ya Mamlaka ya Leseni. Napenda nimfahamishe Mheshimiwa Edson Halinga kwamba, ratiba zipo na zinatumika na vidhibiti mwendo tutaendelea kuviweka kwa kushirikiana na Wizara ya Mambo ya Ndani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Sheria Na.1 ya Leseni ya usafirishaji ifanyiwe marekebisho, lakini nikukumbushe tu kwamba tumepitisha hapa sheria ya *SUMATRA* ambayo tukimaliza uundaji wake nadhani hili suala la *CTLA,* ile sheria hii itakuwa haina haja tena kutumika.

Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu, amesema Serikali izingatie upya agizo lake la kutoyaruhusu magari ya abiria kutembea usiku, lakini wengine wanasema yatembee usiku. Sasa sisi tunasema, kwa usalama wa abiria, tunawaombeni tu muwe wavumilivu mabasi yatembee asubuhi ili tuepushe ajali. Inapotokea ajali usiku sio rahisi sana kupata huduma ya haraka kama inavyokuwa asubuhi, mchana, ni mapema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu kutozingatiwa viwango vya Bodi za Mabasi, nasema viwango vya Bodi vya Mabasi vinasimamiwa na kuwekwa na *TBS* chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara na nina hakika ushauri huu wa Mheshimiwa Mbunge utawasilishwa kwa wahusika na Mheshimiwa Esha Stima, amezungumzia masuala ya *TRC* tutayazingatia, ni kutokana na uhaba hivi sasa wa *engine* na mabehewa lakini hali ikiruhusu tutafanya vizuri sana na Shirika litazingatia kuongeza nafasi za dharura hasa wakati huu wa Bunge kama vile alivyoomba mwenyewe.

Mheshimiwa Stephen Kahumbi, alitaka kujua kuna sehemu ambazo kuna treni hupita kila siku usiku iwe ni treni zinazokwenda Dar es Salaam au kutoka Dar es Salaam, je, kwa nini kusiwe na hata moja itakayopita mchana angalau wasafiri nao wachague treni ya kusafiri. Mimi nasema, katika utengenezaji wa ratiba, moja ya vigezo ambavyo vinaangaliwa ni muda wa treni kuondoka katika stesheni ambayo treni huanza safari yake na muda wa kufika stesheni ambao treni humalizia safari yake. Kwa hiyo, treni zote huondoka Dar es Salaam, Mwanza na Kigoma jioni saa 11.00 au saa 12.00 jioni na kuwasili sehemu hizo saa 12.00 asubuhi au saa 1.00 asubuhi. Lengo ni kwamba usifike pale unapotaka kwenda usiku halafu ukaporwa na majambazi huko njiani. Nalo hilo lina umuhimu kwa uzito wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Eliachim Simpasa, alizugumzia ulinzi wa njia ya reli ya Kati na *TAZARA* ifanyiwe mikakati mahususi na kuhusisha Vijiji jirani, tunazingatia ushauri wake Mheshimiwa Eliachim Simpasa na tunafanya hivyo na tutaendelea kufanya hivyo. Najua ni mengi yaliyopo lakini naomba niyaache mengine na niko tayari kwamba tutawaeleza Waheshimiwa kwa maandishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimalizie kujibu maswali ya Mheshimiwa Jackson Makwetta. Amezungumzia mengi sana kwa maandishi. Je, ni kweli Makampuni ya Afrika Kusini yamepania kuua Reli ya *TAZARA,* Reli ya Kati na Bandari? Sisi tunasema hatuna taarifa na sidhani kama itakuwa hivyo na sisi hatutakubali kusubiri kuona vitu ambavyo vinatuletea tija na uchumi wa nchi hii vinauliwa hivi hiv. Hatuwezi kusubiri hata kidogo! Makampuni ya Afrika Kusini yamechukua uendeshaji wa Reli ya Zambia ni kweli. Kampuni ya Reli ya Afrika Kusini imechukua uendezaji wa *Zambia Railways* kwa niaba ya mwekezaji kutoka nje, lakini hiyo haitufanyi sisi tuwe na hofu na wasiwasi. Zambia imeamua kujenga reli kati ya Bandari ya Mpulungu na Kasama na China na China imetoa fedha kwa ajili ya mradi huo. Inawezekana kuna mpango wa Serikali ya Zambia kujenga Reli kati ya Mpulungu na Kasama, lakini hatuna taarifa rasmi nani anafadhili mradi huu. Lakini vyovyote wafanyavyo, njia ya Reli ya Kati ni rahisi zaidi kuliko hiyo njia wanayotaka kuchukua wao. Sisi kazi yetu ni kuboresha njia yetu ili huduma hizi ziende vizuri na tuweze ku-*capture market* za nchi jirani.

Mheshimiwa Ally Karavina, malengo yake na ya kwetu wala hayapishani. Nia yake na nia yetu iko pale pale kwamba tunafungua *corridor* na ndiyo maana tukawa na *corridors* nyingi tu zilizobuniwa kwa lengo la ku-*capture* uchumi wa nchi jirani. Makampuni ya Afrika Kusini yamechukua Kidatu ili kuchukua biashara na maelezo mengi tu. Stesheni ya Kidatu ina *transshipment facility,* ni kiungo cha ubadilishaji mizigo kati ya *TAZARA* na *TRC* na kufuatia tofauti ya *gauge* ya reli hizo, hivyo basi ina umuhimu wa kuunganisha reli Kusini mwa Afrika na Afrika Mashariki ili kurahisisha biashara kati ya nchi za Kusini na Mashariki na zile za Maziwa Makuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sitaki nipigiwe kengele ya pili, mwisho kwa kumalizia napenda kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ujumla kwa ushirikiano mzuri walionipa kwa kipindi chote. Napenda nikiri kuwa ukaribu wao kwangu kwa kunishauri pia kwa kunipa matatizo yanayowagusa wapigakura wao bila wasiwasi, imenisaidia sana kuyajua Majimbo yao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kwa kiasi kikubwa wengi wao nimeweza kukidhi mahitaji ya wapigakura wao yanayotokana na maombi kwa njia ya ufuatiliaji wa karibu. Nawaomba wale ambao bado hatujaweza kukidhi kukamilisha matatizo yao, basi wasife moyo, tutaendelea kushirikiana nao na kuona ni namna gani tunaweza kutatua matatizo hayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hayo machache, naunga mkono hoja mia kwa mia na kwa unyenyekevu kabisa nakuombeni Waheshimiwa Wabunge muunge mkono hoja hii. Ahsante. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna neno la Kiswahili linaitwa au Waswahili wanasema tumehemewa. Kwa kweli sisi katika sekta hii tumehemewa. Tunawashukuru sana Waheshimiwa Wabunge kwa michango yenu ya kina ya leo hii, michango yenu katika semina mbalimbali za sekta na wanakamati ya Miundombinu, michango yenu katika Kamati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, shukrani kwa Kamati ni za kipekee kwa kweli. Ni kama walezi na wasimamizi wa sekta na Wizara. Wamechangia vizuri sana na kutoa maelekezo walipotembelea maeneo yetu ya kazi. Kamati imechambua kwa kina sana taarifa zetu na kila mara tunapokuwa kwenye Kamati tunapotoka kwa sababu ya uchambuzi tunatoka tukiwa hoi kweli kweli, maana yake Kamati inafanya kazi yake. Kamati wala si muhuri wa kuthibitisha mipango ya sekta hata kidogo. Naweza kuthibitisha kwamba Kamati pia ni chanzo cha sera zetu. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa niwatambue wale wote waliochangia kwa kusema na maandishi leo hapa na hao ni kama wafuatao:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa kusema si wengine bali ni Mheshimiwa Henry Shekiffu, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Miundombinu, Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Dr. James Msekela, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, Mheshimiwa Feteh Saad Mgeni, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Halima Kimbau, Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Ally Karavina, Mheshimiwa Gwassa Sebabili na mwisho Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Bado Mheshimiwa Richard Ndassa.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hamwezi kuamini, niliacha makusudi ili nimtamke peke yake. Mheshimiwa Richard Ndassa. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, waliochangia kwa maandishi ni wengi, wapo sitini na saba na nitawataja wote. Hawa si wengine bali ni Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Gideon Cheyo, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Lephy Gembe, Mheshimiwa Halimenshi Mayonga, Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, Mheshimiwa Eliachim Simpasa, Mheshimiwa Maria Watondoha, Mheshimiwa Mbarouk Mwandoro, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Robert Buzuka, Mheshimiwa Arid Uledi, Mheshimiwa Shamim Khan, Mheshimiwa Beatus Magayane, Mheshimiwa Juma Kidunda, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Shamsa Mwangunga, Mheshimiwa Profesa Henry Mgombelo, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mheshimiwa Frank Mussati, Mheshimiwa Dr. Zainab Gama, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Hamza Mwenegoha, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Robert Mashalla, Mheshimiwa Samuel Chitalilo, Mheshimiwa Salome Mbatia, Mheshimiwa Profesa Pius Mbawala, Mheshimiwa Dr. Pius Ng'wandu, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Ibrahimu Marwa na Mheshimiwa Harith Bakari Mwapachu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wengine ni Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Charles Kagonji, Mheshimiwa Sophia Simba, Mheshimiwa Raphael Mlolwa,

Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mheshimiwa *Capt.* Theodos Kasapira, Mheshimiwa Martha Wejja, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Shoka Khamis Juma, Mheshimiwa Mariam Mfaki, Mheshimiwa Elizabeth Batenga, Mheshimiwa Talala Mbise, Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar, Mheshimiwa James Musalika, Mheshimiwa Profesa Daimon Mwaga, Mheshimiwa Esha Stima, Mheshimiwa Sumri Mohammed, Mheshimiwa Parseko Kone, Mheshimiwa Joel Bendera, Mheshimiwa *Major* Jesse Makundi, Mheshimiwa Lydia Boma, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Gwassa Sebabili, Mheshimiwa Sijamini Shaame, Mheshimiwa Karim Said Othman, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, Mheshimiwa Bujiku Sakila na Mheshimiwa Omar Kwaangw'. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema kwa Mheshimiwa Richard Ndassa kama wapo ambao nimewasahau, basi nataka kuwataja peke yao, kwa umuhimu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwaka nina tabia moja, vile vikaratasi mnavyoniandikia mimi sivichani hasa kama vinahusu maendeleo ya Majimbo yetu. Kwa hiyo, nataja hapa majina ya Waheshimiwa Wabunge walioniandikia ili nifuatilie mwaka mzima tangu nilipowasilisha Bajeti ya mwaka 2003/2004, inawezekana siyo wote, mtanisamehe lakini nimeweka *list* kama kumbukumbu ili niweze kufuatilia.

Hawa si wengine bali ni Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Samuel Chitalilo, Mheshimiwa Wilfred Lwakatare, Mheshimiwa Dr. Diodorus Kamala, Mheshimiwa Aggrey Mwanri, Mheshimiwa Bujiku Sakila, Mheshimiwa Edward Ndeka, Mheshimiwa Khalid Suru, Mheshimiwa Paul Makolo, Mheshimiwa Stephen Kahumbi, Mheshimiwa Mathew Ole-Timan, Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Dr. Lawrence Gama, Mheshimiwa Said Nkumba, Mheshimiwa Lucas Selelii, Mheshimiwa Dr. Chrisant Mzindakaya, Mheshimiwa Mgana Msindai na Mheshimiwa Dr. Amani Warid Kabourou. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafanya hivi kwa makusudi ili wananchi wajue kwamba Bunge halifanyi kazi wakati wa Bunge tu bali linafanya kazi wakati wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ni nyingi, tutashindwa kuzijibu zote kwa kipindi cha muda wa dakika arobaini na tano. Tunaomba mtuamini kwamba tutazijibu kwa maandishi na kutoa kitabu cha majibu ya hoja zote. Kwa hiyo, hapa natoa majumuisho tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, majumuisho yenyewe ni kuzungumzia masuala ya kijumla ya kisera. Nakubaliana kabisa na Mheshimiwa Ally Karavina, Mheshimiwa Henry Shekiffu, Mheshimiwa Dr. Thadeus Luoga, Mheshimiwa Richard Ndassa na Mheshimiwa Gwassa Sebabili kuhusu umuhimu wa sekta ya uchukuzi kuwa mhimili wa uchumi. Tunachofanya sisi ni kutoa huduma, lakini vile vile tunafanya biashara.

Kwa hiyo, kwa pande zote tunachangia katika kukua kwa uchumi wa nchi. Kwa kweli uchumi hauwezi kukua bila ya uchukuzi, bila mawasiliano na nikisema uchukuzi ni kwa ujumla wake. Uchukuzi ni pamoja na barabara. Sisi barabara tunaichukua kama ni sekta katika uchukuzi lakini Kiwizara tumegawanya katika sekta mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchumi wa kijiografia umezungumzwa. Hili ni suala muhimu sana na lazima tuanze kulizingatia. Kwa sababu gani? Nchi ndogo kama vile Singapore ambayo ni jabali, ni mawe tu, si kisiwa kikubwa kama Zanzibar au Mafia. Hapana, ni kidogo sana. Lakini kimeweza kutumia jiografia yake kubadilisha maisha yake na uchumi wake kuwa moja ya chumi zinazoendelea sana duniani, lakini ni nchi ndogo kabisa. Nchi kama Hong Kong ambayo sasa ni sehemu ya China, inaogopwa karibu dunia nzima, hakuna kitu pale, ni kakisiwa kadogo tu, lakini kwa sababu jiografia yake imeweza kutumika vizuri, wameendelea. Miji kama Dubai sasa hivi ina uchumi mkubwa kabisa kutokana na jiografia. Sasa sembuse Tanzania ambayo Mwenyezi Mungu ametujaalia kuwa na mwambao wa kilometa 800, kuwa na Visiwa vya Zanzibar, Mafia, kuwa na nchi nane zinazotuzunguka, kuwa katikati ya Cairo na *Cape Town,* kuwa na bandari za mwambao na bandari za Maziwa Makuu, Mwenyezi Mungu atupe nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kinachotakiwa sasa ni kubadilisha mtazamo, kuweka mkazo katika jiografia hii ili tuweze kuinua uchumi wetu. Maana yake lazima tuwekeze katika uchukuzi na tuendeleze miundombinu yetu ili tuweze kuongeza kipato cha nchi na vile vile uchumi wa Taifa. Tuendeleze reli zetu na tuendeleze kwa pamoja njia za uchukuzi na mawasiliano. Sasa hivi tunaweza kukiri kwamba tumetoa msimamo au mwelekeo zaidi katika barabara. Lakini lazima tuangalie uchukuzi kwa uwiano na kwa ujumla wake kwa sababu utamaliza barabara, shehena zote zitahamia kwenye barabara basi barabara zitaharibika wakati reli wala hujaiimarisha.

Kwa hiyo, tunapoimarisha barabara lazima tukumbuke reli. *Alhamdulillah* mwaka huu kwa reli kwa fedha za Tanzania mmetupa shilingi 200,000,000/= tu. Linganisheni na barabara mlizozipa shilingi bilioni 49. Hatutafanya miujiza, lakini tunawashukuru kwa hicho ambacho mtatupa baada ya muda si mrefu. Kwa hiyo, nimeona nilizungumzie hili kwa sababu ni muhimu sana. Lakini tunashukuru kwa kile mlichotupa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *ATCL,* tunashukuru sana Mheshimiwa Richard Ndassa na wengine wote waliozungumza. Tumepokea, tumesikia na tutayafanyia kazi yote ambayo tumeyapata. Tunawahakikishia wafanyakazi wa *ATCL* kwamba yote mliyoyaleta kwetu tutayafanyia kazi. Kama mnavyojua Bodi ya *ATCL* ina wajumbe nane, sita kati yao ni Watanzania. Hilo linatupa faraja kwamba hawawezi kuiacha nchi yao na kampuni yao. *(Makofi)*

Kuhusu tiketi suala ambalo ni kiini kikubwa sasa cha malalamiko tumetoa maagizo na Bodi bila shaka itatusikia kwamba ifikapo Desemba na mdhibiti ambaye ni *TCIAA* amesema hivyo kwamba ifikapo Desemba, 2004 ili kuendelea kutumia njia

ambazo ni za Tanzania ambazo zimetolewa na *TCAA* basi ni lazima tiketi za *Air Tanzania* zitumike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itaondoa utata mwingi ambao hata sasa kwa mfano India wanasema sisi hatukubali kuzungumza na nyie kuhusu njia za kuja India kwa sababu hatujui kama *Air Tanzania* ni ya kwenu au ya *South Africa.* Tatizo kubwa hasa ni hili la tiketi. Kwa hiyo, hili tutalimaliza. Tunawashukuru sana. *(Makofi)*

Kuhusu ndege ya Serikali, picha ya ndege ni hii hapa, ni nzuri na inapendeza. Kama mnaona nje inapendeza, ndani ndio zaidi. *(Makofi)*

*(Hapa Vielelezo vya Ndege ya Rais inayotarajiwa kununuliwa vilionyeshwa Bungeni)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Ahsanteni sana, mwezi wa tisa itakuwa imefika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie kwa kifupi tu kuhusu udhibiti wa sekta. Nathibitisha kwamba *SUMATRA* itaanza kazi hivi karibuni, tunakamilisha taratibu za kuteua Bodi kama nilivyosema pamoja na Mkurugenzi Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile Mamlaka ya Usalama wa Usafiri wa Anga, tunakamilisha mchakato wa kuchagua Bodi na vile vile Mkurugenzi Mkuu. Bahati nzuri hii mamlaka ipo na inaendelea na inafanya kazi yake vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mamlaka ya Mawasiliano ilianza kazi tarehe 1 Novemba, 2003. Baada ya mimi kusaini *order* ya kuanzisha hiyo mamlaka kutokana na uwezo miliyonipa kisheria. Mchakato wa uteuzi wa Bodi ukaanza mara moja, tulianza na uteuzi wa Baraza la Watumiaji. Kwa sababu gani? Kwa sababu lazima mmoja wa wale walio katika Baraza awemo katika Kamati ya Uteuzi. Kwa hiyo tulianza na hilo.

Baraza la Watumiaji limeteuliwa chini ya Mwenyekiti wake Mzee Rajab Yusuf. Sasa baada ya hapo ikabidi tuteue Kamati ya Uteuzi. Kamati ya Uteuzi ni pamoja na ndugu Salim Msoma ambaye ni Mwenyekiti, Mama Rose Lugembe, Profesa Luhanga, Bwana Kabyemela aliyekuwa *TTCL* zamani na wamesaidiwa na wataalam wengi sana katika shughuli hii ya uteuzi wa Bodi pamoja na Mkurugenzi Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tangazo lilitolewa ili watu waombe nafasi hizo. Kwa kweli tulikuwa na watu wengi sana walioomba. Walioomba Bodi walikuwa 89, ndio sheria ilivyo siku hizi. Lazima *Board Members* waombe na walioomba nafasi ya Mkurugenzi Mkuu walikuwa 38. Kwa hiyo, ilikuwa ni kazi. Mapendekezo yaliletwa kama sheria inavyosema kwa Waziri kuhusu Bodi na lile la Mwenyekiti lilipelekwa kwa Mheshimiwa Rais na akafanya uteuzi. Kuhusu Bodi, utaratibu ni kwamba baada ya kuchujwa walibakia kumi ndio walioitwa kwenye usaili. Katika hao kumi wakachujwa wakabakia watano. Watano hao wakapelekwa kwa ajili ya sisi tunaita katika shughuli za Kiserikali, upekuzi. Sasa siwezi kutoa taarifa za upekuzi katika Bunge wala mahali pengine popote pale, lakini hatma yake ndio uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sikutaka kuwa *personal* katika suala hili kama lilivyoletwa kwa sababu kawaida yangu mimi wala sipendi kuuliza mtu umezaliwa wapi, ukiwa Mtanzania ni Mtanzania tu. Ulizaliwa wapi unaweza kuwa umezaliwa Tabora lakini wewe ni mtu wa Musoma ,Tanzania tumechanganyika sana, kwa hiyo, hata kuzaliwa wapi hakuna sababu ya kuuliza. Kwa sababu nimeombwa niseme huyu Mkurugenzi Mkuu Profesa Nkoma, amezaliwa wapi, mimi sikujua, nimemwuliza mchana huu, ulizaliwa wapi? Ananiambia alizaliwa *Mbambabay.*

Kama mnataka kufahamu yuko hapa na Mheshimiwa Hassan Kigwalilo, wamesoma naye tangu shule ya msingi. Kwa hiyo mnaweza kuhakikisha kwamba sijui walitoka wapi huko mpaka kufika Chuo Kikuu pamoja. Lakini sikutaka kuwa *personal* katika suala hili kwa kweli. *Mbambabay* ipo wapi? Ipo Jimbo la Mbinga Magharibi, Wilaya ya Mbinga, Mkoa wa Ruvuma. Isije ikafikiriwa anatoka Mkoa wa Mbeya. Nasisitiza hilo. Amesoma wapi? Amesoma Chuo Kikuu cha Dar es Salaam hapa Tanzania na Uingereza. Amefanya kazi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kama Mkuu wa Idara ya Fizikia. Vile vile Chuo Kikuu cha Botswana kama Mkuu wa Kitivo cha Fizikia na vile vile Mkuu wa Idara ya Fizikia. Ni Mtanzania, aliomba kazi, amesailiwa, amepita katika *process,* mchakato na amepata hiyo kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani wote 38 wangepata, lazima mmoja na kati ya wale 37 lazima mmojawapo atalalamika, ni kawaida ya ubinadamu. Kwa hiyo, tunaelewa kwa nini inatokea hivi kati ya wale walioshindwa wataeneza, watazua maneno, kuna wengine tulishawaambia, waliandika sana kwenye magazeti hili suala. Tulipobaini ni nani, tukamwandikia barua tukamwambia ni wewe na ukome na akakoma. *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nina tabia moja, mtu akifanya mambo ya namna hiyo huwa nam-*face* moja kwa moja. Haya mambo ya kumzunguka kumsema nyuma mimi sikubali kabisa. Kwa hiyo, nilimwambia acha na akaacha na hakuna tena yaliyotokea kwenye gazeti kuhusu uteuzi huu wa Mkurugenzi Mkuu wa *TCRA.* Sasa labda yale yale yanakuja kwa njia nyingine, lakini tutapambana nayo tu. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo mimi nimemwambia Mheshimiwa au nimewaambia Profesa Nkoma kwamba sasa umeingia kazini, ndio tanuru la moto, ni vizuri kwamba unabatizwa na moto, maana yake utakomaa na utakuwa mkakamavu na utaliendesha hili Shirika.

Nikamwambia mchana huu kwamba wewe ungejua mambo yanayotupata sisi wanasiasa na yanayozungumzwa mahali kama hapa Bunge, ungesema huyu Profesa mbona anasimama na *courage* yote hii ni nini. Lakini ndio hali halisi hiyo, unapambana na mambo haya na tukifika katika uchaguzi mwaka kesho tutakuwa hoi lakini tutafanyaje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo haya tutapambana, tutapakana matope, lakini tutazidi kuyatoa tu, kwa sababu ndiyo hali halisi na kama mnavyojua tukishindwa kupata

kura sisi wanasiasa hatukosi sababu. Tuna majibu ya haraka. Tutasema kura zilikuwa za itifaki au kwamba vyombo vya dola vilipanga kura. Basi tuendelee. Nadhani niliachie hapa. Namtakia kila la kheri Profesa Nkoma katika kazi zake na tutampa ushirikiano mkubwa sana katika kuliendeleza hili. *(Makofi)*

Nizungumzie kuhusu suala la maingiliano ya simu *(interconnection).* Ni maingiliano ya kuunganisha simu ndani ya mtandao wenyewe au kutoka mtandao mmoja kwenda mtandao mwingine. Sasa watoa huduma baina ya makampuni toka mtandao mmoja kwenda mwingine lazima waingie Mkataba wa kibiashara. Unapogonga hodi kuingia nyumba ya mtu, hiyo nyumba ya mtu ni kampuni nyingine, anakwambia ingia lakini unalipa. Ndiyo maana ya *interconnection,* hakuna kitu kikubwa zaidi ya hicho. Lakini hayo malipo baadaye analipa ni wewe na mimi mtumiaji. Sasa inabidi wakubaliane kibiashara, wanaposhindwa kukubaliana ndio matatizo na kampuni hizi zimeshindwa kabisa kukubaliana, inabidi refa aingilie kati, refa sasa ndiye huyu *regulator* ambaye ni Mamlaka ya Mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tarehe 16 Januari, 2002, refa alitoa uamuzi wa kwanza kwamba makampuni yaingie Mkataba wa kuunganisha mitandao yao kwa senti 17.5 za Marekani. Awali ya hapo ilikuwa senti 25 wakati wa ukiritimba wa *Mobitel* peke yake, ni juu kweli, lakini zikapungua kufikia 17.5. Tarehe 19 Aprili, 2002, Tume ilitoa uamuzi wa pili kwamba *Zantel* na *Celtel* wao wanaweza ku-*charge* yaani wanaweza kulipa au ku-*charge* senti kumi, *Mobitel, Vodacom* na *Celtel* wao wakasema watabakia pale pale juu yaani senti 17.5. Hao wengine walisema sisi tunaweza kuendesha kampuni na kupata faida kwa hii bei ya chini tu.

Tarehe 1 Oktoba, 2002 uamuzi wa tatu, *Vodacom, Tritel* na *Mobitel* walilalamika wakati Tume ilipotaka kushusha kufikia senti 12.5. Wakasema nini? Wakasema atafutwe mtu wa nje ambaye atakuwa huru afanye huo utafiti, aangalie gharama halisi. Tukasema kwa nini tuanze kubishana jamani katika hili suala mbona wanatoa mawazo mazuri tu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Tume ikatangaza zabuni za Kimataifa, kampuni ya Uingereza inaitwa *Analysys,* kampuni ambayo ni maarufu sana katika masuala haya ambayo inatambuliwa na *financial times* ikapata zabuni. Tarehe 9 Mei, 2003 ikaanza kazi. Ilijulishwa kwa wadau wote na kampuni zote za simu, ikaanza kukusanya na takwimu ambazo zilitolewa na wenyewe ma-*opareter*. Tarehe 15 Mei, 2003 walifanya warsha na hao watu, Kampuni zote hizi za simu wakaeleza na njia watakayotumia kufikia *determination,* makampuni yakatoa mawazo na dukuduku zao zote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya Mei, 2003 na Septemba, 2003 *Analysis* alikutana na kampuni zote moja moja kupitia tena takwimu pamoja na njia ya kufikia uamuzi. Kwa hiyo, kila mtu alihusika. Septemba, 2003, wakatoa ripoti ya kwanza na kueleza kwamba gharama wanazohisi wao kutokana na utaalam wao si zaidi ya senti 8 kutoka senti 17, ni kati ya senti 6 na 8. Hata uamuzi huu wakawapa kampuni zote za

simu ili watoe mawazo yao tena. Kwa hiyo, hakuna kitu kilichofichwa na hii *process* ilikuwa *interactive* kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa mwishoni kilichotokea ni kwamba Novemba, 2003, *Analysis* wakatoa ripoti yao ya mwisho. Lakini Tume ilikuwa katika mabadiliko kwa sababu tulikuwa sasa tunatarajia kuwa na mamlaka mpya. Kwa hiyo, wakaifungia katika *safe* ingoje mamlaka mpya. Sasa mamlaka mpya imekamilika mwezi uliopita, ndio ikaifanyia kazi. Kazi hiyo imeifanyia namna gani? Tarehe 28 Juni, Bodi ilikutana na kupewa taarifa na hao *Analysys.* Tarehe 29 Juni, hao wataalam wa *Analysys* wakakutana na washirika wote pamoja na kampuni za simu na Bodi ya *TCRA* na wawakilishi wa Serikali na watu wengine kama vile Kamishna wa Ushindani wa Haki. Basi tarehe 30 Juni, Bodi ikatoa *determination.*

Sasa mpaka lini mtumiaji aendelee kulipa gharama za simu za juu kuliko zote Afrika jamani ili tuendelee kuwa na *interaction* na hao watu? Nani ambaye hajapata nafasi ya kusikilizwa katika mlolongo huu niliotoa. Mimi leo imenishangaza kwa kweli, lazima niseme katika uwazi na ukweli kwamba, siku zote kilio cha Wabunge, gharama ziko juu. Leo *determination* inatoka tunaambiwa ahaa, lazima muanze kufikiria kuzungumza na hao watu ili waweze nao kutoa maoni yao zaidi ya haya niliyoyasema katika *process* hii, katika mchakato! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tunawatendea haki wananchi wa Tanzania? Tumejibu swali jana na kusema kweli gharama za simu kwa Tanzania zina gharama kuliko zote Kusini mwa Afrika na Afrika Mashariki. Leo hii tunaambiwa *take your time,* wapeni siku endeleeni kuzungumza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niendelee kwa simu niliache hilo hapo kwa sababu uamuzi mwishoni ni wenu ninyi na wananchi wala siyo sekta. Nianzie na yule mama wa Mheshimiwa Edson Halinga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yule mama anatufanyia kazi nzuri sana, kwa sababu zamani ilikuwa ukiinua simu inakuudhi kwa sababu inakupigia kelele kuonyesha mlio kwamba *engaged.* Sasa hivi angalau *Alhamdulillah,* ukiinua simu kama iko *engaged* unapata sauti murua, unasikiliza inakutuliza. Sasa vipi tena Mheshimiwa Edson Halinga, anachukia hilo? *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, isipokuwa nimeambiwa kwamba baadhi yetu ukisikia yale maneno ambayo ni *recorded voice,* unaanza kujibishana naye, kwa hiyo, utachukia sana kwa sababu atarudia tena. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda hili niliachie hapa lakini wale watoa huduma wamekusikia, labda watajaribu kuangalia jinsi gani ya kulirekebisha ili liwe zuri zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema mambo ni mengi kweli kweli, hatuwezi kuwatendea haki kama tutachagua tu machache tukajibu hasa yale yaliyozungumzwa na Waheshimiwa Wabunge kwa maeneo yao hasa. Kwa hiyo, sisi

tutachambua na kuyatolea kitabu cha majibu. Namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Kivuli toka Upinzani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, alipoanza kuchangia hotuba ya Bajeti, mimi naona kuna ile kukaa kwenye Kamati zetu na kupishana pishana na Wabunge wa CCM naona mnaanza ku-*improve.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake nimeisoma ile nikasema ahaa, mbona *research* kubwa sana imefanyika hapa, safi sana. Kwa hiyo, namsifia ingawa mwishoni aliwasilisha lakini najua moyoni mwake ameunga mkono hii hoja. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimalizie kwa taarifa chache nilizopata kuhusu maendeleo ya simu za mkononi kuanzia sasa mpaka Desemba. Wale ambao zitakuwemo naomba mzipokee, wale ambao hamtakuwemo nafikiri zitakuwemo Januari mpaka Juni mwaka kesho.

Kwa upande wa *Celtel* kuanzia Julai mpaka Desemba zitakuwepo Ihumwa, Tunduru, Ndanda, *Moshi TPC, Rifle Range* - Tabora, Mtwango, *Kiwira Prison,* Kiruru Tanga, Chunya, Ileje, Kiziru, Chato, Biharamulo, Kasumuro, Ndala, Mkuranga, Namkalamuka, Kibiti, Mingoyo, Kondoa, Kamachumu, Liwale, Mugumu, Utamutamu, Mahenge, Mbuyuni, Mazimbu, Kanyigo, Sikonge, Mkome na Mchangani. Hiyo ndiyo programu ya *Celtel* kufikia Desemba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna maeneo mengine kama vile Kwimba, Ngudu wamesha-*survey* tayari, nalo watalifikiria na maeneo mengine vile vile yapo hapa wameshaniarifu ambayo yamekuwa *surveyed* lakini mpaka watakapokuwa na mpango na kuagiza vyombo tutayataja.

Kwa upande wa Mchinga kama ilivyo Rungwe Mashariki nafikiri itakuwa ni mwaka kesho, *Mobitel* nao watafika Longido, Simanjiro, Babati, Kondoa, Mvumi, Mafinga, Kashai, Ngara, Karagwe, Buzebazeba, Rungufu, Same, Tarakea, Lindi, Kilwa, Butiama, Newala, Tandahimba, Misungwi, Manyoni, Tabora, Mombo na Pangani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilijaribu kutafuta majina ya namna hii kwa upande wa *Vodacom* hayakunifikia mapema, yatakaponifikia nayo nitayatangaza, lakini kwa taarifa za leo ni kwamba *Vodacom* watakuwa wamefika Mafia. Vile vile napenda kutangaza kwamba *Vodacom* wameishafika Butiama mpaka kule Mwitongo kwa Marehemu Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, heshima kubwa wametupa *Vodacom,* tunawashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema watuwie radhi mambo ni mengi kweli kweli, fedha tulizopata tunawashukuru kwa kile mlichotupa hatuwezi kufanya maajabu, lakini tutajitahidi kwa ushirikiano wenu. Nirudie tena fedha watakazotupa matumaini yetu watatupa, fedha tunazoomba hatutafanya maajabu lakini maajabu yanawezekana kutokana na ushirikiano kati yenu na sisi. Tumeweza kufanya mengi

katika kipindi cha miaka mitatu na nusu iliyopita katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi na tunawashukuru sana sana Waheshimiwa Wabunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**KAMATI YA MATUMIZI**

**MATUMIZI YA KAWAIDA**

**FUNGU 62 - WIZARA YA MAWASILIANO NA UCHUKUZI**

Kifungu 1001 - *Administration and General* ... ... ... ... 1,134,663,000/=

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. La kwangu ninahitaji tu kupata ufafanuzi hasa kuhusu masuala ya mabasi madogo aina ya daladala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria ya soko huria ni kwamba mtu anaweza kupanga bei ya usafiri wake kulingana na soko na watu wamekuwa wakifanya hivyo. Lakini kumekuwa na matatizo ambapo Mkoani Kilimanjaro, wananchi waliwahi kuandamana wakaenda kwa Mkuu wa Mkoa wakitaka kujua ni kwa nini bei za usafiri zimepanda sehemu nyingine mahali pa kilometa 20 ni shilingi 400/= mahali pa kilometa 10 ni shilingi 400/= hiyo hiyo lakini Mkuu wa Mkoa alisema hilo ni soko huru, kwa hiyo, hawezi kuamua chochote.

Lakini walivyopandisha bei za nauli Mkoani Dar es Salaam liliingiliwa na Waziri wa Fedha na Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na kusema kwamba hairuhusiwi na watu watakiona cha moto na bei za nauli zikapungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kupata ufafanuzi kwamba inakuwa kama *double standard,* Mikoani wanauliza mbona Dar es Salaam bei ya nauli imeshuka huku hakuna soko huru, mbona huku Mkuu wa Mkoa anashindwa kusimamia? Ningeomba kupata ufafanuzi kwa hilo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, subiri kifungu namba 2001, *Transport and Communication.* Tunaendelea na Mheshimiwa Jackson Makwetta.

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Katika kuchangia kwa maandishi nilitaka Mheshimiwa Waziri aelezee jinsi Wizara yake inavyojiandaa kupambana na mikakati ya chini chini ya kutaka kuua reli ya *TAZARA.*

Katika majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri nadhani inaelekea hakuelewa. Hatua zinazochukuliwa na majirani zetu sishangai chini ya uchumi wa soko, lakini ni kweli kwamba wakijenga reli ya kutoka Mpurungu mpaka Kasima, Nachipata na

Mchinji Malawi na hatua nyingine hizi ambazo zinafanyika hivi sasa za management ya reli ya Zambia ambayo sasa iko chini ya Makampuni binafsi na kushusha ushuru kwa bandari za Kusini. Sisi upande wa Tanzania reli ya *TAZARA,* Bandari ya Kigoma, reli ya Kati vitapungua nguvu yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipendekeza kwamba ili kupambana na ujanja huu, tujenge reli kutoka Tunduma mpaka Kasanga ili tuweze kuchukua mizigo ya Kongo ambayo ni kati ya tani 10 mpaka 12, tunachogombania hapa ni tani 50 ni kuanzia hiyo tu chini ya utaratibu wa sasa wa uchumi wa soko tunaweza tukalinda *TAZARA,* Reli ya Kati na Bandari yetu ya Kigoma. Nilidhani Mheshimiwa Waziri alinielewa na Bandari yetu ya Dar es Salaam ambayo ni *gateway to East and Central Africa* na kwamba angejibu mikakati ya kufanya Taifa letu lisipate hasara na njia zake. Naomba kupata maelezo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jackson Makwetta, hiyo iko kwenye *Policy and Planning* kifungu 1003 litakuja kujibiwa.

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Kifungu tunachokijadili mshahara wa Mheshimiwa Waziri, namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu aliyotoa kuhusiana na *DG* wa *TICRA* na mimi nataka nimhakikishie kama alivyosema hata mimi siko *personal* hii ni nchi yetu wote, lazima tuishughulikie, tuhakikishe kwamba inapata *the best.* Katika *submission* yangu nili-*quote* kipengele au kifungu cha 13 cha sheria ambayo imeunda *TCRA* na kwenye kipengele kidogo *under 13(2)* imetoa sifa nne kwenye makundi manne a, b, c, d ambazo zote anatakiwa kuwa nazo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *option* imetolewa kwenye c() tu kwamba anaweza kuwa na *Management* au *Law* au *Engineering* au kitu kama hicho lakini hizi zingine zote anatakiwa kuwa nazo. Sasa ningependa Mheshimiwa Waziri kama ambavyo alimuuliza alizaliwa wapi, basi atusaidie labda kwa sababu kwenye *CV* yake haionekani amuulize pia uzoefu wake kwenye *Sector* ya *Telecoms* hauonekani pale na ile ni *essential requirement* hakuna kwenye ile *CV* ambayo iko kwenye *Website by the way* nataka niwaeleze hii *CV* ambayo nilii-*quote,* iko kwenye *Website* unaweza kuipata tu ukienda kwenye *Google,* ukaweka *search screen* yako ya J.S. Nkoma utapata tu moja kwa moja. Hiyo nilikuwa napenda Mheshimiwa Waziri atusaidie.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia ningependa anisaidie chini ya kifungu namba 13(4) ambapo kifungu kinasema: "Huyu atakayeteuliwa basi anatakiwa asiwe kwenye ajira nyingine inayolipa fedha." Nilisikia kwamba ana Mkataba kwenye Chuo Kikuu cha Botswana Idara ya Fizikia unaondelea mpaka mwaka 2007 *and that is paying job.*

Sasa nilikuwa nimeomba hapa atueleza ameacha kazi kule na kama hajaacha ina maana amepata kazi wakati ana kazi nyingine ambayo ina mshahara. Hilo ningependa kama ataweza kwa sababu yuko karibu tunayemzungumza amekaa hapo kwenye *gallery* Mheshimiwa Waziri kwa ruhusu yako labda anaweza akamwuliza kama ameacha kazi huko.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri maelezo mengine, jibu lingine unaweza ukaacha lakini mengine naomba majibu.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Dr. James Msekela. Nikiri kwamba yote aliyozungumza ni mambo muhimu tu kama nilivyosema katika hali ya uwazi lazima tuwe wazi. Kwa hiyo, anachotaka ni taarifa za ziada ili naye akiulizwa aweze kujibu vizuri. Kwa hiyo, nitajaribu kulieleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Uteuzi kama nilivyosema ilikuwa na watu 38 walioomba hii kazi, ilipitia masuala yote yanayoulizwa na Mheshimiwa Dr. James Msekela mpaka mwishowe ikajiridhisha huyu awe mmoja wa wale watano ambao wangependekezwa kuangaliwa kwa kufanya upekuzi ili ijulikane kati yao anaweza kupendekezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nimewataja waliokuwa katika Kamati wakati mwingine tuwaamini, tuaminiane Watanzania. Lakini pamoja na hilo, nadhani Mheshimiwa Dr. James Msekela, tunafahamiana sana kwa upande ni mwanafunzi wangu na kwa upande ni mwenzangu kwa sababu tumefanya kazi pamoja baada ya kufaulu mtihani na anafahamu kwa sababu tuko katika fani moja ya Uhandisi. Labda tukumbushe tu kwamba Fizikia ndiyo chimbuko la Uhandisi, Fizikia ndiyo mhimili wa Uhandisi. Kwa hiyo, uzoefu gani anaoutaka katika kazi ya u-*director General* katika sifa zile kama mtu mwenye Udaktari wa Falsafa katika Fizikia, Mkuu wa Kitivo cha Fizikia Dar es Salaam na Botswana, unatafuta uzoefu gani huo zaidi?*(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tukumbushane na mwenzangu kwamba waliogundua mawimbi ya redio ni wataalam wa Fizikia na wala siyo Ma-*engineer* sisi tumekuja kudandia baadaye. Mheshimiwa Mbunge atakumbuka akina Michael Faraday, atakumbuka akina Alexander Graham Bell, atakumbuka akina Marconi, wote hawa ni watu wa Fizikia. Halafu atajua kwamba katika ngazi ya Udaktari wa Falsafa katika Chuo Kikuu chochote katika Uhandisi na Fizikia mara nyingi dunia hakuna tofauti. Hakuna tofauti kati ya *Engineering* na kitu tunachoita *Applied Physics.* Unaweza ukamaliza *Degree* ya *Electrical Engineering* ukaingia Udaktari wa Falsafa wa Fizikia, unaweza kuanzia Fizikia ukaishia *Electrical Engineering.* Sasa hili linatoka wapi na mwenzangu tunafahamiana na haya yote tunayajua pamoja! Ahsante.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu labda kama kazi ameacha ni wiki iliyopita amepata barua siku ya Ijumaa na tukamwambia lazima aje awepo hapa Bungeni na bahati nzuri amekuja na ameyasikia yeye mwenyewe haya tunayoyazungumza ili apate uzoefu. Kwa hiyo, aliitikia wito, amekuja, hajaja hata na mizigo anakwenda kuandika au kutoa barua ya ku-*resign* ili aje achukue kazi yake hii. Kwa hiyo, Mkataba wa mwaka 2007 haupo tena. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mimi ninadhani maelezo ni mazuri. Hebu Mheshimiwa Dr. James Msekela, kama kuna la nyongeza.

**MHE. DR. JAMES A. MSEKELA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia haki yangu.

Napenda niseme majibu ya Mheshimiwa Waziri ni mazuri. Ingawa kuna mjadala mrefu kwa sababu yeye na mimi tunafahamu kwamba *extent* ya *specialization* sasa hivi duniani ni kubwa mno kiasi kwamba ukisema uzoefu kwenye *Telecoms* mtu yeyote na *particularly* hata mtu wa *Physics* anafahamu kabisa *Telecoms* ni nini mathalani *Physics.* Lakini si haja yangu kuendeleza mjadala huo. Lakini niseme tu katika jibu lake hapa mwisho kama nimemwelewa amesema kwamba hii kazi huyu *DG* amepewa wakati bado ni muajiriwa wa Chuo Kikuu cha Botswana na kwamba baada ya hapa sasa ataenda ku-*resign* kule. Sasa hapa ningependa msaada hata wa *Attorney General,* tafsiri ya sheria hiyo ndiyo hiyo?

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali tusaidie katika hilo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimshukuru sana Mheshimiwa Dr. James Msekela, kwa kupenda sana kuona sheria za nchi zinafuatwa. Lakini kama alivyoeleza Mheshimiwa mtoa hoja unapoomba kazi yoyote kuna kupata na kukosa. Sasa katika hatua ya awali ambapo Dr. Nkoma na wengine walioomba walikuwa na shughuli zao. Maana unaomba tu ni pale unapopata sasa unajua kwamba sheria inanitaka mimi nifanye hivi, na kwa maana hiyo katika hatua tuliyofikia sasa itabidi mhusika atekeleze matakwa ya sheria ya nchi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. SAMWEL M. CHITALILO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kifungu 1001 kuhusiana na mshahara wa Waziri, sina shida ya kuchukua senti ya Mheshimiwa Waziri na vilevile sina maana nyingine mbali tu ilikuwa mwaka 2003 mwezi Novemba, ndani ya Bunge lako Tukufu wakati Naibu Waziri wake akijibu swali langu kuhusiana na mawasiliano kule Buchosa aliahidi kwamba kufikia mwezi Desemba, mwaka 2003 kungekuwa tayari na mawasiliano ya simu za *Celtel* pale Nyanguge, lakini hadi leo bado na hata hivyo leo wakati nachangia kwa mchango wa maandishi nimezungumzia hiyo habari. Basi ninachohitaji ni kwamba Mheshimiwa Waziri anipe maelezo ili niweze kuelewa na wananchi wangu waweze kujua. Ahsante sana.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimiwa Samwel Chitalilo, kama kawaida yake amekuwa mstari wa mbele sana kutetea haki za wananchi wa Jimbo lake na si katika hili tu tumezungumza suala la gati nalo tumelifikisha mahali pazuri. Hata hili tutalifikisha mahali pazuri tu. Ahsante.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts* ... ... ... ... ... ... ... ... 599,253,100/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 1003 - *Policy and Planning* ... ... ... ... ... ... ... ... 960, 592,700/=

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Natumaini maelezo yangu ya kwanza yameeleweka. Lakini labda nifafanue tu kwamba mikakati inayofanywa na majirani zetu inaelekea kudhoofisha uchumi katika Reli ya *TAZARA* kwa sababu zifuatazo: -

Moja kwa kujenga reli ya Mpurungu na Kasama, katika reli ya *TAZARA* na kuelekeza mizigo upande wa Kusini, *TAZARA* itakuwa haina kazi na kwa kujenga reli kati ya Nchinji na Chipata, Zambia na Malawi mizigo hii ya Zambia itakwenda Malawi Nakara. Kwa kufufua reli ya Nakara na Baira kuelekea Zambia na Zimbabwe na Malawi hali ya Malawi na Zambia itarudi kama ilivyokuwa kabla ya vita ambapo 95% ya mizigo yao ilikuwa inapitia Nakara na Baira.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilipendekeza kwamba kutokana na mikakati hii inayofanywa hata kama siyo ya wazi licha kwamba ugumu wa kukutana na Mawaziri wa Reli ya *TAZARA* sasa umekuwa ni mgumu na kwamba ndani ya Zambia reli ya Zambia sasa inaongozwa kwa Mkataba wa Kampuni ya Afrika Kusini wa miaka 20 ni kwamba tusipokuwa na mikakati yetu sisi huku tutajikuta kwamba reli ya *TAZARA* imebaki haina kazi.

Mhesimiwa Mwenyekiti, nikapendekeza kwamba tujenge reli kati ya Tunduma na Kasanga ili tuchukue mizigo ya Kongo ambako kuna *potential* ya mizigo kati ya tani milioni 10 mpaka milioni 12 na barabara vile vile ya Tunduma kwenda Kasanga na vile vile kuunganisha Mtwara na Makambako ili bandari hizi mbili ziweze kutumika vizuri kwa faida yetu. Tusipoangalia suala la wakati mikakati ya kujenga reli ya *TAZARA* na *Mtwara Corridor* itakuwa *taken* na *time* na tutajikuta kwamba tunatwanga maji ndani ya jiwe. Nadhani mapendekezo hayo kwa lengo la kulinda *TAZARA* na kulinda reli ya Kati, Bandari ya Kigoma na uchumi wa nchi kwa maana ya kutumia jiografia yetu ungepokelewa. Naomba Mheshimiwa Waziri anipe maelezo.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mawazo ya Mheshimiwa Jackson Makwetta ni mazuri sana, mimi ninachofanya ni kufuata nyayo zake alikuwa Waziri wa Wizara hii, kwa hiyo,sisi tunayachukua na tunayapokea kwa moyo mkunjufu na tutayafanyia kazi. Ahsante. *(Makofi)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2001-*Transport and Communication* ... ... ... ...19,399,485,300/=

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, nafikiri nililizungumzia lakini nilikuwa sijalimalizia vizuri kwamba pamoja na sheria hiyo ya soko huria wenye mabasi hayo wameunda ushirika na ushirika ule hupanga bei na kama mtu akija na gari lake akiamua kupunguza bei kulingana na soko, hupigwa au gari lake hupasuliwa pasuliwa vioo kuhakikisha kwamba anafuata masharti ya ushirika ule fulani. Kwa mfano, AKIBOA na mengine mengi. Sasa Mheshimiwa Waziri anasemaje kuhusu hilo?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Thomas Ngawaiya, labda nianzie na yale aliyozungumza mwanzo kuhusu kilichotokea Dar es Salaam na Moshi. Hakuna lililoharibika Moshi ambalo liliwezekana Dar es Salaam. Ni kwamba ni maeneo tofauti na kesi zilikuwa mbili tofauti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba mamlaka ya udhibiti kwa uchukuzi Dar es Salaam si Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi. Mamlaka ni Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam na alifanya kazi yake kama inavyobidi katika sheria. Mamlaka ya Uchukuzi katika Mkoa wa Kilimanjaro iko chini ya Mkuu wa Mkoa akiwa Mwenyekiti wa Bodi inayohusika. Kwa hiyo, alifanya maamuzi hayo kutokana na hali aliyoiona Moshi.

Katika suala la udhibiti inakatazwa kabisa kupanga bei kwa pamoja hilo siyo soko huria ni kinyume cha sheria ndiyo maana Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam aliweza kuidhibiti hiyo hali, kwa sababu aliwambia tunafahamu kabisa kwamba watu wa daladala mmekaa na mmepanga bei kwa hiyo hapo akaweza kuwadhibiti. Kwa hiyo, kama Moshi mambo yanaendelea kama yalivyo kutokana na jinsi mdhibiti alivyoona na hakuna tatizo la uchukuzi maana yake hakuna la kulalamikiwa lakini tunakushukuru Mheshimiwa Thomas Ngawaiya kwa kulileta. Namshauri Mheshimiwa Mbunge kwamba atakapokwenda kwenye *RCC* ya Mkoa aweze akalizungumzia kwa sababu naye ni mjumbe. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi ni ufafanuzi tu wa kuomba kufahamu maeneo yapi ya Same yatapata huduma ya *Celtel* ifikapo mwezi Desemba mwaka huu?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri umelielewa swali sijui?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Namshukuru sana Mheshimiwa John Singo, katika *list* niliyoisoma *Celtel* wameniambia Same, na mimi ninaamini wataanzia na Same Mjini. Lakini hata ikifika Same Mjini maana yake sasa kwenda vijijini ni rahisi zaidi kazi kubwa ni kufika Same Mjini. Sasa maeneo mengine yale ni *incremental costs* siyo tatizo kubwa. Kwa hiyo, naamini kabisa kwamba amefurahia taarifa hiyo na vilevile wananchi wa Same wameifurahia na kwa sababu amenialika niende Same kwenye Jimbo lake na Same katika Wilaya nadhani tutakuwa na nafasi ya kuliendeleza suala hili kwa maanufa ya wananchi wa Same.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa John Singo, bado?

**MHE. JOHN E. SINGO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake, lakini huduma ya *Celtel* iko pale kwa muda mrefu sana sasa ndiyo maana nikauliza kwamba ipo muda mrefu sasa ilipotajwa nikafikiri bila shaka ni kule ndani.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda katika kusoma nilikosea lakini *Mobitel* nao wanakwenda Same.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2002 - *Central Transport and Licensing* ... ... ... 964,800,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

**MIPANGO YA MAENDELEO**

Kifungu 1003 - *Policy and Planning* ... ... ... ... ... ... ... ...100,000,000/=

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)*

Kifungu 2001 - *Transport and Communication* ... ... ... 17, 865,541,900/=

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, nimemtambua na Mheshimiwa Elizabeth Batenga. Lakini naomba kwanza Mheshimiwa Waziri atoe maelezo kwa sababu alishatuletea taarifa kwamba atatoa maelezo katika kifungu hiki. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Bunge lako Tukufu liniwie radhi kuna masahihisho madogo tu ambayo hayabadili takwimu zozote zile isipokuwa ni maelezo.

Katika kifungu 2001 - *Transport and Communication* kuna mradi *6224 Railways Telecommunication Network phase III,* Dodoma-Tabora ukurasa wa 98 naomba tubadili mfadhili wa mradi huu ambaye ni Netherlands badala ya Ujerumani kama inavyoonekana kwenye kitabu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu mradi *6227 Development of 8 Berths in Tanganyika and Lake Victoria* ukurasa 99 usomeke *Development of 9 Berths in Lake Tanganyika and Lake Victoria.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kunipa nafasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nimechangia kwa maandishi nilikuwa nimetoa hoja kuhusu kifungu cha 106 katika hotuba ya Waziri ambayo nilikuwa nimeomba ufafanuzi. Labda kwa sababu ya muda Waziri hakupata muda wa kuifafanua. Sasa naomba nitumie nafasi hii kupata ufafanuzi wa kina.

Katika kifungu hiki Mheshimiwa Waziri katika hotuba yake amezungumzia juu ya kununua ndege ndogo tegemezi kwa ajili ya safari fupi na za dharura za viongozi wa Serikali. Sasa hapa ametuonyesha ndege ambayo tayari imenunuliwa. Lakini hapa bado anazungumzia ununuzi wa ndege nyingine tena tegemezi kwa safari fupi na za dharura. Nilitaka kujua maana ya maneno haya ni nini? Lakini vile vile nikastuka zaidi kwa sababu utaratibu huu wa kununua ndege hii umesemwa utatekelezwa ili uwakala uimarike zaidi. Ndiyo kusema unatekelezwa katika Bajeti hii?

Nimeangalia katika kifungu *Sub Vote 2001,* kimsingi sikuona mahali popote ambapo zimetengwa fedha kwa ajili hii. Lakini kwa kuwa utaratibu wetu unaruhusu fedha kutumika na baadaye ikatolewa taarifa sikutaka kuachia ipite tu kwa maana kauli hii ya Waziri nilitaka uhakika kama hii programu inatekelezwa vipi, Bajeti yake iko wapi, ndege inanunuliwa shilingi ngapi, inanunuliwa kutoka nchi gani na ni kwa nini tunanunua ndege ndogo kwa safari za dharura wakati tumepata ndege nzuri tu ambaye Waziri ametuonyesha hapa mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba ufafanuzi.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ndege za Serikali katika ununuzi wake si mradi wa maendeleo zinakuwa kwenye *recurrent expenditure* na huko tumeweka *100 token.* Kwa hiyo, tutakapopata fedha za kutosha, tutakapopata bei nzuri, tutakapopata ndege nzuri na hali tutakavyoiona wakati ule, basi tutafanya uamuzi maadam mtakuwa mmeshapitisha hicho kifungu cha *100 token* kwa ajili ya ununuzi wa ndege. Ndege tunayoisema kwa kweli itakuwa ni *helicopter.* Mheshimiwa Rais anaweza akatua Mwanza lakini kwenda Maisome atahitaji *helicopter* kwa kweli. Nadhani kwenda na gari kwa saa tisa kwa kweli hapana. Nchi hii ni kubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumekuwa Malawi huko juzi juzi, nilipata bahati ya heshima ya kuwa katika ujumbe wa Mheshimiwa Rais. Nchi ndogo kama ile tulichukuliwa na helikopta Mawaziri peke yetu, Marais ya kwao na wasindikizaji wengine kutoka mji mmoja kwenda mji mwingine ambao ingetuchukua saa sita kwa gari. Kwa hiyo, Tanzania tumechelewa sana.

**MBUNGE FULANI:** Na maafa?

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Na maafa na dharura ni nyingi sana kila wakati. Kwa hiyo, tunaomba mkubali.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na makofi mengi naomba iingie kwenye kumbukumbu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kujua kwamba tumenunua ndege kwa mabilioni wakati nchi yetu ina uchache wa fedha na shughuli muhimu. *(Kicheko)*

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walizomea)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nashukuru kwa sababu anayezomea kumbukumbu inaingia kwenye *Hansard.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesema hivi *priority* ya nchi yetu tumenunua ndege ya mabilioni, sasa baada ya kutumia ndege ya mabilioni wakati ule Kambi ya Upinzani tulisema kwa nini tusinunue *Presidential helicopter* inayotua katika viwanja vyote vya nchi hii? Leo ndege hii tulioonyeshwa hapa inathibitika kwamba haiwezi kutua kumbe sehemu fulani fulani.

Sasa ninataka kujua na nipate kwa uhakika je, ndege itakayonunuliwa kwa sababu hapa haielezwi ni helikopta ambayo itatumika kwa maafa au inaitwa tu ndege kwa maana ya ndege kama ndege za kawaida? Nilitaka nipate uhakika ili tunapopitisha tuwe tunapitisha kitu ambacho ni kwa manufaa ya wananchi wetu. Lakini kama ni ndege ya kawaida mimi sitaridhika nitatoa shilingi. *(Makofi/Kicheko)*

**MWENYEKITI:** Mmmh, lakini Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, mimi nimemsikia Waziri anaongea juu ya helikopta. Kwa hiyo, mimi kama Mwenyekiti, nimesikia anasema helikopta. Kwa hiyo, kama ni helikopta bora uridhike kwamba ni helikopta.

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli lakini haki yangu inasema Waziri alisema wanafikiria. Sasa inaelekea kwanza haijaamuliwa kama ni helikopta au ni ndege ya kawaida. Hapa tunapopitisha ni vizuri tukapitisha kitu ambacho tuna uhakika nacho. Sasa Waziri alikuwa anapendekeza ni helikopta ili tunapopitisha tujue kama ni helikopta.

**MWENYEKITI:** Mimi kama Mwenyekiti, nasema alisema helikopita. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nipate tu ufafanuzi kidogo.

Kwa kutumia kifungu 2001, ningependa Mheshimiwa Waziri anisaidie. Kwa sababu katika mchango wangu wa maandishi niliomba kujua tatizo la mizigo inayokwenda kwa mabehewa ya treni ya reli ya kati kuanzia Dodoma badala ya Dar es

Salaam. Nilitaka kujua tatizo hilo litakwisha lini? Kwa sababu wananchi wanaotegemea usafiri wa reli kwa kusafirisha mizigo hasa bidhaa kutoka viwandani kwenda Mikoa ya Kanda ya Ziwa, Kigoma na Tabora.

Kwa hiyo, hawa watu wanaumia sana, wananchi wanaumia sana kwa sababu bei za bidhaa hizo zimepanda sana. Sasa ningeomba kujua sababu ya tatizo ya bidhaa hizo kuanzia Dodoma na hilo tatizo litakwisha lini ili wananchi waweze kupata nafuu. Kwa sababu mikoa hiyo inaendelea kuwa maskini yaani matatizo yanazidi kuwa mengi wanaendelea kuwa maskini.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumtaarifu kupitia kwako Mheshimiwa Elizabeth Batenga kwamba kulikuwa na tatizo katika Bandari yetu ya Dar es Salaam kulikuwa na mlundikano wa shehena mwezi Januari ambao ulikuwa unapelekea Bandari kufungwa na kukosa sifa ambazo tumeimwagia Bandari yetu kwa muda mrefu.

Tatizo lilikuwa kiungo cha reli kutokana na mabehewa kuwa machache, lakini vile vile vichwa vya treni *(locomotives)* kuwa chache. Kwa hiyo, tulikuwa na operesheni ya muda ya kusukuma mizigo kutoka Bandari ya Dar es Salaam na tukakubaliana na wadau kwamba njia mojawapo ni kutumia barabara vile vile ili kuondoa msongamano. Kwa hiyo, tuliweza kufanya hiyo operesheni ili shehena ije Dodoma na kutoka Dodoma kwenda Bara zaidi ilikuwa haina tatizo. Kwa hiyo, hii operesheni tuliifanya na ilifanyika kwa ufanisi sasa tumeweza kuondoa tatizo hilo katika Bandari ya Dar es Salaam na hali inaanza kurudia ya kawaida na vile vile sasa shehena inaanza kutoka Dar es Salaam moja kwa moja kwenda Bara badala ya kuja Dodoma. Tutarudia tena kama kutakuwa na mlundikano wa shehena katika Bandari ya Dar es Salaam. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Elizabeth Batenga bado hujaridhika?

**MHE. ELIZABETH N. BATENGA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Waziri lakini nadhani yeye alifikiri au aliamua pengine kutatua tatizo hilo lakini wananchi waliumia. Sasa sijui anatambua hilo na anatarajia kufanyaje na anawaeleza nini?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri una maelezo? Wameshaumia tayari. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tunasikitika. *(Makofi/Kicheko)*

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

Kifungu 3001 - *Aerodroms* ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... ... 1,300,000,000/=

**MHE. OMAR S. KWAANG'W:**Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Mimi ya kwangu kwa kweli ni kutaka maelezo mafupi tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri na timu yake walifanya ziara Mkoa wa Manyara nadhani ni baada ya Bunge la mwezi Aprili na alikuja na wataalamu ikiwa ni pamoja na wataalamu wa Mamlaka wa Viwanja vya Ndege. Nina hakika walitembea katika maeneo kuona uwezekano wa kupata uwanja wa ndege ambao utakuwa karibu na Makao Makuu ya Mkoa mpya wa Manyara yaani Babati. Sasa nilitaka tu maelezo kwa sababu nimeangalia vitabu vyake vyote kwenye hotuba na kitabu hiki cha 4 sioni mahali panapoonyesha kwamba jambo hilo linaweza kufanyiwa kazi. Lakini vile vile kwenye maandishi yangu nimemwandikia kwamba kwa kweli nasikitika kwamba sikuona. Lakini pengine anayo maelezo mazuri ili nalo liweze kuingia kwenye rekodi basi na sisi tulioko kwenye mkoa mpya tupate na sisi uwanja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni hayo tu.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutumia nafasi hii kupitia kwako kumshukuru sana Mheshimiwa Omar Kwaangw' kwa kuungana nami katika ziara niliyoifanya Babati ambayo kwa upande wetu wa Mawasiliano na Uchukuzi ilikuwa ya mafanikio. Tulifanya ziara mkoa mzima isipokuwa Wilaya ya Hanang, lakini tutarudi huko tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli tulikagua maeneo ambayo tulifikiri yanaweza kuwa muhimu kwa ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Mkoa wa Manyara. Ni jambo zuri ambalo tumelifanya kwa pamoja na uongozi wa Mkoa wa Manyara kwa sababu lazima tuanze kupanga sasa. Tumeangalia site mbili tumeona moja inaweza kuwa bora kuliko nyingine. Tunachofanya sasa ni kuiweka katika *master plan* mpango kamambe wa uendelezaji wa viwanja vya ndege Tanzania hasa mpango huo ndio tutakaotumia pale tunapopata fedha za kutosha ili tuweze tukauendeleza.

Lakini kwa sasa tunamwomba Mheshimiwa Omar Kwaangw', pamoja na uongozi wa Mkoa wa Manyara wajaribu kuhifadhi hilo eneo kwa sababu tuna tatizo moja kubwa sana la kuingilia hifadhi ya maeneo ya maendeleo ili baadaye tusije tukaanza kuweka X tena na kuanza kutoa fidia ambayo inakuwa gharama kubwa sana ya ujenzi. Kwa hiyo tunaomba hilo lifanyike.

Lakini la pili, vile vile labda tufanye kwa pamoja inapowezekana maana yake tunaelekea vile vile kuanza kuwaomba wenzetu wa sekta binafsi tuwahusishe nao katika ujenzi wa miundombinu. Kwa hiyo, kwa pamoja tunaweza tukafanya kazi hiyo ili tuweze tukaona kama tukaweza kumpata mwekezaji ambaye anaweza kusaidiana na sisi katika ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Mkoa wa Manyara. Namshukuru Mheshimiwa Omar Kwaangw'.

**MHE. WILFRED M. LWAKATARE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Katika mchango wangu wa maandishi nilijaribu kuzungumzia suala la kiwanja cha Bukoba na hasa tukizingatia hali ya uwanja wenyewe na nashukuru Mheshimiwa Waziri

kwa awamu ya kwanza kushughulikia *VIP Lounge* ni kwamba Wizara imeshughulikia hivi sasa tuna *VIP Lounge* pale Bukoba Mjini. Lakini hali halisi ya uwanja wenyewe ile *runway* ni mbaya sana. Mheshimiwa Waziri anayo taarifa hiyo kwa sababu uongozi wa mkoa pamoja na Waheshimiwa Wabunge tuliwahi kumtembelea na akalipokea na akaliahidi kulifanyia kazi. Lakini ninapoona katika mafungu haya nashangaa kwamba Bukoba haitajwi sasa sijui Mheshimiwa Waziri ana mkakati gani wa kushughulikia uwanja huo ikizingatiwa kwamba kila mvua inaponyesha ina maana Bukoba hakuna ndege yoyote inayoweza kwenda kule.

Sasa naomba kufahamu Mheshimiwa Waziri suala hili analichukulia vipi na hasa ikizingatiwa kwamba wananchi wengi wa Bukoba wanautumia uwanja ule na namba ya abiria kwa kweli ni kubwa sana inayotumia uwanja ule? Nashukuru.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kuupongeza uongozi wa Mkoa wa Kagera kwa kazi kubwa wanayoifanya katika kutafuta njia za aina mbalimbali ili kwa pamoja tuweze tukaimarisha kiwanja cha ndege cha sasa cha Bukoba wakati tukiandaa mpango kabambe kuendeleza kiwanda cha ndege cha Omokajunguti.

Kwa sasa kupanga ni kuchagua, ni vigumu kufanya kila kitu kwa fedha chache hizi ambazo hata hizo zilizopo tunategemea wafadhili. Kwa hiyo, tunaweza tukafanya machache kwa mwaka huu. Lakini pamoja na uchache wa Bajeti tunawahakikishia kwamba kwa maana ya Mamlaka ya Viwanja vya Ndege tumetenga kiasi cha shilingi milioni 70 ili kukifanya kiwanja kiweze kikapitika hata wakati wa mvua. Kwa hiyo, tutajitahidi iwezekanavyo kufanya hilo liwezekane. *(Makofi)*

**MHE. ABDULKARIM E. H. SHAH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Mimi nilikuwa nina ombi au maelezo kwa Mheshimiwa Waziri. Ombi langu, jitihada zako kama nilivyosema tunazifahamu, tunazisikia, tunaziheshimu na tunazikubali. Ombi langu ili tuweze kusaidiana na yeye, inaelekea labda upande wa Wizara ya Fedha ndiyo kwenye kidogo tatizo.

Sasa nataka nimwambie Waziri kwamba tunaomba aitishe kikao cha pamoja kati ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi, Wizara ya Fedha na sisi Wabunge tunaotoka Mafia pamoja waihusishe na Wizara ya Maliasili na Utalii na ikiwezekana basi na Mheshimiwa kwa heshima zote naomba niseme na Waziri Mkuu aingie kwenye kikao hicho kama Kiongozi Mkuu wa Serikali tumweleze matatizo yetu ili aweze kutia nguvu ya kuweza kuongea yale ambayo tutayaongea kwa ajili ya kuombea fedha mradi huu wa kiwanja cha ndege cha Mafia. Kwa sababu zimetengwa fedha tumeziona, lakini labda mwenzangu tu ataweza. Lakini inaelekea labda nilivyomtaja Kiongozi Mkuu kuna maneno. Lakini tunasema hivi tunaomba basi aone kwamba kunawekwa kikao cha pamoja sisi Wabunge, wataalamu wake na Wizara ya Fedha ikiwezekana na Wizara ya Maliasili na Utalii ili tuweze kujua angalau wanaweza kuongeza nguvu kwa ajili ya kukitengeneza kiwanja hiki ili tuweze kufanikisha, kuboresha na kuweza kupunguza hizi gharama ndogo ndogo za kila siku za uwanja wetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mheshimwa Abdulkarim Shah na vile vile namshukuru Mheshimiwa Halima Kimbau, wametetea sana Mafia na bahati nzuri Mafia nimefika na nimekagua, nimeona hilo tatizo na nimeahidi kutumia uwezo wetu katika Wizara kuhakikisha kwamba tunatekeleza miradi miwili. Mmoja wa gati na wa pili ni wa kiwanja cha ndege. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Abdulkarim Shah, ananiomba niitishe kikao, namhakikishia kwamba ukiitisha kikao na hao wenzangu wengine maana yake nimeshindwa. Mimi sioni kama nimeshindwa. Hili suala bado ni letu na tumelivalia njuga na gati itapatikana na tutaboresha kiwanja cha ndege cha Mafia. Tunajua ni nini tunafanya. Atuamini tu, Mafia iko karibu sana na mioyo yetu. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Halima Kimbau, mimi nafikiri ni yale yale?

**MHE. HALIMA O. KIMBAU:** Ni tofauti kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nilikuwa namwomba Waziri, je, anatambua kwamba Mafia sasa hivi ni ndege moja tu inayokwenda ya *Coastal.* Hiyo ndege na fedha alizozitenga ni kwa maana ya mwaka mzima.

Katika mwaka huo kuna hali za mvua za vipindi karibu vitatu sisi Mafia na kwa fedha hizo ambazo zimetengwa na matengenezo ambayo wanayategemea kuyatengeneza kuna hatari ya hata ndege ya *Coastal* kutokutua Mafia. Sasa je, gati bado halijawa tayari. Kiwanja cha ndege, ndege hiyo nayo ikisimama anategemea sisi pamoja na wenzetu tutazifanyaje kazi hasa kwa wananchi hata kwa kuja Bungeni tutasafiri vipi?

Kwa hiyo, ningeomba kama hii fedha ndogo basi bora iachwe kabisa kuliko kupoteza fedha hii ikaingizwa mahali ambapo tuna hakika haitasaidia kitu. Je, atakubaliana na mimi aidha kuacha kabisa au tuongezewe fedha ili tuweze kuhakikishiwa kwamba mwaka huu kiwanja kile angalau ndege ya *Coastal* inaendelea kutua?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri ulisema umelivalia njuga. Hebu eleza maelezo mengine zaidi. *(Makofi/Kicheko)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeomba fedha kidogo lakini tunaomba hata hicho kidogo tusinyang'anywe. Kwa sababu tunaamini kidogo kitazaa kikubwa. Sasa haya mengine ya utekelezaji ni siri zetu atafika tu Bungeni Mheshimiwa Halima Kimbau, tunamhakikishia. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. DR. WILBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati mbaya kifungu tunachokiongelea ndicho hicho kimeunganisha Arusha na Mafia. Sasa katika hotuba ya Waziri ameeleza na ametenga fedha kwa ajili ya ukarabati wa uwanja wa Arusha, sina tatizo na ukarabati wa uwanja wa Arusha. Lakini niliomba ufafanuzi kwenye mchango wangu wa maandishi. Waziri anifafanulie vizuri kinachofanyika

Arusha ni kujenga uwanja mpya na kama ni kujenga uwanja mpya kama alivyoeleza mwenyewe.

Kwa kuwa kupanga ni kuchagua na kwa kuwa tuna mikoa mingi ambayo hatuna uwanja wa ndege. Na kwa kuwa uwanja wa *KIA* ni dakika 45 tu kutoka Arusha. Sasa tunajenga uwanja mwingine pale na sasa tumeshaanza kutumia fedha kwa uwanja wa Arusha.

Mimi nilifikiri kulikuwa na haja ya kukamilisha kazi mikoa yote ipate kwanza viwanja vya ndege ndipo tuanze kujenga uwanja wa Arusha. Lakini Waziri hakugusia hilo nilitaka kupata ufafanuzi tunapoongeza eneo la ardhi kama anavyosema kwenye Ibara ya 96 ni kazi gani tunayofanya na ni uwanja wa hadhi gani na ni kwa nini tunaufanya uwanja huu wakati tuna uwanja mwingine pale karibu tu wa *KIA*.

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumhakikishia Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, kwamba hatujengi uwanja mpya wala hatujengi uwanja wa Kimataifa pale Arusha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachofanya ni kukarabati kiwanja kilichopo kwa kukarabati njia ya kurukia na njia ya kuegeshea ndege. Kiwanja cha ndege cha Arusha ni kiungo muhimu sana kwa watalii na kinafanya kazi kwa kushirikiana na kiwanja cha ndege cha *DIA* na kwa mapato ni kiwanja cha tatu nchini kutuletea mapato. Kwa hiyo, ng'ombe anayekuletea maziwa hutaki kumwaacha afe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

*(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila ya mabadiliko yoyote)*

*(Bunge lilirudia)*

**WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa taarifa kwamba Bunge lako Tukufu likiwa limekaa kama Kamati ya Matumizi limepitia Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka 2004/2005 kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa mwaka 2004/2005.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi yalipitishwa na Bunge)*

**MHE. DR. ZAINAB A. GAMA:** Mwongozo wa Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asante, nilikuwa tu nataka mwongozo wako utusaidie ili tuone kama kuna mabadiliko ya kanuni basi kwenye Bunge twende kwa utaratibu huo.

Tunapokaa katika wakati wa Kamati huwa kawaida Mbunge anainuka kusema kifungu namba fulani, kifungu kidogo namba fulani. Kwa sababu kile kifungu kipo pale anaposema. Kwa hiyo, anapewa ruhusa, lakini leo nilichoona tumefika kwenye kitabu cha maendeleo na hasa tulipofika kwenye *Transport and Communication* kuna baadhi ya Wabunge waliinuka hawakusema kifungu kidogo kipi. Lakini wakaruhusiwa wakasema na Waziri akajibu.

Kuna mengine alitamka hata pesa hizo hazipo kwa sababu tunachoidhinisha kilikuwemo humu. Sasa tunaomba tu msaada wako kama mambo yamebadilika na sisi siku nyingine tukiona hakuna tunaweza kuzungumzia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, asante.

**MWENYEKITI:** Haya mwongozo wa Mwenyekiti, kwanza kama suala limeeleweka kwa Mwenyekiti mwenyewe na kama limeeleweka kwa Waziri mwenyewe basi anaweza akajibu. *(Makofi)*

Tunapotamka kifungu kwa ujumla wake kama ambavyo kile cha *Policy and Planning* basi mtu akitaka kuwa *specific* anaweza kusema hasa kakifungu fulani. Lakini kama unataka kuwa *general* tu kwamba mambo ya *Policy and Planning* anaweza akasemea lote hilo na kama Waziri ameelewa anajibu na kama vile vile Spika au Mwenyekiti ameelewa anajibu. Lakini kama hajaelewa anasema Mheshimiwa Mbunge hebu nitajie ni kifungu gani hasa unachosemea wewe. Kwa hiyo, hakuna lililoharibika hapo.

Nashukuru amenielewa Mheshimiwa Dr. Zainab Gama.

*(Saa 01.30 usiku Bunge liliahirishwa mpaka siku ya Jumatatu tarehe 5 Julai, saa tatu asubuhi)*